Nakala ya Mtandao (Online Document)

MAJADILIANO YA BUNGE

_____

MKUTANO WA ISHIRINI

_____

Kikao cha Ishirini na Moja - Tarehe 5 Juni, 2015

(Kikao Kilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole wote kwa msiba uliotupata, msiba ulitokea wakati nikiwa Geneva ambapo tulikuwa na kikao cha Kamati Ndogo ya maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Maspika wote duniani utakaofanyika mwezi wa Nane, sasa kuna Maspika kumi ndiyo tupo kwenye maandalizi ya mkutano huo na kilikuwa ni kikao chetu cha mwisho kabla ya mkutano huo.

Kwa hiyo, wakati msiba unatokea nilikuwa huko, nilipewa taarifa na nilisikitika sana. Kwa hiyo, tutatangaza baadaye mchana, ni akina nani watakaokwenda kuzika kesho. Katibu!

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES M. KITWANGA):

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

NAIBU WAZIRI WA MAJI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa Fedha, 2015/2016.

MHE. DAVID H. MWAKYUSA (k.n.y. MHE. PROF. PETER M. MSOLLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016.

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (k.n.y. MHE. MAGDALENA H. SAKAYA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 149

Ahadi ya Maji kwa Wananchi wa Wilaya ya Karagwe

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA (k.n.y. MHE. GOSBERT B. BLANDES) aliuliza:-

Mwaka 2013 Mheshimiwa Rais aliahidi kuwapatia maji wananchi wa Wilaya ya Karagwe kutoka Ziwa Rwakajunju lililopo Kata ya Bweranyange:-

Je, ni lini mradi huu utaanza na kukamilika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe inakadiriwa kuwa na asilimia 48 ya wakazi wanaopata huduma ya maji. Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali imeanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi ya maji kutoka Ziwa Rwakajunju umbali wa takribani kilomita 35 hadi Makao Makuu ya Wilaya ya Karagwe.

Mradi huu utahusisha maeneo yote yatakayopitiwa na mradi pamoja na Mji wa Kayanga na Omurushaka. Kazi hii ya Upembuzi imeanza na inafanywa kwa ushirikiano wa Wizara ya maji na Mamlaka ya Maji ya Mji wa Bukoba ambayo imeajiri mtaalam Mshauri *M/S Basler Holffman Limited* wakishirikiana na *M/S RWB* na WILALEX kuanzia mwaka wa fedha wa 2013/2014 na inatarajiwa kukamilika mwaka wa fedha 2015/2016. Aidha, rasimu ya taarifa ya upembuzi imetolewa na sasa wanaendelea na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa kuchukua maji kutoka Ziwa la Rwakajunju unatajia kunufaisha Mji Mdogo wa Kayanga/Omurushaka katika maeneo ya Ndama, Kayanga, Miti, Kagutu, Bujuruga, Kishao, Bugene, Nyabwegira, Nyakahanga na Ihanda yenye jumla ya wakazi 81,591.

Mheshimiwa Spika, aidha, vijiji vinavyotarajiwa kupitiwa na mradi huo na kunufaika ni pamoja na Vijiji vya Rukole, Chonyonyo, Kiruruma, Nyakagoyegoye, Nyamieli, Chabalisa, Ahakishaka, Nyakashenyi, Nyabiyonza, Nyakaiga na Kibondo. Azma ya Serikali ni kuhakikisha kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatekelezwa mara baada ya kukamilika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mradi wa maji kutoka Ziwa Rwakajunju.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutaja sehemu nyingi na kuonesha kuwa anajua kinachoendelea, lakini naomba nimuulize swali, utafiti tu umechukua miaka mitatu na sasa hivi mwenye swali alitaka kuuliza, ni lini itaanza hiyo shughuli ya kupatia wananchi maji na akawa anataka kuuliza, huo utaratibu utakamilika lini?

Mheshimiwa Spika, swali la nyongeza, hili swali liko sawasawa na wana Misenyi ambao tuliuliza Mto Kagera uko katikati ya Mji wetu Mkuu wa Wilaya ya Misenyi na Misenyi hakuna hata bomba moja la maji, hakuna kabisa, hivyo, tunauliza ni lini mtatuwekea maji na Waziri wa Maji

alituambia karibuni wataanza kutupa maji salama. Ni lini sasa wataanza kutupatia maji wana Misenyi ikizingatiwa kuwa tumezungukwa na maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mshama kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa nikubaliane na majibu ya Msingi ya Mheshimiwa Naibu Waziri na niseme tu kwamba, hii ni ahadi ya Rais, kwa maana ya pale Karagwe, alitoa Mheshimiwa Rais na tumesema kwamba tutatekeleza lakini mradi wowote wa maji ni lazima upitie hatua zote. Kwa hiyo, kwa sasa tunafanya usanifu wa kina, lakini pia katika bajeti ya mwaka huu kumetengwa fedha bilioni moja kwa ajili ya mradi huu. Kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa awe na subira na apitishe bajeti yetu ambayo ni leo ili ahadi hii ya Rais tuanze kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu Misenyi ni kweli na nimekuwa nikiongea naye na ameshamwona Waziri tunatekeleza Mradi wa Vijiji Kumi na wazo alilotoa sisi kama Wizara tunalipokea na tunataka kutumia maeneo mengi ambayo yana vyanzo, maziwa na mito kuona kwamba tunapata maji ya uhakika. Kwa hiyo, azma ya Serikali iko pale pale, tutashirikiana naye kuona kwamba yale aliyoshauri tunayafanyia kazi.

MWENYEKITI: Ahsante, Wizara ipo mtayasema vizuri. Sasa tuendelee na Mheshimiwa Joseph Selasini swali linalofuata Mheshimiwa Suzan Lyimo kwa niaba yake, naona watu wamekwenda kutangaza nia hawapo humu ndani.

Na. 150

Kupandisha Hadhi Mji wa Rombo kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo

MHE. SUZAN A.J. LYIMO (k.n.y. MHE. JOSEPH R. SELASINI) aliuliza:-

Mji wa Rombo uko katika Kijiji cha Kelamfua hadi sasa:-

(a) Je, Serikali iko tayari kuupandisha hadhi Mji huo ambao una vigezo vyote vinavyotakiwa kama vile Hospitali, Mahakama, soko, idadi ya watu na kituo cha mabasi kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kulipa fidia kwa wananchi ambao watalazimika kutoa mashamba yao ili kupanua eneo la Mji huo?

SPIKA: Ahsante. Naona watu wamekwenda kutangaza nia, hawamo humu ndani. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kuwa Mji wa Rombo umekidhi vigezo vyote vya kupanda hadhi na kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo. Kupitia Bunge lako naomba kutoa taarifa kuwa, tayari Serikali imekwisharidhia na kupandisha hadhi Mji wa Rombo kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Rombo na sasa unatambulika kama Mamlaka ya Mji

Mdogo wa Mkuu Rombo na umekwishatangazwa kwenye tangazo la Serikali *(GN)* Na. 431 la tarehe 31 Oktoba, 2014.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa makazi nchini unaongozwa na Sera ya Taifa pamoja na Sheria ya Mipango Miji, Sheria Namba 8 ya mwaka 2007. Kwa miongozo hiyo, shughuli zotye za uendeshaji wa makazi zinasimamiwa na Halmashauri ya Miji, Wilaya, Majiji na Manispaa husika.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imepanga kuwashirikisha wananchi wa maeneo yaliyo karibu na mji huo ili waridhie kuachia maeneo yao kwa ajili ya upanuzi wa huduma za jamii kama shule, maeneo ya ibada, soko, kituo cha polisi, kituo cha mabasi na huduma zingine muhimu pasipo kuhusisha ulipaji fidia. Endapo itabainika wako wananchi wanaohitaji kulipa fidia, Serikali itafanya uthamini wa maeneo hayo ili waweze kulipwa kulingana na Sheria na miongozo yetu iliyopo.

SPIKA: Mheshimiwa Suzan Lyimo, swali la nyongeza!

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, nashukuru na vile vile naishukuru sana Serikali kwa kuweza kupandisha hadhi huu Mji wa Rombo. Maswali ya nyongeza; kwa imekuwa ni hulka ya Serikali kutokulipa fidia kwa wakati na kwa bei ya soko, hivyo kufanya wananchi wengi kukataa au kugoma kuhama kwa ajili ya masuala mbalimbali ikiwemo hospitali, shule na vitu vingine. Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuhakikisha kwamba watawalipa wananchi hao fidia kwa gharama ya soko la wakati huo?

Mheshimiwa Spika, la pili, imekuwa vile vile ni tabia ya Serikali kupandisha hadhi Mikoa, Miji kwa matangazo, lakini vile vile haitoi kipaumbele cha kibajeti, kwa mfano, tunashuhudia Mikoa kama vile Geita, Katavi na Mkoa wa Njombe ambayo imepandishwa kuwa Mikoa, lakini unaona kabisa kuwa bado bajeti hairuhusu na hivyo masuala mbalimbali ya kijamii, kwa mfano, hospitali na mambo mengine unakuta yako palepale. Sasa naomba kujua ni kwa nini Serikali inapandisha hadhi lakini miundombinu inabaki vile vile na hivyo kufanya wananchi washindwe kupata maendeleo kwa wakati?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunapopandisha Miji hii midogo kupata Mamlaka husika ni lazima kuwe na zoezi la upimaji na ongezeko la huduma mbalimbali ili kukidhi mahitaji ya kuwa Mji kwenye eneo husika na pale ambapo tunagusa maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa fidia, tathimini hufanyika.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi Halmashauri inapopendekeza maeneo hayo kuwa Miji, jambo la kwanza tunawataka wao wenyewe waweke mipango yao ya ndani ya kuhakikisha kwamba tunapata maeneo ya kuweka hizo huduma mbalimbali kwa masharti nafuu na wananchi husika kwa sababu maombi yale yanakuwa ni ya wananchi wenyewe. Kwa hiyo, jambo la kwanza ni kuhamasisha Halmashauri ili waende kwa wananchi wahamasishe kupata maeneo, lakini inapoonekana ni lazima tulipe, fidia huwa inafanywa baada ya kufanya tathimini kwa gharama ya soko kama ambavyo inafanyika, kwa sababu Sheria zipo na jambo hili linaongozwa Kisheria.

Mheshimiwa Spika, la pili, tunapopandisha hadhi Miji hii ni kweli kuwa tunaweza kuwa tunakwazwa na uboreshaji ule wa huduma kutokana na matatizo ya bajeti tuliyonayo na kwa hiyo, mara nyingi utakuta Halmashauri zinapoomba kupata hadhi ya Miji midogo na kwa kuwa

Sheria lazima unapopandisha Mji ni lazima huduma zote ziboreshwe, tunapoona tunakwazwa na bajeti ya kuupandisha Mji huo, mara nyingi huwa tunaiomba Halmashauri ifanye subira mpaka pale ambapo sisi tutakuwa tayari kwenye bajeti tuweze kuuweka.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Bajeti hii tunaporidhia, tunawashirikisha Halmashauri husika katika kuweka bajeti. Kwa hiyo, bajeti inaweza kuwa ni kutoka TAMISEMI lakini pia na Halmashauri yenyewe. Kwa hiyo, utakuta tunapokubaliana kama Halmashauri kama ilikuwa haijawa tayari, kunaweza kuwa na uchelewaji lakini pia malengo yetu ni kuhakikisha kuwa huduma zote zinapatikana pindi tunapopandisha hadhi Miji yetu.

SPIKA: Ahsante. Swali linalofuata ni la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine, ataulizwa swali hilo na kwa niaba yake Mheshimiwa Ester Bulaya!

Na.151

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka

MHE. ESTER A. BULAYA (k.n.y. MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE) aliuliza:-

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 iliyozinduliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 13 Februari, 2015, inaweza kuwa au isiwe mkombozi wa elimu hapa nchini:-

(a) Je, ni lini Sera hiyo itaanza kutumika rasmi?

(b) Je, Serikali imefanya mapinduzi yapi ya kuifanya lugha ya Kiswahili viwango vyote vya elimu kwa mujibu wa Sera hiyo?

(c) Matumizi ya kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo katika elimu ya msingi kwa mujibu wa Sera hiyo ni tishio kwa waandishi na wachapaji wa vitabu. Je, Serikali inawashauri nini wadau hao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Chacha Nyambari Nyangwine, Mbunge wa Jimbo la Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ilianza kutumika mara tu baada ya kuzinduliwa na Mheshimiwa Rais tarehe 13 Februari, 2015. Kama nilivyoojibu swali namba 242 katika Mkutano wa 16 wa Bunge tarehe 28 Novemba, 2014, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Sera mpya ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Ibara ya 3.2.16, imetamka bayana kwamba lugha ya Taifa ya Kiswahili itatumika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo na Serikali itaweka utaratibu wa kuwezesha matumizi ya lugha hii kuwa endelevu na yenye ufanisi katika kuwapatia walengwa elimu na mafunzo yenye tija Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, hivyo kuwa na tamko la Kisera ni hatua muhimu sana na ya kimapinduzi kuhusu umuhimu wa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika ngazi zote za elimu. Sambamba na dhamira hiyo ya Serikali lugha ya Kiingereza itaendelea kutumika katika kufundishia na kujifunzia kama lugha ya pili. Hii ni kutokana na umuhimu wake kama lugha ya mawasiliano Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kitabu kimoja cha kiada yataondoa mkanganyiko katika Sera ya Elimu, sekta ya elimu uliotokana na tofauti za upimaji wa ufundishaji, ujifunzaji na kusababisha wanafunzi wengi kushindwa mitihani kutokana na kutokujua kusoma, kuandika na kuhesaba (KKK).

Mheshimiwa Spika, aidha, uamuzi huu hautawaathiri waandishi na wachapishaji binafsi wa vitabu kwa kuwa wataendelea na utaratibu uliokuwepo wa kuandika na kuchapisha vitabu vya ziada *(reference books)* na vifaa vingine vya kujifunzia na kufundishia chini ya uratibu wa Taasisi ya Elimu Tanzania *(TET)* kulingana na Waraka wa Elimu, Namba 4 wa mwaka 2014.

SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya, maswali ya nyongeza!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wote tunatambua umuhimu wa Kiswahili, lakini kumekuwa na tatizo kubwa, wanafunzi wamezoea kufundishwa lugha ya Kiswahili kwa ngazi ya *Primary* inapofika Sekondari na Chuo Kikuu unakuta kabisa lugha ya Kiingereza kwao inakuwa ni ngeni. Sasa kwa dunia ya leo ya Upinzani, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa lugha hizi zote kutumika kuanzia ngazi za shule msingi na isiwe lugha ya pili kutokana na hali halisi kwamba lugha ya Kiingereza ndiyo lugha ya dunia na sisi Tanzania hatuko kwenye kisiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa Sera hii iliyopo na changamoto za elimu katika nchi yetu, mnadhamni Sera hii inaweza kutengeneza vijana wanaoweza kushindana kitaaluma kwenye soko la dunia?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba maswali mawili ya nyongeza yote aliyoyauliza Mheshimiwa Ester Bulaya ni ya muhimu. Hata hivyo, Waheshimiwa Wabunge, nawakumbusha kwamba tuliwagawia Sera ya Elimu na nafikiri kila Mbunge anayo. Nafikiri kama wote mngekuwa mmesoma ukurasa wa 38, tamko la Serikali, ibara ya 3:2:19, naomba niwasomee kwa kifupi sana, inasema hivi:

"Serikali itaendelea na utaratibu wa kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiingereza katika kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo".

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hapo hatukusema kwamba lugha ya Kiingereza itaachwa kabisa, lakini naomba niwasihi kwamba, sasa hapa naomba nijibu na swali lake la pili, baada ya awamu ya kwanza ya kutoa sera mpya ya elimu tunakwenda awamu wa pili ya kutoa mikakati ya jinsi ya kutekeleza mikakati ya Sera mpya ya Elimu. Hapo tutakuwa tumechambua ni kiasi gani tutatumia lugha ya Kiswahili, pamoja na lugha ya Kiingereza na kwa hiyo, hapo wakati wa kimkakati tutawahusisha wadau wote ikiwa ni pamoja na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naomba Watanzania wasiwe na wasiwasi kabisa. Hatuwezi kujiweka wenyewe ndani ya chupa na kuacha kutumia lugha ya Kiingereza ama sivyo tutashindwa kuwasiliana na Mataifa mengine.

SPIKA: Mheshimiwa Laizer!

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, swali la pili la Mheshimiwa Ester Bulaya lilihusu vijana, naomba nimhakikishie kwamba, kulingana na ambavyo tutatoa mikakati ya kutekeleza Sera yetu ya Elimu, tutaweka vijana katika hali nzuri sana ya kuweza kuwasiliana na ulimwengu wa kwanza kupitia lugha ya Kiingereza.

SPIKA: Alijibu! Isipokuwa hakutaja vijana. Mheshimiwa Laizer, swali moja la nyongeza!

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika nchi yetu kuna wanafunzi wengi ambao hawajui kusoma na kuandika, hasa vijana wanaotoka Vijijini na tatizo ni kwamba vitabu hivi vya kiada na kufundishia havipo, pamoja na upungufu wa Walimu, yote mawili yakiwa ni changamoto hao watoto wanashindwa kusoma na kuandika. Je, Serikali itapeleka lini vitabu katika shule hizo zilizopo kule Vijijini?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Laizer kwa kuuliza swali hilo kwa sababu limekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali iligundua kwamba, tuna tatizo la watu wengi hasa wanafunzi kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu. Kwa hiyo, Serikali imeweka utaratibu maalum ambao tumekuwa tunafundisha Walimu wa darasa la kwanza na la pili, tunawapa mafunzo ya siku tisa. Jana mimi mwenyewe nimekwenda kuzindua mafunzo hapo *UDOM* ikiwa ni awamu ya nne ya kuwapa mafunzo Walimu wa darasa la kwanza na la pili kwa ajili ya kutatua tatizo la KKK.

Mheshimiwa Spika, naomba kutangazia nchi hii kwamba, tangu tumeanza kutoa mafunzo hayo jana ndiyo tunakamilisha kwamba tumetoa mafunzo kwa Walimu 18,000 kwa hapa *UDOM*. Pia tuna madarasa 68, leo ni siku ya tatu pale *UDOM* na Walimu wale wa darasa la kwanza mpaka la pili watakaa pale *UDOM* kwa siku tisa kwa ajili ya kuboresha KKK.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Kahigi!

MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Uelewa mdogo wa lugha za kigeni hapa Tanzania ambao ni pamoja na Kiingereza unatokana na ukosefu wa Walimu ambao ni weledi wa lugha hizi, pamoja na njia mbovu za kufundishia zilizopo katika shule zetu za Msingi na Sekondari. Je, Serikali itatatuaje matatizo haya?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wote na Watanzania wote kwamba hilo tatizo la Kiingereza kwa Walimu wanaofundisha watoto wote tumeligundua. Sambamba na mafunzo tunayotoa kwenye KKK, tunatoa mafunzo ya Walimu wanaofundisha Kiswahili, Kiingereza na Hisabati kwa nchi nzima sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme ukweli kwamba, nilikwenda Mkoa wa Kilimanjaro kuzindua mafunzo haya na tutakuwa tunachukua Walimu watatu watatu, kwa nchi nzima kwa shule zote mpaka ikifika mwezi wa Tisa tutakuwa tumemaliza kutoa mafunzo haya.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (ELIMU): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini pia niweke nyongeza ya namna nzuri au njia nzuri inayotumika sasa katika kufundisha ili kuleta matokeo mazuri ni kwamba, tumebadilisha kutoka *content based* katika ufundishaji, sasa tupo katika *competence based* ambayo inamshirikisha mtoto katika matendo huku akiwa anapata taaluma hiyo. Njia hiyo ndiyo nzuri zaidi katika kuweza kutambua lugha yenyewe. Hiyo ndio njia ambayo sasa hivi tunatumia katika ufundishaji, kuliko ile ya kwanza ya *content based.*

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara!

WABUNGE FULANI: Bado swali moja la Wizara ya Elimu.

SPIKA: Aaa, moja *okay*, liko wapi?

WABUNGE FULANI: Swali linalofuata.

SPIKA: Okay, hili la 152, ni kwa sababu ya akina Mheshimiwa Nassari, wamenipeleka hapa.

Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga tafadhali, swali linalofuata!

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kuwa mzima na leo nikaweza kusimama katika Bunge lako Tukufu kuuliza swali ambapo nilikuwa sikutarajia kurudi tena kwenye Bunge hili.

MBUNGE FULANI: *Allah Akbar!*

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga naomba swali namba 152, lipatiwe majibu.

Na. 152

Kupungua kwa Idadi ya Wanafunzi Wanaokwenda Kusoma Kenya na Uganda

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR (k.n.y. MHE. MKIWA A. KIMWANGA) aliuliza:-

Katika miaka ya 1985 hadi 1998 hivi tulishuhudia idadi kubwa ya watoto wanaotoka Tanzania kwenda nchini Kenya na Uganda kusoma elimu ya msingi na sekondari:-

Je, ni sababu gani zimesababisha kupungua kwa kiasi kikubwa kwa idadi ya wanafunzi wanaokwenda kusoma kwenye nchi hizo?

SPIKA: Mheshimiwa Amina aliugua sana hapa. Kwa hiyo, leo ndiyo siku ya kwanza anaingia humu ndani. Ndiyo maana amesema hivyo. Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baadhi ya wazazi wamekuwa wakipeleka watoto wao Kenya, Uganda na baadhi ya nchi za Ulaya kabla na baada ya mwaka 1985 kusoma elimu ya msingi au sekondari. Kwa kuwa jambo hili lilikuwa ni utashi binafsi wa wazazi, halikuwa linaratibiwa na Serikali kwa maana ya iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, sababu zinazoweza kuwa zinachangia baadhi ya wazazi kupeleka watoto wao Kenya na Uganda katika kipindi hicho ni kama ifuatavyo:-

Baadhi wa wazazi wamekuwa wakiwapeleka watoto wao Kenya, Uganda na nchi nyingine kwa kudhani kuwa elimu iliyokuwa inatolewa katika nchi hizo ilikuwa ni bora zaidi kwa kigezo cha matumizi ya lugha ya Kiingereza. Kwa mfano, baadhi ya wazazi walipeleka watoto wao kujua lugha ya Kiingereza cha kuzungumza na kuandika kuanzia elimu ya msingi, kama ilivyo sasa. Lugha ya kufundishia na kujifunzia kuanzia ngazi ya elimu ya msingi nchini Unganda na Kenya ni Kiingereza ambapo Tanzania ni Kiswahili na Kiingereza.

Mheshimiwa Spika, idadi ya shule za msingi zilizokuwa zinafundisha kwa lugha ya Kiingereza hapa nchini katika kipindi cha mwaka 1985-1998 zilikuwa 41 tu, ukilinganishwa na shule 740 zilizopo sasa. Aidha, nafasi za kuendelea na elimu ya sekondari katika kipindi hiko zilikuwa chache ikilinganishwa na idadi ya wahitimu wa darasa la saba. Kwa mfano, idadi ya wanafunzi waliohitimu darasa la saba na kuchaguliwa kidato cha kwanza walikuwa asilimia 5.5 (mwaka 1985) na asilimia 19.1 (mwaka 1998) ya wahitimu wote ikilinganishwa na asilimia 55.5 (mwaka 2014).

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Amina swali la nyongeza!

MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna wazazi bado wanapeleka watoto wao nje ya nchi kwa ajili ya masomo na tayari hapa Tanzania kuna shule ambazo zimeboreshwa ambazo hayo wanayoyapata nje na hapa watayapata yale yale. Je, ni lini na Serikali itaboresha shule zetu ili wazee wasiendelee kupeleka nje watoto?

SPIKA: Haya. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, mimi ni Mwalimu, naomba kusema kwamba, kitu hasa ambacho kilikuwa kinawasukuma wazazi wengi kupeleka watoto wao hasa Kenya na Uganda na watoto hawa wakiwa ni wadogo ni watoto wa shule za msingi, ilikuwa ni kisaikolojia tu kwamba watoto wanapokwenda Kenya na Uganda watapata Kiingereza kizuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, wazazi sasa wameshajua kwamba Kenya na Uganda watoto walichokuwa wanapata ni kile Kiingereza cha kuzungumza na kuandika, lakini upande wa elimu bora, Tanzania elimu bora bado ipo. Sasa hivi tumepanua elimu sana, tunajitahidi kuboresha elimu ya msingi na naomba wote tukubali kwamba tumeboresha elimu yote kwa sababu nyie wote hapa mmesoma Tanzania na mko ndani mna elimu bora. Kwa hiyo, tukubali elimu ya Tanzania ni bora na Kiingereza tutaendelea kukipata. Ahsante.

SPIKA: Susan umesimama weee! Sasa nikuite! *(Kicheko)*

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mwanasaikolojia maarufu sana ulimwenguni Sigmund Freud and Erik Erikson na Erick Erickson katika *child development*

theories, wanasema kwamba mtoto katika ile miaka ya mwanzoni ni vyema sana akae na wazazi, kwa ajili ya mapenzi na vilevile kum-*groom*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba wazazi wanaendelea kuwapeleka watoto wao nje na Mheshimiwa Waziri anasema elimu imeboreka, hivi karibuni Rais wa Rwanda ametangaza rasmi kwamba ni marufuku watoto wa chini ya miaka sita kuwa shule za *boarding*. Je, Serikali inalizungumziaje hilo? Kwa sababu kwenda kule maana yake mmomonyoko vile vile wa maadili unapungua kwa sababu hawako na wazazi hasa wanapokwenda nje ya nchi. Je, Serikali mnasemaji kuhusu hilo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, niwaombe Watanzania wanisikilize vizuri. Kwanza licha ya kuwa ni Mwalimu lakini pia ni mzazi. Kwa hiyo, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba mtoto anapokuwa mdogo sana mpaka umri wa miaka kumi na nne, anahitaji kuwa chini ya malezi ya mzazi wake. Kwa hiyo, hili suala la kuwapeleka watoto wadogo Kenya, Uganda nje ya mikono ya wazazi ni suala ambalo linawaharibu watoto sana, hasa wanapokuwa ni wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikiri na mimi nimesikia kwamba Serikali ya Rwanda imezungumza hayo, lakini naomba niwaambie Watanzania kwamba ni vyema Rwanda tuwaache na mitazamo yao na sisi Watanzania tuwe na misimamo yetu na tusimame pale pale kwamba, mtoto anapokuwa mdogo kuanzia mwaka wa kwanza mpaka wa kumi na nne, ni vyema wazazi wakaa na watoto wao kwa sababu wanahitaji malezi mengi, si elimu tu, lakini na malezi ya watoto.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Naomba tuendelee na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Albert Ntabaliba atauliza swali linalofuata!

Na. 153

Mpango wa Kujenga Masoko Maeneo ya Mipakani

MHE. ALBERT O. NTABALIBA aliuliza:-

Mpango wa kujenga masoko katika maeneo ya mipakani ulijumuisha pia ujenzi wa soko la Mnanila/Buhigwe:-

(a) Je, kwa nini Serikali inawadharau wananchi kwa kutotekeleza mradi huo?

(b) Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza mradi huu?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ADAM K. MALIMA (k.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na masoko kwa ajili ya wananchi wake na hivyo haiwezi kudharau utekelezaji wake. Mpango wa

kujenga soko la Mnanila ulikuwa chini ya Mradi wa Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo Wilayani *(District Agriculture Sector Investment Project (DASIP)* kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(African Development Bank)*, ambao ulikusudiwa kujenga masoko saba katika maeneo ya Mtukula (Misenyi), Kabaga (Ngara), Nkwenda (Karagwe), Mrongo (Karagwe), Mnanila (Buhigwe), Remagwa (Tarime) na Busoka (Kahama).

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Masoko mawili ya Mnanila na Mtukula haukuanza kutokana na kucheleweshwa kwa taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi waliotoa ardhi yao kwa ajili ya ujenzi wa masoko hayo. Kutokana na taratibu za malipo ya fidia kuchukua muda mrefu, Benki ya Maendeleo Afrika ambayo ndiyo ilikuwa inafadhili miradi hiyo, ilishindwa kutoa fedha kutokana na mradi huo kubakiza muda mfupi wa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, masoko matano yaliyopata ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika yanayojengwa katika Halmashauri za Kahama (Bandari Kavu), Karagwe (Mkwenda na Mirongo), Ngara (Kabaga) na Tarime (Sirari) yamekamilika kwa asilimia 45 hadi 60.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha ahadi ya kujenga soko la Mnanila, Serikali imeuweka mradi huo kwenye mradi wa pili wa *DASIP* ambapo maombi ya kuomba kuongeza muda wa mradi na fedha yalishakamilika na kuwasilishwa Benki ya Maendeleo ya Afrika, ili kuweza kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa soko la Mnanila na kukamilisha ujenzi wa masoko matano ambayo yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi ipo katika mazungumzo na Benki ya Maendeleo Tanzania, zamani *TIB* kwa lengo la kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa Soko la Mtukula.

Mheshimiwa Spika, wakati Halmashauri ikisubiri ridhaa ya Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AFDB)* kuongeza muda wa mradi *(DASIP II),* namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe kuiga mfano wa Halmashauri ya Misenyi kuanza kufanya mawasiliano na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuona uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya soko la Mnanila kutoka vyanzo vya ndani.

SPIKA: Mheshimiwa Obama swali la nyongeza!

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali mawili.

La kwanza, kwa kuwa mmekiri kwamba, ujenzi wa soko hili ni muhimu na nyie wenyewe umepeleka maombi *African Development Bank* kwa ajili ya kulifadhili. Je, unahisi ni lini *extension* hiyo mtaweza kukubaliwa?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa ujenzi wa masoko haya ni mpango wa Wizara ya Viwanda na Biashara, je, hamwoni haja ya kuendelea na mazungumzo na Benki yetu ya Maendeleo iliyopo hapa nchini?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ADAM K. MALIMA (k.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA): Mheshimiwa Spika, kwanza ujenzi wa soko kama tulivyosema ni muhimu, ndiyo maana Serikali ikakingia kifua na kwenda kuomba fedha chini ya mpango huu wa *DASIP II (African Development Bank)*.

Mheshimiwa Spika, sisi na *African Development Bank* tuna *programmes* nyingi kwenye sekta mbalimbali, kwa hiyo zote zipo katika taratibu za kupitishwa na Bodi yao na tunatarajia kwamba kwa kuwa kikao cha Bodi kimemalizika hivi karibuni, tutapata maeneo ambayo yatafadhiliwa katika mwaka huu unaokuja na kama ipo katika program ya miaka mitatu tutapata maelezo. Naomba tuendelee kuwasiliana hasa sisi wa Wizara ya Fedha ili tumwambie hii *DASIP II* sisi na *African Development Bank* tumekubaliana itaanza lini na itatolewa kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, hili la pili ni kweli kwamba Wizara ya Viwanda na Biashara ndiyo inayoshughulikia hili, lakini kuna Wizara ya Kilimo inayohusika na mambo ya *DASIP* moja kwa moja na Wizara ya Fedha ambayo inashughulika na upatikanaji wa fedha za wafadhili hasa hizi za *African Development Bank*.

Sasa naomba nimsihi Mheshimiwa Mbunge, amewahi kuja ofisini kwetu kwa ajili ya kufuatilia hizi fedha za *African Development Bank* na nampongeza sana. Naomba tuendelee kufuatilia kwa upande wetu ili tujue kwamba hizi pesa za *African Development Bank* zinapatikana lini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa pili, hii kufuatilia pesa za *African Development Bank,* ahimize Halmashauri bado zitakuwa katika utaratibu na sisi Wizara ya Fedha tutasaidia kusukuma ili mradi huu na miradi mingine inayotegemea vyanzo vya ndani ipate ufadhili kutoka *African Development Bank.*

SPIKA: Mheshimiwa Susan Kiwanga!

MHE. SUSAN. L. A. KIWANGA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali inajenga masoko madogo madogo mengi hususan Wilaya ya Kilombero kwenye Kata ya 35, kuna masoko mengi yamejengwa lakini hayatumiki. Je, haioni kwamba kuna haja ya kujenga soko kubwa ambapo wakulima wanaweza kupeleka mazao yao na wafanyabiashara kutoka nje wanaweza wakanunua mazao hapo, ukizingatia Wilaya ya Kilombero ina kilimo kikubwa cha mpunga, *cocoa* na ndizi na matokeo yake yale masoko madogo madogo hayatumiki kabisa?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ADAM K. MALIMA (k.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA): Mheshimiwa Spika, yale masoko madogo nayo yana kazi yake, kwa sababu lengo lake ni kuhakikisha kwamba wakulima wanaweza kufikisha bidhaa zao pasipo na umbali mkubwa na ndiyo maana tulipokuwa Kilimo tukasema tujenge hii *concept* ya masoko madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, bado pia kuna *contradiction* upande wa pindi kwamba wafanyabiashara wanapenda ku-*access* masoko makubwa kwa sababu pale anakuwa na uwezo wa kupata bidhaa nyingi. Kama ulivyosema pale atakuta mpunga mwingi, ndizi, *cocoa* na bidhaa mbalimbali.

Mheshimwia Spika, kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba bado tuna nafasi ya masoko madogo, lakini wazo la Mheshimiwa Susan la kuwa na masoko makubwa kwenye maeneo

yenye uzalishaji mkubwa wa kilimo hasa pale uzalishaji unapokuwa wa bidhaa mbalimbali ni jambo zuri, naomba lianzie kwenye Halmashauri yako likienda TAMISEMI, sisi Wizara ya Fedha pia tutalizingatia kama ni jambo muhimu na kulitengenezea utaratibu.

SPIKA: Mheshimiwa Zungu, swali lingine la nyongeza!

MHE. MUSSA A. ZUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka kuiomba Serikali, masoko ni pamoja na mazingira ya biashara. Je, ni lini Serikali sasa itafikiria au kama inayo mkakati wa kuwa na *offshore business environment* ili kutanua wigo mkubwa sana wa biashara na ku-*attract foreign investors*?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ADAM K. MALIMA (k.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA): Mheshimiwa Spika, hili la *offshore business environment,* sura yake ni kwamba lina-*address* kwa upana zaidi Tanzania kama chanzo cha bidhaa mbalimbali kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, nadhani hili kwa upande wa Serikali tumelizungumzia kwa namna nyingi, tumezungumzia pia kuwa na *economic station* huko nje kwenye Balozi zetu, lakini hiki ni kituo mahsusi anachozungumzia Mheshimiwa Zungu cha kuwa na mfumo wa kuwa na *off shore business environment*. Nadhani ni wazo zuri, tutakaa Serikalini tuliangalie, tuangalie uwezekano wa kulitekeleza. Ni jambo zuri kwa sababu pia linasaidia kupatia *branding* bidhaa za Tanzania kwa maana ya ubora na viwango na wingi wa bidhaa zetu zinazoweza kwenda nje bila kuwa na masuala ya wafanyabiashara kutoka nje kuhangaika kupata bidhaa zetu na uwekezaji.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Kazi na Ajira, Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Rajab!

Na. 154

Serikali Kuleta Bungeni Mkataba Kuhusu Kazi Zenye Staha kwa Wafanyakazi wa Majumbani

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (k.n.y. MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI) aliuliza:-

Je, Serikali italeta lini Mkataba Na. 189 unaohusu Kazi Zenye Staha kwa Wafanyakazi wa Majumbani ili uridhiwe Bungeni?

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sekta ya huduma za majumbani ni moja kati ya sekta zenye mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Idadi kubwa ya wafanyakazi wa majumbani duniani kote wanajihusisha na kazi za kuangalia watoto na kuchangia malezi yao, kutunza wazee na kadhalika. Kwa kufanya hivyo, wanawezesha waajiri wao kufanya kazi kwa ufanisi katika sekta mbalimbali hivyo kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango huo mkubwa wa wafanyakazi wa majumbani, Serikali imechukua hatua mbalimbali kuwezesha kuridhia kwa mkataba huu kama ifuatavyo:-

(i) Kujenga uelewa wa wadau kuhusu haki za wafanyakazi wa majumbani;

(ii) Kujenga uwezo wa Maafisa Kazi juu ya mbinu za ukaguzi kazi na usimamizi wa haki za kazi kwa wafanyakazi wa mjumbani; na

(iii) Kufanya utafiti linganifu kuhusu sheria za kazi dhidi ya matakwa ya mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kuwasilisha mkataba huu Bungeni mara baada ya Baraza la Mawaziri kuupitisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchakato huu wa kuridhia Mkataba Na. 189 unaohusu wafanyakazi wa majumbani kuendelea, wafanyakazi hawa kama walivyo wafanyakazi wote wanaendelea kulindwa na Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004. Aidha, Serikali imetangaza kima cha chini kwa sekta hii ambacho waajiri wa wafanyakazi hao wa majumbani hawaruhusiwi kulipwa.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Rajab, swali la nyongeza!

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwanza nasikitika sana kwa kuchelewa kupelekwa kwa Mkataba huu katika Baraza la Mawaziri ili kuweza kuletwa hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tukubali kwamba hali ya unyanyasaji wa hawa wafanyakazi wa majumbani ni kubwa na bado inaendelea kuwepo hali ambayo kwa kweli inasikitisha sana kwa wafanyakazi hawa. Nataka kujua tu kutoka Serikalini, wakati tunasubiri mchakato huu na kwa vile sheria nyingine tayari ipo, je, hadi sasa hali halisi Tanzania juu ya wafanyakazi hawa wa majumbani ikoje?

Mheshimiwa Spika, la pili; Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la kima cha chini hapa cha mshahara anaweza kuutangazia umma leo hii ni kiasi gani wanapaswa hasa kulipwa wafanyakazi hawa wa majumbani?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba bado kuna unyanyasaji wa wafanyakazi hawa wa majumbani kwenye maeneo kadha wa kadha na waajiri hasa waajiri binafsi. Wengine ni viongozi kama sisi hapa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasikitika sana na unyanyasaji huu na imekuwa ikichukua hatua za kukagua, lakini tumekuwa tukitoa wito vile vile kwa wafanyakazi hawa wa majumbani wasikubali kukaa tu na kunyanyaswa, wajaribu kutoa taarifa za unyanyasaji ambazo zinatokea, ikiwa ni kwenye malipo au masaa ya kupitiliza na kadha wa kadha. Serikali itaendelea kufanya kazi ya kukagua ili kuona kwamba wanapata haki zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kima cha chini, kima cha chini kimetangazwa katika sekta hii ambayo hatakiwi kulipwa chini ya shilingi laki moja.

SPIKA: Ahsante. Tuendelee na Wizara ya Nishati na Madini tumepita muda. Mheshimiwa Said Mtanda kwa niaba yake Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

Na. 155

Utekelezaji wa REA - Mchinga

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (k.n.y. MHE. SAID M. MTANDA) aliuliza:-

Mradi wa *REA* unaoendelea kutekelezwa kwenye Jimbo la Mchinga umeviacha Vijiji vichache vya Matapwa, Ruvu, Dimba, Lihimilo, Mnyangara, Namkongo, Kiwawa na Mputwa ambavyo viko umbali wa mita chache kutoka eneo la mradi:-

(a) Je, ni sababu ipi ya msingi iliyofanya vijiji hivi kuachwa?

(b) Je, baada ya maombi haya Serikali itakuwa tayari kuvipatia umeme vijiji hivi?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES P. MWIJAGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Mohammed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini kwa kushirikiana na *TANESCO* wamefanya upembuzi wa awali wa kazi ya kupeleka umeme katika Vijiji vya Matapwa, Ruvu, Dimba, Lihimilo, Mnyangara, Namkongo, Kiwawa na Mputwa, mradi unaohusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 umbali wa kilomita 53, ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4, umbali wa kilomita 14 na ufungaji wa transfoma au mashine umba saba. Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.5

Mheshimiwa Spika, vijiji hivyo havikujumuishwa kwenye mpango kabambe wa umeme vijijini awamu ya pili chini ya ufadhili wa Mfuko wa …

SPIKA: Sasa mmeingia mnapiga kelele aaah! Mheshimiwa Waziri, endelea.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES P. MWIJAGE): Mheshimiwa Spika, vijiji hivyo havikujumuishwa kwenye mpango kabambe wa umeme vijijini awamu ya pili chini ya ufadhili wa Mfuko wa Nishati Vijijini (*REF*) kutokana na ufinyu wa bajeti. Hata hivyo, vijiji hivyo vitapewa kipaumbele katika miradi ya kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu kama ilivyoainishwa kwenye *National Electrification Investment Prospectus* kwa mwaka wa Fedha 2015/2016.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Murtaza maswali ya nyongeza!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naishukuru Serikali kwa majibu yanayoleta matumaini. Ningependa kuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, nini ahadi ya Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu kwamba vijiji vyote vinavyopita bomba la gesi kuanzia Mtwara hadi kufika Dar es Salaam, kwa maana ya maeneo ya Kilwa pamoja na Mchinga, Kilwa Kaskazini, maeneo ya Kilanjelanje, Mandawa na kadhalika. Lini mradi huu utaanza kutekelezwa na ahadi hii itatekelezeka lini maana wananchi wamekaa wakitumaini kwamba hili litatekelezwa?

Pili, kuna ahadi ya utekelezaji wa mradi wa *REA* kwenda Kijiji cha Mtoni pamoja na Kijiji cha Kinjumbi katika eneo la Kata ya Somanga. Lini mradi huu utaanza na utatekelezwa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. CHARLES P. MWIJAGE): Mheshimiwa Spika, maagizo ya Serikali ya kujenga mfumo wa umeme kwenye mkuza wa bomba unatekelezwa na nisingependa kufungua kasha la mkubwa wangu wa kazi, kesho tutawaeleza bayana. Ninachoweza kuwaambia, Wakandarasi wawili wameshapewa kazi wanafanya upimaji na wakati wowote wataanza kazi. Kama nilivyosema Mkuu wangu wa kazi kesho anafungua kasha lake, ataweka mambo hadharani sitaki kuharibu shughuli ya Bwana.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Kijiji cha Mtoni na Kinjumbi, Mheshimiwa Mangungu tumepeleka umeme kilomita 200 Mpatimo na Maguruwe, hatuwezi kushindwa kijiji hiki kipo kwenye *scope* tunakishughulikia. Nawaagiza watekelezaji, muanze kutafuta Kijiji hiki cha Mtoni na Kinjumbi muanze kazi wakati bosi wangu kesho anasoma taarifa.

SPIKA: Ahsante, kwa kuzingatia huyo Bosi wa mwenzetu tunaruka maswali haya, tunakwenda Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Assumpter Mshama!

Na. 156

Uwanja wa Ndege cha Omukajunguti

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA aliuliza:-

Mwaka 2010 Mheshimiwa Rais katika kampeni za uchaguzi aliahidi ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Omukajunguti na mpaka leo watu wamezuiliwa kulima katika maeneo yao wakiwa bado hawajalipwa fidia:-

(a) Je, ni lini ahadi hiyo itatimizwa?

(b) Watu waliozuiliwa kutumia maeneo yao watalipwa lini fidia zao?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI - MHE. CHARLES M. KITWANGA (k.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mbunge wa Nkenge, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ina mpango wa kujenga kiwanja kipya cha ndege, Mkoa wa Kagera kitakachokuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa katika eneo la Omukajunguti lenye ukubwa wa hekta zipatazo 2,400 linalojumuisha vitongoji vya Mushasha, Bulembo na Bugorora. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa uthamini wa mali za wakazi wa eneo la Omukajunguti ulifanywa mwaka 2010, ulibainisha fidia ya shilingi bilioni 12. Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege yaani *TAA*, itaanza kulipa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya kuendeleza kiwanja cha ndege cha Omukajunguti kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali katika jibu la sehemu (a) ya swali hili, malipo ya fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa na Serikali kwa ajili ya kuendeleza kiwanja cha Ndege cha Omukajunguti ni stahili yao. Hivyo Serikali kupitia

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* itaanza kulipa fidia kwa wakazi hao kwa awamu kuanzia mwaka wa fedha 2015/2016.

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa namna alivyojaribu kujibu hili swali, lakini naomba tu nimuulize maswali mawili ya nyongeza. Kama alivyotamka mwenyewe Mheshimiwa Waziri kwamba ni hekta nyingi, ni hekta zaidi ya 2000 na zaidi ni nyingi sana na unaweza ukaangalia ni wananchi wangapi waliokuwa wamo katika maeneo hayo na wamechukua eneo lililo *fertile* kuliko maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza, Waziri ametaja kabisa kwamba hayo makadirio yalikadiriwa 2010 na kwamba watalipwa bilioni 12. Je, atawalipa hizo hizo bilioni 12 au ataangalia sawa sawa na soko lilivyo kwa sasa ili aweze kuwalipa kadiri inavyotakiwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, watu hawa wamekaa muda mrefu wakisubiri kufidiwa na kama wangekuwa wamelima wangelima na kupata mazao ya kutosha, ni zaidi ya miaka saba wamechukua eneo hilo. Je, watakuwa tayari kuhakikisha kwamba wanapowalipa wanawalipa na fidia ya muda wote waliopoteza?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI - MHE. CHARLES M. KITWANGA (k.n.y. WAZIRI WA UCHUKUZI) Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Assumpter kwa jinsi anavyofuatilia mambo mbalimbali katika Jimbo lake pamoja na Mkoa wa Kagera akishirikiana na Wabunge wenzake. Kikubwa ninachoweza kusema ni kwamb, malipo ya fidia yatatolewa kulingana na Sheria ya Ardhi, Na. 4 ambayo inatamka wazi kabisa malipo yatafanyika kulingana na thamani ya soko wakati huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kulipa fidia, nimtaarifu tu Mheshimiwa kwamba tutazingatia sheria zaidi badala ya kuanza kuzungumzia mambo ya fidia kwa kulipa kulingana na thamani ya soko wakati huo, maana yake na fidia hiyo itakuwa imeshatolewa.

SPIKA: Ahsante. Tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi.

Na. 157

Migogoro ya Mipaka

MHE. MODESTUS D. KILUFI aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaainisha mpaka kati ya wananchi wanaopakana na hifadhi mpya ya Ruaha Usangu *National Park* iliyokuwa Usangu *Game Reserve* ili kuondoa migogoro ya mipaka kati ya *TANAPA* na wananchi?

(b) Je, Serikali itafuata makubaliano ya kutumia ramani ya awali kufuata makubaliano yaliyofikiwa kwenye kikao cha pamoja kati ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Utalii na Wataalam wa Wizara pamoja na Waziri wa Maliasili na Utalii ili kuwatendea haki wananchi wa Mbarali ambao wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu juu ya Serikali kuongeza ardhi nje ya eneo ambalo Serikali iliwalipa fidia?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi, Mbunge wa Mbarali, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Aprili, 2015, nilitembelea Wilaya ya Mbarali na nilipata fursa ya kuzungumza na wananchi wa Vijiji vinavyozunguka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha. Aidha, nilitoa ahadi ya Serikali ya kurejea upya mipaka ya hifadhi hiyo na kulifanyia marekebisho Tangazo la Serikali Na. 28 la mwaka 2008, ili mipaka halisi iliyokuwa imekubaliwa kati ya wananchi na Serikali iweze kufanyiwa marekebisho na kwamba vijiji 21 ambavyo vilikuwa katika hati hati ya kuhamishwa sasa havitahamishwa.

Mheshimiwa Spika, mchakato huu ukikamilika, Serikali italeta Bungeni Azimio la kuliomba Bunge lako Tukufu, liliridhie mabadiliko hayo ya mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Kilufi, swali la nyongeza!

MHE. MODESTUS D. KILUFI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yanaonesha kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inawajali wananchi wake. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; pamoja na nia nzuri ya Serikali kurejesha vijiji hivyo 21, lakini wapo watu ambao wanaendelea kuwapotosha wananchi wa Mbarali kwamba Serikali inawadanganya uhamisho upo pale pale. Naomba Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali awathibitishie Wanambarali kwamba tamko la Serikali ni tamko halali na halina upotoshwaji wowote.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa vile uhamisho huu ulikwenda sambamba na malipo ya nyongeza ya fidia kwa wale waliohamishwa na kupunjwa, vile vile wananchi wa Mbarali hasa hawa Wahanga wangependa kujua ni lini fidia hiyo pengine ingelipwa au ni utaratibu gani unaendelea kwa ajili ya kuwalipa nyongeza hiyo ya fidia. Ahsante sana.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyosema katika jibu langu la msingi Serikali haitawahamisha wananchi kutoka vijiji 21 ambavyo tumevitaja. Naomba wananchi wa eneo hili la Mbarali waendelee kukaa kwa amani na kufanya kazi zao na utaratibu niliousema utafanyika mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili linahusiana na fidia. Niseme tu kwamba, baada ya wananchi hawa wa Mbarali kuhamishwa katika utaratibu wa kwanza, utaratibu wa mipaka ambayo tulikubaliana kati ya Serikali na wananchi, fidia hiyo ilipwa, kasoro kuna wananchi ambao walikuwa wamepunjwa fidia. Naomba nitoe *commitment* ya Serikali kupitia Bunge lako Tukufu kuwahakikishia wananchi hao wote ambao wanadai hiyo fidia, baada ya sisi kukamilisha *verification* ya hiyo fidia, tutawalipa fidia kamili kupitia Shirika letu la *TANAPA*.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali linalofuata, kwa niaba yake Mheshimiwa Nassari!

Na. 158

Hotel Levy Hoteli za Karatu

MHE. JOSHUA S. NASSARI (k.n.y. MHE. CECILIA D. PARESSO) aliuliza:-

Wilaya ya Karatu ina Hoteli 52 za kitalii zinazowahudumia wageni wanaotembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Ngorongoro, lakini pamoja na uwepo wa Hoteli hizo, Halmashauri haipokei "*Hotel Levy*":-

Je, ni kwa nini Serikali imekataza Halmashauri isitoze kodi hiyo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *Local Government Financing Act* na mabadiliko ambayo yamefanywa mwaka 2003, Kifungu cha 16(2), Hoteli za Kitalii hazikutakiwa kulipa *Service Levy*.

Mheshimiwa Spika, *Finances Act No. 8 of 2012,* Kifungu cha (6) kinasema naomba kunukuu, "*All monies derived from service levies payable by corporate entities or any person conducting business with business license at the rate not exceeding 0.3 percent of the turnover net of the value added tax and excise duty: Provided that, the branches of corporate entities shall pay services levy to the urban authorities in whose area of jurisdiction they are located.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, umetokea mgogoro wa kisheria kati ya wawekezaji wa mahoteli, Hoteli za Kitalii na Halmashauri kadhaa kuhusu ulipaji wa *Service Levy*. Wawekezaji wameweka pingamizi Mahakamani na hukumu hiyo inatarajiwa kutolewa mwezi Juni, 2015.

Mheshimiwa Spika, katika Juhudi za Serikali za kukuza na kuendeleza utalii nchini na ili kuendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia, Serikali ilitunga Sheria Mpya ya Utalii ya Mwaka 2008. Sheria hii ilifuta Sheria za Hoteli, *Cap No.* 105 na Wakala wa Biashara za Utalii, *Cap No. 65,* ya mwaka 1972.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufutwa Sheria ya Hoteli na Wakala wa Biashara za Utalii, Sheria Mpya ya Utalii inaruhusu kuanzishwa kwa Kanuni ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii ambayo inatamka kuwa, mwenye Hoteli atapaswa kumtoza kila mtalii au mgeni anayelala katika Hoteli yake kwa kitanda kwa siku Dola moja na nusu ya Kimarekani.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekataza kutoza *Hotel Levy* kwa sababu, Sheria iliyounda Kanuni ya Tozo iliifuta. Kwa sasa Serikali inakusanya tozo ya maendeleo ya utalii *(tourism development levy)* ambayo, hutozwa kwa kila mgeni anayelala hotelini na fedha zote zinakwenda Serikali Kuu kusaidia kuendeleza utalii nchini.

SPIKA: Mheshimiwa Nassari maswali ya nyongeza!

MHE. JOSHUA S. NASSARI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nina maswali mawili ama moja la nyongeza. Kwanza kabisa sipendi kuongelea habari ya kesi iliyoko Mahakamani kwa sababu, tutaingilia Mhimili mwingine, lakini nihoji tu kwamba, sasa ni nini manufaa ya Hoteli hizi za Kitalii kwa watu wanaozunguka Hoteli hizi au Halmashauri ambazo Hoteli hizi ziko ndani yake?

Mheshimiwa Spika, nazungumza hapa nikiwa ni mdau mzuri kwa sababu kule kwangu Arumeru Wilaya yangu ndiyo inayoongoza kwa Hoteli nyingi za Kitalii. Sasa kama kuna tatizo la ajira kwamba, wananchi wanaozunguka Hoteli nyingi za Kitalii hawapati ajira kwenye Hoteli hizo, badala yake tunaona idadi kubwa ya watu kutoka nje na hususan Wakenya, mpaka kwenye kufagia, mpaka kwenye upishi, mpaka kwenye kupaka *polish*-rangi ndani ya hoteli na ushahidi ninao.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kwenye suala la *Corporate Social Responsibility* bado hatuoni ni kwa namna gani uwekezaji huu ambavyo kweli unasaidia jamii zinazozunguka. Sasa na Serikali hii vile vile imefuta *Hotel Levy,* lakini tozo ya maendeleo ya utalii kwa maana ya *tourism development levy* inakwenda moja kwa moja Serikali Kuu. Sasa ni nini manufaa ambayo wanapata wananchi wanaozunguka Hoteli hizi za kitalii ama Halmashauri ambazo Hoteli hizi za Kitalii zimo ndani yake?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi!

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, moja nimhakikishie kwanza Mheshimiwa Nassari kwamba, katika maeneo ambayo yanaongoza kwa utalii na kwa ajira ni mahoteli ambayo kwa sasa yanaongoza katika kuajiri vijana wetu. Ni kweli, kuna baadhi ya mahoteli ambayo yalijenga desturi ya kuleta meneja kutoka nje ya nchi mpaka wafanyakazi wa kawaida, lakini tumeukataza huo utaratibu na kisheria hauruhusiwi. Kama kuna mwenye hoteli yeyote anayefanya hivyo na kuingiza watu kinyemela ambao hawana vibali vya kufanyia kazi nchini, atakuwa anatenda kosa na atachukuliwa hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nimhakikishie vile vile kwamba, hoteli hizi zinalipa kodi nyingi. Hapa tumezungumzia tu *Hotel Levy* na hii *Tourism Development Levy,* lakini hoteli hii inalipa *Corporate Tax* 30%, Hoteli hiyo hiyo inalipa *VAT,* Hoteli hiyo hiyo inalipa *Concession Fee,* Hoteli hiyohiyo inalipa *VETA!* Kuna jumla ya kodi 52 tofauti tofauti ambazo ziko *applicable* kwa hoteli na zinachangia kwa kiwango kikubwa sana maendeleo ya nchi na kodi hizi zinaingia katika Mifuko mbalimbali ya Serikali na tutaendelea kuboresha sheria hizi kuhakikisha hoteli zinaendelea kuwepo, zinaendelea kujengwa, lakini kuhakikisha zinawafaidisha wananchi kupitia ajira na kupitia malipo ya moja kwa moja yanayolipwa katika Serikali zetu. Ahsanteni sana.

SPIKA: Ahsante. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Amina Andrew Clement!

Na. 159

Mabati ya *Asbestos*

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT aliuliza:-

Serikali inatambua kuwa, mabati ya Asbestos ni hatari kwa afya ya binadamu kwa sababu ungaunga unaomung'unyuka na maji yanayotiririka kwenye mabati hayo husababisha kansa – *Asbestosis*:-

Je, kwa nini taasisi za Serikali bado zinatumia ofisi na nyumba za kuishi Askari zilizoezekwa kwa bati hizo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Andrew Clement, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *asbestos* ni aina ya madini yanayopatikana ardhini katika umbo la nyuzinyuzi, *(Bundles for Fibres)*. Madini ya *asbestos* yana sifa ya kuhimili joto au moto mkali na hulika kutokana na mguso wa kemikali. Mara nyingi yametumika kwenye kutengeneza vifaa vya ujenzi ambavyo ni dari, vigae, mabati na vifaa vya magari, kama vile *brake* na *clutch*. Madini haya yapo katika makundi makubwa mawili ya *Serpentine Asbestos* na *Amphible Asbestos*. Tofauti yake ni urefu wa nyuzi.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya *asbestos* yamepigwa marufuku katika nchi nyingi duniani; Tanzania kupitia Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura ya 182 ya mwaka 2003, Kifungu cha 30, kinazuia matumizi ya bidhaa ya kemikali aina ya *asbestos*.

Mheshimiwa Spika, tafiti nyingi duniani zinaelezea kuwa *asbestos* ni chanzo cha saratani na madhara makubwa kwa wanaoishi kwenye nyumba zenye bidhaa zinazotokana na *asbestos*. Madhara ya *asbestos* yanaanza kuonekana kuanzia miaka 10 hadi 30, watu wanaweza kuathirika wakiwa kwenye mazingira ya kazi anayoshughulika na *asbestos,* majumbani au katika jamii iwapo wanavuta hewa yenye vumbi la *asbestos* ambapo husafirishwa mpaka kwenye mapafu na iwapo vumbi hilo litakaa kwa muda mrefu huweza kusababisha kovu na uvimbe kwenye mapafu na hatimaye kusababisha kupumua kwa shida na kusababisha matatizo ya afya.

Mheshimiwa Spika, athari za *asbestos* kwenye mazingira ni pamoja na uchafuzi wa hewa, maji na chakula, ambavyo vyote hivi vikitumiwa na binadamu huleta athari za kiafya. Aidha, kuwepo kwa madhara ni mpaka pale ambapo *asbestos* itaharibiwa aidha kwa kubomolewa pale ilipo na kupukutisha vumbi au kufanya kazi kwenye viwanda vya *asbestos* na hivyo wafanyakazi kama hawana vifaa vya kujikinga binafsi, wanaweza kuwa katika mazingira hatarishi. Hivyo, kwa kuwepo mabati ya *asbestos* kwenye nyumba hakuna madhara ya kiafya mpaka pale *asbestos* hiyo inapokuwa imeharibiwa. Mwezi Oktoba 2013, Wataalam wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, *NEMC,* walitembelea mitambo inayoweza kuteketeza *asbestos* na taka hatarishi huko Afrika Kusini na Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya majengo yenye *asbestos* itafanywa ili kubaini aina ya *asbestos* iliyopo katika mabati hayo, ili kuweka makubaliano na kampuni mojawapo yenye mitambo ya kuharibu *asbestos*. Hii ni kwa sababu, taratibu za kuteketeza *asbestos* zinahitaji utalaam wa hali ya juu na ni kampuni iliyopata usajili wa kufanya shughuli hizo tu inaweza kufanya kazi hiyo, hivyo, ubomoaji wowote lazima ufuate taratibu husika za Kitaifa na Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, wananchi na Taasisi wasiharibu mabati hayo mpaka hapo watakapopewa ushauri wa kitaalam.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Amina, swali la nyongeza!

MHE. AMINA ANDREW CLEMENT: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, napenda kumuuliza maswali mawili ya nyongeza. Katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Waziri amesema hivi, watalaam wa Wizara ya Afya pamoja na wa *NEMC* tayari wameshakwenda Afrika ya Kusini ili kuangalia viwanda vinavyoteketeza mabati hayo. Je, Serikali imejipanga lini kuanza zoezi hilo ili kuteketeza mabati yale mabovu yaliyoko katika

nyumba za askari, hasa katika Mji wa Zanzibar, Kijiji cha Machui, Kambi ya Machui, kuna mabati tayari yameshaezuka yako chini na ni hatari? Pia, yaliyoko juu ya nyumba za Askari wetu mabovu yanabomoka na yanamung'unyuka kila siku? Je, Serikali mmejipanga vipi kuyaezua mabati yale ili kulinda afya za askari wetu ili wawe wazima waweze kutulinda, hasa katika wakati huu karibu na uchaguzi?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, Serikali inatoa tamko gani kwa wale wananchi binafsi ambao wanaendelea kuishi ndani ya nyumba zile ili wajihadhari wakati wa kuezua mabati yale na waweze kubadilisha mabati mengine?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi!

NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza kwamba, mabati yale Serikali ina utaratibu gani? Kama nilivyoeleza utafiti huo ambao ulifanyika utaendelea kufanyika katika maeneo mengi, ikiwemo sehemu ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja. Kikubwa ni kubaini ni muda gani mabati hayo yamekaa na yako katika hali gani katika nyumba ambazo ametoa mfano kwenye Kambi hiyo ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, pia, utafiti huo ambao ulifanyika kama nilivyoeleza ni kwamba, hali ile ya kudhurika kwa maeneo, si kila eneo lenye *asbestos* kuna madhara, yamepukutika kiasi gani kwa sababu, madhara zaidi yanatokea pale yanapopukutika.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili kama alivyouliza, wale ambao watabainika wanaishi katika maeneo hayo, likifika zoezi la kuezua watashirikishwa na sehemu kama aliyoitaja ni Kambi ya Jeshi, ni eneo maalum lazima kuwe na mawasiliano ya kiutaratibu kazi ile iweze kufanyika vizuri na kwa kutumia utaalam ambao unahusika.

SPIKA: Mmeongeza muda sana. Kwa hiyo, naomba niwatambue baadhi ya wageni walioko humu ndani ambao majina yao yamenifikia ofisini:-

Tuna Wageni wa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu na Mbunge wa Katavi, ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Kata 12 na Waheshimiwa Madiwani wanne wa Viti Maalum wakiongozwa na Mheshimiwa Wilbroad Mayala. Naomba hawa wasimame wote walipo, kama wapo. Aah! Wako kule juu! Ahsante sana; karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia yuko Ndugu Lucy Chami, Katibu Msaidizi wa CCM wilaya ya Mlele. Yuko wapi Mheshimiwa Ndugu Lucy. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna Wataalam watatu wa Halmashauri na madereva watatu. Nao hawa wasimame hapo walipo! Aah, mlikuwa katika kundi moja!

Halafu kuna Ndugu Adolph Mbata, Mwandishi wa Habari *TBC* Katavi! Naye asimame alipo! Ahsante sana; inaashiria hapa mambo hapa. *(Makofi)*

Vile vile tuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Waziri wa Maji ambao ni familia yake. Kuna ndugu Kudra Maghembe, Mke wake; naomba asimame, ahsante. Ndugu Namcheja Maghembe, mtoto wake na ndugu Rega Avevo, shemeji yake! karibuni sana; leo mzee ana kazi humu ndani. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe kutoka Wizarani kwake, ambao ni Katibu Mkuu, *Engineer* Mbogo Futakamba! Ahsante Injinia. *(Makofi)*

Tuna Mwenyekiti wa Kamati ya Washirika wa maendeleo wa Sekta ya Maji na Meneja Mwandamizi, ndugu Katrin Blandes! Naomba asimame! Ahsante. Halafu tuna Ndugu Khan Nassoro Charokiwa, Mkuu wa Chuo cha Ualimu, *Capital* – Dodoma! Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna Ndugu Rahim Suleiman Varisanga, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Cha Ualimu, *Capital* – Dodoma! Asante sana. Tuna Mheshimiwa Balozi Lusinde, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maji Dodoma! Mheshimiwa Balozi! Ahsante yupo. Tuna Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo wa Wizara na pia, kuna Wakurugenzi wasaidizi wa Rasilimali Maji. *(Makofi)*

Kuna Wakurugenzi wa Mamlaka za Maji Nchini. Wako Viongozi wa Taasisi mbalimbali chini ya Wizara ya Maji, Wenyeviti wa Bodi za Mamlaka za Maji na Maafisa wa Mabonde ya Maji Nchini. Kwa hiyo, watu wote hawa wapo, mkiwa na maneno nao basi, nadhani watawapeni nafasi. *(Makofi)*

Tuna Wageni 23 wa Mheshimiwa Amos Makalla, Naibu Waziri wa Maji, wanaotoka Jimboni kwake Mvomero, wakiongozwa na Ndugu Frank Mwananziche! Hao kwanza, wasimame hawa 23 walipo hapo! Ahsante sana, karibuni sana, lakini wakati huo huo kuna wanafunzi sita kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma – *UDOM!* Nao wasimame pia, wanafunzi! Ahsante na karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, wakiongozwa na Ndugu Patric Mbigima Mnyota! Wasimame hawa wageni wa Mheshimiwa! Aah, wako wenyewe wako sehemu ile kule! *(Makofi)*

Tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu). Hawa wageni wa Mheshimiwa Nagu wasimame na wenyewe wako upande huu. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ambao ni Mheshimiwa Alex Moshohi Kebwe! Sasa huyu ni nani? Diwani au nani? Diwani! Haya, Mheshimiwa Diwani simama ulipo! Yuko ndugu Michael Flavianus Kichele na yuko ndugu Mwinyi Ramadhani. Ahsanteni na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu ambao ni Ndugu Yahya Hamisi na Ndugu Kassim Mohamed, hawa wasimame walipo na wenyewe wako upande huu huku. *(Makofi)*

Halafu tuna Wageni wa Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Naibu Waziri wa TAMISEMI na Mheshimiwa *Engineer* Gerson Hosea Lwenge, Naibu Waziri wa Ujenzi, ambao ni Wanausharika 30 kutoka Usharika wa Omurushaka *KKKT* Dayosisi ya Karagwe, wakiongozwa na Mchungaji Restituta Teobard. Hawa na wenyewe wasimame wote walipo. Ahaa, asanteni sana Wanakwaya, nashukuru kuwaoneni. *(Makofi)*

Tunao wageni 35 kutoka Usharika wa Imani, Kanisa Kuu Mwanza KKKT Dayosisi ya Mashariki ya Ziwa Victoria wakiongozwa na Mama Askofu Elifaraja Gulle. Naomba hawa nao wasimame hapo walipo. Ahsante sana Mama Askofu tumefurahi kuwa na Mama Askofu hapo. *(Makofi)*

Tuna wageni 20 kutoka Kanisa Kuu la KKKT, Dayosisi ya Dodoma wakiongozwa na Msaidizi wa Askofu Mchungaji Samweli Mshana, naomba wasimame pale walipo. Ahsanteni na karibuni sana. Tunaomba watu wote tuombee nchi yetu inaanza kupita katika vipindi vigumu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo, hapa ni wanafunzi 35 na walimu 10 kutoka Shule ya Sekondari Kilimo Kilosa, wanafunzi hawa nao wasimame walipo. Ahsante sana someni kwa bidii. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe, Morogoro na hawa wasimame walipo. *Okay* ahsanteni. Karibuni sana tunawatakiwa masomo mema na sie tulipita huko. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 33 na Walimu wanne kutoka shule ya msingi ya *Dar-Ul-Muslimeen,* naomba wanafunzi hawa wasimame. *Okay* ndiyo hao mmependeza sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi, Tawi Maalum Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan, Morogoro. Hao nao wasimame kama wamepata nafasi. Nafikiri hawajapata nafasi.

Kuna wanakwanya 90 akina mama kutoka Usharika wa Imani Mwanza na Usharika wa Omurushaka Karagwe, si ndiyo niliowataja hawa. Nadhani ni hao hao, kama wanaweza kusimama tena kama ni wenyewe sijui. Karibuni. Kwa hiyo, kwaya zimeunganika kama nilivyosema tunaombeni, fanyeni kazi kabisa ya kumwomba Mungu, anasema wachache wakiomba basi yeye atasikia. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 40 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma na hao pia wasimame kama wamepata nafasi. Nafikiri hawa wamekosa nafasi labda baadaye wataingia.

Waheshimiwa Wabunge, matangazo yamekwisha. Katibu!

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 - Wizara ya Maji

HOTUBA YA WAZIRI WA MAJI - MHE. PROFESA JUMANNE ABDALLAH MAGHEMBE (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji, Mheshimiwa Peter M. Msolla, Mbunge wa Kilolo, ambayo ilichambua bajeti ya Wizara ya Maji, naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015 pamoja na mpango wa bajeti wa Wizara yangu kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuwa Mwenyekiti wa Jopo la Ngazi ya Juu kuhusu mwito wa Kimataifa wa Majanga ya Afya au *High Level Panel on Global Responses to Health*. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika kuiongoza Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kukupongeza wewe kwa kazi nzuri unayoifanya ya kuliongoza na kuliwakilisha vizuri Bunge letu hapa nchini na Kimataifa. Nichukue fursa hii ya pekee kukupongeza kwa kuchaguliwa kwako mwezi Novemba mwaka jana kuwa Rais wa Bunge la *SADC* kwa kipindi cha miaka miwili. Nakuombea kila la kheri na mafanikio katika kutekeleza majukumu hayo.

Mheshimiwa Spika, tumepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya msiba ya Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Eugen Mwaiposa na Mheshimiwa John Damiano Komba, Wabunge wenzetu ambao walifariki katika nyakati tofauti. Mwenyezi Mungu uziweke roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumpa pole sana Mheshimiwa Zabein Mhita Mbunge wa Kondoa Kaskazini ambaye alifiwa na mume wake. Naye Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa bajeti mwaka 2014/2015 na malengo ya mwaka 2015/2016 kwa sekta ya maji umejikita katika usimamizi na utekelezaji wa rasilimali za maji na upatikanaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira maeneo ya vijijini na mijini. Taarifa ya mapitio ya utekelezaji wa bajeti hiyo na malengo kwa mwaka ujao imechambuliwa kwa undani katika kitabu chetu cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, rasilimali za maji. Rasimali zetu za maji hapa nchini zimegawanywa katika mabonde tisa. Kila bonde linasimamiwa na Bodi iliyoteuliwa kisheria. Wizara yangu kupitia Bodi hizo ina wajibu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji kote nchini. Kazi zinazotekelezwa na Bodi hizo ni pamoja na kuandaa mipango shiriki ya kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji, kusanifu na kusimamia ujenzi wa miundombinu ya kipaumbele na aidha Bodi hizo zinaendelea kujengewa uwezo na kuimarishwa ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Maelezo ya kina kuhusu rasimali hizo hapa nchini yanapatikana kwenye ukurasa wa 15 hadi 43 wa kitabu chetu cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, usimamizi na uendelezaji wa rasimali za maji. Mwenendo wa rasilimali hizo. Wizara yangu inaendelea kuimarisha vituo vya kupimia wingi na ubora wa rasilimali za maji nchini kote. Hadi mwezi Aprili mwaka 2015, kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa vituo tisa katika mabonde ya Rufiji, Ruvuma na Pwani ya Kusini na Ziwa Victoria na ukarabati wa vituo 118 katika mabonde ya Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Mto Pangani, Mto Rufiji na Wami Ruvu. Hadi sasa kuna jumla ya vituo 633 vya kupimia mtiririko wa maji mtoni, kupima wingi wa mvua, hali ya hewa na kupima usawa wa maji kwenye maziwa na mabwawa katika mabonde mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Kuhifadhi Mazingira na Vyanzo Maji; katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu ilitekeleza mpango maalum wa kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji ambapo, vyanzo saba vya maji katika Bonde la Ziwa Rukwa vilitangazwa kuwa maeneo tengefu. Vile vile vyanzo 59 viliainishwa na kati ya hivyo 31 viliwekewa mipaka tayari kwa ajili ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali na vyanzo 24 viko katika hatua mbalimbali za upimaji.

Mheshimiwa Spika, kutafuta vyanzo vipya vya maji; katika mwaka 2014/2015, jumla ya vyanzo 114 vinavyohitaji uhifadhi vilitambuliwa kwenye mabonde ya Ziwa Rukwa, Mto Rufiji na Mito ya Wami na Ruvu na Bonde la Ziwa Tanganyika kwa ajili ya kuvihifadhi na kuvilinda. Vile vile maeneo 413 yalifanyiwa utafiti wa maji chini ya ardhi ili kubaini maeneo yanayofaa kwa ajili ya uchimbaji wa visima.

Mheshimiwa Spika, kazi za upembuzi yakinifu, uchunguzi wa kina wa miamba, usanifu na utayarishaji wa makabrasha ya zabuni ya mabwawa makubwa ya Farkwa na Ndembela zinaendelea na zitakamilika mwezi Julai mwaka huu. Katika mwaka 2015/2016, Wizara itaendelea na taratibu za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyanzo hivyo vikubwa vya maji.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa rasilimali ya maji shirikishi; nchi yetu ina jumla ya mabonde sita na kati ya hayo mabonde saba yanavuka mipaka ya nchi yetu na hivyo kuwa na ulazima wa kushirikiana na nchi nyingine 17 kwa kuunda vyombo vya pamoja vya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, Bonde la Mto Nile. Jana tu tulikuwa na kikao cha Mawaziri wa Bonde la Mto Nile hapa Mjini Dodoma. Napenda kumpongeza sana na kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutufungulia na kutuanzishia kikao chetu. Aidha, Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile *(Nile Basin Initiative)* unaundwa na jumla ya nchi 11 ambazo ni Burundi, Ethiopia, Kongo DRC, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan, Sudan Kusini, Uganda na Tanzania. Umoja huo ni chombo cha mpito kuelekea kwenye uundwaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Nile.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kusimamia matumizi ya maji yenye uwiano na haki, baina ya nchi wanachama, kusimamia utekelezaji wa miradi ya kuhifadhi ya Bonde la Mto Nile, Mazingira, Nishati, Kilimo, Mafunzo na kujenga uwezo wa taasisi zilizopo katika nchi husika. Katika kufikia lengo hilo, nchi shirika sita za Burundi, Ethiopia, Rwanda, Uganda, Kenya na Tanzania zilisaini mkataba wa msingi wa ushirikiano na hivyo kukidhi matakwa ya kuingia hatua ya kuridhia mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa kuridhia Mkataba huo katika Bunge la 19 tarehe 26 Machi, mwaka huu. Tanzania imekuwa nchi ya tatu kuridhia baada ya Ethiopia na Rwanda. Kamisheni ya Bonde la Mto Nile itaundwa pindi nchi sita zitakaporidhia mkataba huo.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Tanganyika linaendelea kukumbwa na changamoto ya kupungua kwa kina cha maji kama ilivyojidhihirisha katika Bandari ya Kigoma upande wa Tanzania na Bandari ya Kalemii, Uvila na Moba kwa upande wa Kongo DRC, hivyo kuathiri matumizi ya Bandari hizo. Miongoni mwa sababu zinazochangia changamoto hiyo ni kubomoka kwa banio la Mto Lukuga uliopo DRC unaotoa maji kutoka Ziwa Tanganyika kupeleka kwenye Mto Kongo. Marais wa Serikali zetu mbili walitoa maelekezo kwa Mawaziri wa Maji wa Tanzania na Kongo DRC kukutana ili kujadili na kupata ufumbuzi wa changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, tumefanya mikutano mitatu na katika mkutano wa mwisho Kamati ya wataalam wa nchi zetu mbili iliwasilisha rasimu ya pamoja ya hati ya makubaliano kuhusu ushirikiano wa pamoja wa usimamizi wa rasimali za maji za Bonde la Ziwa Tanganyika na ujenzi wa Banio kwenye Mto Lukuga. Hati hiyo ya makubaliano ilisainiwa tarehe 7 Mei, Jijini Kinshasa. Katika mwaka 2015/2016, Serikali ya Tanzania itaendeleza ushirikiano na Serikali ya Kongo ili kutekeleza kwa pamoja shughuli ambazo ni muhimu katika kulilinda na kulihifadhi Bonde la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, Juhudi za Kuondoa Madini ya *Fluoride* katika maji ya kunywa na matumizi ya nyumbani. Katika mwaka wa 2014/2015, Wizara yangu iliendelea kutambua vyanzo vyote vya maji kwa ajili ya kuandaa ramani inayoonesha maeneo yenye ukanda wa madini wa *fluoride*. Utambuzi huo ulifanyika katika Halmashauri za Wilaya za Arusha Mjini, Karatu, Arumeru, Longido, Monduli na Ngorongoro Mkoani Arusha na Wilaya za Simanjiro, Hanang, Babati, Mbulu na Kiteto katika Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, jumla ya vyanzo vya maji 954 vimekaguliwa na kufanyiwa uchunguzi wa uwepo wa madini ya *fluoride*. Aidha, Kituo cha Utafiti wa Kutambua na Kudhibiti Kemikali Ndani ya Maji cha Ngurudoto kimeanza utafiti katika maeneo yenye madini ya *phosphate* yanayowezesha kutengeneza *artificial hydroxylapatite* inayotumika katika uondoaji wa madini ya *fluoride* katika vyanzo vya maji. Kemikali hiyo inafanya kazi kama chengachenga za mifupa ambazo zimetafitiwa na kugundulika katika kituo hicho.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyoanza kufanyiwa utafiti wa ubora wa udongo wenye madini hayo ya *phosphate* ni Matombo Morogoro, Mlimapanda Mkoa wa Mbeya na Mijingu Mkoani Arusha. Katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kutekeleza mkakati wa kuondoa madini ya *fluoride* katika maji ya kunywa na kupikia kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia inayoondoa *fluoride* katika ngazi ya kazi na ili kutekeleza jambo mitambo 1,000 ya kuondoa madini ya *fluoride* kwenye maji itasambazwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imepokea mtambo mpya wa majaribio wa kusafisha na kutibu maji kutoka Kampuni ya Maji ya Marekani au *International Water Company* na majaribio ya awali yameonesha kuwa, mtambo huo una uwezo ya kuondoa ya *fluoride* ndani ya maji na kuondoa *bacteria* za *chlorine*. Kwa sasa majaribio ya ziada yanaendelea ili kujua uwezo wa machujio mbalimbali. Matokeo ya majaribio hayo yatawezesha Wizara kutoa mwongozo juu ya matumizi ya teknolojia hiyo na nyingine kwa Halmashauri na Mamlaka za Maji zilizo kwenye maeneo yaliyoathirika na madini ya *fluoride*.

Mheshimiwa Spika, aidha ili kuweza kuhakikisha kwamba, maji yanafahamika ubora wake vizuri, Wizara yangu imeanza kuyapandisha hadhi maabara mbalimbali mpaka kufikia kiwango cha kupewa ithibati. Katika hotuba yangu ya mwaka jana, nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba Maabara ya Maji ya mjini Mwanza ilikuwa inaelekea hatua nzuri ya kupata ithibati. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 30 Machi, mwaka huu Maabara hiyo imepewa ithibati kutoka *SADCAS* na kukabidhiwa rasmi cheti cha ithibati hiyo kinachoitambua kwa viwango cha *ISO* hapa Mjini Dodoma tarehe 15 mwezi Mei, 2015.

Mheshimiwa Spika, huduma ya Maji Vijijini. Mpango wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa. Serikali iliandaa program ya kuboresha huduma ya upatikanaji wa maji safi na salama vijijini chini ya Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ambayo ilianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2007/2008. Program hiyo iligubikwa na urasimu mkubwa katika utekelezaji wake kutokana na masharti yaliyokuwa yamewekwa kabla ya kuanza ujenzi wa mradi wowote.

Mheshimiwa Spika, masharti hayo yalikuwa ni pamoja na kupata kibali cha *no objection* cha Benki ya Dunia katika uteuzi wa Wahandisi Washauri katika kila mradi na kupata kibali cha Wizara ya Maji cha *no objection* katika kuteua Wakandarasi wa kila mradi na kupata michango ya watakaofaidika na miradi hiyo, michango inayofikia asilimia tano ya thamani ya mradi kabla ya ujenzi wa mradi wowote; kuhitajika kwa Halmashauri kutoa elimu, kuanzisha na kusajili vyombo vya watumia maji katika kila eneo la mradi kabla ya ujenzi wa mradi wowote kuanza na Halmashauri kutaka kupokea fedha zote zinazohitajika kujenga mradi kabla ya kuanza kujenga mradi wowote.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Julai, 2007 hadi mwezi Juni, 2012, ni Wilaya 12 tu kati ya 132 zilikuwa zimeweza kutimiza masharti hayo na kuanza utekelezaji wa miradi. Kutokana na kasi hiyo ndogo ya utekelezaji wa miradi ya maji vijijini, kuanzia mwezi Julai, 2013, Wizara kupitia Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa, iliondoa urasimu huo ili kuharakisha uandaaji na utekelezaji wa miradi hiyo unakwenda haraka.

(i) Zoezi hilo lilihusu kukasimu madaraka yote ya kubuni, kuandaa, kutekeleza na kusimamia miradi ya maji vijijini kwa Serikali za Halmashauri za Wilaya ili kuwa na miradi na huduma endelevu;

(ii) Kutenga bajeti katika Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa kazi za ujenzi wa miradi; na

(iii) Wizara kuendelea na majukumu yake ya kutafuta fedha, kuandaa miongozo, kutoa utaalam unaohitajika na kuzijengea uwezo Halmashauri kwa kuzipatia wataalam wa nyanja mbalimbali wakiwemo Wahandisi na Mafundi Sanifu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kutekeleza mpango wa *BRN,* idadi ya wakazi wapya wa vijijini waliokuwa wanapatiwa huduma ya maji safi ni wastani wa watu 200,000 hadi 400,000 kila mwaka. Baada ya kuondolewa kwa urasimu huo, jumla ya miradi ya maji 248 kwenye Halmashauri 98 ilijengwa katika kipindi cha mwaka mmoja. Utekelezaji wa mradi huo uliongeza idadi ya wakazi wa vijijini wanaopata huduma ya maji safi na salama kutoka wakazi milioni 15.2 mwezi Julai, 2013, hadi wakazi milioni 17.8 mwezi Juni, 2014, sawa na ongezeko la wakazi milioni 2,600,000.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maji Vijijini. Wizara yangu imeendelea kutekeleza miradi 1,814 ya maji vijijini katika Halmashauri zote nchini. Miradi hiyo inahusu ujenzi wa miradi ya Vijiji 10, miradi ya kimkakati, miradi ya upanuzi na ukarabati pamoja na miradi inayofadhiliwa na wadau mbalimbali wa sekta ya maji. Hadi mwezi Aprili, mwaka huu, jumla ya miradi ya maji 975 katika vijiji 1,206 imekamilika kwenye Halmashauri 148 na kuwanufaisha wakazi milioni 5,760,000. Idadi hiyo imeongeza watu wanaopata huduma ya majisafi vijijini kufikia 20,957,800, sawa na asilimia 55.9.

Mheshimiwa Spika, Jedwali Namba 6 katika Kitabu cha Bajeti, linaonesha orodha ya vijiji 1,206 vilivyopata huduma ya maji kutoka kwenye miradi iliyokamilika na wakazi walionufaika na miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wizara inaendelea kutekeleza miradi 839 iliyobaki katika vijiji 1,115 inayohitaji jumla ya shilingi bilioni 234.6 kuikamilisha. Miradi hiyo imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji na ikikamilika itahudumia watu 5,594,493. Katika miradi hiyo, utekelezaji wa miradi 262 kwenye vijiji 311 upo katika ya asilimia kati 71 hadi asilimia 95 na jumla ya shilingi bilioni 40.14 zinahitajika kuikamilisha miradi hiyo kwa kipindi kifupi na kuwanufaisha watu 1,732,800. Jedwali Na. (7) kwenye kitabu chetu cha hotuba linaonesha miradi hiyo 262 ambayo utekelezaji wake upo katika hatua ya kukamilisha ya asilimia 71 hadi 95.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, upatikanaji wa rasilimali fedha umekuwa changamoto kubwa. Katika mwaka 2014/2015, shilingi bilioni 270.98 zilitengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji vijijini. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu, kati ya fedha hizo, ni shilingi bilioni 76.52 sawa na asilimia 28 zilitolewa na kutumiwa kwenye Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Wizara yangu itaendelea kujenga, kupanua na kukarabati miundombinu ya maji chini ya mpango wa *Big Results Now*. Jumla ya shilingi bilioni 269.57 zimepangwa kutumika na kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 167.82 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 101.75 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kimkakati, Mradi wa Maji Tabora. Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inatekeleza awamu ya pili ya miradi ya maji katika vijiji 19 kwenye Wilaya zote saba za Mkoa wa Tabora inayogharimu shilingi bilioni 25.2. Hadi mwezi Aprili, 2015, jumla ya visima 38 vimekamilika katika Halmashauri za Wilaya za Sikonge, Kaliua, Uyui na Manispaa ya Tabora. Vile vile, kazi ya ujenzi wa matanki ya maji; ujenzi wa nyumba ya pampu na ulazaji wa mabomba katika Vijiji vya Mabama, Kakola, kwa pamoja utekelezaji umefikia wastani wa asilimia 70. Mradi wote huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni au mwezi huu na kunufaisha watu 40,352.

Mheshimiwa Spika, Huduma ya Maji Mijini; Wizara inaendelea kujenga, kupanua na kukarabati mifumo ya majisafi na uondoaji majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka zote za Maji Mijini na Miradi ya Kitaifa. Katika kutekeleza mpango wa maendeleo ya Sekta ya Maji kwenye miradi ya maji mijini kupitia mpango wa *Big Results Now*, nimesaini mikataba ya matarajio ya kazi na viashiria vya utekelezaji (*Key Performance Indicators*) na kila Mwenyekiti na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka hizo ili kupima ufanisi wa utoaji wa huduma katika maeneo yao. Taarifa kamili ya utoaji wa huduma katika miji yetu imetolewa kati ya ukurasa 63 na ukurasa 104 wa kitabu changu cha bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kuboresha Huduma za Maji Mijini. Miradi ya Maji katika Miji saba; Serikali kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo, hasa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (*AFD*), Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake (*KFW*) na Umoja wa Ulaya, imeendelea kutekeleza miradi ya kukidhi mahitaji ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji saba ya Bukoba, Musoma, Lindi, Kigoma, Sumbawanga, Mtwara na Babati.

Mheshimiwa Spika, katika Manispaa za Bukoba na Musoma, ujenzi wa miradi ya majisafi kwa Manispaa za Bukoba na Musoma, unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa. Hadi mwezi Aprili, 2015, utekelezaji wa mradi wa Bukoba unaogharimu shilingi bilioni 27.54 umefikia asilimia 85. Aidha, kwa upande wa Manispaa ya Musoma, ujenzi wa mradi unagharimu shilingi bilioni 40.62 na utekelezaji wake umefikia asilimia 80.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Lindi, Kigoma na Sumbawanga; kwa Manispaa za Lindi, Kigoma na Sumbawanga, ujenzi wa miradi ya maji na usafi wa mazingira inatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na Umoja wa Ulaya kwa gharama ya *Euro* milioni 62.6. Katika Manispaa ya Lindi, kazi za muda wa kati za ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji katika Manispaa hiyo, iliyogharimu shilingi bilioni 4.7 zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa mradi huo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 1.2 hadi kufikia lita milioni 2.4 kwa siku. Hivi sasa, Wizara inajenga miundombinu zaidi ya majisafi katika Manispaa ya Lindi kwa gharama ya *Euro* Milioni 11.9 na utekelezaji wa kazi hizo umefikia asilimia 48. Kazi zitakapokamilika upatikanaji wa maji utaongeza kutoka lita milioni 2.4 na kufikia milioni 7.1 na kukidhi mahitaji ya mji huo.

Mheshimiwa Spika, mradi wa upanuzi wa maji kwa Manispaa ya Sumbawanga umekamilika kwa gharama ya shilingi bilioni 5.3 na kuongeza upatikanaji wa maji kutoka asilimia 62 hadi asilimia 70 ya wakazi wa mji huo. Kwa sasa Wizara yangu inajenga miundombinu zaidi ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Sumbawanga kwa gharama ya *Euro* Milioni 14.9. Ujenzi wa mradi huo kwa ujumla umefikia asilimia 43 na utakapokamilika umekadiriwa kuongeza

upatikanaji wa maji kutoka lita milioni 5.4 hadi kufikia lita milioni 19 kwa siku na kukidhi mahitaji ya maji katika Manispaa hiyo.

Mheshimiwa Spika, Manispaa ya Mtwara; ujenzi wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika Miji ya Mtwara unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani chini ya Programu ya *Millennium Development Goals Initiative*. Jumla ya *Euro* milioni 8.7 zimetengwa na Serikali ya Ujerumani kupitia Benki yake ya *KFW*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi huo, Mji wa Mtwara kutokana na uchumi wa gesi unapanuka kwa haraka na viwanda zaidi ya 50 vimepangwa kujengwa na wananchi wengi watahamia katika mji huo. Kwa sababu hiyo, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa muda mrefu wa kutoa maji kutoka Mto Ruvuma kupeleka Mtwara-Mikindani na vijiji 26 vitakavyopitiwa na bomba kuu ndani ya kilomita 12. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa chanzo katika Mto Ruvuma; chujio la kutibu maji; nyumba ya mtambo wa kusukuma maji; tanki kuu la ujazo wa lita milioni 30 na matanki mengine 26.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, kazi ya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha ya zabuni umekamilika pamoja na *Environmental and Social Impact Assesment*. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, imewasilisha maombi ya Serikali kwa Serikali ya China kupitia *Exim Bank of China* kwa ajili ya kupata fedha za kutekeleza ujenzi wa mradi huo. Kukamilika kwa mradi huo kutaongeza uzalishaji wa maji katika Mji wa Mtwara Mikindani, kutoka lita milioni nane kwa siku kwa sasa na kufikia lita milioni 120 kwa siku na kutosheleza mahitaji ya Mji wa Mtwara kutoka sasa hadi mwaka 2032.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji ya Kukidhi Mahitaji ya Muda Mrefu katika Mji wa Tabora; katika mwaka 2014/2015, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la Maendeleo *(SECO)* imetekeleza mradi wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya maji katika Manispaa ya Tabora. Mradi huo uliogharimu Dola za Marekani milioni 4.84 umekamilika na kuwanufaisha watu 171,526. Aidha, Serikali inatekeleza sasa mradi wa ziada wa ukarabati na upanuzi wa chujio la maji katika kituo cha Igombe kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 4.74.

Mradi huo unalenga kuzalisha lita milioni 30 kwa siku katika Mji wa Tabora kutoka lita milioni 15 za hivi sasa. Ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 40 na utakapokamilika mwezi Agosti, mwaka huu utakuwa msaada mkubwa sana kwa watu wa Mji wa Tabora. Hata hivyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliwaahidi wananchi wa Tabora, Igunga, Nzega, Uyui, Sikonge na Urambo kuwaletea maji kutoka ziwa Victoria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2015/2016, Serikali itaanza upanuzi wa mradi huo wa maji kutoka Ziwa Victoria kuanzia katika Kijiji cha Solwa katika Mkoa wa Shinyanga, hadi Miji ya Tabora, Igunga, Nzega na vijiji vilivyomo kilomita 12 kila upande vinavyopitiwa na bomba kuu. Vile vile, mradi huo utahudumia Vijiji vya Uyui na Miji ya Sikonge na Urambo. Mradi huo utahusisha ujenzi wa matanki, ulazaji wa bomba kubwa na ukarabati wa mitandao ya usambazaji maji katika miji yote hiyo.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu umekamilika na Dola za Marekani milioni 268.35 zimepatikana kutoka Serikali ya Jamhuri ya India na Mkataba wa Makubaliano ya Kifedha unatazamiwa kusainiwa mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji Jijini Arusha. Wizara inatekeleza mradi wa Maji wa Moshono, Jijini Arusha kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji kwa wakazi 28,124 wa Kata za Moshono na Engutoto. Uchimbaji wa kisima kirefu umekamilika na kazi nyingine

zitakazotekelezwa ni pamoja na uboreshaji wa chanzo cha maji ya chemichemi ya Machare; ujenzi wa tanki; kulaza bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji kwenye mitaa yote ya Kata hizo. Pamoja na kazi hiyo, katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga shilingi bilioni 2.78 ili kuboresha hali ya upatikanaji wa maji katika Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi hiyo itakayofanywa, Jiji la Arusha lina matatizo makubwa sana ya maji na hivi sasa upatikanaji wa maji Jijini Arusha unafikia asilimia 37 peke yake. Aidha na kwa sababu hiyo, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika, imepanga kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika Jiji la Arusha kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 218.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa chanzo cha maji katika Mto Malala; uchimbaji wa visima virefu 18; ujenzi wa mtambo wa kutibu maji na ulazaji wa mabomba ya kusambaza maji na kukamilika kwa mradi huo kutaongeza upatikanaji wa maji kuanzia lita milioni 46 za sasa hadi lita milioni 86.24 kwa siku, mradi ukikamilika.

Mheshimiwa Spika, iko miradi mingi inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali hapa nchini na nitachagua miradi ambayo imekuwa inaulizwa maswali mengi sana hapa nchini, vinginevyo miradi yote imeorodheshwa katika kitabu chetu cha bajeti na nawaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kukisoma.

Mheshimiwa Spika, Miji ya Geita, mradi wa kwanza wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Mji wa Geita unatekelezwa kupitia programu ya Ziwa Victoria ya majisafi na usafi wa mazingira kwa gharama ya Shilingi bilioni 6.67 na ujenzi unatarajiwa kuanza mwezi Julai, mwaka huu. Kazi zitakazotekelezwa kwa upande wa mradi ili kuboresha huduma ya maji safi, ni pamoja na uchimbaji wa visima virefu vitatu, kufunga pampu, kulaza bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji na kujenga matenki manne ya kuhifadhi maji.

Mheshimiwa Spika, mradi wa pili wa kuupatia Mji huo wa Geita ni mradi wa kutoa maji katika Ziwa Victoria hadi mjini ambao unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Mgodi wa Dhahabu wa Geita. Mchango wa Serikali ya Tanzania ni Dola za Marekani laki nne na mchango wa Mgodi wa Dhahabu wa Geita ni Dola za Marekani milioni moja. Mradi huo unahusu ujenzi wa mtandao wa kusambaza majisafi kwa kujenga vituo 15 vya kuchotea maji katika maeneo mbalimbali ya mji huo na magati matano na ujenzi umefikia asilimia 70.

Mheshimiwa Spika, Miradi mipya katika Eneo la Ziwa Victoria; Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(European Investment Bank)* na Shirika la Maendeleo la Ufaransa inatekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Misungwi, Lamadi pamoja na mradi wa uondoaji wa majitaka katika Miji ya Bukoba na mji wa Musoma kwa gharama ya *Euro* milioni milioni mia moja na moja nukta nne. Kwa upande wa mradi wa uboreshaji wa huduma ya majisafi, Mtaalam Mshauri ameanza kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni na kazi hizo zitakamilika mwezi Aprili, 2016 na ujenzi utaanza baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa miradi ya majitaka kwa Miji ya Bukoba na Musoma, ujenzi wa mabwawa ya kusafisha majitaka katika Mji wa Bukoba umekamilika mwezi Desemba, mwaka jana na kwa Mji wa Musoma, ujenzi wa mabwawa ya kumwaga majitaka katika eneo la Bweri umefikia asilimia 70 na utakamilika mwezi Julai mwaka huu. Vile vile, magari mawili ya kuondoa majitaka katika Miji wa Musoma yamenunuliwa na yataanza kutumika katika mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Kuboresha Huduma ya Maji katika Miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi. Wizara inatekeleza miradi ya huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika Miji ya Mpanda, Njombe na Bariadi. Miji hiyo ni Makao Makuu ya Mikoa mipya ya Katavi, Njombe na Simiyu ambayo hali yake ya upatikanaji wa huduma ya maji bado ipo chini sana. Utekelezaji wa miradi ya maji katika miji hiyo ni kama ifuatavyo:-

Katika Mji wa Mpanda Serikali kwa mwaka 2014/2015, ilituma shilingi milioni 550 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji katika Mji wa Mpanda. Kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa tenki la maji, ulazaji wa mabomba, kununua dira na kufunga pampu kwenye kisima. Kukamilika kwa kazi hizo kumeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni tatu nukta nne hadi kufikia lita milioni tano kwa siku na muda wa upatikanaji wa maji umeongezeka au umeboreka kutoka saa sita mara mbili kwa wiki hadi saa sita kila siku.

Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni nne ili kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika mji huo. Aidha, tunaendelea kuongea na Serikali ya Austria ili kupata ufadhili wa Shilingi bilioni 15 katika Mwaka 2015/2016, kwa ajili ya kutengeneza miundombinu ya kudumu katika Mji wa Mpanda.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Njombe; katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu imetumia shilingi bilioni 1.38 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji katika Mji wa Njombe. Ujenzi wa mradi umefikia asilimia 81 na unategemewa kukamilika mwezi Julai, 2015. Mradi huo utakapokamilika utaongeza wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 43 ya wakazi hadi asilimia 81. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuendelea kuboresha huduma ya maji katika mji huo.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Bariadi; katika mwaka 2014/2015, Wizara yangu imekamilisha kazi za uchimbaji wa visima vitano na kuweka umeme kwenye visima vitatu; kuongeza mtandao wa mabomba na ujenzi wa matenki katika eneo la Kidinda. Katika mwaka 2015/2016, Serikali imetenga shilingi bilioni 3.5 fedha za ndani kwa ajili ya kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika mji huo.

Mheshimiwa Spika, mradi huo utakapokamilika, utaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 30 hadi kufikia asilimia 50. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW)* imepanga kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Bariadi. Mtaalam Mshauri anaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa makabrasha ya zabuni na kazi itaanza kutekelezwa Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Kutoa Maji Kutoka Ziwa Victoria Kupeleka Miji Mbalimbali. Miji ya Bariadi, Lagangabilili, Mwanhuzi, Sumve na Malya na mingine; Mtaalam Mshauri amewasilisha taarifa ya awali mwezi Machi, 2015, kwa ajili ya usanifu wa mradi wa majisafi kutoa Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Bariadi, Lagangabilili na Mwanhuzi. Ujenzi wa mradi huo utaanza katika mwaka 2015/2016 na utanufaisha wakazi wa miji hiyo pamoja na vijiji 40 vilivyopo umbali wa kilomita 12 kandokando ya bomba kuu litakalotokea Ziwa Victoria.

SPIKA: Ya kwanza.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, bado dakika tano.

SPIKA: Eee, chache sana.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kumi, kumi na tano?

SPIKA: Hapana.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, Miradi katika Jiji la Dar es Salaam; Wizara yangu inaendelea kutekeleza miradi ya kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira kwa Jiji la Dar es Salaam na Miji ya Kibaha na Bagamoyo. Hadi mwezi Aprili, 2015 miradi inayoendelea kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Bwawa la Kidunda; Mradi huu tumeuelezea mara nyingi hapa, lakini kipya Serikali kupitia *DAWASA* imeingia makubaliano ya kushirikiana katika kujenga bwawa la Kidunda na Kampuni *AVIC* ya Jamhuri ya Watu wa China tarehe tarehe 23 Juni, 2014,. Makubaliano hayo yalihusu kutafuta fedha kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera; Mkandarasi anaendelea na uchimbaji wa visima virefu 20 vya uzalishaji wa maji katika maeneo ya Kimbiji na Mpera. Aidha, mradi wa utafiti wa kuangalia mwenendo wa maji katika hifadhi hiyo ya maji unaendelea. Kati ya visima nane vilivyopangwa kuchimbwa visima saba vimekamilika na kazi yote inategemewa kukamilika mwezi huu.

Mheshimiwa Spika, Upanuzi wa Mtambo wa Ruvu Juu na Ulazaji wa Bomba Kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara; Wizara yangu inatekeleza mradi wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu na ulazaji wa bomba kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara kwa gharama ya Dola za milioni 39.7. Upanuzi wa mtambo huo umefikia asilimia 70 ya ujenzi. Mradi utakapokamilika utaongezeka uwezo wa uzalishaji maji kuanzia lita milioni 82 za sasa hadi kufikia lita milioni 196 kwa siku. Kazi ya ulazaji wa Bomba Kuu kutoka Mlandizi hadi Kimara umekamilika kwa asilimia 45 na mradi huo utagharimu Dola za kimarekani Milioni hamsini na tisa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ruvu Chini, mradi wa Upanuzi wa Mtambo wa Kuzalisha maji umekamilika na una uwezo wa kuongeza maji yanayofika Dar es Salaam kutoka lita 180,000,000 hadi 270,000,000. Ulazaji wa bomba kuu umekamilika kwa kilometa 53, sawa na asilimia 97. Tunategemea kwamba mwezi huu maji yatafika katika matenki ya Chuo Kikuu cha Ardhi. Aidha, tunaandaa mradi wa kuondoa Maji Taka katika Jiji la Dar es Salaam na mradi huo tungependa tuunganishe na miradi miwili, mradi wa kwanza ni wa kuondoa maji ya mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam na kusambaza maji katika maeneo yote ambayo hayapati maji kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, ngoja nitoe shukrani; napenda sasa kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Napenda kuzishukuru nchi rafiki zikiwemo Serikali ya Ujerumani, Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Marekani, Serikali ya Japan, Hispania, Ufaransa, China, Uswisi, Ubeligiji, Ireland, Korea Kusini, Sweden, Denmark, Norway, India, Misri, Saudi Arabia na Kuwait. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, natoa shukrani kwa taasisi za fedha za Kimataifa na zikiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya ya Ujerumani *(KfW)*, Benki ya Ufaransa (*AFD*), Benki ya Uwekezaji nchi za Ulaya *(EIB)*, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo kwa Afrika *(BADEA)*, Mfuko wa Maendeleo ya Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OFID)*, Mfuko wa Maendeleo wa Nchi ya Saudia (*SFD*), Umoja wa Ulaya, Shirika la Marekani la Changamoto za Milenia (*MCC*), Shirika la Misaada ya Maendeleo la Norway *(NORAD), DFID, GIZ, UNDP, JICA)*, *UN HABITAT*, *UNICEF, SIDA (Sweden), CIDA (Canada), DANIDA* na Misaada kutoka Shirika la la Marekani *(USAID)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kunisaidia kuiongoza Wizara ya Maji. Aidha, nimshukuru Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote, Wakuu wa Vitengo, Wataalam wetu na wakuu wa mashirika yote yaliyoko chini ya Wizara yetu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri sana ambayo wanaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nachukua fursa hii kuishukuru sana familia yangu, akiwepo mke wangu mpenzi Kudra Maghembe na watoto wetu Dkt. Ngwaru Maghembe na Dkt. Mwanamkuu Maghembe, Namcheja na Namvumo Maghembe kwa upendo na msaada wao katika kipindi chote ili kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, ninayo furaha kubwa kuendelea kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mwanga ambao wamekuwa nami bega kwa bega katika wakati wote ambao nilikuwa hapa Bungeni. Natumaini tutaendelea kushirikiana katika kipindi kijacho ili kuiletea maendeleo Wilaya yetu ya Mwanga.

Kama mnavyofahamu, changamoto zilizopo mbele yetu ni kukamilisha miradi mbalimbali na mingine mikubwa ambayo bado inaendelea kutekelezwa. Napenda kuwahakikishia kwamba, nitaongeza nguvu za ziada katika kushirikiana nanyi ili tuweze kuliletea Jimbo letu maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Spika, maombi ya Fedha kwa mwaka 2015/2016; baada ya maelezo narefu, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liidhinishe sh. 458,900,981,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara yangu katika 2015/2016. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni sh. 31,643,077,000 ambapo sh. 13,682,361,000 ni kwa ajili ya kugharamia Matumizi Mengineyo *(OC)* na sh. 17,960,716,000 sawa na asilimia 56.7 ya fedha zote za matumizi ya kawaida ni mishahara.

Mheshimiwa Spika, aidha, jumla ya bajeti ya maendeleo ni sh. 427,257,904,000 ambapo kati ya fedha hizo sh. 315,000,000,000 sawa na asilimia 74 ni fedha za ndani na sh. 112,257,904,000 sawa na asilimia 26 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Sasa nitamwita Mwenyekiti au Makamu wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii. Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Msolla!

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIFUGO, KILIMO NA MAJI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa pole za dhati kwako wewe pamoja na familia ya Mheshimiwa Eugen Mwaiposa kwa kuondokewa na mpendwa wao. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara na Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na Changamoto za Utekelezaji. Aidha, Kamati ilipokea maelezo kuhusu malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Serikali ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara hususan katika kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa ujumla Kamati imeridhika na juhudi za Wizara katika kutekeleza maoni na ushauri wa Kamati kwa kipindi hicho isipokuwa katika baadhi ya maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na ufinyu wa bajeti. Maeneo hayo ni pamoja na kutokukamilika kwa miradi mikubwa ya maji kama vile miradi ya maji ya Kimbiji na Mpera katika Wilaya ya Temeke na Mradi wa Masoko katika Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Spika, changamoto. Wizara ya Maji ilikumbana na changamoto mbalimbali wakati wa kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Kutopatikana kwa fedha za maendeleo na matumizi mengineyo *(OC)* kwa wakati. Hii ilikuwa ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(b) Upungufu wa wataalam katika sekta ya maji;

(c) Hujuma kwenye miundombinu ya maji inayochangiwa na biashara ya vyuma chakavu;

(d) Kuongezeka kwa idadi ya watu kusikoendana na kasi ya uwekezaji;

(e) Mabadiliko ya tabianchi ambayo yanasababisha kutokutabirika kwa misimu na mtawanyiko wa mvua, ukame wa muda mrefu na mafuriko ya mara kwa mara na hivyo kuathiri ujenzi wa miundombinu ya maji na upatikanaji wa rasilimali za maji; na

(f) Uharibifu wa vyanzo vya maji unaochangiwa na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo ya vyanzo hivyo.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha. Katika mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Maji inatarajia kukusanya jumla ya Sh.3,198,000,000/=. Kati ya fedha hizo, Sh.175,000,000/= ni makusanyo ya maduhuli kutoka Makao Makuu ya Wizara ikiwa ni tozo za huduma ya maabara za ubora wa maji, mauzo ya nyaraka za zabuni na kodi za nyumba za Serikali. Aidha, Sh.3,023,000,000/= ni makusanyo ya maduhuli kutoka Bodi za Mabonde ya Maji. Makusanyo hayo yatatokana na ada za kutumia maji, utafiti na upimaji maji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara hii ilipanga kukusanya jumla ya Sh.2,736,143,684/=. Mpaka kufikia tarehe 31 Machi 2015, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Sh.2,173,873,737/= sawa na 79% ya fedha iliyokasimiwa. Kutokana na kiwango cha ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka 2014/2015, Kamati inaamini kuwa Wizara itafanikiwa kukusanya mapato kama ilivyojipangia.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na Matumizi. Ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa mwaka wa fedha 2015/2016, Wizara ya Maji chini ya Fungu 49 inaomba jumla ya Sh.458,900,981,000/=. Kati ya fedha hizo, Sh.31,643,077,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.427,257,904,000/= ni za kutekeleza miradi ya maendeleo. Fedha inayoombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016, ni pungufu kwa asilimia 12.6 ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni 26% tu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge 2014/2015, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe fedha itakayoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2015/2016 inatolewa yote na kwa wakati. Hii itafanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo mingi imekwama kutokana na uhaba wa fedha.

Mheshimiwa Spika, fedha inayoombwa na Wizara inalenga kutekeleza kazi mbalimbali katika malengo makuu matatu yafuatayo:-

(a) Uendelezaji na utunzaji wa rasilimali za maji pamoja na ubora wa maji;

(b) Uboreshaji wa huduma za maji mijini na vijijini; na

(c) Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara na watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Ni ukweli ulio dhahiri kwamba maji yana umuhimu mkubwa katika kufanikisha maendeleo ya sekta za uchumi na ustawi wa jamii. Hata hivyo, upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini ni 55% tu. Kamati inatoa maoni na ushauri katika sekta hii kama ifuatavyo:-

(a) Ucheleweshwaji na kutopatikana kwa fedha. Kutopatikana kwa fedha kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kumeendelea kuikwamisha Wizara katika kufikia malengo yaliyowekwa. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara ya Maji iliidhinishiwa jumla ya Sh.488,878,252,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, katika hali ya kusikitisha, mpaka kufikia mwezi Machi 2015, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Sh.129,383,831,230/= sawa na asilimia 26 tu ya fedha zote za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa kutopatikana kwa fedha za maendeleo kwa wakati kumepelekea ongezeko la gharama za utekelezaji wa miradi zinazotokana na malimbikizo ya madeni. Aidha, kasi ya utekelezaji wa miradi pamoja na ufuatiliaji umeathirika hususan kwa miradi iliyopo kwenye Mpango wa Taifa wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa *(Big Results Now - BRN)*. Hali hii inadhihirisha Serikali kutokuwa na nia ya dhati ya kufanikisha mipango muhimu ya Wizara hii.

Kamati inaishauri Serikali kuheshimu bajeti inayopitishwa na Bunge ili kutekeleza miradi mingi ya maji kwa wakati na hivyo kupunguza tatizo la maji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara ilipokea 26% tu ya fedha za ndani za maendeleo na wadau wa maendeleo walikuwa wametoa 27% tu ya fedha

walizoahidi. Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele katika kutoa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili pamoja na mambo mengine, kupunguza utegemezi wa fedha ya nje ambayo upatikanaji wake hauna uhakika.

(b) Utaratibu wa utoaji fedha za maendeleo. Serikali imeendelea na utaratibu wa kutoa fedha za maendeleo kutoka Hazina kupitia Benki Kuu kwenda Halmashauri (*Exchequer*) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara za kukagua miradi ya maendeleo mwezi Machi, 2015, Kamati ilibaini kuwa kutokana na mfumo huu wa *exchequer,* fedha iliyotolewa na Hazina huonekana kwenye mtandao bila kuzifika halmashauri. Hali hii inasababisha madeni ya wakandarasi kutolipwa na matokeo yake ni kutokamilika kwa miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mfumo huu upo kisheria na ndiyo mfumo rasmi unaotambulika na Serikali, Kamati inaishauri Serikali iuangalie upya utaratibu huu ili kuondoa changamoto zilizopo.

(c) Mheshimiwa Spika, tatizo la wakandarasi. Kamati imebaini kuwa baadhi ya wakandarasi hawana uwezo kitaaluma. Wakandarasi hawa wamechangia kwa kiasi kikubwa kutokamilika kwa wakati kwa baadhi ya miradi au miradi mingine kutekelezwa chini ya kiwango.

Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kuchagua makandarasi wenye uwezo wa kitaaluma na uzoefu wa kutosha katika ujenzi wa miradi. Aidha, makandarasi wanaoharibu kazi wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa sheria zilizopo.

(d) Mheshimiwa Spika, usimamizi wa malipo ya ankara za maji. Katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo mwezi Machi 2015, Kamati, pamoja na mambo mengine, ilibaini kuwa Mamlaka nyingi za Maji zinazidai baadhi ya taasisi za umma ambazo hadi sasa zimelimbikiza madeni makubwa ya ankara za maji. Taasisi zinazoongoza ni pamoja na majeshi, shule na hospitali.

Mheshimiwa Spika, ili kuepukana na tatizo hili sugu la taasisi za umma kutokulipa ankara za maji, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha utaratibu mpya wa kutumia mita za maji za kulipia huduma kabla ya kutumia kwa wateja wake wote wa maji yaani hii itakuwa ni LUKU ya maji kama inavyofanywa na *TANESCO*.

(e) Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa vyanzo vya maji. Ni dhahiri kuwa mabadiliko ya tabianchi yanasababisha ukame wa muda mrefu. Aidha, kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kama vile kilimo, ufugaji, ukataji miti hovyo na uchimbaji wa madini, kumechangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yanaathiri uhakika wa rasilimali maji, Kamati inaishauri Serikali, hususan Halmashauri za Wilaya, kutunga sheria ndogo zitakazodhibiti uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji kwa kuzuia shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo oevu, maeneo ya milimani na katika chemichemi za maji. Aidha, elimu kwa umma iendelee kutolewa kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira na vyanzo vya maji na vilevile athari za mabadiliko ya tabianchi.

(f) Mheshimiwa Spika, upungufu wa wataalam. Moja ya changamoto zinazoikabili Wizara ya Maji ni upungufu wa wataalam. Kamati ilibaini hali hii ya upungufu huo pamoja na

uhaba wa vitendea kazi katika kila halmashauri iliyotembelewa wakati wa ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maji mwezi Machi 2015.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa idadi ya wataalam wanaohitajika katika sekta ya maji katika ngazi za Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni 8,749 wakati wataalam waliopo ni 1,848, sawa na 21% tu ya mahitaji kamili. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, Aprili, 2015, ukurasa wa 65.

Kamati inazishauri mamlaka zote tatu kutenga bajeti na kuendelea kuomba vibali vya kuajiri wataalam zaidi wa Idara za Maji.

(g) Mheshimiwa Spika, utozwaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye dawa za kutibu maji. Kodi ya Ongezeko la Thamani imeendelea kutozwa kwenye dawa za kutibu maji kinyume na ushauri wa Kamati uliotolewa mara nyingi huko nyuma. Kodi hii inaongeza gharama za uendeshaji wa miradi kwa mamlaka za maji na hivyo kulazimika kuongeza gharama za maji kwa watumia maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwa mara nyingine, kuona umuhimu wa kuweka dawa za kutibu maji kwenye orodha sawa na madawa ya binadamu ili kodi hizi zifutwe kwa pamoja kwani dawa za kutibu maji nazo zinalenga kuhakikisha usalama wa afya za watumiaji maji.

(h) Mheshimiwa Spika, hujuma kwenye miundombinu ya maji. Moja ya changamoto zinazoikabili Wizara hii ni pamoja na wizi wa dira za maji na kutoboa au kukata mabomba. Hali hii inachangiwa na biashara ya vyuma chakavu na uunganishaji haramu wa maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo na matumizi ya nyumbani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutunga sheria kali itakayowadhibiti wahujumu wote wa miundombinu ya maji.

(i) Mheshimiwa Spika, uvunaji wa maji ya mvua. Pamoja na Kamati kuishauri Serikali mara kadhaa kuhusu umuhimu wa kuvuna maji ya mvua, Serikali bado haijawa na mpango madhubuti wa kuhakikisha uvunaji huu unafanyika kupitia mabwawa, malambo na paa za nyumba.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa maji mengi yanapotea bure wakati wa masika kutokana na kukosekana mipango mahsusi ya uvunaji maji. Kamati inaendelea kuishauri Serikali, kusimamia na kuhakikisha kuwa halmashauri zote nchini zinatunga sheria ndogo ambazo zitahakikisha kuwa nyumba zote zinazojengwa zinawekewa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua. Aidha, mabwawa na malambo zaidi yajengwe na yaliyopo kukarabatiwa ili yatumike kwa ajili ya shughuli za uzalishaji wa umeme, umwagiliaji na uboreshaji wa huduma za maji safi kwa matumizi ya binadamu na mifugo.

(j) Mheshimiwa Spika, uwiano wa miradi ya maji. Serikali imeonesha juhudi katika kutekeleza miradi ya maji vijijini kupitia Programu ya Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*. Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2015, miradi mipya 684 ya vijiji 10 katika kila halmashauri ilikuwa imekwishakamilika na miradi mingine 241 ilikuwa imekarabatiwa na kufanyiwa upanuzi. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, April2015, ukurasa wa 65. Hii ni kwa mujibu

wa Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, Aprili, 2015, ukurasa wa 34.

Mheshimiwa Spika, juhudi hizi zinatajwa kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini kutoka 40% mwezi Juni 2013 hadi kufikia 55% mwezi Machi 2015. Hii ni kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, Aprili, 2015, ukurasa wa 34. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa hakuna uwiano katika utekelezaji wa miradi hii kwani wakati kanda nyingine zina miradi mingi, kanda nyingine zimesahaulika kabisa.

Kamati inaishauri Serikali kuweka uwiano wa utekelezaji wa miradi hii katika maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla ni kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa gharama za uendeshaji wa baadhi ya miradi ya maji ni kubwa kutokana na matumizi ya umeme na mafuta ya dizeli kuendeshea mitambo ya kusukuma maji, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia nishati mbadala kama vile umeme wa jua na upepo;

(ii) Kwa kuwa kumekuwa na mwamko mdogo wa wananchi katika kuchangia gharama za uendeshaji wa miradi ya maji, Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha uundwaji wa Kamati za Watumia Maji na kuanzisha Mifuko ya Maji ili kuwa na miradi iliyo endelevu;

(iii) Kwa kuwa baadhi ya watendaji wa Mamlaka za Maji ni wabadhirifu au wamekuwa wakicheleweshe kwa makusudi utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa maslahi binafsi, Kamati inashauri kuwa watendaji hao wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa sheria; na

(iv) Serikali itoe kipaumbele katika kukamilisha miradi mikubwa ya maji ambayo imechukua muda mrefu kabla ya kuanzisha miradi mingine. Hii itawezesha Serikali kuwa na miradi michache lakini yenye tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe (Mb) na Naibu Waziri Mheshimiwa Amos Makalla (Mb) kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Eng. Mbogo Futakamba pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Charles Mloka na Katibu wa Kamati hii Ndugu Grace Bidya akisaidiwa na Ndugu Sophia Vumbi, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa mara nyingine tena napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kilolo kwa kuendelea kunipa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu. Nawasihi wananchi wa Kilolo kuendelea kujiandikisha kwa wingi ili ifikapo wakati muafaka tukachague viongozi wa vitendo na siyo viongozi wa maneno matupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji (Fungu 49) jumla ya Sh.458,900,981,000/=

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA MAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

1.1 Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

1.2 Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara na maoni na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 pamoja na changamoto za utekelezaji. Aidha, Kamati ilipokea maelezo kuhusu malengo na maeneo ya kipaumbele pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

2.0 UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI

2.1 Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali kwa Serikali ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara hususan katika kuwapatia wananchi huduma ya maji safi na salama**.**

2.2 Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa ujumla Kamati imeridhika na juhudi za Wizara katika kutekeleza maoni na ushauri wa Kamati kwa kipindi hicho isipokuwa katika baadhi ya maeneo ambayo utekelezaji wake ulikwamishwa na ufinyu wa bajeti. Maeneo hayo ni pamoja na kutokukamilika kwa miradi mikubwa ya maji kama vile miradi ya maji ya Kimbiji/Mpera katika Wilaya ya Temeke, na Mradi wa Masoko katika Wilaya ya Rungwe.

3.0 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

3.1 Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji ilikumbana na changamoto mbalimbali wakati wa kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Changamoto hizo ni pamoja na:-

(a) Kutopatikana kwa fedha za maendeleo na matumizi mengineyo (OC) kwa wakati; hii ilikuwa changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(b) Upungufu wa wataalam katika sekta ya maji;

(c) Hujuma kwenye miundombinu ya maji inayochangiwa na biashara ya vyuma chakavu:

(d) Kuongezeka kwa idadi ya watu kusikoendana na kasi ya uwekezaji;

(e) Mabadiliko ya tabianchi ambayo yanasababisha kutokutabirika kwa misimu na mtawanyiko wa mvua, ukame wa muda mrefu na mafuriko ya mara kwa mara na hivyo kuathiri ujenzi wa miundombinu ya maji na upatikanaji wa rasilimali za maji; na

(f) Uharibifu wa vyanzo vya maji unaochangiwa na ongezeko la shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo ya vyanzo hivyo.

4.0 MAOMBI YA FEDHA NA MALENGO YA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

4.1 Makusanyo ya Maduhuli

4.1.1 Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2015/2016 Wizara ya Maji inatarajia kukusanya jumla ya shilingi **3,198,000,000/=.** Kati ya fedha hizo, shilingi **175,000,000/=** ni makusanyo ya maduhuli kutoka Makao Makuu ya Wizara ikiwa ni tozo za huduma ya maabara za ubora wa maji, mauzo ya nyaraka za zabuni na kodi za nyumba za Serikali. Aidha, shilingi **3,023,000,000/=** ni makusanyo ya maduhuli kutoka Bodi za Mabonde ya Maji. Makusanyo hayo yatatokana na ada za kutumia maji, utafiti na upimaji maji.

4.1.2 Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara hii ilipanga kukusanya jumla ya shilingi **2,736,143,684/=.** Mpaka kufikia tarehe 31 Machi 2015, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **2,173,873,737/=** sawa na asilimia **79** ya fedha iliyokasimiwa. Kutokana na kiwango cha ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka 2014/2015, Kamati inaamini kuwa Wizara itafanikiwa kukusanya mapato kama ilivyojipangia.

4.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi

4.2.1 Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, Wizara ya Maji chini ya **Fungu 49** inaomba jumla ya **shilingi 458,900,981,000/=.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 31, 643,077,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 427,257,904,000/=** ni za kutekeleza miradi ya maendeleo.

4.2.2 Mheshimiwa Spika, fedha inayoombwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016, ni pungufu kwa asilimia **12.6** ikilinganishwa na bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015**.**

4.2.3 Mheshimiwa Spika, kwa kuwa fedha iliyotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni asilimia **26** tu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge 2014/2015, Kamati inaishauri Serikali ihakikishe fedha itakayoidhinishwa na Bunge kwa mwaka 2015/2016 inatolewa yote na kwa wakati. Hii itafanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo mingi imekwama kutokana na uhaba wa fedha.

4.2.4 Mheshimiwa Spika, fedha inayoombwa na Wizara inalenga kutekeleza kazi mbalimbali katika malengo makuu matatu yafuatayo:-

(a) Uendelezaji na utunzaji wa rasilimali za maji pamoja na ubora wa maji ;

(b) Uboreshaji wa huduma za maji mijini na vijijini; na

(c) Kuzijengea uwezo taasisi zilizo chini ya Wizara na watumishi wake.

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

5.1 Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio dhahiri kwamba maji yana umuhimu mkubwa katika kufanikisha maendeleo ya sekta za uchumi na ustawi wa jamii; hata hivyo upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini ni asilimia **55** tu.

Kamati inatoa maoni na ushauri katika sekta hii kama ifuatavyo:-

a) Ucheleweshwaji/ kutopatikana kwa fedha kwa wakati kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika, kutopatikana kwa fedha kwa wakati kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kumeendelea kuikwamisha Wizara katika kufikia malengo yaliyowekwa. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2014/2015, Wizara ya Maji iliidhinishiwa jumla ya shilingi **488,878,252,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, katika hali ya kusikitisha, mpaka kufikia mwezi Machi 2015, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi **129,383,831,230/=** sawa na asilimia **26** tu ya fedha zote za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu wa kutopatikana kwa fedha za maendeleo kwa wakati kumepelekea ongezeko la gharama za utekelezaji wa miradi zinazotokana na malimbikizo ya madeni. Aidha, kasi ya utekelezaji wa miradi pamoja na ufuatiliaji umeathirika hususan kwa miradi iliyopo kwenye Mpango wa Taifa wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa (Big Results Now- BRN). Hali hii inadhihirisha Serikali kutokuwa na nia ya dhati ya kufanikisha mipango muhimu ya Wizara hii.

Kamati inaishauri Serikali kuheshimu bajeti inayopitishwa na Bunge ili kutekeleza miradi mingi ya maji kwa wakati na hivyo kupunguza tatizo la maji nchini.

Mheshimiwa Spika, Kama nilivyoeleza hapo awali, Wizara ilipokea asilimia **26** tu ya fedha za ndani za maendeleo na wadau wa maendeleo walikuwa wametoa asilimia **27** tu ya fedha waliyoahidi. Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele katika kutoa fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili, pamoja na mambo mengine, kupunguza utegemezi wa fedha ya nje ambayo upatikanaji wake hauna uhakika.

b) Utaratibu wa utoaji fedha za Maendeleo

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na utaratibu wa kutoa fedha za maendeleo kutoka Hazina kupitia Benki Kuu kwenda Halmashauri (Exchequer) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji.

Mheshimiwa Spika, wakati wa ziara za kukagua miradi ya maendeleo mwezi Machi, 2015, Kamati ilibaini kuwa kutokana na mfumo huu wa *exchequer* fedha iliyotolewa na Hazina huonekana kwenye mtandao bila kuzifika Halmashauri. Hali hii inasababisha madeni ya wakandarasi kutolipwa na matokeo yake ni kutokamilika kwa miradi kwa wakati.

Kwa kuwa mfumo huu upo kisheria na ndio mfumo rasmi unaotambulika na Serikali, Kamati inaishauri Serikali iuangalie upya utaratibu huu ili kuondoa changamoto zilizopo.

c) Tatizo la wakandarasi

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa baadhi ya wakandarasi hawana uwezo kitaaluma; hawa wamechangia kwa kiasi kikubwa kutokamilika kwa wakati kwa baadhi ya miradi au miradi mingine kutekelezwa chini ya kiwango.

Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kuchagua makandarasi wenye uwezo wa kitaaluma na uzoefu wa kutosha katika ujenzi wa miradi. Aidha, makandarasi wanaoharibu kazi wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa sheria zilizopo.

d) Usimamizi wa Malipo ya Ankara za maji

Mheshimiwa Spika, Katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo mwezi Machi 2015, Kamati, pamoja na mambo mengine, ilibaini kuwa Mamlaka nyingi za Maji zinazidai baadhi ya Taasisi za umma ambazo hadi sasa zimelimbikiza madeni makubwa ya ankara za maji. Taasisi zinazoongoza ni pamoja na majeshi, shule na hospitali.

Mheshimiwa Spika, ili kuepukana na tatizo hili sugu la Taasisi za umma kutokulipa Ankara za maji, Kamati inaishauri serikali kuanzisha utaratibu mpya wa kutumia mita za maji za kulipia huduma kabla ya kutumia kwa wateja wake wote wa maji**.**

e) Mabadiliko ya Tabianchi na Uharibifu wa vyanzo vya maji

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa mabadiliko ya tabianchi yanasababisha ukame wa muda mrefu. Aidha, kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii kama vile kilimo, ufugaji, ukataji miti hovyo na uchimbaji wa madini, kumechangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yanaathiri uhakika wa rasilimali maji, Kamati inaishauri Serikali, hususan Halmashauri za Wilaya, kutunga Sheria ndogo zitakazodhibiti uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji kwa kuzuia shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo oevu, maeneo ya milimani na katika chemichemi za maji. Aidha, elimu kwa umma iendelee kutolewa kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira na vyanzo vya maji na vilevile athari za mabadiliko ya tabianchi.

f) Upungufu wa wataalam na vitendea kazi katika Idara za Maji

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto zinazoikabili Wizara ya Maji ni upungufu wa wataalam. Kamati ilibaini hali hii ya upungufu huo pamoja na uhaba wa vitendea kazi katika kila Halmashauri iliyotembelewa wakati wa ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maji mwezi Machi 2015.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa idadi ya wataalam wanaohitajika katika sekta ya maji katika ngazi za Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri ni **8,749** wakati wataalam waliopo ni **1,848,** sawa na asilimia **21** tu ya mahitaji kamili[1]. Kamati inazishauri Mamlaka zote tatu kutenga bajeti na kuendelea kuomba vibali vya kuajiri wataalam zaidi wa Idara za Maji.

---

[1] Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, April2015, UK 65

g) Utozwaji wa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye dawa za kutibu maji

Mheshimiwa Spika, kodi ya ongezeko la thamani imeendelea kutozwa kwenye dawa za kutibu maji kinyume na ushauri wa Kamati uliotolewa mara nyingi huko nyuma. Kodi hii inaongeza gharama za uendeshaji wa miradi kwa mamlaka za maji na hivyo kulazimika kuongeza gharama za maji kwa watumia maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kwa mara nyingine, kuona umuhimu wa kuweka dawa za kutibu maji kwenye orodha sawa na madawa ya binadamu ili kodi hizi zifutwe kwa pamoja kwani dawa za kutibu maji nazo zinalenga kuhakikisha usalama wa afya za watumiaji maji.

h) Hujuma kwenye miundombinu ya Maji

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto zinazoikabili Wizara hii ni pamoja na wizi wa dira za maji na kutoboa au kukata mabomba. Hali hii inachangiwa na biashara ya vyuma chakavu na uunganishaji haramu wa maji kwa ajili ya kunyweshea mifugo na matumizi ya nyumbani.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutunga sheria kali itakayowadhibiti wahujumu wote wa miundombinu ya maji.

i) Uvunaji wa maji ya mvua

Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kuishauri Serikali mara kadhaa kuhusu umuhimu wa kuvuna maji ya mvua, Serikali bado haijawa na mpango madhubuti wa kuhakikisha uvunaji huu unafanyika kupitia mabwawa, malambo na paa za nyumba.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa maji mengi yanapotea bure wakati wa masika kutokana na kukosekana mipango mahususi ya uvunaji maji.

Kamati inaendelea kuishauri Serikali, kusimamia na kuhakikisha kuwa Halmashauri zote nchini zinatunga sheria ndogo ambazo zitahakikisha kuwa nyumba zote zinazojengwa zinawekewa miundombinu ya uvunaji wa maji ya mvua. Aidha, mabwawa na malambo zaidi yajengwe na yaliyopo kukarabatiwa ili yatumike kwa ajili ya shughuli za uzalishaji wa umeme, umwagiliaji na uboreshaji wa huduma za maji safi kwa matumizi ya binadamu na mifugo.

j) Uwiano wa miradi ya maji

Mheshimiwa Spika, Serikali imeonesha juhudi katika kutekeleza miradi ya maji vijijini kupitia programu ya Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa *(BRN)*. Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2015, miradi mipya **684** ya vijiji **10** katika kila Halmashauri ilikuwa imekwishakamilika na miradi mingine **241** ilikuwa imekarabatiwa na kufanyiwa upanuzi[2].

[2] Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, April2015, UK34

Mheshimiwa Spika, juhudi hizi zinatajwa kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi waishio vijijini kutoka asilimia **40** mwezi Juni 2013 hadi kufikia asilimia **55** mwezi Machi 2015[3] . Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa hakuna uwiano katika utekelezaji wa miradi hii kwani wakati kanda nyingine zina miradi mingi, kanda nyingine zimesahaulika kabisa.

Kamati inaishauri Serikali kuweka uwiano wa utekelezaji wa miradi hii katika maeneo yote.

MAONI YA JUMLA

1. Kwa kuwa gharama za uendeshaji wa baadhi ya miradi ya maji ni kubwa kutokana na matumizi ya umeme na mafuta ya dizeli kuendeshea mitambo ya kusukuma maji, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia nishati mbadala kama vile umeme wa jua na upepo;

2. Kwa kuwa kumekuwa na mwamko mdogo wa wananchi katika kuchangia gharama za uendeshaji wa miradi ya maji, Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha uundwaji wa Kamati za watumia maji na kuanzisha mifuko ya maji ili kuwa na miradi iliyo endelevu;

3. Kwa kuwa baadhi ya watendaji wa Mamlaka za Maji ni wabadhirifu au wamekuwa wakichelewesha kwa makusudi utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa maslahi binafsi, Kamati inashauri kuwa watendaji hao wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa sheria; na

4. Serikali itoe kipaumbele katika kukamilisha miradi mikubwa ya maji ambayo imechukua muda mrefu kabla ya kuanzisha miradi mingine. Hii itawezesha Serikali kuwa na miradi michache lakini yenye tija kwa wananchi na Taifa kwa ujumla.

6.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Said J. Nkumba, Mb - M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Prof. David Homeli Mwakyusa, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Subira Hamis Mgalu, Mb ‘’
5. Mhe. Asaa Othman Hamad, Mb ‘’
6. Mhe. Abdulsalaam S. Ameir, Mb “
7. Mhe. Abdalla Haji Ali, Mb “
8. Mhe. Namelok E. M. Sokoine, Mb “
9. Mhe. Dr. Christine G. Ishengoma, Mb “
10. Mhe. Sylvestry Francis Koka, Mb “
11. Mhe. Moshi S. Kakoso, Mb “
12. Mhe. Kheri Khatib Ameir, Mb “
13. Mhe. Meshack Jeremia Opulukwa, Mb “
14. Mhe. Philemon Kiwelu Ndesamburo, Mb “
15. Mhe. Sadifa Juma Khamis, Mb “

---

3 Taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2015/2016, April2015, UK34

16. Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa, Mb ‘’
17. Mhe. Amina Nassoro Makilagi, Mb “
18. Mhe. Donald Kelvin Max, Mb “
19. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya, Mb ‘’
20. Mhe. Haji Juma Sereweji, Mb ‘’
21. Mhe. Jitu VRAJLAL Soni, Mb ‘’
22. Mhe. Dkt Lucy Sawere Nkya, Mb ‘’

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Maji, Mhe. Prof. Jumanne Maghembe (Mb) na Naibu waziri Mhe. Amos Makalla, (Mb) kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Eng. Mbogo Futakamba pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Charles Mloka na Katibu wa Kamati hii Ndugu Grace Bidya akisaidiwa na Ndugu Sophia Vumbi kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati**.**

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji (**Fungu 49**) jumla ya **shilingi 458, 900, 981, 000 /=**.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI
KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI
03 Juni, 2015

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, Mheshimiwa Rajab, Una Wizara ngapi? Haya, ahsante. *(Kicheko)*

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA MAGDALENA H.SAKAYA (MB) WIZARA YA MAJI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 KAMA ILIVYOSOMWA BUNGENI

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (k.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI): Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kwa Wizara ya Maji kuhusu Mapitio ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 ambayo imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, natanguliza pongezi kwa uongozi wa vyama vinne vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA), kwa kuamua kuweka maslahi ya vyama vyao pembeni na kuja na lengo moja la kuwakomboa Watanzania kutokana na udhalimu na uonevu wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi chote kilichotawala Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nakishukuru chama changu cha Wananchi *CUF*, kwa kutimiza Katiba yao kwa kufanya Kikao cha Baraza Kuu na kutoa maamuzi ya kuwapata wagombea. Vilevile na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza na kumshukuru sana mke wangu mpenzi, Bi. Farida Juma Ngwali kwa namna ambavyo amenitia moyo katika kipindi hiki kigumu ambacho kilikuwa cha mchakato wa uchaguzi ndani ya chama.

Mheshimiwa Spika, sababu ya msingi ya kuwa na Sera ya Maji ya mwaka 2002, ni kuweka mfumo madhubuti na ulio endelevu wa kuendeleza na kusimamia kikamilifu rasilimali za maji hapa nchini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba upatikanaji wa maji safi na salama ni hitaji la msingi na haki ya kila mtu. Kama zilivyo rasilimali nyingine za taifa, kikatiba na kisheria, mmiliki mkuu wa rasilimali ya maji nchini kote ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwamba kila mwananchi anayo haki sawa ya kutumia rasilimali hii kwa manufaa yake na taifa.

Mheshimiwa Spika, japokuwa kuna sera hiyo, lakini takwimu zilizopo zinaonesha kuwa zaidi ya 30% ya miradi iliyojengwa vijijini haifanyi kazi vizuri kutokana na hali duni ya matengenezo na uendeshaji. Miradi ya maji iliyo endelevu ni ile inayomilikiwa na jamii kisheria. Miradi iliyojegwa bila kushirikisha walengwa katika kuibuni, kuipanga na kuisimamia, mara nyingi haipati matengenezo kama inavyostahili na hivyo kuifanya isiwe endelevu. Watumiaji wa huduma itolewayo na miradi kama hiyo, hawaioni kama ni yao na wala watumiaji hao hawamilikishwi miradi hiyo kisheria. Hali hii hufanya watumiaji waone kuwa hawahusiki na uendeshaji na matengenezo ya miradi hiyo. Ili kutatua tatizo hili, jamii zinahamasishwa na kuwezeshwa katika kubuni, kumiliki kisheria na kusimamia miradi yao ya maji ikiwa ni pamoja na visima vya maji.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya mwaka 2025 inayolenga kuinua hali ya maisha ya wananchi, maji ni moja ya nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya Dira hiyo. Taasisi isiyo ya kiserikali ya Twaweza katika utafiti wake wa mwaka 2014 inaonesha changamoto ambazo zimeonesha hali halisi ya upatikanaji wa maji safi na salama hapa nchini. Lengo la Serikali la kufikisha maji safi na salama kwa Watanzania takriban milioni 15.4 waishio vijijini ambayo ni sawa na asilimia 75% kwa mwaka 2015, utafiti wa Twaweza unaonesha kuwa lengo hilo lilikuwa ni la kisiasa mno kulingana na mazingira na hali halisi ya watendaji katika nchi yetu. Taarifa inasema kwamba, ule muda uliowekwa kwenye malengo ya milenia wa kituo cha maji safi na salama kuwa umbali ambao utamchukua mwananchi kutumia dakika 30 kwenda na kurudi, sasa muda huo umeongezeka na kuwa saa moja.

Mheshimiwa Spika, aidha, takribani moja ya tatu ya waliohojiwa walisema tatizo la maji ni moja katika matatizo makubwa yanayoikabili nchi kwa sasa. Hii maana yake ni kwamba Serikali ya CCM imeshindwa kutimiza jukumu lake la msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kulinganisha takwimu za Bara la Afrika ni kwamba, upatikanaji wa maji umekuwa ukipanda kutoka 49% miaka ya 1990 hadi 63% mwaka 2011. Hii inaakisi kiasi gani wananchi wa vijijini kwa nchi nyingi za Kiafrika upatikanaji wa maji unavyopanda lakini kwa Tanzania ukweli ni kwamba kwa miongo miwili upatikanaji umeshuka kutoka 55% hadi 53% kwa waishio mijini na kushuka kwa 46% hadi 44% kwa wananchi waishio vijijini. Hapo hapo *Big Results Now* imeweka lengo la asilimia 75% kwa mwaka 2015. Hii inahitaji miujiza mikubwa kufikia kwani itaichukua Tanzania miaka 2-3 kufanikisha kilichoshindikana kufanikishwa na mataifa mengi ya Kiafrika kwa miaka 20 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa bajeti ya maji kwa kila Mtanzania kutoka miaka ya 1999 ya shilingi 1,000 hadi sasa ya shilingi 3,000 hakushabihiani na hali halisi ya upatikanaji wa maji kwa wananchi. Kwa upande wa wahisani kwa sekta ya maji kwa kipindi cha kuanzia 1995-2005, Tanzania imepokea dola za Marekeni 57 kwa kila mnufaikaji lakini upatikanaji wa maji umeshuka kwa asilimia 1%. Kwa nchi za Ethiopia, Kenya na Uganda zote wanufaikaji wake wanapokea dola 9, dola 17 na dola 16 kwa mfuatano lakini upatikanaji wa maji kwa mataifa hayo ni mkubwa kuliko sisi ambao tunapokea kiasi kikubwa kwa kulinganisha na mataifa tajwa.

Mheshimiwa Spika, rasilimali za maji. Ni muhimu vilevile kuzichukulia rasilimali za maji kama kiungo muhimu kati ya uzalishaji na usalama wa chakula na ustawi wa mazingira na baionuai. Kutokana na kiwango cha maji kwa kila mwananchi kuzidi kupungua kadiri idadi ya watu inavyoongezeka, upo umuhimu wa kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa chakula kwa kutumia maji kidogo. Lililo muhimu zaidi ni kuwa na mizania sahihi ya matumizi ya maji, mahitaji ya maji na kiasi cha maji kilichopo. Kwa kuwa maji ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hapana budi kuandaa mikakati madhubuti ya kusimamia rasilimali hiyo ili iweze kutoa msukumo unaostahili kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kufanya tafiti zake iligundulika kwamba katika eneo la Mabama, Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora kuna rasilimali kubwa ya maji safi na salama, kiasi kwamba hazina hiyo ya maji ingeweza kuhudumia wananchi wa Wilaya hiyo ya Uyui, Urambo na Kaliua. Kwa mshangao mkubwa Serikali hiyohiyo imetoa kauli kwamba inafanya utaratibu wa kutoa maji katika Ziwa Viktoria kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa maeneo husika. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hivi kwa kulinganisha gharama za kuchimba maji hayo toka eneo husika na kusambaza maeneo ya wilaya za jirani na kwa kutoa maji Ziwa Viktoria hadi kwenye maeneo husika ni mradi upi unatoa unafuu zaidi na wa uhakika?

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa rasilimali ya maji. Hapa Tanzania, kiasi cha maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu na kinachopatikana kwa sasa ni kilomita za ujazo 89 sawa na mita za ujazo 2,700 kwa mtu kwa mwaka. Kufuatia ongezeko la watu nchini kutoka milioni 33 mwaka 2001, hadi milioni 59.8 ifikapo mwaka 2025, kiasi hiki cha upatikanaji wa maji kwa mtu kwa mwaka kitapungua kwa 45% na kufikia mita za ujazo 1,500 ikiashiria kwamba wakati huo patakuwepo na uhaba wa maji, kwani kiasi cha maji chini ya mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka ni kiwango kinachoonesha kuwa kuna uhaba wa maji.

Mheshimiwa Spika, upoteaji wa maji. Pamoja na upatikanaji finyu wa rasilimali ya maji kwa wananchi kwa umbali unaohitajika ili kukidhi malengo yaliyowekwa kitaifa, hata hivyo bado kiasi kikubwa cha maji kimekuwa kikipotea njiani kutokana na miundombinu chakavu au kutumia mabomba ambayo ubora wake ni hafifu. Suala hili limeripotiwa takribani kila kona ya nchi hii na hasa kwenye miradi ya maji ya vijiji kumi kwa kila halmashauri.

Mheshimiwa Spika, miundombinu mingi ya maji hasa maeneo ya mijini ni ya muda mrefu na hakuna mpango ulioendelevu wa kuhakikisha kuwa miundombinu hiyo inabadilishwa, ili kupambana na tatizo la upotevu wa maji. Maeneo mengi ya mijini zaidi ya asilimia 30 ya maji yanayotoka kwenye vyanzo yanapotea njiani kabla ya kufika katika maeneo husika kwa matumizi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu kwa wananchi kulipishwa fedha za ankara za maji wakati mabomba hayatoi maji na mita zinakuwa zimesimama muda mrefu. Ankara hizo zinapelekwa kwenye maeneo ambayo Mamlaka za Maji zinajua kabisa maji hayatoki katika mabomba. Aidha, maeneo mengi maji yanatoka kwa

mgawo wa wiki mara moja au mbili tu lakini ankara zinaletwa sawa na kuwa umetumia maji mwezi mzima wa siku 30.

Mheshimiwa Spika, licha ya maji kutoka kwa staili hiyo, wananchi wananunua maji kwa ndoo moja au dumu kwa shilingi kati ya 300-500/- wakati wanalipia ankara zao za maji bila ya kupatiwa maji. Kwa Mkoa wa Dar es Salaam tatizo hili limekuwa sugu kutokana na ukweli kwamba, kati ya mamlaka husika na Halmashauri za Manispaa za Kinondoni au Temeke kushindwa kuwa na mawasiliano mazuri pale wanapokwenda kuchonga barabara kwenye maeneo mbalimbali kwani miundombinu mingi ya maji inaharibiwa kwa mtindo huo na hivyo kupelekea usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Mpango huu ulibuniwa ili kuwekeza kwenye upatikanaji wa maji safi na salama na pia kurekebisha miundombinu ya maji. Programu hii iliyoanza rasmi mwaka 2007 ikiwa na ufadhili wa jumla ya dola za Kimarekani bilioni moja kutoka Benki ya Dunia, AfDB, Serikali ya Germany, Serikali ya Uholanzi na mchango wa Serikali ya Tanzania. Ni ukweli kwamba programu hii ya maendeleo ya sekta ya maji ilikuwa na fedha nyingi kwa kulinganisha na fedha ambazo zilizowahi kutolewa katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, chini ya sera ya *D by D* uwekezaji wa miundombinu ya maji vijijini unatakiwa ufanywe na Halmashauri za Wilaya na Miji chini ya usimamizi wa TAMISEMI na Serikali Kuu ilitakiwa kuangalia zaidi masuala ya kisera, miongozo, kujengea uwezo watumishi na pia kuifanyia tathmini miradi hiyo. Kwa miaka mingi suala la kujenga miundombinu ya maji limeshindikana hadi Progamu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ilipoanza mwaka 2007. Hata hivyo, miradi mingi ya maji vijijini imeendelea kuratibiwa toka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, mamlaka za maji mijini. Hizi ni mamlaka za maji mijini ambazo zinadhibitiwa na mamlaka yenye mamlaka kamili kwa mujibu wa sheria ya *EWURA*. Kwa mujibu wa taarifa inaonesha kuwa kuna mwingiliano wa majukumu kati ya *EWURA* na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwani baadhi ya majukumu kama yale ya ufuatiliaji na tathmini ambayo yanatakiwa kufanywa na Mamlaka ya Udhibiti yanafanywa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, hizi mamlaka ambazo zimeanzishwa nchi nzima bado haziwezi kusimama zenyewe licha ya kuwapo kwa fursa kubwa ya kufanya hivyo lakini bado zinategemea ruzuku toka Serikali kuu au TAMISEMI kwa ajili ya kuendesha shughuli zao. Hali hii inasababisha mamlaka hizi zisiwe na akili ya kujitanua na kuweza kujitegemea zenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ambayo imeendelea kuleta mtafaruku kati ya *DAWASA* na *DAWASCO* ambazo zote ni taasisi za Serikali na zinafanya kazi katika Mkoa wa Dar es Salaam. *DAWASA* ikiwa ni taasisi inayomiliki miundombinu ya maji na *DAWASCO* ni kampuni inayokodisha miundombinu na kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, Bodi za Wakurugenzi za taasisi hizi zinaruhusu Mwenyekiti wa Bodi ya taasisi moja kuwa mjumbe katika Bodi ya Wakurugenzi kwa taasisi nyingine. Hili linapelekea vinara hawa wanapokuwa kwenye Bodi zao kutoruhusu mawazo huru kutoka kwa Wajumbe wa Bodi husika kujadili masuala ya uendeshaji wa taasisi zao kwa mujibu wa mkataba husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona sasa ni muda mwafaka taasisi hizi mbili kuwa taasisi moja. Kwa kuwa, Serikali ya CCM imeshindwa kuliona hili kuwa linaleta mgongano wa kimaslahi ambao unapelekea utoaji wa huduma usiokidhi viwango, hivyo basi Serikali ijayo ya UKAWA ikiishapita na *inshallah* itapita ikipata ridhaa ya Watanzania tutarekebisha muundo mzima wa taasisi hizi ili wananchi wa Dar es Salaam wapate kile kinachotakiwa kupata kwa kulingana na uwekezaji unaofanyika (*value for money service*).

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maji Mbeya *(Mbeya Urban Water Supply Authority),* ni mfano mzuri wa matumizi mabaya ya fedha za umma kwani kuna mambo machafu yanaendelea kama vile wateja kulipa ankara lakini fedha zinaingia mifukoni mwa watumishi, kampuni za watendaji kupata kandarasi lakini kazi hazifanyiki na kadhalika. Serikali ya CCM inaelewa matatizo hayo lakini hakuna hatua zozote ambazo zimekwisha chukuliwa. Je na hili nalo hadi wananchi waandamane kupinga uwepo wa watendaji hao katika mamlaka hiyo?

Mheshimiwa Spika, mapitio ya bajeti ya maendeleo. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa katika utafiti wa kitaifa katika eneo la sekta ya maji inaonyesha kuwa kwa sasa wananchi wanaopata maji safi na salama ni asilimia 42 tu na siyo asilimia 57.8 kama ilivyorekodiwa katika taarifa ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, kwa kulinganisha takwimu zilizopo kwenye taarifa (*National Key Results Areas)* kuhusu utengaji wa fedha za ndani ili kuondokana na tatizo la maji, kwa mwaka 2013/2014 fedha za ndani zilizotakiwa kutolewa ni shilingi bilioni 195.1 lakini zilizotolewa ni shilingi bilioni 166 ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 29.1. Kwa mwaka 2014/2015, fedha za ndani zilizotakiwa kutolewa ni shilingi bilioni 332 lakini fedha zilizotolewa hadi mwezi Machi ni shilingi bilioni 129.4 ikiwa ni sawa na upungufu wa shilingi bilioni 202.6

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba tatizo la maji bado litaendelea kuisumbua nchi hii kwa miaka kadhaa ijayo kama Serikali ya CCM itaendelea kuwa madarakani kwani takwimu haziongopi. Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka Watanzania wote, kuwa muda muafaka umefika wa kuiondoa madarakani Serikali hii ya CCM kwani imeshindwa kutekeleza yale yote inayoyaamini kama yalivyoandikwa kwenye Sera ya Maji ya mwaka 2002 na kuifanya Serikali kuwa chini ya muungano wa vyama vinavyounda UKAWA.

Mheshimiwa Spika, mbali na changamoto za utolewaji wa fedha kutoka Hazina kwa ajili ya miradi ya maji, pia kuna tatizo kubwa la upungufu wa wataalam katika sekta ya maji ambalo linafikia 6,901, unaotokana na Serikali kutoajiri kwa muda mrefu, kuongezeka kwa idadi ya mikoa, wilaya, halmashauri pamoja na kustaafu kwa baadhi ya watumishi. Tatizo hili la kuongeza mikoa na wilaya palepale ikishindwa kutoa vibali vya kuajiri ni sababu tosha ya kuonesha kuwa Serikali hii ya CCM haiko-*coordinated* katika utoaji wa maamuzi na utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa randama ya Wizara idadi ya wataalam wanaohitajika kwenye sekta ya maji ni 8,749 wakati wataalam waliopo ni 1,848 tu. Kambi Rasmi ya Upinzani inahitaji kuelewa ni wahitimu wangapi wanaomaliza masomo yao kila mwaka kutoka Chuo cha Maji cha Rwegulila na ni wangapi wanamaliza kozi za uhandisi wa maji kutoka vyuo vikuu vingine?

SPIKA: Hakuna chuo cha namna hiyo. *(Kicheko)*

MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED (k.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAJI): Mheshimiwa Spika, Rwegarulila.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Awamu ya kwanza ya programu hii inakadiriwa kugharimu dola za Marekani milioni 434. Programu hii inatekelezwa kupitia mfuko wa pamoja (*basket funding*) na kwa kupitia wahisani wanaofadhili miradi maalum.

Mheshimiwa Spika, lengo lilikuwa ni kuwapatia wananchi wapatao milioni nane maji safi na salama kwa kujenga vituo 41,900 katika kipindi cha miaka mitano. Fedha zilizotolewa mpaka

Mei, 2013 ni dola za Marekani 340 milioni. Hadi sasa mwaka 2015 ni kiasi gani cha fedha kimetolewa?

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulihoji kwamba:-

"Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi miradi hiyo imefikia wapi, kwani hali halisi kuna mwingiliano mkubwa katika matumizi ya fedha za maji na mwisho unakuta mradi mmoja unatekelezwa na programu mbili au tatu jambo ambalo tathmini inakuwa siyo sahihi kwa mradi husika".

Mheshimiwa Spika, kile ambacho Kambi Rasmi imekuwa ikikisema mara zote kuwa kuna programu nyingi za miradi ya maji katika ngazi ya halmashauri lakini miradi hiyo imekuwa haitolewi maelezo halisi, kwani mradi mmoja unajikuta umejengwa na programu zaidi ya moja na bado mradi huo haukamiliki kwani fedha zinaingia kwenye mifuko binafsi ya watendaji.

Mheshimiwa Spika, kitabu cha Wizara kinakubaliana na hoja yetu hiyo kwenye changamoto zinazoikabili Wizara kifungu cha 2.5.3, upatikanaji wa takwimu sahihi na taarifa za utekelezaji kwa miradi. Kifungu hicho kinasema:-

"Kutokana na programu kushirikisha taasisi mbalimbali ambazo Wizara ya Maji haina mamlaka ya kiutawala moja kwa moja, limekuwepo tatizo la kupata takwimu sahihi za matumizi ya fedha ikilinganishwa na kazi zilizotekelezwa kwenye miradi ya maji katika halmashauri mbalimbali nchini."

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa nyakati tofauti tumekuwa tukiiambia Serikali kuwa taarifa zinazotolewa kuhusu utekelezaji wa malengo ya milenia kuwa zinatia shaka na huu ndiyo ushahidi wenyewe kwani Waheshimiwa Wabunge wengi mara zote wamekuwa wakilalamika kuhusiana na miradi inayojengwa kukamilishwa lakini haitoi maji wakati fedha tayari zimetumika. Hili pia ni chanzo cha kutolewa kwa takwimu ambazo si sahihi kuhusu kiwango cha kufikiwa kwa malengo ya milenia.

Mheshimiwa Spika, kuna kisima cha maji katika Kijiji cha Olboroti, Kata ya Mrijo, Wilaya ya Chemba, kilipata ufadhili wa kisima cha maji mwaka 2013. Serikali ya kijiji hicho ilisimamia mradi huo hadi ukakamilika na maji yakapatikana na wananchi wakaanza kutumia maji hayo. Mwaka 2014, kijiji hicho kiligawanywa na kuzaliwa kijiji kingine cha Kaloloni na wananchi wa kijiji mama waliendelea kutumia maji ya kisima kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni pale Mkuu wa Wilaya ya Chemba na Mbunge wa Jimbo hilo wametumia nafasi zao za uongozi kupora usimamizi wa kisima hicho kutoka Kijiji cha Olboroti na kuhamishia kijiji kipya cha Kaloloni. Jambo hili limeleta mgogoro usiokuwa na ulazima wowote kwa uongozi wa vijiji hivi viwili.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inamtaka Waziri mwenye dhamana na maji alitolee kauli suala hili. Je, kwa viongozi wa wananchi wanaosababisha migogoro kweli wanastahili kupewa heshima ya kuongoza jamii? Je, hiyo si aina nyingine ya ufisadi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Miradi ya *Quick Wins*. Lengo la miradi hiyo kwa wananchi lilikuwa ni zuri sana lakini kutokana na udhahifu wa kiutendaji, miradi hiyo imekuwa ni kichaka cha kujificha kwa wabadhirifu wa fedha za maji. Ukweli umebainishwa hasa kwa utendaji usioridhisha wa chombo cha Serikali cha kuifanyia tathmini miradi hiyo kabla ya kuingia kwa awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa vijiji kumi.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kutekeleza miradi ya aina moja kwa halmashauri zilezile na watendaji wale wale ni tatizo kubwa. Hata hivyo, kwa kuwa wahusika wakubwa ngazi za juu nao ni sehemu ya ufisadi huo, inakuwa vigumu sana kubadilisha mfumo na kuthibiti wizi huo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni muda muafaka kwa wananchi kuibadilisha Serikali hii ambayo imeshindwa kuthibiti ufisadi huo na Serikali mpya ya UKAWA kuwaonesha kwa vitendo ni jinsi gani fedha za kodi zao zinavyoweza kuwaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi ya wWizara kwa mwaka 2015/2016, katika kiambatanisho namba 3 kinachohusu utekelezaji wa miradi ya vijiji 10 kwa kila halmashauri, hadi tarehe 31 Machi, 2015, kwa kifupi ni kama ifuatavyo:-

(i) Wilaya ya Kaliua kati vijiji 10 vilivyopatiwa miradi hii ni visima vitatu tu vilipatikana na maji ambavyo ni Ushokela, Uhindini na Kazaroho. Kisima cha Uhindini kilipatikana na maji ya kutosha kusambaza vitongoji vyote vinne vya kijiji hicho na mkataba wa ukandarasi ulieleza kwamba maji yatasambazwa vitongoji vyote.

Cha ajabu maji yamepelekwa vitongoji viwili tu. Mkandarasi ameweka pampu ndogo ambayo haina nguvu ya kusukuma maji kujaza tenki. Wananchi wameendelea kutaabika kwa kukosa maji wakati maji tayari yapo pale. Kutokana na udogo wa *pump* inachukua zaidi ya masaa 36 – 48 kujaza tenki na gharama za mafuta ni kubwa na wananchi wanashindwa kumudu. Siku ya wiki ya maji na mwenge ulipofika pale iliwekwa *pump* kubwa maji yakamwagika siku mbili, mwenge ulipoondoka *pump* nayo hiyo ikaondolewa.

Mradi wa maji Kijiji cha Ushokela nao pia umekuwa kiini macho. Fedha iliyotolewa kwa ajili ya mradi huo ni shilingi milioni 210 na nguvu za wananchi waliochangia shilingi milioni saba. Maji yamepatikana ya kutosha cha ajabu hayasambazwi kwa wananchi na hakuna kiongozi yeyote anayeeleza mabomba yaliyokuwa yameletwa yamepelekwa wapi na mpango wa kujenga tenki la kuhifadhia maji umeishia wapi? Serikali ieleze wananchi lini watasambaziwa maji hayo ili waondokane na adha ya maji? Aidha, Serikali ieleze ni kwa nini mkandarasi ameshindwa kuweka *pump* kubwa yenye uwezo wa kusukuma maji kwa muda mfupi wananchi wapatiwe maji?

(ii) Mradi wa Maji wa Jibondo, Kijiji cha Jibondo, Wilaya ya Mafia wenye wanufaikaji 2,580 hadi sasa utekelezaji wake ni 0%;

(iii) Miradi ya maji Kaliua kati ya miradi ya visima 12 ni visima vitatu (3) tu ndivyo vinavyotoa maji;

(iv) Mradi wa Fukayosi, kijiji cha Fukayosi, Wilaya ya Bagamoyo wenye wanufaikaji 5,000 hadi sasa utekelezaji ni 0%;

(v) Mradi wa Mjembe, kijiji cha Mjembe, Wilaya ya Bagamoyo wenye wanufaikaji 5,000, hadi sasa utekelezaji wake ni 0%;

(vi) Mradi wa Nalingu, Mtendachi na Mnete uliopo Halmashauri ya Mtwara, wenye wanufaikaji 4,781 hadi sasa utekelezaji wake ni 0%;

(vii) Miradi ya Wilaya ya Newala karibia yote haijakamilika yenye wanufaikaji takriban 53,950;

(viii) Miradi katika vijiji vya Wilaya ya Mbulu vya Masieda ambao unaonesha kuwa utekelezaji wake ni 100% lakini ukweli ni kuwa hakuna maji, mabomba yaliyotumiwa ni feki yanapasuka ovyo. Mradi wa Dongobesh umejengwa chini ya viwango, mradi wa Mongahay - mkandarasi amekwishahama *site*. Mradi wa *Harsha Gravity* nao hauna fedha. Hii ni aibu kwani karibu awamu ya kwanza ya mradi inamalizika; na

(ix) Mradi wa maji wa Nyumbigwa, Wilayani Kasulu, Jimbo la Kasulu Mjini. Kimsingi mradi huo hauna magati 17 zenye *double tapes* kama inavyoelezwa katika taarifa ya Wizara ya maji bali mradi huo una magati 23 yenye *double tapes.* Hata hivyo, taarifa kutoka Serikali ya Kijiji cha Nyumbigwa ni kwamba mradi huo ulipaswa kuwa na magati 60 lakini Idara ya Maji, Wilayani Kasulu inatajwa kupunguza idadi ya magati kwa kushirikiana na mkandarasi mjenzi pamoja na mtaalamu mshauri. Hii ya kupunguza magati 37 maana yake ni kuwanyima wanufaikaji wengi huduma za maji kwa umbali unaotakiwa na hivyo kutokupunguza adha ya kusafiri kutafuta maji. Pia ni kuficha au kutokutumia fedha ambazo zilikuwa zimetengwa na kutolewa kwa ajili ya mradi wenye magati 60. Je, wahusika mambo hayo hawayaelewi?

Mheshimiwa Spika, mradi huo uligharimu zaidi ya shilingi milioni 890 za Kitanzania. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepata kutembelea mradi huo na kubaini kasoro zifuatazo. Mojawapo, ni tenki kuu la kuhifadhia maji kuwa na nyufa sehemu za juu ambapo likijazwa maji huvuja ili hali mradi haujakabidhiwa kwa wananchi. Je, miradi ya aina hii iko mingapi kwa nchi nzima? Mradi huu muda wake wa matumizi *(life span)* ni miaka mingapi baada ya kukabidhiwa kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, miradi mingi ya vijiji kumi inaendeshwa kwa mashine za *pump* zinazotumia mafuta ya dizeli. Jambo hili limepelekea uendeshaji wa miradi hii kuwa ghali sana na hivyo wananchi wanabebeshwa mzigo wa kununua mafuta hayo. Hata fedha zinazokusanywa kutokana na uuzaji wa maji ni kidogo mno kukidhi gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, kwa kuwa suala la kuweka nishati ya umeme ambao hautumii mafuta kwa ajili ya kuendeshea miradi hiyo ya maji imeshindikana, basi wananchi wote watuunge mkono ili Serikali ijayo iongozwe na Vyama vya Upinzani chini ya umoja wa UKAWA. Kwa njia hiyo tu miradi ya maji itakuwa endelevu na maji ambayo ni haki ya msingi ya kila mwananchi itapatikana kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ni sampuli tu ya utekelezaji wa miradi ya maji ya vijiji kumi kwa kila halmashauri na miradi ambayo inaonekana imetekelezwa kwa asilimia zaidi ya 80 kwa mujibu wa kiambatanisho husika, ukweli ni kwamba bado wananchi maeneo mengi hawapati maji.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ambayo miradi imefanyika na wananchi wanapata maji, unakuta miradi hiyo imesimamiwa na taasisi zingine mbali na halmashauri au halmashauri zimejivika mradi wakati mradi huo umefadhiliwa na watu wengine lakini kwenye vitabu inaonesha kuwa ni mradi wa vijiji kumi. Mambo haya yapo maeneo mengi na Serikali ya CCM inayaelewa vyema.

Mheshimiwa Spika, sote tutambue kuwa tupo chini ya dari moja yaani sekta ya maji, kwa hiyo, ushirikiano wa dhati unatakiwa kuwepo kutoka ngazi ya Taifa (Wizara ya Maji na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI), ngazi ya Mkoa (Sekretarieti za Mkoa, Mamlaka za Maji, Ofisi za Mabonde), ngazi ya Halmashauri zote zinazohusika na maji ikiwa ni pamoja na Ujenzi na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilikwishatoa ushauri kwa Serikali kwamba ili miradi hiyo iwe na tija kwa wananchi, usimamizi wa TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Maji wafuatilie utekelezaji wa miradi ya maji inayotekelezwa kwenye halmashauri. Hata hivyo, ushauri huo waliuona hauna maana na kinachotokea ni hali halisi kwamba asilimia kubwa ya awamu ya kwanza ya mradi wa vijiji kumi kwa kila halmashauri maji hayatoki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii. Vilevile niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kupokea na kusikiliza hotuba yetu hii ya Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA MAGDALENA H.SAKAYA (MB) WIZARA YA MAJI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Inatolewa chini ya Kanuni 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2013)

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Natanguliza pongezi kwa uongozi wa vyama vine vinavyounda umoja waKatiba ya wananchi UKAWA kwa kuamua kuweka maslahi ya vyama vyao pembeni na kuja na lengo moja la kuwakomboa watanzania kutokana na udhalimu na uonevu wa Serikali ya chama cha mapinduzi kwa kipindi chote kilipotawala Serikali ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Nakishukuru chama changu cha wananchi-CUF, viongozi wakuu wa chama pamoja na wanachama wote kwa heshima kubwa waliyonipa ya kuwa NAIBU KATIBU MKUU-CUF BARA. Nimeweka historia katika nchi yetu na kwa vyama vyote vya siasa kuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi hii tangu tupate uhuru. Nawaahidi wanachama,wapenzi wote na watanzania kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa uaminifu na uadirifu mkubwa ili tufikie malengo ya ukombozi. Aidha, naishukuru familia yangu hasa mume wangu na watoto kwa kunivumilia kipindi chote ninapokuwa kwenye majukumu ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, Sababu ya msingi ya kuwa na Sera ya maji ya mwaka 2002 ni kuweka mfumo madhubuti na ulio endelevu wa kuendeleza na kusimamia kikamilifu rasilimali za maji hapa nchini. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, upatikanaji wa maji safi na salama ni hitaji la msingi na haki ya kila mtu,kama zilivyo rasilimali nyingine za taifa, kikatiba na kisheria, mmiliki mkuu wa rasilimali ya maji nchini kote ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwamba kila mwananchi anayo haki sawa ya kutumia rasilimali hii kwa manufaa yake na Taifa.

Mheshimiwa Spika, Japokuwa kuna sera hiyo, lakini kwa takwimu zilizopo zinaonesha kuwa zaidi ya 30% ya miradi iliyojengwa vijijini haifanyi kazi vizuri kutokana na hali duni ya matengenezo na uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya maji iliyo endelevu ni ile inayomilikiwa na jamii kisheria. Miradi iliyojegwa bila kushirikisha walengwa katika kuibuni, kuipanga na kuisimamia, mara nyingi haipati matengenezo kama inavyostahili, na hivyo kuifanya isiwe endelevu. Watumiaji wa huduma itolewayo na miradi kama hiyo, hawaioni kama ni yao na wala watumiaji hao hawamilikishwi miradi hiyo kisheria. Hali hii hufanya watumiaji waone kuwa hawahusiki na uendeshaji na matengenezo ya miradi hiyo. Ili kutatua tatizo hili, jamii zitahamasishwa na

kuwezeshwa katika kubuni, kumiliki kisheria na kusimamia miradi yao ya maji, ikiwa ni pamoja na visima vya maji.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Mwaka 2025 inalenga kuinua hali ya maisha ya wananchi maji ni moja ya nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya Dira hiyo.

Mheshimiwa Spika, Miradi mingi ya maji inakwama kutokana na ukweli kwamba inakuwa sio shirikishi, na pale wananchi wanapotaka kuhoji wahusika wanahamishwa na kupelekwa maeneo mengine na pengine wananchi wanatishiwa na vyombo vya dola. Hii ndio sababu kubwa mradi mkubwa wa Benki ya Dunia wa maji kwa kila halmashauri kuwa na vijiji 10 vitakavyochimbiwa visima umekwama wakati fedha tayari zimetumika na vijiji havina maji.

Mheshimiwa Spika, Taasisi isiyoya kiserikali Twaweza katika utafiti wake wa mwaka 2014 inaonesha changamoto ambazo zimeonesha hali halisi ya upatikanaji wa maji safi na salama hapa nchini. Lengo la Serikali la kufikisha maji safi na salama kwa watanzania takriban milioni 15.4 waishio vijijini ambayo ni sawa na asilimia 75% kwa mwaka 2015. Utafiti wa Twaweza unaonesha kuwa lengo hilo lilikuwa ni la kisiasa mno kulingana na mazingira na hali halisi ya watendaji katika nchi yetu. Taarifa inasema kwamba ule muda uliowekwa kwenye malengo ya milenia wa kituo cha maji safi na salama kuwa umbali ambao utamchukua mwananchi kutumia dakika 30 kwenda na kurudi, lakini sasa muda huo umeongezeka na kuwa saa moja.

Mheshimiwa Spika, Aidha, tariban moja ya tatu ya waliohojiwa walisema tatizo la maji ni moja katika matatizo makubwa yanayoikabili nchi kwa sasa. Hii maana yake ni kwamba Serikali ya CCM imeshindwa kutimiza jukumu lake la msingi.

Mheshimiwa Spika, Kwa kulinganisha takwimu za bara la AFRIKA ni kwamba upatikanaji wa maji umekuwa ukipanda kutoka 49% miaka ya 1990 hadi 63% mwaka 2011. Hii ina akisi kiasi gani wananchi wa vijijini kwa nchi nyingi za ki-Afrika unavyopanda. Lakini kwa Tanzania ukweli ni kwamba kwa miongo miwili kumekuwepo upatikanaji umeshuka kutoka 55% hadi 53% kwa waishio mijini na kushuka kwa 46% hadi 44% kwa wananchi waishio vijijini.

Mheshimiwa Spika, Hapo hapo Big Results Now imeweka lengo la asilimia 75% kwa mwaka 2015. Hii inahitaji miujiza mikubwa kufikia kwani itaichukua Tanzania miaka 2-3 kufanikisha kilichoshindikana kufanikishwa na mataifa mengi ya ki-Afrika kwa miaka 20 iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Kuongezeka kwa bajeti ya maji kwa kila mtanzania kutoka miaka ya 1999 ya shilingi 1,000 hadi sasa ya shilingi 3,000 hakushabihiani na hali halisi ya upatikanaji wa maji kwa wananchi. Kwa upande wa Wahisani kwa sekta ya maji kwa kipindi cha kuanzia 1995-2005, Tanzania imepokea dolla za Marekeni 57 kwa kila mnufaikaji lakini upatikanaji wa maji umeshuka kwa asilimia 1%. Lakini kwa nchi za Ethiopia, Kenya na Uganda zote wanafaikaji wake wanapokea dolla 9, dolla 17, na dolla 16 kwa mfuatano lakini upatikanaji wa maji kwa mataifa hayo ni mkubwa kuliko sisi ambao tunapokea kiasi kikubwa kwa kulinganisha na mataifa tajwa.

2. RASILIMALI ZA MAJI

Mheshimiwa Spika, Ni muhimu vilevile kuzichukulia rasilimali za maji kama kiungo muhimu kati ya uzalishaji na usalama wa chakula na ustawi wa mazingira na baionuai. Kutokana na kiwango cha maji kwa kila mwananchi kuzidi kupungua kadiri idadi ya watu inavyoongezeka, upo umuhimu wa kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa chakula kwa kutumia maji kidogo. Lililo muhimu zaidi ni kuwa na mizania sahihi ya matumizi ya maji, mahitaji ya maji na kiasi cha maji kilichopo. Kwa kuwa maji ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hapana budi kuandaa mikakati madhubuti ya kusimamia rasilimali hiyo ili iweze kutoa msukumo unaostahili kama ilivyoainishwa kwenye Dira ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kufanya tafiti zake iligundulika kwamba katika eneo la MABAMA wilaya ya UYUI mkoa wa Tabora kuna rasilimali kubwa ya maji safi na salama, kiasi kwamba hazina hiyo ya maji ingeweza kuhudumia wananchi wa wilaya hiyo ya Uyui, Urambo na Kaliua. Lakini kwa mshangao mkubwa Serikali hiyo hiyo imetoa kauli kwamba inafanya utaratibu wa kutoa maji katika ziwa Viktoria kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hivi kwa kulinganisha gharama za kuchimba maji hayo toka eneo husika na kusambaza kwa maeneo ya wilaya za jirani na kwa kutoa maji ziwa Viktoria hadi kwenye maeneo husika ni mradi upi unatoa unafuu zaidi na wa uhakika?

3. UPATIKANAJI WA RASLIMALI YA MAJI

Mheshimiwa Spika, Hapa Tanzania, kiasi cha maji yanayofaa kwa matumizi ya binadamu na kinachopatikana kwa sasa ni kilomita za ujazo 89 sawa na mita za ujazo 2,700 kwa mtu kwa mwaka. Kufuatia ongezeko la watu nchini kutoka milioni 33 mwaka 2001, hadi milioni 59.8 ifikapo mwaka 2025, kiasi hiki cha upatikanaji wa maji kwa mtu kwa mwaka kitapungua kwa 45% na kufikia mita za ujazo 1,500 ikiashiria kwamba wakati huo patakuwepo na uhaba wa maji, kwani kiasi cha maji chini ya mita za ujazo 1,700 kwa mtu kwa mwaka ni kiwango kinachoonesha kuwa kuna uhaba wa maji.

4. UPOTEVU WA MAJI

Mheshimiwa Spika, Pamoja na upatikanaji finyu wa rasilimali ya maji kwa wananchi kwa umbali unaohitajika ili kukidhi malengo yaliyowekwa kitaifa, hata hivyo bado kiasi kikubwa cha maji kimekuwa kikipotea njiani kutokana na miundombinu chakavu au kutumia mabomba ambayo ubora wake ni hafifu. Suala hili limeripotiwa takribani kila kona ya nchi hii, na hasa kwenye miradi ya maji ya vijiji kumi kwa kila halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Miundombinu mingi ya maji hasa maeneo ya mijini ni ya muda mrefu na hakuna mpango ulioendelevu ya kuhakikisha kuwa miundombinu hiyo inabadilishwa, ili kupambana na tatizo la upotevu wa maji. Maeneo mengi ya mijini zaidi ya asilimia 30 ya maji yanayotoka kwenye vyanzo yanapotea njiani kabla ya kufika katika maeneo husika kwa matumizi.

Mheshimiwa Spika, Kumekuwepo na malalamiko ya muda mrefu kwa wananchi kulipishwa fedha za Ankara za maji wakati mabomba hayatoi maji na meter zinakuwa zimesimama muda mrefu. Ankara hizo hizo zinapelekwa kwenye maeneo ambayo mamlaka za maji zinajua kabisa maji hayatoki katika mabomba. Aidha, maeneo mengi maji yanatoka kwa mgawo wa wiki mara moja au mbili tu lakini Ankara zinaletwa sawa na kuwa umetumia maji mwezi mzima wa siku 30.

Mheshimiwa Spika, Licha ya maji kutoka kwa staili hiyo, wananunua maji kwa ndoo moja au dumu kwa shilingi kati ya 300-500/- wakati wanalipia Ankara zao za maji bila ya kupatiwa maji.

Mheshimiwa Spika, Kwa mkoa wa Dar es Salaam tatizo hili limekuwa sugu kutokana na ukweli kwamba, kati ya mamlaka husika na Halmashauri za Manispaa za Kinondoni au Temeke kushindwa kuwa na mawasiliano mazuri pale wanapokwenda kuchonga barabara kwenye maeneo mbalimbal. Kwani miundombinu mingi ya maji inaharibiwa kwa mtindo huo na hivyo kupelekea usumbufu mkubwa sana.

5. MAJI NA MAENDELEO YA TAIFA KIUCHUMI NA KIJAMII

Mheshimiwa Spika, Maji ni rasilimali muhimu kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Binadamu anahitaji maji ya kunywa ili aishi, na pia kwa ajili ya matumizi yake mengine ya nyumbani. Aidha, maji yanahitajika katika shughuli mbalimbali za kiuchumi kama vile uzalishaji viwandani, umwagiliaji mashamba, ufugaji, usafishaji wa madini, uzalishaji wa umeme, usafiri na uchukuzi, burudani na utalii.

6. PROGRAMU YA MAENDELEO YA SEKTA YA MAJI (WSDP)

Mheshimiwa Spika, Mpango huu ulibuniwa ili kuwekeza kwenye upatikanaji wa maji safi na salama na pia kurekebisha miundombinu ya maji, program hii iliyoanza rasmi mwaka 2007 ikiwa na ufadhili wa jumla ya dolla za Kimarekani bilioni 1 kutoka Bank ya Dunia, AfDB, Serikali ya Germany, Serikali ya Uholanzi na mchango wa Serikali ya Tanzania. Ni ukweli kwamba program hii ya maendeleo ya sekta ya maji ilikuwa na fedha nyingi kwa kulinganisha na fedha ambazo zilizowahi kutolewa katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, Chini ya sera ya D by D uwekezaji wa miundombinu ya maji vijijini unatakiwa ufanywe na Halmashauri za wilaya na miji chini ya usimamizi wa TAMISEMI, na serikali kuu ilitakiwa kuangalia zaidi masuala ya kisera, miongozo, kujengea uwezo watumishi na pia kuifanyia tathmini miradi hiyo. Lakini hilo kwa miaka mingi suala la kujenga miundombinu ya maji limeshindikana hadi Progamu ya maendeleo ya sekta ya maji ilipoanza mwaka 2007. Hata hivyo miradi mingi ya maji vijijini imeendelea kuratibiwa toka Serikali kuu.

Mheshimiwa Spika, Kuratibiwa kwa miradi hii toka Serikali kuu kunawafanya wanufaikaji kuondolewa dhana nzima ya umiliki wa miradi ambayo wao ni wanufaikaji. Aidha, jambo hili limepelekea kwa kiwango Fulani ubadhirifu unaofanywa na watendaji na mwisho wanaishia kuhamishwa vituo vya kazi.

7. MAMLAKA ZA MAJI MIJINI-(urban water supply authorities -UWSAs)

Mheshimiwa Spika, Hizi ni mamlaka za maji mijini ambazo zinadhibitiwa na mamlaka yenye mamlaka kamili kwa mujibu wa sheria ya EWURA. Lakini kwa mujibu wa taarifa[1] inaonesha kuwa kuna muingiliano wa majukumu kati ya EWURA na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwani baadhi ya majukumu kama yale ya ufuatiliaji na tathmini ambayo yanatakiwa kufanywa na Mamlaka ya Udhibiti yanafanywa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Hizi mamlaka ambazo zimeanzishwa nchi nzima **(UWSAs)** bado haziwezi kusimama zenyewe licha ya kuwapo kwa fursa kubwa ya kufanya hivyo, lakini bado zinategemea ruzuku toka Serikali kuu au TAMISEMI kwa ajili ya kuendesha shughuli zao. Hii inasababisha mamlaka hizi zisiwe na akilia ya kujitanua na kuweza kujitegemea zenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kuna hoja ambayo imeendelea kuleta mtafaruku kati ya DAWASA na DAWASCO hizi zote ni taasisi za Serikali na zinafanyakazi katika mkoa wa Dar es Salaam. DAWASA ikiwa ni taasisi inayomiliki miundombinu ya maji na DAWASCO ni kampuni inayokodisha miundombinu na kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, Bodi za wakurugenzi za taasisi hizi zinaruhusu Mwenyekiti wa bodi ya taasisi moja kuwa mjumbe katika bodi ya wakurugenzi kwa taasisi nyingine. Hili linapelekea vinara hawa wanapokuwa kwenye bodi zao kutoruhusu mawazo huru kutoka kwa wajumbe wa bodi husika kujadili masuala ya uendeshaji wa taasisi zao kwa mujibu wa mkataba husika.

---

[1]The African Ministers' Council on Water (AMCOW)-Water supply and sanitation in Tanzania, turning finance into services for 2015 and beyond.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona sasa ni muda mwafaka taasisi hizi mbili kuwa ni taasisi moja. Kwa kuwa Serikali ya CCM imeshindwa kuliona hili kuwa linaleta mgongano wa kimaslahi ambao unapelekea utoaji wa huduma usiokidhi viwango, hivyo basi Serikali ijayo ya UKAWA ikishapata ridhaa ya watanzania tutarekebisha muundo mzima wa taasisi hizi ili huduma ya kiwango kwa wananchi wa Dar es Salaam wapate kile kinachotakiwa kupata kwa kulingana na uwekezaji unaofanyika-**Value for money service**.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Maji Mbeya **(Mbeya Urban water supply authority-MBEUWSA)** ni mfano mzuri wa matumizi mabaya ya fedha za umma, kwani kuna mambo machafu yanaendelea kama vile wateja kulipa ankara lakini fedha zinaingia mifukoni mwa watumishi, kampuni za watendaji kupata kandarasi lakini kazi hazifanyiki n.k. na Serikali ya CCM inaelewa matatizo hayo lakini hakuna hatua zozote ambazo zimekwisha chukuliwa. Je, na hili nalo hadi wananchi waandamane kupinga uwepo wa watendaji hao katika mamlaka hiyo?

8. MAPITIO YA BAJETI YA MAENDELEO KWA WIZARA YA MAJI 2014/15

Mheshimiwa Spika,Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa katika utafiti wa Kitaifa katika eneo la sekta ya maji (National Key Results Area) inaonyesha kuwa kwa sasa wananchi wanaopata maji safi na salama ni asilimia 40 tu na sio asilimia 57.8 kama ilivyorekodiwa katika taarifa ya MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, Naomba kurejea tena taarifa ya matokea ya maji kwa maeneo mbalimbali nchini(National key Results Area) inayoonesha kwamba ili kuondokana na matatizo ya maji yanayowakabili watanzania. Tunahitaji kutenga fedha za kutosha kama ifuatavyo:

i. 2013/14 bilioni 437.3 kati ya hizo shilingi bilioni 195.1 ni fedha za ndani.

ii. 2014/15 bilioni 563.2 kati hizo bilioni 332.0 ziwe fedha za ndani.

iii. 2015/16 bilioni 451.9 kati hizo bilioni 206 ziwe fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika,Hali halisi ya bajeti ya fedha za maendeleo kwa miaka hiyo mitatu kama ambavyo ilipitishwa na Bunge na kiasi kilichotolewa na Hazina ni kama ifuatavyo**:**

Mheshimiwa Spika, Kwa kulinganisha takwimu zilizopo kwenye taarifa National Key Results Areas kuhusu utengaji wa fedha za ndani ili kuondokana na tatizo la maji.

Kwa mwaka 2013/14 fedha za ndani zilizotakiwa kutolewa ni shilingi bilioni 195.1 lakini zilitolewa ni shilingi bilioni 166. Ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 29.1

Kwa mwaka 2014/15 fedha za ndani zilizotakiwa kutolewa ni shilingi bilioni 332. Lakini fedha zilizotolewa hadi mwezi March ni shilingi bilioni 129.4 Ikiwa sawa na upungufu wa shilingi bilioni 202.6

Mheshimiwa Spika, Nidhahiri kwamba tatizo la maji bado litaendelea kuisumbua nchi hii kwa miaka kadhaa ijayo kama Serikali ya CCM itaendelea kuwa madarakani, kwani takwimu haziongopi?

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inawataka Watanzania wote, kuwa muda mwafaka umefika wa kuiondoa madarakani Serikali hii ya CCM kwani imeshindwa kutekeleza yale yote inayo yaamini kama yalivyoandikwa kwenye sera ya maji ya mwaka 2002. Na kuifanya Serikali kuwa chini ya muungano wa vyama vinavyounda UKAWA.

Mheshimiwa Spika, Mbali na changamoto za utolewaji wa fedha toka Hazina kwa ajili ya miradi ya maji, pia kuna tatizo kubwa la upungufu wa wataalam katika sekta ya maji ambalo linafikia 6,901, unaotokana na Serikali kutoajiri kwa muda mrefu, kuongezeka kwa idadi ya mikoa, wilaya, Halmashauri pamoja na kustaafu kwa baadhi ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Tatizo hili la kuongeza mikoa na wilaya pale pale ikishindwa kutoa vibali vya kuajiri ni sababu tosha ya kuonesha kuwa Serikali hii ya CCM haiko-cordinated katika utoaji wa maamuzi na utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa randama ya Wizara idadi ya wataalam wanaohitajika kwenye sekta ya maji ni 8,749 wakati wataalam waliopo ni 1,848 tu. Kambi Rasmi ya Upinzani inahitaji kuelewa ni wahitimu wangapi wanaomaliza masomo yao kila mwaka kutoka chuo cha Maji cha Rwegalulila na ni wangapi wanamaliza kozi za uhandisi wa maji kutoka vyuo vikuu vingine?

9. PROGRAMU YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

Mheshimiwa Spika,Awamu ya kwanza ya Programu hii inakadiriwa kugharimu Dola za Marekani 434 millioni. Programu hii inatekelezwa kupitia mfuko wa pamoja (*basket funding*) na kwa kupitia Wahisani wanaofadhili miradi maalum *(earmarked funding*)

Mheshimiwa Spika, Lengo lilikuwa ni kuwapatia wananchi wapatao **milioni 8** maji safi na salama kwa kujenga **vituo 41,900** katika kipindi cha miaka mitano. Fedha zilizotolewa mpaka Mei, 2013 ni Dola za Marekani 340 millioni. Hadi sasa mwaka 2015 ni kiasi gani cha fedha kimetolewa?

Mheshimiwa Spika, Mwaka jana tulihoji yafuatayo;

"*Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iwaeleze wananchi miradi hiyo imefikia wapi, kwani hali halisi kuna muingiliano mkubwa katika matumizi ya fedha za maji na mwisho unakuta mradi mmoja unatekelezwa na program mbili au tatu jambo ambalo tathmini inakuwa siyo sahihi kwa mradi husika*".

Mheshimiwa Spika, Kile ambacho Kambi Rasmi imekuwa ikikisema mar azote kuwa kuna Programu nyingi za miradi ya maji katika ngazi ya Halmashauri lakini miradi hiyo imekuwa haitolewi maelezo halisi, kwani mradi mmoja unajikuta umejengwa na programu zaidi ya moja na bado mradi huo haukamiliki kwani fedha zinaingia kwenye mifuko binafsi ya watendaji.

Mheshimiwa Spika, Kitabu cha Wizara kinakubaliana na hoja yetu hiyo kwenye changamoto zinazoikabili wizara ***kifungu cha 2.5.3 –Upatikanaji wa takwimu sahihi na taarifa za utekelezaji kwa wakati***. Kifungu hicho kinasema,

"*kutokana na program kushirikisha taasisi mbalimbali ambazo wizara ya maji haina mamlaka ya kiutawala moja kwamoja, limekuwepo tatizo la kupata takwimu sahihi za matumizi ya fedha ikilinganishwa na kazi zilizotekelezwa kwenye miradi ya maji katika halmashauri mbalimbali nchini.*"

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa nyakati tofauti tumekuwa tukiiambia Serikali kuwa taarifa zinazotolewa kuhusu utekelezaji wa malengo ya milenia kuwa zinatia shaka, na huu ndio ushahidi wenyewe. Kwani kwa waheshimiwa wabunge wengi mara zote wamekuwa wakilalamika kuhusiana na miradi inayojengwa kukamilishwa lakini haitoi maji wakati fedha tayari zimetumika. Hili pia ni chanzo cha kutolewa kwa takwimu ambazo si sahihi kuhusu kiwango cha kufikiwa kwa malengo ya milenia.

Mheshimiwa Spika, Kuna kisima cha maji katika KIJIJI CHA OLBOROTI kata ya MRIJO wilaya ya CHEMBA, kijiji hiki kilibata ufadhiri wa kisima cha maji mwaka 2013. Serikali ya kijiji hicho ilisimamia mradi huo hadi ukakamilika na maji yakapatikana na wananchi wakaanza kutumia maji hayo. Mwaka 2014, kijiji hicho kiligawanywa na kuzaliwa kijiji kingine cha KALOLONI na wananchi wa kijiji mama waliendelea kutumia maji ya kisima kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Jambo la kusikitisha ni pale Mkuu wa Wilaya ya Chemba na Mbunge wa Jimbo hilo Mhe Juma Nkamia wametumia nafasi zao za uongozi kupora usismamizi wa Kisima hicho kutoka Kijiji cha OLBOROTI na kuhamishia kijiji kipya cha KALOLONI. Jambo hili limeleta mgogoro usiokuwa na ulazima wowote kwa uongozi wa vijiji hivi viwili.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri mwenye dhamana na maji alitolee kauli suala hili, na kwa viongozi wa wananchi wanaosababisha migogoro kweli wanastahili kupewa heshima ya kuongoza jamii, je huo sio aina nyingine ya ufisadi?

10. MIRADI YA QUICK WINS NA MIRADI YA VIJIJI KUMI KWA KILA HALMASHAURI

Mheshimiwa Spika, Miradi ya maji Vijiji kumi kwa kila Wilaya inayofadhiliwa na Bank ya Duni tangu 2007 imeendelea kuwa kitendawili hapa nchini.

Bajeti ya mwaka jana 2014/2015 serikali ilitenga fedha na Bunge kupitisha kwa ajili ya kukamilisha miradi hii ambayo ni kero kubwa kwa wananchi. Hata hivyo hakuna kilichofanyika kusogeze mbele miradi ambayo kwa kiasi kikubwa mingi imefeli na kukwama. Zaidi ya asilimia 75% ya miradi ya World bank ambayo ilileta matumaini makubwa kwa wananchi imefeli na kukwama. Hii ni aibu kubwa sana kwa serikali hii.

Mheshimiwa Spika, Lengo la miradi hiyo kwa wananchi lilikuwa ni zuri sana, lakini kutokana na udhahifu wa kiutendaji miradi hiyo imekuwa ni kichaka cha kujificha kwa wabadhirifu wa fedha za maji. Ukweli umebainishwa hasa kwa utendaji usioridhisha wa chombo cha Serikali cha kuifanyia tathmini miradi hiyo kabla ya kuingia kwa awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi wa vijiji kumi.

Mheshimiwa Spika, Kitendo cha kutekeleza miradi ya aina moja kwa halmashauri zile zile na watendaji wale wale ni tatizo kubwa. Lakini kwa kuwa wahusika wakubwa ngazi za juu nao ni sehemu ya ufisadi huo inakuwa vigumu sana kubadilisha mfumo na kuthibiti wizi huo.

Mheshimiwa Spika, Sasa ni muda mwafaka kwa wananchi kuibadilisha Serikali hii ya CCM ambayo imeshindwa kuthibiti ufisadi huo na Serikali mpya ya UKAWA kuwaonesha kwa vitendo ni jinsi gani fedha za kodi zao zinavyoweza kuwaletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ukiangalia taarifa ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka 2015/16 katika kiambatanisho namba 3 kinachohusu utekelezaji wa miradi ya vijiji 10 kwa kila Halmashauri hadi tarehe 31 Machi,2015, kwa kifupi ni kwamba, mfano:

1. Wilaya ya Kaliua kati Vijiji 10 vilivyopatiwa miradi hii ni visima vitatu tu vilipatikana na maji ambao ni Ushokela, uhindini na Kazaroho. Kisima cha uhindini kilipatikana na maji ya kutosha kusambaza vitongoji vyote vinne vya kijiji hicho, na mkataba wa ukandarasi ulieleza kwamba maji yatasambazwa vitongoji vyote.

Cha ajabu maji yamepelekwa vitongoji viwili tu. Mkandarasi ameweka pampu ndogo ambayo haina nguvu ya kusukuma na maji kujaza tank. Wananchi wameendelea kutaabika

kukosa maji wakati maji tayari yapo pale. Kutokana na udogo wa pamp inachukua zaidi ya masaa 36 – 48 kujaza tank na gharama za mafuta ni kubwa wananchi wanashindwa kumudu. Siku ya wiki ya maji na mwenge ulipofika pale iliwekwa pump kubwa maji yakamwagika siku mbili mwenge ulipoondoka pump hiyo ikaondolewa.

Mradi wa maji Kijiji cha Ushokela nao pia umekuwa kiini macho. Fedha iliyotolewa kwa ajili ya mradi huo ni milioni 210 na nguvu za wananchi waliochangia Milioni 7.

Maji yamepatikana ya kutosha cha ajabu hayasambazwi kwa wananchi – na hakuna kiongozi yeyote anayeeleza mabomba yaliyokuwa yameletwa yamepelekwa wapi na mpango wa kujenga tank la kuhifadhia maji umeishia wapi?

Serikali ieleze wananchi lini watasambaziwa maji hayoili waondokane na adha ya maji? Aidha, Serikali ieleze ni kwanini mkandarasi ameshindwa kuweka pump kubwa yenye uwezo wa kusukuma maji kwa muda mfupi wananchi wapatiwe maji?

2. Mradi wa Maji wa Jibondo, Kijiji cha Jibondo Wilaya ya Mafia wenye wanufaikaji 2580 hadi sasa utekelezaji wake ni 0%

3. Miradi ya maji Kaliua kati ya miradi ya visima 12 ni visima vitatu (3) tu ndivyo vinavyotoa maji.

4. Mradi wa Fukayosi, kijiji cha Fukayosi wilaya ya Bagamoyo wenye wanufaikaji 5000 hadi sasa utekelezaji ni 0%

5. Mradi wa Mjembe, kijiji cha Mjembe wilaya ya Bagamoyo wenye wanufaikaji 5000, hadi sasa utekelezaji wake ni 0%

6. Mradi wa Nalingu, Mtendachi na Mnete uliopo Halmashauri ya Mtwara, wenye wanufaikaji 4781 hadi sasa utekelezaji wake ni 0%

7. Miradi ya Wilaya ya Newala karibia yote haijakamilika yenye wanufaikaji takriban 53,950

8. Miradi katika vijiji vya Wilaya ya Mbulu vya Masieda ambao unaonesha kuwa utekelezaji wake ni 100% lakini ukweli ni kuwa hakuna maji, mabomba yaliyotumiwa ni feki yanapasuka ovyo. Mradi wa Dongobesh umejengwa chini ya viwango, mradi wa Mongahay-mkandarasi amekwisha hama site. Mradi wa Harsha Gravity nao hauna fedha. Hii ni aibu kwani karibu awamu ya kwanza ya mradi inamalizika.

9. Mradi wa maji wa Nyumbigwa wilayani kasulu jimbo la kasulu mjini.

Kimsingi mradi huo hauna magati 17 zenye double tapes kama inavyoelezwa katika taarifa ya wizara ya maji bali mradi huo una magati 23 yenye double tapes. Hata hivyo taarifa kutoka serikali ya kijiji cha Nyumbigwa ni kwamba mradi huo ulipaswa kuwa na magati 60 lakini idara ya maji wilayani Kasulu inatajwa kupunguza idadi ya magati kwa kushirikiana na mkandarasi mjenzi pamoja na mtaalamu mshauri. Hii ya kupunguza magati 37 maana yake ni kuwanyima wanfaikaji wengi huduma za maji kwa umbali unaotakiwa na hivyo kutokupunguza adha ya kusafiri kutafuta maji. Pia ni kuficha au kutokutumia fedha ambazo zilikuwa zimetengwa na kutolewa kwa ajili ya mradi wenye magati 60. Je, wahusika mambo hayo hawayaelewi?

Mheshimiwa Spika, Mradi huo uliogharimu zaidi ya shilingi milioni 890 za kitanzania, Hata hivyo kambi rasmi ya upinzani bungeni imepata kutembelea mradi huo na kubaini kasoro zifuatazo; mojawapo ni Tank kuu la kuhifadhia maji kuwa na nyufa sehemu za juu ambapo likijazwa maji huvuja ilihali mradi haujakabidhiwa kwa wananchi. Je, miradi ya aina hii iko mingapi kwa nchi nzima? Na mradi huu muda wake wa matumizi(life span) ni miaka mingapi baada ya kukabidhiwa kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, Miradi mingi ya vijiji kumi inaendeshwa kwa mashine za pump zinazotumia mafuata ya dizeli. Jambo hili limepelekea miradi hii kuwa ghali sana uendeshaji wake, na hivyo wananchi wanabebeshwa mzigo wa kununua mafuta hayo. Hata fedha zinazokusanywa kutokana na uuzaji wa maji ni kidogo mno kukidhi gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, kwa kuwa suala la kuweka nishati ya umeme ambao hautumii mafuta kwa ajili ya kuendeshea miradi hiyo ya maji imeshindwa, basi wananchi wote watuunge mkono ili Serikali ijayo iongozwe na vyama vya upinzani chini ya umoja wa UKAWA, kwa njia hiyo tu miradi ya maji itakuwa endelevu na maji ambayo ni haki ya msingi ya kila mwananchi itapatikana kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, Hiyo ni sampuli tu ya utekelezaji wa miradi ya maji ya vijiji 10 kwa kila halmashauri. Na miradi ambayo inaonekana imetekelezwa kwa asilimia zaidi ya 80 kwa mujibu wa kiambatanisho husika, ukweli ni kwamba bado wananchi maeneo mengi hawapati maji.

Mheshimiwa Spika, Kwa maeneo ambayo miradi imefanyika na wananchi wanapata maji, unakuta miradi hiyo imesimamiwa na taasisi zingine mbali na halimashauri au halimashauri zimejivika mradi wakati mradi huo umefadhiliwa na watu wengine lakini kwenye vitabu inaonesha kuwa ni mradi wa vijiji 10. Mambo haya yapo maeneo mengi na Serikali ya CCM inayaelewa vyema.

Mheshimiwa Spika, Sote tutambue kuwa tupo chini ya dari moja yaani Sekta ya Maji, Kwa hiyo ushirikiano wa dhati unatakiwa kuwepo kutoka Ngazi ya Taifa (Wizara ya Maji na OWM –TAMISEMI) ngazi ya Mkoa (Sekretarieti za Mkoa, Mamlaka za Maji, Ofisi za Mabonde) Ngazi ya Halmashauri zote zinazohusika na maji ikiwa ni pamoja na Ujenzi na Sekta binafsi).

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani ilikwishatoa ushauri kwa Serikali kwamba, ili miradi hiyo iwe na tija kwa wananchi, usimamizi wa TAMISEMI ikishirikiana na Wizara ya Maji wafuatilie utekelezaji wa miradi ya maji inayotekelezwa kwenye Halmashauri. Lakini ushauri huo waliona hauna maana na kinachotokea ni hali halisi kwamba asilimia kubwa ya awamu ya kwanza ya mradi wa vijiji 10 kwa kila halimashauri maji hayatoki.

Mheshimiwa Spika, Baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

Mohamed Rajab Mbarouk (Mb)
K.n.y Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani –Wizara ya Maji na Umwagiliaji.
05.06.2015

SPIKA: Ahsante sana. Sasa tunaanza na uchangiaji na ataanza Profesa David Mwakyusa, atafuatia Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Ali Keissy, Mheshimiwa Godfrey Mgimwa nafikiri na Mheshimiwa Mansoor anaweza kufikiwa.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni zetu, Kanuni ya 64(a) kinachoeleza kwamba wakati wa majadiliano Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli wowote.

Mheshimiwa Spika, mzungumzaji aliyezungumza sasa, ameelezea jinsi miradi ya vijiji kumi ilivyoshindwa kila mahali na ametoa taarifa ya Wilaya ya Newala. Kwa maneno yake anasema hivi:-

"*Miradi ya Wilaya ya Newala karibu yote haijakamilika yenye wanufaika takribani 53,950*".

Mheshimiwa Spika, mimi ndiye Mbunge wa Newala, nataka kulieleza Bunge hili Tukufu kwamba mnataka kutuma ujumbe uende leo, kijiji kimoja tumechimba kisima, mwaka jana sherehe za juma la maji kimkoa zimefanyika katika kijiji hicho baada ya kuwa maji yamechimbwa. Sasa leo anapokuja mtu kuniambia hapa kwamba Newala vijiji vyote yaani kwamba Mheshimiwa mwenzangu huyu anayekaa Pemba anaijua Newala kuliko mimi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, mradi wa maji Malatu katika vile vijiji kumi tumesukuma maji kutoka Malatu Chini yamefika Malatu Juu, imefanyika sherehe ya kuzindua mradi ule wa maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nimesimama hapa kuzungumzia miradi ya Wilaya yangu ya Newala, siyo kweli kwamba miradi yote ya Newala haijatekelezwa. Kwa hiyo, naomba kutoa taarifa hiyo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MBUNGE FULANI: Anachangia.

SPIKA: Mimi ndiye ambaye nasikiliza, ni haki yake kujibu.

MHE. HALIMA J. MDEE: Sasa kama anadanganya na yeye si ndiyo natoa taarifa juu kwa juu, naona anachangia halafu anapotosha.

SPIKA: Waheshimiwa, siyo suala la kuchangia, *he has got a right to answer*. Kwa hiyo, nakuomba ukae chini Mheshimiwa Halima, malizia Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, kama anatoa taarifa potofu *then* inabidi na sisi tumpe taarifa.

SPIKA: Ana haki ya kujibu ni Mbunge wa sehemu hiyo.

MHE. HALIMA J. MDEE: Kama anapotosha na sisi tuna haki ya ku-*respond*.

SPIKA: Halima bwana muache amalize, kwa nini mnakuwa na fujo? Mheshimiwa endelea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, nataka kurudia tena kusema, mimi ni mtu mzima, anayebisha twende Newala leo tukaone kama mradi umekwisha au haujaisha? Haiwezekani mtu anasimama hapa anasema uwongo kuhusu Jimbo ambalo najua kinachoendelea halafu nikae kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, amekubali au hakuikubali taarifa hiyo, nataka kusema kwamba Mbunge amesema uwongo kwamba Wilaya ya Newala vijiji vyote hakuna maji yalikotoka, twende leo akaone.

SPIKA: Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa…

WABUNGE FULANI: Ni nafasi yetu kujibu.

SPIKA: Waheshimiwa, nimeshakaa hapa sitaki ubishi Mheshimiwa Profesa Mwakyusa...

(Hapa baadhi ya Wabunge wa Upinzani walikuwa wakiongea kuonyesha kutokubaliana na uamuzi wa Spika)

SPIKA: Newala haiko hapa na ninyi wenyewe hamko Newala, tuko humu ndani…

(Hapa baadhi ya Wabunge wa Upinzani walikuwa wakiongea kuonyesha kutokubaliana na uamuzi wa Spika)

SPIKA: Mheshimiwa Profesa endelea.

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Waziri kwa hotuba yake nzuri lakini pia kumshukuru kwamba maji yanapopatikana wanapewa watu wote bila ya kufuata itikadi yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mjumbe wa Kamati iliyochambua hotuba hii. Kwa hiyo, nakubaliana na yote yaliyoandikwa kwenye hotuba yetu na nachojaribu kufanya sasa hivi ni kuweka mkazo katika maeneo kadhaa.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua, maji ni huduma ya jamii ambayo ni muhimu na ndiyo maana ni lengo la Serikali kwamba 100% ya wananchi wote wapatiwe maji ambayo ni safi na salama. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inasema kwamba mwezi Juni, 2013, ni 40% ya wananchi waishio vijijini ambao walipata huduma ya maji safi na sasa hivi ni 55% na maoteo ni kwamba baada ya bajeti hii mwaka kesho tutafikia 74%.

Mheshimiwa Spika, takwimu ni muhimu kwa sababu inatueleza tulikuwa wapi, tuko wapi na tunakoelekea. Hata hivyo, takwimu zisipotumika vizuri zinaweza kutumika kupotosha. Kwa mfano, miradi hii haimlengi mtu mmoja mmoja tunaipeleka kwenye vijiji. Kwa hiyo, kinachokosekana hapa ni kwamba kwa sababu tunajua ni vijiji vingapi tulivyo navyo Tanzania ingekuwa ni bora tujue ni vijiji vipi na vingapi ambavyo vimepatiwa maji na hii itatusaidia kwa sababu kutoa wastani wa 55% ya wananchi inaleta hisia kwamba ukienda kwenye kijiji fulani

utakuta watu 55% wanapata maji wakati siyo sahihi, kumekuwa na mgawanyiko tofauti kabisa kati ya wilaya na kanda.

Sisi katika Kamati yetu mwezi wa tatu tulikwenda kwenye mikoa 17 kukagua miradi ya maji. Tulishangaa kuona kwamba kuna wilaya zingine ambapo vijiji vyote vimepatiwa maji isipokuwa vinne. Sasa ukileta wastani kwa vijiji vingine kama kijiji nachotoka hatuna maji, watu wanashangaa wanaona sisi pengine hatufanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, nachopendekeza ni kwamba ndiyo tungependa kujua ni watu wangapi wamepatiwa maji lakini vilevile tungependa kupata mtawanyiko, hawa waliopata maji wako wapi. Kwa hiyo, kungekuwa na ramani kubwa tujue ni kina nani wamepata maji na labda ingewasaidia wenzetu wanapopanga wangeona labda eneo fulani kusema ukweli hawajapa huduma hii mipango ya baadaye waelekeze huko. Kwa sababu kumekuwa na kauli nyingi kwamba miradi siyo ya maji tu, miradi mingi inapelekwa sehemu fulani au kanda fulani wengine wanasahauliwa.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kwamba kila bajeti tunaelezwa kwamba miradi mipya itakuwa maeneo haya na haya. Wabunge ambao watapata hiyo miradi wanafurahi, wananchi wanafurahi na wote tunafurahi tunapiga makofi. Hata hivyo, tunasahau kwamba kuna miradi ambayo imeanza siku nyingi ambayo haijakamilika na hii mipya inapewa pesa wakati mwingine inazinduliwa kabla ya ile ya zamani. Mheshimiwa Waziri ameitaja hapa kuna mradi wa Kidunda, Kimbiji, Mpera na Masoko. Mheshimiwa Waziri na Naibu walipojua kwamba nitachangia wanajua nitautaja mradi wa Masoko.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ya kuibua miradi mingi, tunakuwa na utitiri wa miradi, pesa tunazopata kila mwaka ni kidogo, mwaka huu tumepata 26% ya pesa tulizoidhinisha hapa, ni lazima tuweke kipaumbele katika miradi ambayo tuliibua mapema ili ikamilike. Nataka kuishauri Wizara kwamba wasisifike kwa kuibua miradi, wasifike kwa kukamilisha miradi. Ifike mahali kwamba huko mbele ya safari au bajeti ijayo Waziri asione aibu kusema kwamba kutokana na pesa zinavyokuwa ndogo mwaka huu hatutakuwa na miradi mipya, tunataka kukamilisha iliyopo ili tusiwe na viporo vya miradi ya zamani.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuzungumza kidogo kuhusu miradi ya visima, hili limezungumzwa na mwenzangu wa Kambi ya Upinzani. Tunajua kwamba mchakato wa kupata maji ya visima ni tofauti na maji ya mserereko ambapo tunatafuta mkandarasi wa kufanya *prospecting* halafu kunakuwa na mkandarasi wa kuja kuchimba visima. Kumekuwa na malalamiko mengi kwamba hawa *prospecting* wanapita wanaweka mambo zao kwamba hapa ndiyo kuna maji wanapewa pesa zao wanaondoka lakini anayekuja kuchimba mara nyingi hapati maji na Wizara inatuambia kwamba dunia nzima ni 70% ya mafanikio. Mimi nasema kwamba tunapojenga barabara kutoka hapa mpaka sehemu fulani hatusemi wewe jenga barabara ya lami madaraja umuachie mtu mwingine sisi tunataka barabara ili ikikamilika tuanze kuitumia.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Kamati tumeishauri Wizara mara nyingi kwamba huyo anayechimba visima ndiyo awe huyohuyo anayefanya *prospecting*. Sisi tumwambie kwamba kijiji hiki kina matatizo ya maji tunataka maji. Kwa hiyo, tutamlipa kwa kutafuta lakini pia kwa kuchimba na tuwakabidhi wananchi. Matatizo inakuwa kwamba tumepoteza hela nyingi sana kwa watu wanatafuta na kutuambia hapa kuna maji tunakwenda mita 200 hakuna maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hii miradi ya visima katika kupitapita hasa Wilaya ya Singida Vijijini, tuliona baada ya kisima kupatikana maji tunatafuta pampu ambayo inavuta maji na

kuyapeleka kwenye tenki halafu ndiyo yanasambaa kwenda vijijini, sasa kuna gharama za uendeshaji, ni gharama kubwa. Katika kijiji kimojawapo wanatumia lita kumi na moja za dizeli kwa siku na inachukua saa kumi na sita kujaza tenki la lita za ujazo 70,000 na yakifunguliwa wanatumia kwa saa mbili. Sasa hiyo gharama ya karibu shilingi elfu ishirini kwa siku kwa vijiji vya hapa Tanzania navyovifahamu ni gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niungane na jinsi nilivyoshauri kwamba lazima tutafute nishati mbadala. Kama tutakuwa na umeme wa gridi ni vizuri lakini tufikirie pia umeme jua na umeme wa upepo hasa ukizingatia kwamba mahali kama Singida panasifika kwa upepo mwingi, kwa sababu mafuta hawawezi kuhimili na kuendelea kulipa shilingi elfu ishirini na nne kila siku.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ni suala la uvunaji wa maji. Tulizungumza kwenye Kamati, tumeshauri Serikali na tukaishia kushauri kwamba kuwe na namna ya kuweka *by laws* kwenye halmashauri zetu lakini hili halijafanikiwa. Mimi nadhani lingeanzia kwenye Wizara kuwe na kama sheria, sehemu zote zinapata maji hapa Tanzania, ukanda wa hapa katikati wana matatizo kidogo lakini mvua inapokuja maji yanakuwa mengi tunaona tu yanaondoka yanakwenda baharini ambapo tungeweza kutengeneza mabwawa na majosho, sisi kama Kamati tunashughulika na kilimo na mifugo, maji haya yangeweza kutosha sekta hizi zote tatu.

Mheshimiwa Spika, siku kumi zilizopita kama Kamati tulikuwa Seychelles wao ni visiwa vyenye majabali kila mahali, hatukuona mto hata mmoja, tukawauliza wanapata wapi maji? Wao wanatumia maji ya kuvuna na kwenye kisiwa kikubwa cha Mahe wana matenki mawili makubwa na maji ya ziada ndiyo wanafanya *desalination*. Sasa sisi tunatumia maji, wakati wa mvua maji yanaharibu barabara lakini maji tunayaacha yanaondoka halafu baada ya muda mfupi tunalalamika hakuna maji. Nadhani hili tungeliwekea nia hasa na kuwe na mpango madhubuti. Mungu anatupa maji siyo kwamba yaondoke tu, ni lazima tuyafanyie kazi kwa kuyahifadhi kwenye malambo. Mbona wamissionari …

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya atafuatiwa na Mheshimiwa Azza Hillal.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, unapozungumzia matatizo makubwa yanayowakabili Watanzania na ukayatatua, utarahisisha maisha yao mbali na umaskini unaoukabili, elimu, afya, maji safi na salama. Unapozungumzia leo tatizo la maji katika nchi yetu, waathirika wakubwa ni akina mama ambao wanatembea umbali mrefu kwa ajili ya kwenda kutafuta maji bila mafanikio.

Mheshimiwa Spika, nianze na mradi wa maji wa muda mrefu takribani miaka tisa katika mji wa Bunda. Huu mradi ni wa muda mrefu, wananchi wa Bunda wanapata tabu sana na adha kubwa ya maji, hawajawahi kupata maji safi na salama na Mheshimiwa Waziri huu mradi anaujua. Kuna kipindi nilisema, mkandarasi ni tatizo, anapeleka mabomba akisikia ziara ya Waziri, ukiondoka na yeye anaondoa vifaa. Mkandarasi huyu alifeli Rorya, wakamkataa.

Mheshimiwa Spika, ninazo taarifa hapa, tunajua labda Wizara mna nia ya kutuletea maji lakini mkandarasi hafai, inafikia hatua ninyi wenyewe Wizara mpaka mnampa mabomba mkandarasi. Yaani hatimizi wajibu wake mpaka mnafikia hatua mnampa mabomba huku

mmemlipa kwa kazi aliyoifanya, hafanyi, bado na ninyi mnaingia gharama za kumpa mabomba? Kwa nini msimsimamishe? Kwa nini mnamlea? Anakula na nani huyu? Wananchi wa Bunda wanateseka. Miaka tisa kweli? Hawana tatizo na chama changu wapeni maji safi! Kina mama na vijana wanateseka, kwa nini huu mradi haukamiliki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na taarifa ya Kamati kusema kuna wakandarasi wengi hawana vigezo wala utaalamu, ndiyo haya! Mngefuata *background* kwa nini Rorya walimkataa. *Why* kwetu apigiwe chapuo? Kwa nini hakamilishi kazi bado mnaenda ninyi wenyewe mnampa tena mabomba? Wananchi wa Bunda wanateseka. Tunaomba jamani na sisi tuna shida ya kupata maji safi na salama ili mama zangu kule wasihangaike.

Mheshimiwa Spika, hilo la kwanza, yaani sisi mnatutafutia tu wakandarasi vimeo, kuna mradi wa Mgeta, kijiji cha Nyangaranga, hivi navyozungumza, mkandarasi amepewa pesa zote shilingi milioni 450 lakini hajakamilisha mradi anang'ang'aniza wananchi wapokee na wananchi wale ni wazalendo wamekataa. Kuna Mwenyekiti wa Kijiji pale, tena ameshinda kupitia tiketi ya Chama cha Mapinduzi, wanam-*force* apokee miradi, amekataa! Ukiona viongozi wa chama wanatoa hizi taarifa, ujue kuna kero za msingi ambazo zinawakabili.

Mheshimiwa Spika, wanatakiwa wajenge *DP* kumi kajenga saba na *DP* moja haina bomba wala mitaro. Kwa upande wa Nyangaranga alitakiwa kujenga na maeneo kwa ajili ya kunyweshea mifugo, kajenga moja, bado wananchi wanalazimishwa waupokee mradi huo wamekataa, wananchi sasa hivi ni waelewa. Uongozi wa Serikali ya Kijiji umekataa, Mkuu wa Wilaya anaenda ku-*force* wananchi wakubali mradi, wamekataa, wananchi wanajua *value for money*. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wananchi wa Bunda tuna shida ya maji lakini hatutakubali kupokea miradi ambayo haijakamilika kwa wakandarasi ambao wanabebwabebwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa hapa imesema, miradi mingi haikamiliki kwa sababu kuna wakandarasi wanapewa *tender* hawana vigezo.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Hata koleo hawana.

MHE. ESTER A. BULAYA: Nilivyoendelea kutafuta *information* na Wizara inajua mkandarasi huyohuyo kaharibu Serengeti. Mheshimiwa Keissy hapa alikuwa ananiambia hata Mtwara ni hivyohivyo, halipi hata wafanyakazi wake. Sasa tunabebaje watu wa namna hii? *Why*? Tunahitaji wananchi wapate huduma ya maji, maji ni uhai. Huwezi uka-*survive* kama hupati maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naungana na taarifa ya Kamati, hivi kweli tunataka Watanzania wapate huduma ya maji safi na salama kwa kuwapelekea asilimia 28 ya bajeti? Tutaamini vipi hii asilimia 55 ni sahihi? Asilimia 28 Wizara nyeti kama hii! Mwisho tutakuja kuwakaba bure tu hapa. Wizara ya Fedha watujibu, *why* asilimia 28? Hata hivyo, mwaka jana hizo shilingi bilioni mia nne na zaidi zilizotakiwa kwenda zimeenda shilingi bilioni mia moja na zaidi kidogo, watafanyaje kazi? Watanzania wataondokanaje na matatizo ya maji hasa akina mama wanaohangaika usiku na mchana? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Wizara hiyohiyo wanatoa wakandarasi ambao hawana viwango, Wizara hiyohiyo hela ndogo lakini cha ajabu hawana watumishi, wana watumishi asilimia 28 yaani wanahitaji watumishi elfu nane na zaidi lakini wana elfu moja, *how*? Yaani pesa wasipewe, wataalamu wa maji hawana, bado wakandarasi wanaopewa miradi ya maji hawana viwango, halafu leo hii tunasema tutamaliza tatizo la maji, *how*? *Please,* wananchi wana shida ya maji. Suala la maji tulipe kipaumbele. Wanaoteseka ni wanawake wa nchi hii. Au

mnataka tuseme inabidi sasa hivi tumpe mwanamke aongoze nchi hii? Nashangaa kwa nini Spika hujachukua fomu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya mambo jamani tuongee yanauma. Sisi ambao tunatoka kule na tunaenda huko vijijini kwa akina mama, tuna *feel pitch* ya wanawake wanavyohangaika usiku na mchana kutafuta maji. Siyo Bunda peke yake, nenda Tarime, Rorya, Serengeti na Mkoa wowote ule, kila mtu atakayesimama hapa tatizo ni maji. Jamani tunaomba sana, ni mara mia mkate huko kwenye sambusa na kahawa ili hii Wizara ipewe pesa ifanye kazi ya kuwatengenezea mazingira bora Watanzania kupata maji safi na salama. Ni aibu kila Mbunge anayesimama hapa huu mwaka wa tano analia maji, maji, maji, bila mafanikio! Sasa hii miradi itakamilikaje?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu sahihi kuhusiana na mradi wa Bunda ambao mkandarasi mnapa mabomba lakini hafanyi kazi, Rorya wamemkataa kwetu mnaendelea kutuachia. Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa tamko, naomba atoe tena, wale wananchi wa Mgeta, kijiji cha Nyangaranga wasiwe *harassed* kupokea mradi ambao haujakamilika, mnamlinda mkandarasi huyu wa nini?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Namtafuta wa kunisindikiza kuchukua fomu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Azza Hillal Hamad atafuatiwa na Mheshimiwa David Silinde.

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Waziri wa Maji pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Makalla na watendaji wa Wizara ya Maji, angalau kwa kile kidogo ambacho wameweza kukifanya katika Mji Mdogo wa Tinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini ninashukuru? Mji Mdogo wa Tinde kuna tatizo kubwa la maji na toka nimeingia ndani ya Bunge hili hakuna bajeti ambayo sikuwahi kuzungumzia mradi wa maji wa Mji Mdogo wa Tinde. Mwaka jana mwezi wa tano, Naibu Waziri, Mheshimiwa Makalla alifika Tinde akafanya mkutano mkubwa, aliahidi na alichokiahidi kimeanza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, mmetuchimbia visima viwili virefu lakini mradi ule thamani yake ni shilingi milioni 326. Fedha ambayo mmetoa mpaka sasa hivi ni shilingi milioni 100. Niwaombe sana pamoja na pongezi zote nilizowapa, shilingi milioni 100 haiwezi kukamilisha mradi huu. Kuna kazi ambayo inaendelea ya kuweka vituo vya maji katika Mji Mdogo wa Tinde.

Kuweka vituo peke yake bila wananchi kupata huduma ya maji hakuna ambacho tutakuwa tumekifanya.

Mheshimiwa Spika, niombe sana Wizara ya Fedha, maombi mliyopewa ni ya shilingi milioni 326 lakini mmetoa shilingi milioni 100 tu. Chondechonde, mradi ule utakuwa hauna maana yoyote iwapo fedha ambayo inatakiwa kukamilisha mradi ule hamtaipeleka kama inavyotakiwa.

Nawaomba na kuwasihi sana, ili Mheshimiwa Makalla na Waziri wako muendelee kuwa na sifa katika Mji Mdogo wa Tinde, chondechonde fedha hii ipelekwe na mradi ule uweze kukamilika mapema na uweze kuanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiangalia kwenye kitabu cha bajeti mmesema mpaka Julai mradi huu utaanza kufanya kazi. Nawashukuru sana! Nawaomba kile mlichokiandika basi na kiwe, nawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoka Mji Mdogo wa Tinde, naomba niingie mradi wa maji wa Isaka, Kagongwa na Tinde. Mradi huu umekuwa wa muda mrefu mpaka imekuwa kama vile ni gumzo. Kilichonipa tabu kwa siku ya leo ni baada ya kuona bado usanifu unaendelea. Kidogo nimepata shida ukurasa wa 87 wa bajeti hii ya Wizara ya Maji wanasema hadi sasa kazi ya usanifu inaendelea na ujenzi wa mradi huo utatekelezwa na KASHUWASA chini ya usimamizi wa Wizara ya Maji. Kitabu cha bajeti cha mwaka jana cha Wizara ya Maji, ninacho, ukurasa wa 77 kilikuwa kinasema:-

"Miji Midogo ya Kagongwa, Isaka hadi Tinde itapata huduma ya maji kutoka bomba kuu la Kahama - Shinyanga kutoka Ziwa Viktoria. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara yangu imepanga kutumia fedha kiasi cha shilingi bilioni 8 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo".

Mheshimiwa Spika, sasa nashindwa kuelewa, bajeti ya mwaka huu inasema, usanifu unaendelea wakati bajeti ya mwaka jana inasema shilingi bilioni 8 zimetengwa ka ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Naomba nipewe majibu, hizo shilingi bilioni 8 tulizopitisha mwaka jana kwa nguvu zote mpaka tukapitisha bajeti ya Wizara ya Maji zimefanya kazi gani mpaka sasa hivi? Huo usanifu unaoendelea, ni usanifu ambao unafanyika kwa miaka mingapi?

Mheshimiwa Spika, toka nimeingia ndani ya Bunge hili, ni usanifu, usanifu, usanifu, usanifu huu utaisha lini? Naomba muelewe, maji ni tatizo kubwa, bila wananchi wetu kuwa na maji hakuna kazi ambayo itaweza kufanyika. Naomba Waziri atakapoinuka anijibu zile shilingi bilioni 8 za 2014/2015 tulizipitisha kwa ajili ya kazi gani na kwa nini kwenye bajeti ya leo tunaambiwa usanifu unaendelea? Naomba niambiwe mradi huo umeanza lini au utaanza lini na unategemea kukamilika lini kwa sababu vitabu hivi sasa mimi vimenichanganya, sijui wenzangu kama mmevielewa! Kwa hiyo, naomba nipatiwe majibu ya mradi wa maji ya Ziwa Viktoria kutoka Kagongwa, Isaka na Mji Mdogo wa Tinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka katika eneo hilo, naomba niende katika Mji wa Kahama. Inasikitisha sana, hata mwaka jana nilisema katika mtaa wa Shunu katika Halmashauri ya Mji Kahama ndipo lilipowekwa tanki kubwa la maji linalosambaza maji Mji wa Kahama lakini mtaa ule ambako tenki la maji limewekwa pale hawana huduma ya maji, hatuwatendei haki wananchi hawa. Ni kwa nini basi wasiharibu hiyo miundombinu? Kama mimi nina shida ya maji na mtu aliyepo umbali wa kilomita hamsini anayapata yale maji lakini mimi ambaye tenki lipo kwangu sipati maji hawatendei haki wananchi wa mtaa wa Shunu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalisema hilo kwa makusudi mazima kwa sababu kuna maeneo mengi ya Kahama ambayo hawapati huduma ya maji. Maeneo haya ni ya Halmashauri ya Mji Mdogo wa Kahama ambayo ni Bukondamoyo, Mbulu, Mwendakulima, Mungula na maeneo ya Malunga. Naomba sana, haiwezekani uchukue maji uyapeleke eneo la mbali wakati sehemu unayotoa maji wananchi wale hawapati maji. Naomba Waziri atakaposimama anipe majibu, ni kwa nini wananchi hawa mpaka leo hawapati huduma ya maji? Ni kwa nini wananchi wa Shunu wapo pale wanalinda ule mradi wa maji lakini wao hawapati huduma ya maji? Hii imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Kahama kuendelea kuuona mradi ule unapita kwenye maeneo yao lakini wao hawapati huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la Kahama linafanana kabisa na tatizo lililopo Manispaa ya Shinyanga. Pale Shinyanga, Kata ya Old Shinyanga, kijiji cha Ihapa, kitongoji cha Ihapa A, ndipo lilipo tenki kubwa la maji la mradi wa Ziwa Viktoria. Hata bajeti ya mwaka jana nilisema

wananchi wa kijiji na kitongoji cha Ihapa ambacho kimebeba tenki kubwa la maji hawana huduma ya maji. Unawezaji kubeba maji kumpelekea mtu mwingine wakati walio na tenki la maji hawana huduma ya maji? Tuseme au tufanye nini ili muwaelewe wananchi hawa? Maji wanayaona lakini yanaenda kwa watu wengine, hatuwatendei haki wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ifike pahala tunapokuwa tunasimama sisi kama wawakilishi mtuelewe yale tunayoyasema, hatuyatengenezi, ndiyo uhalisia wa *site* kwenyewe jinsi kulivyo. Naomba nipewe sababu za msingi za watu wa Shunu na Ihapa ni kwa nini wanaendelea kuwa walinzi wa matenki wakati wao hawapati huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini napata tabu sana, kwenye kitabu hiki cha bajeti cha leo, 2015/2016, ukurasa wa 252, utekelezaji wa ile miradi ya visima kumi katika kila Wilaya. Naomba nitoe mfano mdogo tu, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, katika kijiji cha Kazuni, mradi wa Kazuni, wamesema kuna vituo 53 vya kuchotea maji ambavyo vimewekwa, ni uongo! Mimi natoka Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, vituo vya maji vilivyopo katika mradi wa Kazuni ni nane tu na sio 53 kama vilivyoandikwa kwenye kitabu hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika Halmashauri hiyohiyo ya Wilaya ya Shinyanga, mradi wa maji wa Didia kwenye taarifa hii inaonyesha kuna vituo 24, ni uongo! Mradi wa maji wa Didia kuna vituo 15 tu na siyo 24 kama vilivyoandikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba watakaposimama waniambie hivi vituo wamevitoa wapi? Hiyo ni mifano miwili tu ambayo nimeitoa, ukienda Manispaa ya Shinyanga pia ni hivyohivyo. Hizi siyo taarifa sahihi ambazo zimetolewa na tumewekewa kwenye vitabu hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Nitumie fursa hii kuishukuru Wizara, nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri lakini niishukuru pia Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu kilio cha maji cha wananchi wa Kishapu wamekiona. Kazi imeanza kama ambavyo wameandika kwenye kitabu chao, Kolandoto, Kishapu, Mwadui na Mji Mdogo wa Maganzo. Kazi tumeiona imeanza kufanyika lakini tatizo kubwa wanalolalamika KASHUWASA, fedha mliyowapa haitoshi. Kama kweli tumekusudia Miji hii Midogo iweze kupata maji, tunaomba muwape fedha kwa wakati ili miradi hiyo iweze kuwa na tija. Hakuna sababu ya kuendelea kutazama inachimbwa mitaro yanawekwa mabomba halafu mwisho wa siku maji hayatoki. Tunaomba fedha ipatikane, hakuna sababu ya kuanza na miradi mingine wakati ile ambayo mmeianzisha haijakamilika. Nawaomba na nawasihi sana fedha hizo mzipeleke kwa wakati ili kazi iweze kuwa yenye mafanikio makubwa. Niwaombe sana kwa sababu hata kwenye miradi ya visima kumi bado kuna miradi ambayo fedha zinadaiwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa nimuite Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Godfrey Mgimwa na Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran wajiandae. Mheshimiwa Silinde.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia na mimi fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mchanganuo wa orodha ya wachangiaji walioomba kuchangia Wizara ya Maji wapo 107. Nilikuwa napitia Wizara zote, hakuna Wizara iliyozidi watu 62 lakini Wizara ya Maji ni watu 107. Jibu lake ni nini? Jibu lake ni kwamba tatizo la maji bado ni kubwa tofauti na takwimu alizotuletea Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, ukipitia bajeti yote ya Mheshimiwa Waziri, unaona kabisa ni uwongo yaani hamna lugha nyingine ya kuzungumza zaidi ya kusema ni uwongo tena uwongo mtakatifu. Kwa sababu tukisema wananchi waje waeleze shida yao ya maji hakuna Wilaya, hakuna Mbunge, hakuna eneo ambalo hakuna shida ya maji, ni tatizo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hatuwezi kuendelea kudanganya watu kwamba tuna mipango, ikifika mwaka fulani watu milioni 20 sawasawa na asilimia 55, yaani hata takwimu za nchi hawajui kwamba sasa hivi taifa *projection* ni watu milioni 50 mwaka 2015 maana yake *it is less than that one*. *Interpretation* ni kwamba uwezo hakuna!

Mheshimiwa Spika, tuwe wakweli, nchi zote duniani hata zile zilizoendelea zinapokuja kujadili kwenye bajeti zao hazijadili mambo ya maji. Waziri anajadili visima kumi, Wabunge wenye akili timamu tunakuja kujadili *issue* ya visima kumi, *this is a shame*! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanajadili uchumi, sisi tunajadili mahitaji ya lazima ya mwanadamu ya kila siku, haiwezekani! Huwezi kuwa baba wa familia unajisifu kwa watoto wako kula wali ama kuvaa nguo, haya ni masuala ambayo tunasema ni uvivu wa utendaji. Hamna kitu hapa, tumechoka!

Mheshimiwa Spika, watu wanaweza wakaishi bila umeme, lakini Watanzania wote hawawezi kuishi bila maji. Sasa hii maana yake ni nini? Tunajadili kila mwaka, tunazungumza yaleyale lakini bado Serikali wamekuwa waongo! *BRN* uwongo mkubwa.

Mimi nasema uwongo kwa sababu hata Momba waliandika hapa mwaka jana, mwaka juzi, shilingi bilioni 9.3 tutaleta kwa ajili ya miradi ya maji Momba, hata mia kwenye hiyo *BRN* haijafika? Utasemaje kama siyo watu waongo hawa! Utasemaje kwamba hizi *story* ni kwa ajili ya kuombea kura tu hapa. Haiwezekani tukaendelea na uwongo wa namna hii.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi sana, miongoni mwa bajeti ambazo huwa zinakwama ndani ya Bunge ni pamoja na bajeti ya Wizara ya Maji lakini tunaongeza fedha hakuna linalofanyika, *the same story* kila mwaka! Tutaendelea kujadili hivi maji tu! Tutaendelea afya, tutaendelea kujadili madarasa, kuongezeka madawati, haiwezekani! Ndiyo maana mimi nimekuja kuona kama watu tunashindwa kutekeleza wajibu huu, ndiyo leo unasikia kuna mlipuko wa wagombea wa Urais. Kwa sababu watu wanaona kwamba kumbe kila mtu anaweza kuwa Rais na *interpretation* ni rahisi tu kwamba ili uweze kuwa Rais hata usipotekeleza maji na kadhalika watu watakuchagua tu.

Mheshimiwa Spika, hili suala linakera. Rais alikuja Jimboni kwangu Momba mwaka 2005, akaja mwaka 2010, akawaahidi wananchi kuwaletea maji hususan eneo la Tunduma na maeneo mengine yote ya Momba maana yake pale ndipo alipofanyia mkutano. Miaka imeshakwisha, tunategemea na mgombea mwingine naye atakuja kutudanganya hivyohivyo! Sisi safari hii hatuwezi kukubali! Hamuwezi kuendelea kutudanganya kila mwaka maji, maji, maji halafu hayatatuliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sera ya Maji ya Taifa inasema, mwananchi anatakiwa apate maji mita 400 kutoka mahali anapoishi, haya tuambieni nani anapata maji mita 400 kutoka anapoishi? Watanzania wa vijijini tuambieni kama wanapata maji mita 400. Huwezi kujisifu kwenye kijiji kimoja kuweka kisima kimoja, huu ni uwongo. Kwa sababu kijiji kimoja kina vitongoji 12, kutoka kitongoji kimoja mpaka kwenda kwenye kisima ni kilomita 12 ama 13 ni uwongo tu. Hizi takwimu wanaziandika tu ofisini hawaendi *field*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Muhongo pamoja na kashfa ya *ESCROW*, *at least* ameonesha kumbe inawezekana watu wote kupata umeme, angalau kidogo ameonesha hicho kitu, maji hayawezekani? Tanzania ndiyo nchi pekee ambayo inazungukwa na ile *surface water* kila mahali. Libya wana maji asilimia karibu mia moja, Iraq wana maji asilimia 100, Israel wana maji asilimia 100, nchi za kwenye jangwa, Taifa lenye maji kila kona *we speak the same story! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huku ni kushindwa kutekeleza wajibu wetu, tunashindwa kutekeleza mambo ambayo yanatupasa. Hatuwapendi Watanzania, wananchi wa vijijini hatuwapendi kabisa kwa sababu kule ndiko kuliko na tatizo kubwa. Waziri atakuja hapa kutuambia stori zilezile. Nakumbuka hata mwaka jana alisema tukiendelea kumsema vibaya hapeleki maji, mimi kwangu usilete tutafanya wenyewe. Haiwezekani kuendelea kuwa tunatishana kwenye mambo ya msingi ya kuwatetea wananchi. Waziri hutekelezi na huu wajibu umekushinda. Hili jukumu limekushinda, bahati yako tunaenda kwenye uchaguzi, ningeomba wananchi hata wa huko kwao wampumzishe kwa amani kwa kweli, kwa sababu haiwezekani hatuwatendei haki Watanzania! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasikitishwa sana na mwenendo huu wa kuwadanganya Watanzania. Leo ukiangalia vioski vya maji kwenye taifa zima, vioski vya Serikali unaambiwa vinagharimu mpaka shilingi milioni mia moja kujengwa, kioski cha mtu binafsi shilingi milioni kumi mpaka kumi na mbili, hamuoni ni wizi? Ukweli kwenye hili taifa hakuna miradi ambayo watu wanaiba fedha kama kwenye miradi ya maji na umwagiliaji pamoja na miradi ya ujenzi, wizi mkubwa ndiko unakofanyika. Sasa hatuwezi kuendelea kulea mambo kama haya. Fedha iliyoletwa mngekuwa hata mnatupa sisi binafsi tungeonesha mfano. Wananchi wana shida wanahitaji maji, tuna uwezo wa kutatua tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeangalia vipaumbele vya Marais wote wanaogombea humu sijaona hata mmoja ambaye anaweza kusema mimi nitahakikisha ndani ya mwaka mmoja tatizo la maji linatatulika na ni jambo ambalo linawezekana! Sasa tutaendelea kuzungumza hivi, tutaendelea kudanganyana hivi mpaka lini? Kwa nini tuendelee kuwadanganya Watanzania mpaka lini? Nataka tuje kwenye Bunge hili mwaka unaokuja tusijadili maji, madarasa au madawati, haya ni mambo yanayotakiwa yajadiliwe katika ngazi ya Halmashauri. Huku ndiyo tunasema akili ndogo kutawala akili kubwa, watu kushindwa kuwa na uwezo, watu hawana uchungu na hili taifa, watu hawana dhamira ya kweli ya kuwatumikia wananchi, haya ndiyo matokeo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata watumishi walioko kwenye Idara ya Maji kule waliko wanajua wanatudanganya, sisi tunajua mnatudanganya. Mmekaa tu ofisini mnatudanganya hamuendi *field* mkajua watu wanapata shida kiasi gani. Hakuna aibu unapokwenda Jimboni, saa kumi usiku Wabunge wanatoroka Majimboni, wanaogopa wananchi wao kwa sababu tu ya tatizo la maji. Maana unakwenda saa kumi unakuta akina mama wameamka wanachota maji, Mbunge unajisikia vibaya hata machozi yanaweza yakakutoka, ukija kuiambia Serikali linaingia sikio la kulia linatokea sikio la kushoto wamemaliza, *the same story,* bajeti ipite, tukupongeze mwaka umekwenda. Inasikitisha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, biashara ya maji nafikiri kama Bunge tunatakiwa tuazimie, tutenge hata mwaka mmoja tuweke bajeti ya kutosha. Tukubaliane mwaka mmoja tu tutenge bajeti kwa ajili ya kutatua tatizo la maji nchini inawezekana, kama ambavyo tulijaribu kuweka kwenye upande wa nishati. Sasa kama Waziri unashindwa kusimamia kwa sababu tu unamwogopa Rais kwenye *cabinet* kwa sababu atakuambia tu kama hutaki kazi ondoka, ni bora Rais akuambie huwezi kazi lakini simamia maslahi ya Watanzania! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamsamba leo hakuna maji, Mpapa hakuna maji, kila mahali kwenye Jimbo langu, tarafa ya Ndarambo, na tarafa zingine hakuna maji. Mnatupa kazi ya kujitetea sisi Wabunge, kazi yetu sisi ni kuiambia Serikali, tunawaambia hamsikii, tuwachape viboko? Tuwatandike ngumi maana siku nyingine tutakuja tuwapige humu humu ndani, ndicho kitakachokwenda kutokea kwa sababu… *(Kicheko)*

SPIKA: Kanuni haziruhusu.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Spika, kwa kweli yanatukwaza ndiyo maana unaona mtu hawezi kucheka kwa sababu ya watu kuwa na shida ya maji.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Basi ahsante tunaendelea. Mwanasheria Mkuu unasemaje?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu kutoa taarifa kwamba Sheria ya *Parliamentary Immunities, Privileges and Powers* inalifanya kosa la jinai kwa Mbunge kumpiga Mbunge mwenzake.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nitoe taarifa hiyo. *(Kicheko)*

SPIKA: Ndiyo maana nikamwambia sheria haziruhusu, hasa akiua sijui atasemaje. *(Kicheko)*

Sasa nimuite Mheshimiwa Ally Keissy, atafuatiwa na Mheshimiwa Mgimwa na Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran. Mheshimiwa Kessy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, mimi sitaunga mkono hoja ya Wizara ya Maji kwa sababu miaka miwili mfululizo kwenye bajeti yao wamenidanganya. Mwaka 2013/2014 na 2014/2015 walinidanganya kwamba watanipa pesa na alikuwepo hapo Mwenyekiti Mheshimiwa Jenista Mhagama wewe hukuwepo, akathibitisha na vitabu vipo na rekodi zipo waliahidi lakini hakuna pesa mpaka Mtukufu Rais mwenyewe aliponiona ndiyo akanipa shilingi bilioni moja siyo za bajeti. Wasiseme kwamba wamepeleka hela Namanyere hakuna na sitaunga mkono hoja kwa sababu wamenidanganya bajeti mbili mfululizo.

Mheshimiwa Spika, hiki kitabu chao cha bajeti, kwa ushahidi kabisa wa uwongo mtupu, ukurasa 245 wameandika kijiji cha King'ombe, Wilaya ya Nkansi kuna vituo 19 na wanaopata maji ni watu 4500 lakini maji hayatoki hata tone. Huu ni uwongo tena uwongo unaozungumzwa saa saba hii ljumaa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kijiji kingine kinaitwa Matala ambacho mimi ndiye Mbunge kabisa, kuna vitu 23 wananchi 4,056 hakuna chochote ni uwongo wa mchana kweupe. Hii Wizara wanajazwa taarifa na watendaji wa kule ambao ni waongo, wanawaletea taarifa za uwongo, za unafiki wenyewe wanajaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimezungumza mimi hapa kuhusu ubadhirifu unaofanywa Wilaya ya Nkansi, hata hela alizoleta Mtukufu Rais shilingi milioni 500 wameshachakata shilingi milioni 8. Walitoa hapa shilingi milioni 150 kwa ajili ya kusaidia wananchi maji Namanyere zote

wameshachakachua! Wameandika uwongo bomba la kilomita 2.7 ambapo ni uwongo mtupu, kukodisha gari shilingi milioni kumi na mbili, gari hewa! Utakodisha gari Namanyere - Dar es Salaam shilingi milioni 12 hata Dar es Salaam – Lubumbashi haifiki shilingi milioni 12. Huu ni wizi wa mchana kweupe. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Kirando shilingi milioni 201 alinisaidia alipokuwa Naibu Waziri wa Maji, Injinia Mahenge, nikamwambia wafanyakazi wake wanataka kuiba hela mchana kweupe, wanataka kuchukua maji kilomita kumi kwenye mto ambao unakauka na tunafanya *irrigation* na maji yapo kilomita moja Ziwa Tanganyika na kuna mantenki mawili tangu enzi ya Mwalimu Nyerere yapo, gharama itakuwa ndogo, akanisikiliza wakabadilisha mradi. Leo hakuna walichotumia kule wanasema shilingi milioni 201 zimeshateketea. Shahidi alikwenda Katibu wa CCM, Ndugu Kinana aliangalia hakuna kitu, alichimba mitaro hana bomba, utachimba msingi wa nyumba huna tofali, huna mawe, huna saruji, ikaja mvua ikaharibu mitaro yake yote, eti hasara tubebe walipa kodi wa Tanganyika (Tanzania) huu ni wizi wa hali ya juu. Tatizo ni la kuwapa wakandarasi ambao hawana uwezo kama Mheshimiwa Ester alivyosema, wanaingia kwa rushwa ni watoto wajomba na shangazi zao, hatuendi namna hiyo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mradi wa King'ombe nimezungumza leo na Mwenyekiti wa Serikali wa Kijiji cha King'ombe, nikamwambia Bwana nasikia maji yanamwagika kama asali huko nimesoma kwenye kitabu, anasema Mzee hakuna chochote, hakuna kazi na mkandarasi hayupo kakimbia. Sasa tutakuwa tunadanganyana halafu tukubali sisi bajeti ipite kienyeji? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilipinga safari moja bajeti wakasema tutakupa shilingi bilioni 3, zipo wapi? Mara mbili wamenidanganya? Mpaka baadhi ya Wabunge wakanionea wivu, ooh, mtampaje peke yake, sasa ndugu zangu wivu huo chukueni sasa nyie hizo hela zipo wapi? Mnadanganywa, kumbe mngeambiwa nimepigwa viboko mngesema na mimi nipigwe kiboko, hii ni hatari. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kudanganywa maji ni uhai, mji hauwezi kuendelea, utajengaje bila maji, utapikaje chakula, utafuaje nguo? Nilizungumza hapa nikasema nitawaleta akina mama wa Namanyere 60, wakaogopa wakasema watanipa hela ya maji, iko wapi hela ya maji mliyonipa? Rais ameniahidi hela ya maji yeye mwenyewe, Ofisi ya Waziri Mkuu itoe shilingi milioni 500 mpaka leo haijatoa. Tangu tarehe 12 Disemba, wakaniambia kabla ya Christmas tutakuingizia hela, hakuna hela iliyoingia hata moja na Rais anasikia huko.

Mwisho wa Rais ni Novemba bado ni Rais wa nchi hii, Wizara ya Maji ndiyo imeogopa imepeleka shilingi milioni 500 na katika hizo wameshaiba shilingi milioni 8, wameshachakachukua.

Mheshimiwa Spika, kuna ofisi ya maji kule inaandika kwamba saa za ziada Namanyere shilingi bilioni 2. Namanyere hakuna maji saa za ziada zinatoka wapi? Saa za ziada zimetoka wapi wakati Namanyere hakuna maji? Wanajiandikia tu makaratasi. Tulimdai huyo Mkuu wa Idara ya Maji tukamwambia tuletee risiti ya kukodi gari Dar es Salaam - Namanyere kwenye Baraza la Madiwani hakuonesha. Vikao vya Bodi ya Maji mmeshatumia shilingi milioni 2, tuoneshe hivyo vikao vilikaa wapi wakati Namanyere hamna maji. Kuna Bodi ya Maji wakati maji hakuna!

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu hii Wizara sitaiunga mkono hoja na nilizungumza pale, hata Mheshimiwa Spika nadhani kwako maji ni shida. Sasa ukiunga wewe mkono hoja watakufukuza wananchi wako wa Njombe kule, maji hakuna. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanakaa wanawadanganya wananchi hapa, halafu tunakuambia kule Namanyere kuna mchwa halafu unatuma TAKUKURU, inarudi ripoti eti mambo safi! Ndugu zangu hata TAKUKURU tutakuwa na wasiwasi nao sasa. Mambo safi, wafanyakazi wa Idara ya Maji wana magari manne, matano, wana mjumba wametoa wapi hela wakati hakuna bomba, hakuna chochote ni wizi mtupu!

Mheshimiwa Spika, hili suala la manunuzi ndiyo balaa zaidi, kitu cha shilingi kumi wanaandika shilingi mia tano. Mtaro mita moja kuchimba shilingi mia tano wanaandika shilingi elfu tano, tutafika wapi? Tukiwaambia sisi, mnapiga simu, chunguza huku. Mimi ndiye Mbunge wa Jimbo naangalia jinsi wanavyoiba hela, jinsi wanavyochakachua hela. Mradi wa shilingi milioni 200 Kirando hakuna kitu hata kimoja! Huko Matala wamesema shilingi milioni 120 maji hayatoki, King'ombe shilingi milioni 500 maji hayatoki.

Mheshimiwa Spika, asubuhi nimezungumza na Mbunge wa kule Kusini, Mheshimiwa Mipata, nimemwambia kwenye kitabu cha Waziri, Jimbo lako wewe maji yanatoka kama asali huko na maziwa anasema Mzee hamna maji yanayotoka, shilingi milioni 500 zimekwenda. Halafu anasimama Mheshimiwa Rajabu anaitukana Serikali ya CCM kwa ajili ya watendaji, labda ni CUF au CHADEMA wenzake na sisi tunacheka. Hawa watendaji ndiyo wabaya maana wamempa kichwa Mheshimiwa Rajab ametutukana hapo na sisi tunacheka. Wameshirikiana, siyo maji wameiba hela, sizungumzii habari ya maji, nazungumzia wameiba hela shilingi milioni 500; mradi wa King'ombe hamna maji.

MBUNGE FULANI: Ni Serikali yako.

MHE. ALLY K. MOHAMMED: Hawana kadi za CCM.

MBUNGE FULANI: Wanazo!

MHE. ALLY K. MOHAMMED: Mheshimiwa Spika, hawana kadi za CCM, wala siyo wana CCM, ni majambazi kama majambazi wengine! Baada ya mimi kuzungumza, wakamletea Naibu Waziri taarifa wameshachimba mtaro wa 2.7, mtaro hakuna. Hakuna mabomba yaliyofukiwa ni uwongo, unapokea taarifa za simu ni uwongo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nilimwaambia Mhandisi wa Maji, kama umefukia mabomba mapya kilomita 2.7, nioneshe hata bomba za zamani ulizofukua hakunionesha, nioneshe mabomba mapya uliyoleta hakunionesha! Wamenunua pampu za maji za visima vinne kwa shilingi milioni 22 wakati pampu zote ni shilingi milioni 5.6. Ndugu zangu manunuzi gani hayo? *(Makofi/Kicheko)*

Mimi nikisema TAKUKURU angalieni kule, hawa wameshakuwa na hela za kuhonga mpaka TAKUKURU! Wana hela za kuhonga, wana hela za kumziba mtu maana wameiba sana, shilingi milioni 500 maji hamna, shilingi milioni 200 maji hamna, sasa huyo TAKUKURU tumbo lake liko mbele au nyuma? Si watamtwanga tu hela arudi! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, waangalie tu TAKUKURU hapo, fomu za uchaguzi watu rushwa tupu wamemkamata nani, itakuwa maji kule kwetu ambapo tupo karibu na Kongo? Kule unadhani hakuna Serikali, mpaka uende wanapigiana simu anakuja, wameshatayarisha kibunda cha fedha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Waziri wa Maji mimi sitaunga mkono hoja kwa sababu bajeti mbili umenidanganya. Umeandika kwenye kitabu chako maji yanatoka katika

vijiji viwili ni uwongo! Maji Kirandu wameiba hela, haujawachukulia hatua wale watu, King'ombe na Matala wameiba hela.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Kawa shilingi milioni 200,
hakuna kitu! Bwawa la Kawa ambalo nililidai hapa, walitaka kunipora wananchi wajanja, wamepeleka shilingi milioni 200 hakuna maji, hakuna chochote! Miradi ya Nkasi yote ni hela kuibiwa na mimi kudanganywa hapa Bungeni, wanakuja kusoma taarifa za uwongo na bajeti ya uwongo. Hata kitabu kikubwa kama hiki, wamepoteza shilingi ngapi kuchapisha kitabu hiki ambapo robo tatu ya taarifa zake zote si za kweli.

Sasa ndugu zangu tutaendelea sisi kupata hasara kwa kuchapisha vitabu kwa taarifa za kusikia kwenye simu, kwenye makange, ndugu zangu, hii mitandao imekuwa mingi! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kitabu kikubwa kama hiki, tena sijaona Wizara ambayo imeleta hapa kitabu kikubwa kama hiki. Hii ni mara ya kwanza, vitabu vyote vilikuwa vidogovidogo. Hiki kitabu ni kama Msahafu lakini taarifa zake robo tatu ni za uwongo! Wamenidanganya mara mbili mimi hapa, mwaka 2013/2014 na 2014/2015 na vitabu ninavyo naweza kukuletea nimeviacha nyumbani. Vimeandika tutakupa shilingi bilioni 3, hakuna walichonipa hata senti tano. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nitaunga mkono hoja ya Wizara hii si nitaonekana mwendawazimu! Sitaunga mkono hoja hii, hata wote mkiitikia mimi nitasema hapana, hapana, wananchi wasikie kwamba hii Wizara inachakachua mpaka Wabunge inawadanganya. Hatukuja kudanyanywa hapa mpaka Mheshimiwa Rajab anasimama anatanua kifua chake pale anasema na sisi hatutakubali kudanyanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilimuambia Naibu Waziri, Mheshimiwa Makalla, hawa wanaokuletea taarifa angalia ni wanafiki, hawakuchimba mtaro Namanyere. Nikamuendea Mheshimiwa Mkuchika akaniambia andika barua nikaandika barua hii nikamwambia TAKUKURU nayo ishughulikie. Nasikia walikwenda TAKUKURU kule sijui kilichofanyika, hamna kitu! Naonekana mimi napiga bomu lakini nenda kawaulize watu wa Kirando, Namanyere, Matala, King'ombe, Nkundi, hakuna mradi wowote ni hela zimeliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hatuwezi kuitukana Serikali ya CCM wakati watendaji ndiyo wezi na hawachukuliwi hatua, hakuna aliyechukuliwa hatua. Kweli kabisa mtu anakodisha gari anaandika Namanyere – Dar-es-Salaam shilingi milioni 12? Juzijuzi Mkurugenzi kakodisha gari kubeba mabati ya maabara kutoka Dar-es-Salaam mpaka Namanyere kwa shilingi milioni 3…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante!

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Taarifa.

SPIKA: Waziri wa Nchi, Utawala Bora.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA): Mheshimiwa Spika, nimesimama tena kwa mujibu wa Kanuni ya 64 kinachosema, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli.

Nimemsikiliza ndugu yangu, mwana CCM mwenzangu, Mheshimiwa Keissy, nadhani kwa kunogewa tu alifika mahali akasema wanahonga mpaka TAKUKURU. Pia amesema nimempa barua Mheshimiwa Waziri lakini hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, nataka nilieleze Bunge hili barua aliyoiandika Mheshimiwa Keissy kulalamikia suala hili hata wiki mbili hazijapita. Barua wamekabidhiwa, nchi hii hatuonei mtu, tunachunguza ndiyo tunachukua hatua. Kwa hiyo, nataka nimwambie ndugu yangu Mheshimiwa Keissy tu kwamba uchunguzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni lile alilolisema kwamba wanahonga mpaka TAKUKURU. Mimi ni Waziri namsaidia Rais katika masuala haya ya TAKUKURU, kama anao ushahidi aniletee na tutachukua hatua.

SPIKA: Ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Mgimwa atafuatiwa na …

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Kuhusu nini Mheshimiwa Wenje?

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa kabisa, nimekaa humu ndani na ukisikia mijadala ilivyokuwa inaendelea, Mheshimiwa Azza, Mheshimiwa Keissy na Mheshimiwa Silinde walitoa ushahidi kabisa wa takwimu za uwongo zilizopo kwenye kitabu cha Waziri. Kwa utawala bora, ile *concept* ya *good governance* na kwa heshima ya Bunge hili Tukufu, ingependeza kama Kiti chako kingetoa amri Waziri afukuzwe, atoke nje, arekebishe takwimu zake, alete takwimu za ukweli tujadili. Kuendelea kujadili takwimu za uwongo tunapoteza muda wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Azza ametoa uhalisia, anasema kabisa hapa wameandika 24 wakati *on the ground* ni 14! Hapa wameandika sijui 25 wakati *on the ground* ni 16. Ni aibu sisi kuendelea kujadili uwongo! Kwa utawala bora, Mheshimiwa Waziri atoke, alete takwimu sahihi ili tujadili.

SPIKA: Hayo ya utawala bora mnanipotezea muda. Mheshimiwa Wenje una nafasi ya kujadili, utajadili. Tunaendelea, Mheshimiwa Godfrey Mgimwa, anafuatiwa na Mheshimiwa Mansoor Sharif.

MHE. GODFREY W. MGIMWA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema. Vilevile napenda kutoa pole au salamu zangu za rambirambi kwa familia ya marehemu, ndugu yetu, Mbunge mwenzetu Eugen Mwaiposa. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, tunavyozungumzia masuala ya maji tunazungumzia kwa ujumla maendeleo ya nchi yetu. Vilevile tukizungumzia masuala ya maji lazima tuwatizame sana akina mama ambao wanahangaika katika taifa letu kwenda sehemu mbalimbali kutoka katika maeneo yao kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, lakini kitakwimu inaonesha kwamba, upatikanaji wa maji katika vijiji katika nchi yetu ya Tanzania ni 55% tu, maana yake 45% bado hatuna maji. Tatizo hili si dogo, ni kubwa sana ukizingatia kwamba tuna vijiji vingi katika nchi yetu ambapo maeneo mengi ni

makame, lakini upatikanaji wa maji unakuwa ni hafifu. Tatizo hili haliwagusi wanawake peke yake linawagusa pia akina baba ambao kwa namna moja au nyingine inaweza ikasababisha mvurugano ndani ya familia kwa sababu akina mama hawa wanaenda umbali mrefu kwenda kutafuta maji. Kwa hiyo, naishauri Serikali iweze kuangalia ni namna gani inaweza ikasaidia hasa kwenye upande wa vijiji, tuweze kupata maji kwa asilimia zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile takwimu zinaonesha kwamba katika kila kijiji mwananchi mmoja anahitaji lita 5 - 30 kwa siku kwa matumizi ya kawaida lakini mpaka sasa hivi lita tunazozipata kwa wananchi wetu wa vijijini ni ndogo kwelikweli. Kwa hiyo, napenda sana kuona Serikali inafanya jitihada za makusudi kabisa kuweza kuhakikisha kwamba viwango hivyo vya upatikanaji wa maji vinafikiwa katika kiwango ambacho kinastahili ili tuweze kuhakikisha kwamba Serikali yetu inakuwa na nguvu ya kuweza kushindana katika masuala mengi hasa tunapoelekea katika uchaguzi huu unaokuja mwaka huu wa 2015.

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kuangalia masuala machache sana, maeneo mengi katika nchi yetu ambayo yana mifugo ni maeneo ya vijijini ambayo inahitaji maji vilevile. Sasa sijafahamu utaratibu gani ambao Wizara au Serikali inaufanya kuhakikisha kwamba malengo ambayo yanawekwa kwenye Wizara husika na bajeti yake husika yanaenda pia kuwagusa hawa wanyama. Kwa sababu familia au kaya nyingi zinatumia wanyama wake au mifugo yao kwenda sehemu mbalimbali kutafuta maji. Kwa hivyo, unakuta wananchi na wanyama vilevile kwa wakati huohuo wote wanaenda kutafuta kitu kimoja. Kwa hiyo, napenda sana kuona Serikali inafanya jitihada za makusudi kuweza kutenga pesa maalum kwa ajili ya kujenga mabwawa na kuhakikisha kwamba mifugo inapata maji katika wakati unaofaa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kugusia masuala mengine mawili, matatu kuangalia ni namna gani katika miaka mitatu bajeti ya Wizara imekuwa haijafika kiwango kilichokuwa kimekusudiwa. Nikiangalia mwaka 2013, asilimia 75 pekee ndizo zilikuwa zimepokelewa kwenye Halmashauri kwa ajili ya maji, asilimia 25 zilikuwa hazijafikiwa. Kwenye Halmashauri husika ndiko tunakopata matatizo na ndiko kwenye matatizo makubwa ya maji hasa vijijini. Sasa kama tutapeleka asilimia 75 na asilimia 25 hatuzitimizi, tunakuwa tunawaumiza Wakurugenzi wetu, tunawaumiza wananchi wetu, tunawaumiza Wabunge, tunaumiza jamii nzima ya Kitanzania. Kwa hiyo, napenda kuona Serikali inafanya jitihada za makusudi kuhakikisha asilimia hizi zinafikiwa katika miaka yote.

Mheshimiwa Spika, vilevile mwaka 2013/2014 asilimia 47 peke yake. Mwaka uliofuata 2014/2015 ni asilimia 26 tu za maji. Sasa kwa namna hii itakuwa ngumu kweli kweli kupata maendeleo katika jamii zetu kwa sababu wananchi wetu wataendelea kuangamia, mifugo itaendelea kuangamia lakini vilevile Serikali yetu itakuwa inapoteza sifa yake ambayo imekuwa ikijitengenezea kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kugusia masuala mawili kwenye Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha imekuwa nyuma kidogo kuhakikisha kwamba hizi pesa zinapelekwa kwenye Wizara ya Maji. Tunaweza tukamlaumu Waziri husika, tunaweza tukawalaumu watendaji wake, lakini tatizo kubwa tunalolipata ni Wizara ya Fedha kutopeleka fedha zinazostahili au zilizoombwa na Wizara kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo katika nchi yetu. Kama Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, tumejitahidi kwa namna kubwa sana kuona kwamba pesa ambazo tumezitenga *(ring fenced money or funds),* zinakuwemo muda wote kwa mwaka kiasi kwamba Serikali au Wizara inapoomba zile pesa lazima ziwepoo katika mfuko ule ili miradi hii ambayo haijatekelezwa tuweze kuhakikisha kwamba tunaikamilisha.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna tatizo kubwa ambalo Wakurugenzi wa Halmashauri wamekuwa wakilalamika kuhusu masula ya *exchequer.* Kuna pesa ambazo zinakuwa

zimetumwa na Wizara au Serikali lakini kwa uhalisia hizi pesa hazifiki kwenye Halmashauri husika, zinaonekana tu kwenye mfumo wa *computer* lakini haziwafikii walengwa. Tatizo hili linaenda kuwakumba makandarasi ambao wamekuwa wakidai pesa zao kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo hili nikiliangalia katika Jimbo langu la Kalenga, tuna wakandarasi zaidi ya wanne ambao wanadai pesa. Nikiangalia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, inaonesha tumepewa shilingi milioni 65 tu katika mwaka huu wa fedha. Pesa iliyoombwa ilikuwa ni zaidi ya shilingi milioni 800 kwa ajili ya kukamilisha miradi mbalimbali na mimi nina miradi mingi katika Jimbo langu ambayo bado haijakamilika.

Kwa hiyo, napenda sana kuona Serikali au Wizara husika inafanya jitihada za makusudi kabisa kuhakikisha kwamba tunapata pesa kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi lakini vilevile miradi mbalimbali ambayo bado haijakamilika tuweze kuikamilisha ili wananchi nao waweze kuwa na imani na Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, mimi pia napenda kuishukuru Serikali na Wizara husika kwa kazi nzuri waliyoifanya katika Jimbo langu. Ingawa tuna miradi ambayo haijakamilika lakini lazima nichukue nafasi hii kuwashukuru wameonesha mwanga mkubwa sana kuweza kupata maji katika miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuitamka miradi hii kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Magunga ambao unakusanya vijiji vya Itengulinyi, Lumuli na Isupilo;

(ii) Mradi wa Igangidumu ambao naishukuru sana Wizara kwamba umeshakamilika, tunasubiri tu tuweze kuona namna gani maji yanaanza kumwagika; *(Makofi)*

(iii) Mradi wa kijiji cha Mfyome ambao haujakamilika lakini upo kwenye asilimia 70. Tuna matumaini makubwa kwamba Wizara na Waziri husika ataenda kukamilisha kwa mujibu wa muda tuliokuwanao; na

(iv) Miradi miwili ya Mwambao na Weru ambayo nayo ipo kwenye 80% au 85%. Tunaamini tutaenda kupata pesa kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi, miradi hii imesimama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili tuweze kupata maji lazima tuwalipe wakandarasi. Wakandarasi kwa kweli wamekuwa wakipiga kelele siyo tu kumsumbua Mkurugenzi, wamekuwa wakinisumbua pia na mimi kuona kwamba pesa zao zinalipwa. Namshukuru Mheshimiwa Waziri amekuwa karibu sana na mimi, tumekuwa tukijadiliana mara kwa mara, naamini kipindi hiki ataenda kunisaidia tuweze kupata pesa hizi tuwalipe wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, kuna kijiji kimoja ambacho Mheshimiwa Waziri aliahidi mwaka jana, naomba uweze kukikumbuka ni kijiji cha Magunga. Nakuomba sana Mheshimiwa uweze kuhakikisha kwamba tunapata maji katika kijiji hiki. Ni kijiji ambacho kina sifa kubwa lakini hakina maji. Naomba sana Mheshimiwa tuweze kufanya kazi kwa pamoja kuweza kuhakikisha kwamba tunapata maji.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kazi binafsi ambazo zimefanywa na Mkurugenzi wangu wa Halmashauri na Ofisi yake lakini vilevile Mheshimiwa Diwani wa Kata ya Lyamgungu ambaye amefanya kazi kubwa sana kuwapata wahisani kutoka Canada ambao wametukamilishia mradi wiki iliyopita na tumeufungua. Tunashukuru sana kwa sababu hawa watu wamekuwa wakarimu sana katika Jimbo langu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia tu, napenda kuishauri Wizara na Serikali, miradi hii ambayo Wabunge wengi tumekuwa tukiipigia makelele hapa, bado haijakamilika. Nachoomba tuikamilishe miradi hii kuliko kuanza miradi mingine mipya. Ni vyema sana wananchi waweze kuona mwendelezo wa miradi ya miaka iliyopita inakamilika kwanza kabla hatujaanza kuja na miradi mingine mipya kwa sababu tutakuwa tunawakatisha tamaa wananchi na vilevile tutakuwa tunajikatisha tamaa sisi wenyewe kwa sababu bajeti inatengwa kubwa, haifikiwi, haileti malengo lakini cha ajabu tunakuja tena na miradi mingine mipya.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi lakini la mwisho napenda kuunga mkono hoja na Mungu akubariki sana. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Mansoor Hiran, atafuatiwa na Dkt. Christina Ishengoma, Mheshimiwa Abdallah Haji Ali na Mheshimiwa Ezekia Wenje.

MHE. MANSOOR SHARIF HIRAN: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja hii ambayo iko mbele yetu. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyotusomea hapa. Naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wa Kwimba kwa kuwa na ushirikiano mzuri kwenye kunisaidia mimi kusimamia maendeleo ya Jimbo letu la Kwimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2010, wananchi wa Kwimba waliponichagua walinituma kazi moja na hiyo kazi ilikuwa ni kutatua kero ya maji. Wananchi wa Kwimba hususani wa Ngudu Mjini mwaka 2010 walikuwa wananunua maji ndoo moja kwa Sh.800/= mpaka Sh.1,000/=. Kero ya maji ilikuwa ni kubwa sana kwa wananchi wa Ngudu Mjini na maji yalikuwa yanapatikana kwa mgawo, kila siku tatu unapata mgawo, unapata maji madogo unasubiri tena siku tatu. Kwa hiyo, wale walanguzi walikuwa wanauza maji kwa Sh.800/= mpaka Sh.1,000/= kwa ndoo moja. Wananchi kwa kweli walikuwa wanateseka sana na hiyo ndiyo kazi kubwa waliyonituma.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, alipofanya ziara mwezi wa tisa mwaka 2013, hiyo ziara ilikuwa ya historia maana alifanya ziara akiwa na Mawaziri nane, Mawaziri sita kamili na Mawaziri wawili Naibu. Ilikuwa ni historia kwa Jimbo la Kwimba kuonana na Mheshimiwa Rais na Mawaziri wote pale.

Mheshimiwa Spika, siku hiyo alipokuja Mheshimiwa Rais pale nilimwambia Mheshimiwa Rais nina kero ya maji kwa wananchi wa Ngudu. Mheshimiwa Rais alitusaidia, akatuahidi pale kwenye jukwaa mbele ya wananchi wa Ngudu akasema kero ya maji hapa Ngudu nitaitatua ndani ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, sisi kwenye Jimbo la Kwimba, maji ya Ziwa Viktoria yalishafika kwenye tenki la Mhalo kwenye Jimbo la Kwimba. Wakati Mheshimiwa Rais anaahidi nilimueleza kwamba maji yameshafika kwenye Jimbo naomba anivutie yafike Ngudu Mjini. Aliniahidi kwamba maji yatafika ndani ya miezi sita. Leo nilivyosimama mbele yako hapa, nina furaha kubwa sana ya kuwatangazia Watanzania wote kwamba ahadi ya Mheshimiwa Rais ilitekelezwa ndani ya miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo mradi wa maji ulioletwa Ngudu Mjini wa Ziwa Viktoria vijiji vingi pembezoni wamepata maji ya Ziwa Viktoria. Leo wananchi wa Ngudu Mjini wananunua maji kwa Sh.18/= mpaka Sh.25/= ukilinganisha na mwaka 2010 ilikuwa ni Sh.800/= mpaka Sh.1,000/=, hayo ni maendeleo mazuri sana. Mimi naamini kwamba, huyu Waziri amefanya kazi nzuri sana kusimamia huo mradi; mnyonge mnyongeni lakini haki yake mumpe. Mimi kwangu kwenye

Jimbo la Kwimba kwa kweli huyu Waziri na Mheshimiwa Rais wamenisaidia angalau nikienda awamu ya pili nina pa kuanzia kwamba kazi waliyonituma nimetekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mradi wa mfano wa *Big Result Now* basi mfano huo ni mradi wa Ngudu Mjini. Natambua Halmashauri nyingi zimekuja kuangalia huo mradi umetekelezwaje ndani ya miezi sita. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Wahandisi wa Halmashauri ya Wilaya waliotekeleza mradi huo kwa kushirikiana na wahandisi wa KASHUWASA. Mradi huu ulitekelezwa na wahandisi wa ndani kwa gharama ndogo. Naomba Mheshimiwa Waziri ikiwezekana wale wahandisi wapewe zawadi, watambuliwe kwa sababu kazi ambayo wamefanya ni ya kihistoria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupata maji Ngudu Mjini, bado changamoto ya maji ipo kwenye Jimbo la Kwimba. Jimbo la Kwimba tuna vijiji 62, maji ya Ziwa Viktoria yamepatikana kwenye vijiji 19. Bado changamoto ipo kwenye maeneo mengine, namuomba Mheshimiwa Waziri bajeti ya mwaka huu basi anipunguzie kero kwenye vijiji vingine ili wote wapate maji ya Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kwimba kuna maeneo hata ukichimba visima hupati maji hata kama ni visima virefu. Kuna maeneo mfano Kata za Mwakulwe, Mwakilyambiti, Shirembo, Kukibizi, Ilula, ukichimba visima maji huyapati. Wananchi wanateseka sana, wanatumia maji ya malambo na visima vichache sana ambavyo vinatoa maji kwa shida. Naomba Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti yake ya mwaka huu basi atusaidie kusambaza maji kwenye kata hizo ambazo nimezitaja za pembezoni ambazo zina matatizo sana ya maji.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pia naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Kwimba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutekeleza mradi huu wa kuleta maji kwa wananchi wa Ngudu. Mheshimiwa Waziri wananchi wanakupongeza sana, wanakushukuru sana na pia wamenituma nikuambie kwamba wanakusubiri kukupa zawadi ya ng'ombe ukija kututembelea.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nimuite Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Haji Ali na Mheshimiwa Ezekia Wenje atafuatia.

MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nawapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya. Tatizo ni bajeti, bajeti inayopitishwa na Bunge siyo inayotolewa kusudi iweze kufanya kazi. Bila ya hela ya kutosha tutakuwa tunajidanganya. Kwa hiyo, nashauri na kuomba kuwa bajeti tunayopitisha hasa fedha za ndani ziweze kutolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona Wizara imejitahidi kuweka hela za ndani kuwa nyingi kuliko hela za nje. Bajeti kwa mwaka uliopita ni asilimia 26 tu ndiyo iliyotumika kwa maana ya kwamba ndiyo iliyoweza kupatikana. Kwa hiyo, bajeti hii ndiyo inayotukwamisha kwamba miradi mingi bado haijatekelezwa. Kwa hiyo, tunaomba hizi fedha zikitoka kwenye bajeti hii kwanza miradi iliyosimama iweze kutekelezwa. Maji ni uhai na ni ya kila mwananchi. Akina mama ndiyo wanaopata shida sana kwenye matatizo haya kwa sababu akina mama ndiyo wanaochota maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye mradi wa maji kwenye Miji ya Morogoro, nashukuru MORUWASA wanajitahidi kwenye mambo ya maji. Wamesema Mji wa Morogoro sasa hivi tunaopata maji ni asilimia 85 lakini tunashukuru *MCC* ambao walitupatia shilingi bilioni 10. Hata hivyo, nadiriki kusema kuwa bado tuna matatizo ya maji kwenye Mji wa Morogoro, sehemu mbalimbali bado maji hayatoshi. Kwa hiyo, nawaomba MORUWASA na Serikali kwa ujumla wazidishe bidii kusudi wananchi wa Mji wa Morogoro waweze kupata maji ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maji kwenye Miji Midogo ya Dakawa, Kilosa pamoja na Gairo wamesema imesimama. Ni kweli imesimama kwa sababu fedha hazikutolewa. Tatizo ni fedha, siwezi nikasema tatizo ni watendaji, bila ya fedha huwezi kufanya kitu. Kwa hiyo, naomba fedha zikipatikana kwenye bajeti hii, miradi hii ambayo imesimama iweze kutekelezwa ili kusudi wananchi waweze kupata maji. Akina mama wanaendelea kupata shida, ninyi wote mnapita pale Gairo, akina mama wamebeba ndoo za maji, hakuna maji ya kutosha kwa kweli kwenye miji yetu hii. Naomba fedha zikipatikana kwenye bajeti hii tuweze kukamilisha miradi hii ambayo imesimama Mheshimiwa Waziri kusudi watu waweze kupata maji. Hata kwa Mheshimiwa Waziri anakotoka huko Mvomero, Turiani, wananchi bado wana matatizo ya maji. Kwa hiyo, naomba hiyo miradi iliyosimama iweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, wataalam ni wachache, ukiangalia kwenye upande wa Wizara hii ya Maji tuna Chuo cha Maji kimoja tu pale Ubungo kinachotoa wataalam wa maji mfano *engineers* na *technicians*. Nashauri Serikali kama inawezekana tuanzishe chuo kingine. Mbona fani nyingine tuna vyuo vingi kwa mfano sheria na biashara. Kwa hiyo, tungeweza kupata chuo kingine ambacho kingeweza kuungana na Chuo cha Maji cha Ubungo cha Rwegarulila ingekuwa ni vizuri sana tukapata wataalam wa kutosha kwa sababu bado tunahitaji *engineers* na *technicians* ambao hawatoshi. Nashukuru kuona kwenye kudahili wanawake wameongezeka katika chuo hicho lakini bado tunawahitaji wengi ili tuweze kupata wataalam wa sekta hii ya maji.

Mheshimiwa Spika, niongelee kidogo kuhusu Bonde la Mto Nile. Nashukuru sana kuona Mawaziri wanaohusika na Bonde la Mto Nile wamefanya mkutano, tunategemea kupata mambo mazuri kutokana na mkutano huo. Tulipata bahati nzuri ya kwenda Sudan, ni nchi kavu lakini wana maji ya kutosha na wanatumia maji ya Mto Nile kwa asilimia 87 lakini sisi tulikuwa hatutumii maji ya mto huu. Kwa hiyo, tukiweza kuyatumia maji hayo na sisi tutafurahi.

Mheshimiwa Spika, suala la uvunaji wa maji na lenyewe bado ni tatizo hapa Tanzania, hatujawa na tabia ya kuvuna maji. Naomba tuwe na tabia hiyo, Wizara yenyewe ikisaidiana na Wizara nyingine mtambuka na viongozi waweze kuhimiza uvunaji wa maji. Hata kuvuna maji kwenye paa la nyumba tunashindwa kweli? Watanzania sasa wamendelea kwani wengi wao wana nyumba za bati, unaweza ukaweka makinga maji ukavuna maji. Kwa hiyo, naomba angalau tuweze kuvuna maji kwa ajili ya umwagiliaji na mifugo yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuendelea kidogo kuzungumzia miradi ambayo imesimama, naomba iweze kumaliziwa lakini tatizo kubwa ni bajeti. Nasisitiza sana kuwa akina mama ndiyo wanaopata shida, naomba tumalize miradi hii ili akina mama na wananchi wote kwa ujumla na mifugo wote tuweze kupata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuzungumzia vyanzo vya maji. Watanzania tunaharibu vyanzo vya maji sisi wenyewe. Ukiharibu vyanzo vya maji unategemea nini? Maji yatakauka na hatutapata maji. Kwa hiyo, naomba tuache kuharibu vyanzo maji, tupande miti ambayo ni rafiki ya vyanzo vya maji na kwa kufanya hivyo tutaendelea kupata maji.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na mambo yote yaliyoongelewa na Kamati, mimi ni Mjumbe mmojawapo wa Kamati hii, naomba yote tuliongelea kwenye Kamati yaweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamuita Mheshimiwa Abdallah Haji Ali atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekia Wenje na Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

MHE. ABDALLAH HAJI ALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuongelea machache katika mjadala huu. Kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia nikasimama hapa na mimi nikaweza kuzungumza chochote. Pili, nakupongeza wewe binafsi kwa umahiri wa kazi zako na hata baadhi ya watu wengine hapa wamekuambia utangaze nia na watakupeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi ambayo nilitaka kuyazungumza ndiyo hayohayo ambayo tayari yameongelewa lakini nikipata muda nitagusia kwa uchache. Kwanza, niseme tu kwamba na mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. Katika muhula uliopita, tulipata fursa nyingi za Wajumbe kutembelea miradi ya maji. Mimi na baadhi ya wenzangu tulipata fursa ya kuelekea Mikoa ya Kusini, Rufiji, Lindi na Mtwara. Hiki nitakachokisema hivi sasa ni kama salamu kwa sababu sisi tunapotembelea huko baadhi ya matatizo tunayoyakuta huwa ni salamu ambazo tunatakiwa tuzilete hapa na tuiambie Serikali.

Mheshimiwa Spika, kituo cha kwanza tulichokitembelea tulikwenda Wilaya ya Rufiji, pale kuna mradi mmoja mkubwa tu wa maji. Wamejenga tenki kubwa linakaribiana na hata huu ukumbi wetu. Tulipofika pale tulielezwa tuliyoelezwa halafu tukataka twende tukakague tenki lile, tulipofika tukakuta hakuna maji hata tone. Tukauliza tukaambiwa sababu ni kwamba umeme wa uhakika haupo, inawezekana umeme ukakatika mara 24 kwa siku.

Kwa hiyo, hakuna uwezekano wa kupatikana umeme kuzisukuma mashine na kuweza kuyasukuma maji yakaingia katika tenki. Kwa hiyo, walituomba salamu zao tuwapelekee Serikalini kwamba wasaidiwe umeme wa uhakika ili ule mradi ufanye kazi. Mheshimiwa Waziri lile tenki pale ni tasa, halizalishi, nikikuambia hivyo nadhani unafahamu. Kwa hiyo, kilio chao kikubwa wasaidiwe umeme wa uhakika ili ule mradi ufanye kazi kama ulivyokusudiwa, hiyo ni salamu moja.

Mheshimiwa Spika, salamu nyingine katika kutembea kwetu tulifika Jimbo la Mtama, kile kijiji kidogo kimenitoka, kuna mradi mkubwa na ni wa siku nyingi. Kutoka chanzo cha maji mpaka lilipo tenki ni wastani kama wa kilometa saba au nane hivi. Mradi ule unatumia *generator* za zamani, wenyewe walisema ya tangu mwaka 47. Gharama inayowapata pale ni matumizi ya *diesel,* kama sijasahau walituambia kila siku wanalazimika kutumia karibu lita 200 ili kusukuma maji mpaka yafike katika tenki na umeme upo karibu nao wastani wa kilometa sita mpaka kufika kwenye chanzo hicho cha maji. Vilevile na wao walisema tuwaletee salamu zao Serikalini ili wapatiwe umeme wa *grid* ili waondokane na gharama kubwa za matumizi ya *diesel*. Hiyo ni salamu nyingine.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile Kibiti tulipata malalamiko mengine, wananchi wanasema maji yanayo lakini *nature* ya maji hasa huwa hayana rangi lakini yale maji yanayopatikana pale yana rangi. Wanaambiwa na wataalam kwamba maji yale ni safi na salama lakini hofu yao ni kwamba hata vile vyombo wanavyovitumia vimebadilika rangi. Ni uhakika kabisa kwa sababu hata vile vikuta ambavyo wenyewe wanauzia maji pia vimebadilika rangi.

Kwa hiyo, wakasema tuna wasiwasi na afya zetu, tunataka mtupelekee salamu hizi Serikalini kweli tunavyoambiwa maji haya ni safi na salama hayana madhara ikiwa vyombo tunavyovitumia vimebadilika rangi, ikiwa hivi vikuta vimebadilika rangi, je, afya zetu? Hiyo ni salamu nyingine ya watu wa Kibiti kwamba maji yao yana rangi, hayajasafika ingawa wameambiwa ni safi na salama lakini bado wana wasiwasi. Kwa hiyo, nadhani Serikali itakuja na majibu mazuri juu ya masuala haya.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu alizozieleza Waziri kwamba miradi mingi ya vijijini bado haijatekelezwa, ilikadiriwa kwamba wananchi wa vijijini wapate maji safi na salama wastani wa asilimia 65 lakini hadi sasa nadhani ni asilimia 55 iliyotangazwa, kwa hivyo bado kazi ipo. Hali hii inatokana na sababu mbalimbali zikiwemo uhaba au upungufu wa fedha, upungufu wa hao wataalam waliozungumzwa, upungufu au uwezo mdogo wa wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, fedha iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka 2014/2015 ilikuwa ni wastani shilingi bilioni 488.87. Mpaka Machi pesa iliyopatikana ni wastani wa shilingi bilioni 129.38 sawa na asilimia 26, hiyo imeshasemwa na wenzangu sana hapa.

Kwa hiyo, kwa hali hii tukiangalia Serikali inashindwa kutoa fedha ambayo inaidhinishwa na Bunge chombo kikubwa kama hiki, sijui tutegemee nini?

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali tunaposimama tukaomba mambo kama haya ijitahidi angalau ifikie nusu na robo lakini leo asilimia 26 hata nusu hatukufikia. Hayo yanayosemasemwa na wengine inawezekana ni sahihi sana.

Mheshimiwa Spika, athari ya mambo haya Serikali imebaki na madeni makubwa kwa wakandarasi wa maji na matokeo yake miradi kuchukua muda mrefu kutokukamilika na kuongezeka gharama mara tatu zaidi ya hata yale makisio yaliyofanywa mwanzo.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa wataalam, katika ngazi ya Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri mahitaji halisi ni 8,749 lakini watalaamu tulionao ni 1,848. Nchi yetu ni kubwa, tukiwa na kiasi cha upungufu mkubwa huu wa wataalamu sijui tutegemee nini au sijui kuna maendeleo gani yatakayopatikana hapa ikiwa hata wataalam tunashindwa kuwaajiri tukafika pahali tukaona labda tumeshindwa lingine, lakini rasilimali watu tunao. Watu wanamaliza vyuoni kila siku. Ilisemwa hapa na Kambi ya Upinzani kwamba, itolewe takwimu, ionyeshe ni watu wangapi wamemaliza, watu wameajiriwa, bila shaka watu wapo, lakini Serikali ifanye juhudi ya kuwaajiri hawa watu, tushindwe lingine, lakini tusishindwe na wataalam ambao tunao ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika hali hii namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake atueleze ataikabili vipi hali hii? Idadi itakiwayo ni hii lakini tuliyonayo ni hii ataikabili vipi hali hii?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

SPIKA: Ahsante sana. Sasa kwa dakika hizi naweza kumpata Mheshimiwa Ezekiel Wenje na Mheshimiwa Jerome Bwanausi, wawili tu wanatosha.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mimi pia kupata fursa ya kuchangia Wizara hii ya Maji ambayo ni muhimu sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianzie pale nilipoishia nilipokuwa naomba mwongozo kutoka kwako kuhusu uhalali wa Ripoti ya Waziri, *the credibility of The Minister's Report tabled in this House this afternoon. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wametoa takwimu sahihi, amesema Mheshimiwa Azza, Mbunge wa Chama cha Mapinduzi kuwa, kijiji kinachoitwa Kazuni huko Mkoa wa Shinyanga, Ripoti ya Waziri katika ukurasa 253 inasema vituo 53, wakati hali halisi kwenye *ground* kule ni vituo vinane tu. Kijiji cha Didia, badala ya vituo 24, hali halisi kwenye *ground* ni vituo 15. Kila mtu amesimama hapa akatoa takwimu akijaribu kutoa uthibitisho kwamba, Ripoti ya Waziri imejaza uongo na ubabaishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tungekuwa tuko *serious*, Bunge *serious* na Serikali *serious*, kama kuna nchi inaweza ikampiga Waziri risasi kwa sababu amesinzia tu mbele ya Rais, hivi watamfanyaje Waziri anayekuja kulidanganya Bunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusingekuwa Bunge linalokuja kufanya *rubber stamp*, tunafanya *business as usual,* ili ni bajeti ipite tu, Waziri alitakiwa afukuzwe ndani ya Bunge, arudi apitie upya taarifa yake, atuletee taarifa yenye ukweli, ili tujadili taarifa halisi yenye ukweli na uhakika kutoka huko *ground*. Wabunge wanasema kabisa kwamba, hii Ripoti ya Waziri, imejaza ubabaishaji na uongo na takwimu za uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa tena mfano, tunapokuja hapa tunadanganya Taifa kwa mfano hiki Kijiji cha Shinyanga kwamba, kuna vituo 53, hivi vituo vinajengwa kwa fedha, lakini *in real sense* kuna vituo vinane tu, yaani hata kwenye mahesabu *margin error* katika kukosea mahesabu, haiwezi ikawa zaidi ya 100%. Kwamba, *in real sense* kuna vituo vinane, kwenye kitabu kuna 53, yaani *this margin error is more than one thousand percent is too big!* Hata kwenye mahesabu hii haijakosewa, hii imeandikwa kwa makusudi kupotosha Bunge na kudaganya kwamba kuna kazi inafanyika, kumbe *in real sense* hakuna kazi inayofanyika.

Mheshimiwa Spika, tunavyodanganywa hivi kila kituo kuna thamani ya fedha ya walipa kodi ya Watanzania inayojenga kila kituo. Maana yake hapa kuna vituo vingi hewa ambavyo havijaandikwa, lakini kuna fedha ya walipa kodi imetumika. *(Makofi)*

Sasa hizi fedha zilizotumika kwenye vituo hewa ziko wapi? Ziko wapi hizi fedha? Zimeenda wapi? Zimefanya nini kwa sababu ni vituo hewa na takwimu imetolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *if this House were serious,* huyu Waziri kwa mara ya kwanza tungemfukuza arudi akakae na watalamu wake, wajadaliane upya, walete ripoti yenye uhalisia na ripoti ya ukweli. Leo nimethibitisha Mheshimiwa Keissy amesema kwamba, kuna sehemu wanasema wamechimba wameweka mambomba, wakati hakuna kitu kilichochimbwa mle ndani, hakuna mambomba yaliyofukiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia kusema, Taifa hili lipo hapa lilipofika kwa sababu ya rushwa na ufisadi. Tuko kwenye Taifa leo ambalo mtu akiiba, anaiba halafu tunatafuta maneno mazuri ya kufunika wizi walioufanya. Serikali iliiba fedha za *radar,* kwa kufunika tunaita *change* za *radar*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *a time has come*, tunahitaji Rais atakayejipambanua kabisa na atueleze Watanzania kwamba, akiingia madarakani kipaumbele namba moja chake kitakuwa ni rushwa na aweke bayana mikakati gani atakayopambana kuzuia rushwa. Rushwa ndiyo

inafanya akina mama wanakosa maji vijijini, rushwa ndiyo inafanya Watanzania wanakosa maji. *(Makofi)*

Katika ukurasa 48, Mheshimiwa Waziri anasema, katika mkakati wao wa Miradi ya Kupeleka Maji Vijijini, mpaka leo miaka 50 ya Uhuru ni asilimia 55 tu ya Watanzania na bado haijafika. Hii takwimu inakuwa *doubted* kwamba ni ya uongo pia. *50 years after Independence, is only 55% of our people* kwenye vijiji wanaopata maji safi. Hii inayobaki *fourty something percent*, hawa watu wanakunywa maji kwenye visima pamoja na ng'ombe, nyoka, fisi na wanyama wote wanakunywa nao maji hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ufisadi huu kwenye maji, kinachofanya Watanzania wanakosa maji, ilikuja hapa Miradi ya *World Bank* ya Visima Kumi kila Kijiji, kila wilaya ilikuwa. Nyamagana ninakotoka hakuna kisima hata kimoja kilichotoa maji. Tuliwekewa visima Buhongwa, Lwanima, Kanindo, Fumagira, kulikuwepo na visima Bulale, hakuna kisima hata kimoja kwenye Mradi wa *World Bank* kilichotoa maji! Ule pia ulikuwa ni ufisadi mingine kwenye Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rushwa ndiyo inafanya tunakosa maji na hii rushwa ndiyo inafanya hata Waziri anadanganywa, kwa sababu yawezekana haiendi *field*, analetewa hizi takwimu ambazo zimekuwa *cooked* za uongo. Profesa hafanyi *research* hata ku-*verify* hizi takwimu alizopewa. Profesa husomi, maana yake husomi vitu unavyoletewa, wewe ukiletewa unakuja tu hapa kusoma, ndiyo maana unatudanganya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jiji la Mwanza, ninakotoka tuna kilomita moja tu kutoka Ziwa Victoria, *in fact* tumezungukwa na Ziwa lakini hatuna maji! Dar es Saalam watu wanalalamika hakuna maji, Mwanza hakuna maji, Mbeya hakuna maji, Arusha hakuna maji, Kasulu hakuna maji, Iringa maji ni tatizo; maji ni tatizo kila kona. Mimi natoka Ziwa Victoria, nilipoingia katika Bunge hili swali langu la kwanza kama Mbunge lilikuwa kwa nini Buhongwa hakuna maji wakati *just one kilometer from* Ziwa Victoria? Maji yanatoka kule yanapelekwa sehemu nyingine mpaka Egypt sisi pale hatuna maji!

Mheshimiwa Spika, nimeona katika Mradi uliowekwa hapa kwa ajili ya Jiji la Mwanza ni Miradi inayofadhiliwa, fedha nyingi zitatoka *European Investment Bank,* niliyoona hapa. Sasa Jiji la Mwanza mnavyoliona ni Jlji la pili kwa ukubwa Tanzania, hakuna maji kwenye ile milima, ukienda Bugarika hakuna maji, Nyegezi majengo mapya hakuna maji, maeneo mengi hatuna maji kwenye lile Jiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa wa 47 kwenye Ripoti ya Waziri, tatizo kubwa kwenye Taifa letu Waziri anasema, mwaka 2014/2015, fedha zilizotengwa kwenye Wizara yake kupeleka maji ilikuwa bilioni 270, lakini mpaka Aprili 15, 2015, fedha zilizopelekwa ni bilioni 77.5, ni asilimia 28 tu mpaka na bajeti sasa hivi inaisha.

Mheshimiwa Spika, kama tunapitisha hizi bajeti za kiini macho, yaani tunapitisha bajeti ambayo fedha zinawekwa kwenye karatasi haziendi kufanya kazi hivi tunafanya nini?

Tunahitaji *commitment* ya hii Serikali ya ku-*fund* hizi bajeti tunazopitisha hapa ili tupeleke maji kwa Wananchi kwa kasi. Ni aibu alivyosema ndugu yangu Silinde, kwa Karne hii Wabunge tumevaa suti zetu za gharama tuko hapa tunajadili kupeleka maji vijijini wakati wengine wanajadili watafikaje hata kwenye jua. Wengine huko duniani wanajadili namna ya kutengeneza *nuclear technology, is the one of nuclear*, sisi bado tunajadili ni namna gani tutachimba visima kwenye vijiji vyetu na vyoo kwenye shule za msingi*! This is pathetic. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *you know*…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa ahsante.

MHE. EZEKIA D. WENJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru.

SPIKA: Tungefunga usingeweza kujimwaga namna hiyo, afadhali hivyo.

Mheshimiwa Jerome Bwanausi!

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika Hotuba ya Waziri wa Maji.

Mimi napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji, kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Jitihada za Serikali yetu ni kubwa sana katika kuhakikisha maji yanasambazwa vijijini. Tatizo ambalo ninalona ni bajeti inayopangwa kwa Wizara hii siyo fedha zinazopelekwa Wizarani. Kama fedha zote tunazopanga zingekuwa zinafikia Wizarani, tungekuwa na nafasi nzuri sana ya kuilaumu sana Wizara. Mimi nilikuwa nasema tatizo siyo Wizara zetu, tatizo ni Hazina kutofuata bajeti tunazopitisha. *(Makofi)*

Wizara zetu zingekuwa zinapata fedha kulingana na jinsi tunavyopitisha ndani ya Bunge, kwa kweli manung'uniko haya tunayoyatoa hapa Waheshimiwa Wabunge yangeweza kupungua sana.

Mheshimiwa Spika, mimi nina ushauri kwa Watendaji wetu; ni kweli kuna baadhi ya Watendaji wetu katika Wizara hii siyo waaminifu, lakini siyo kweli kwamba Watendaji wote wa Wizara wanafanya vitu tofauti na utaratibu ulivyo.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu ninao Mradi ambao tulianza kuupitisha tangu mwaka 2013/2014 nao ni Mradi maarufu kwa jina la Mradi wa Chiwambo. Mradi huu ungeweza kuisha mapema, lakini tatizo kubwa ni fedha zinazopatina Wozarani kwa ajri ya kuhudumia Mradi huu hazitoshelezi. Kwa hiyo, naiomba Wizara sasa itazame ile Miradi ambayo imeanza muda mrefu, ipewe kipaumbele ili iishe na tusianzishe Miradi mingine mipya, ili kazi zile ambazo tumeanza nazo tuzimalize kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuna huu wimbo wa vijiji kumi, tumeanza kuuimba muda mrefu sana. Mimi naiomba Wizara, sasa badala ya kutegemea tu fedha za wafadhili, basi tutenge na fedha za ndani kukamilisha hivi vijiji ambavyo tumevianza muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hakika siyo vyema sana kila wakati kumfukuza Waziri nje kwa sababu Wizara yake haikupata fedha. Mimi nilikuwa nadhani ni jambo muhimu sana kuhakikisha tunapokuja kwenye bajeti ama kwenye Wizara ya Fedha, tuwabane watu wa Hazina, wahakikishe vipaumbele muhimu kama maji, vinapewa fedha za kutosha. Mimi nadhani tukifanya hivyo, naamini kabisa, fedha zikipatikana na Miradi hii ina uwezo kabisa wa kupatikana.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara kwamba, moja ya sifa alizofanikiwa Profesa Muhongo, hakutegemea sana fedha za bajeti, alikuwa anahangaika kwenye Taasisi mbalimbali za Kimataifa kutafuta fedha. *(Makofi)*

Kwa kweli naiomba Wizara ijaribu kuangalia uwezekano pia na Watendaji wake, watafute Taasisi zingine za Kimataifa ambazo huwa zinatoa misaada, wapate kupata fedha za kutekeleza kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasisitiza tu kwamba, Miradi ile ya Vijiji Kumi katika Jimbo langu; Mradi wa Mkululu, Mradi wa Mkaliwata na Mpindimbi, ambayo inahudumia maeneo mengi, iweze kupatiwa fedha. Pia Mradi wa Chiwambo, ambao Wananchi wa maeneo ya Mpeta, Chanika na maeneo mengine ambayo mabomba yamelazwa lakini bado hayajafukiwa, hebu ipata fedha ili Mradi huu uweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Hotuba ya Wizara ya Maji. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa!

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, kule Jimboni kwangu wamekuwa wakikagua ujenzi wa maabara. Sasa Mkuu wa Wilaya anawakamata Watendaji wa Mitaa, ameanza jana Kata ya Ilala na Mwembetogwa, wale ambao wameshindwa kuwachangisha Wananchi kufikisha lengo la ujenzi wa maabara.

Mheshimiwa Spika, hiki ni kinyume kabisa cha utawala bora na kuwa-*intimidate* watu, tumevuka hizo zama za kuwatisha watu. Michango ya maabara siyo ya lazima, niliomba mwongozo wako Serikali inasemaje kuhusu suala hili, kwa sababnu linaleta migogoro ya nafsi kwa Wakazi wa Jimbo langu, kunakuwa na msongamano kidogo linaleta tabu. Naomba mwongozo wako Serikali inasemaje kuhusu jambo hili.

SPIKA: Naona Serikali ipo, ingekuwa imetokea humu ndani ningekuongoza. Sasa kinoti ulichoniandikia nimempa Waziri Mkuu hapo, kwa hiyo tutategemea wao ndiyo watatuambia.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge. Tukirudi hapa Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Omari Rashid Nundu-, Mheshimiwa Rachel Mashishanga, Mheshimiwa Dkt. Goodluck Ole Medeye, Mheshimiwa Profesa Msolla, Mheshimiwa Michael Laizer, atafuatia Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimwa David Kafulila.

Naomba wawahi na wengine tuwahi, hicho mnachokifanya huko mimi sikijui. Mnabakia mpaka mnachelewa mimi sikijui huwa mnafanya nini! Mkani-*surprise* siku ile Rais wa Msumbiji alipokuja, maana nilikuwa najua *empty house, and it was full, I was surprised!* Sijui inakuwaje! *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi.

(Saa 7.56 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 mchana Bunge lilirudia)

SPIKA: Wengi niliowataja asubuhi nawaona, tunaanza na Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Mntangi, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Genzabuke. Mheshimiwa Deo Sanga!

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Maji. Niseme tu kwamba, naishukuru Serikali kwa namna ambavyo inahangaika juu ya maji na changamoto zipo, lakini lazima penye kushukuru tushukuru. Nianze kwa Wilaya ya Njombe na Jimbo la Njombe Kaskazini, Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa mchakato mzuri ambao inaendelea Image, Ihang'ana, Tagamenda, Welela, Ibumila, Itambo na Kifumbe, ambapo mpaka sasa tunaendelea vizuri na Wananchi wanategemea kupata maji hivi karibuni na baadhi ya maeneo wameshapata maji. Kwa mfano, Kifumbe tayari maji yapo, Naibu Waziri alienda akaweka Jiwe la Msingi na Mwenge unaenda kufungau hivi sasa. Vilevile katika Wilaya ya Njombe kule Lumage, Igominyi, tunaishukuru Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuishukuru Serikali ziko changamoto. Kwa mfano, pale Lugenge, tunaishukuru Serikalii imeweza kutupa hela kupitia wewe mwenyewe Spika, nadhani wanaendelea vizuri. Vilevile tunaishukuru Serikali kwa namna ambavyo iliweza kutupa hela juu za mji wetu wa Makambako ambako kulikuwa na changamoto kubwa sana juu ya maji ya mji ule wa Makambako. Tunaishukuru Serikali ilitupa hela tuliweza kuchimba visima zaidi ya saba ambavyo tunavuta kwa pampu za umeme kuweka kwenye *line* ili ku-*supply* kwenye matenki makubwa kuongeza nguvu. Uhaba wa mwaka wa jana na mwaka huu angalau tunaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iniambie imejipangaje juu ya kutatua tatizo la maji katika Mji wa Makambako.

Mheshimiwa Spika, kazi ya usanifu tunaishukuru Serikali walishaifanya, lakini mpaka sasa hawajatuambia nini kinachoendelea. Naomba Waziri atakapokuwa anahitimisha, atuambie wamejipangaje juu ya kutatua tatizo la Mji wa Makambako na hususan Mji wa Njombe ingawa asubuhi alielezea pale Njombe Mjini kwamba tunaendelea vizuri, wametupatia zaidi ya shilingi milioni tatu na kitu. Cha ajabu, mtu wa kawaida anapopita pale Njombe, maji yako hata kilometa mbili hazifiki, Luhuji pale tuna maji ya kutosha; hivi kuna tatizo gani Serikali kuweka ubunifu wa kuvuta maji ya pale Luhuji wakati kuna maji yaliyotoka Mwanza yamefika mpaka Shinyanga ambako ni Kilometa nyingi sana?

Mheshimiwa Spika, nimewahi kuchangia hapa kwamba, maji yale kuna tatizo gani yakienda Njombe Mjini, yakija Makambako, wakati Makambako ni kilometa 60 tu, ingawa usanifu ulifanyika kwenye kijiji kimoja kinaitwa Tagamenda?

Ombi langu, Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unahitimisha hebu tuambie umejipanga vipi kutatua tatizo kubwa sugu la Mji wetu wa Makambako.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo kuna vijiji ambavyo bado kuna changamoto kubwa; kwa mfano, Lupembe, Kata ya Lupembe kwenda Kata ya Ikondo, kuna tatizo kubwa la maji. Wakati huo huo tayari pale Ukalawa ambapo maji yalikuwa yatoke Image na Image chanzo ni kizuri wanapata maji. Tegemeo langu ataniambia tumejipangaje juu ya kutatua tatizo la maji katika vijiji ambavyo tuna changamoto ya kupata maji.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Kitandelilo pale Mbugani, pana Mradi ambao tayari walishatupa fedha, Mradi ule umekwama, sijajua nini kinachoendelea. Vilevile kwenye kitabu

hapa kuna Mradi ule Mheshimiwa Naibu Waziri uliambiwa ulipokuja pale Kifumbu ulipokuwa unaweka Jiwe la Msingi pale Manga, pana Mkandarasi alikuwa anaendelea, ameingia mitini hatujui tatizo ni nini! Mabomba yako pale, hakuna kinachoendelea mpaka sasa, ingawa hivi karibuni mlitupa fedha bado mkandarasi yule ameingia mitini.

Mheshimiwa Spika, alipokuja Rais kule Lupembe, mkutano alioufanya Lupembe tulimwomba juu ya changamoto ya Mji wa Makambako vilevile kwamba, angalau tungepata kama shilingi milioni mia sita, tuna bwawa letu la asili pale litengenezwe liweze kusaidia tuweke pampu ya kuvuta kuingiza kwenye *line*. Mheshimiwa Rais alituahidi shilingi milioni mia sita, nikuombe kupitia Wizara yako iweze kufuatilia jambo hili ili Rais aweze kukamilisha ahadi ya Wananchi wa Mji wa Makambako.

Mheshimiwa Spika, unajua penye mazuri ndani ya Serikali ni lazima tuseme; hivi ni kweli Serikali hii maji hakuna ni tatizo kubwa katika nchi? Wapinzani wanasema hakuna kitu kabisa ambacho kimefanyika. Ndugu zangu, niseme hapa, tuseme ziko changamoto. Kuna baadhi ya maeneo kama hivi tunaishukuru Serikali, kwa namna ambavyo imekuwa ikijitahidi kutatua tatizo la maji. Sasa Wizara na wao tunawalaumu kwamba hawajatatua matatizo bajeti ya 2014/2015. Wizara hapa wanalalamika Hazina hawajatoa fedha. Hazina wangekuwa wametoa fedha, Wizara tungekuwa na haki ya kuwaambia kwa nini hamjatupa maji wakati bajeti ilitengwa na Hazina wamewapa fedha?

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Serikali, kwa mwaka huu wa fedha, naungana na wenzengu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Chakula na Maji kwamba, ni vizuri sasa Serikali ijikite kumaliza Miradi ile ambayo ilishaanzwa. Kwa mfano, pale Makambako kuna kijiji kimoja kinaitwa Kiumba, kijiji hiki hawajawahi kupata maji tangu kabla ya Uhuru na baada ya uhuru. Wana tatizo kubwa na kuna maji yamepita pale ya Fukulwa lakini hayawezi kupandisha kwenda katika Kijiji hicho cha Kiumba. Tukipata huu Mradi mkubwa ambao Mheshimiwa Waziri tumewahi kuteta ofisini kwako; huu Mradi mkubwa wa zaidi ya shilingi bilioni hamsini na saba ambao tuliombea, ambao usanifu ulifanyika kutoka pale Tagamenda, Mradi huu ukikamilika ndiyo utakamilisha sasa kupeleka maji mpaka Kiumba na vijiji vingine na kadhalika na mji wetu utakuwa salama.

Mheshimiwa Spika, niseme jambo lingine. Visima hivi ambavyo vimekuwa vikichimbwa, niungane na wenzangu, vinachimbwa kwa gharama kubwa, wakati fulani maji hayapatikani, aliyesanifu mtu mwingine. Niungane na wenzangu kwamba, atakayesanifu na kuchimba awe huyo huyo ili atakapochimba mahala ambapo hapana maji, tumwambie wewe si ndiyo ulisema hapa pana maji ili aweze kuchimba mahala pengine. Unakuta fedha wakati fulani zinapotea, kisima kile kimechimbwa kwa hela nyingi na baadaye maji hakuna, halafu tunalipa fedha, anaanza kuchimba tena, kwa hiyo tunapoteza hela nyingi kwa ajili ya kuweka watu wawili, wa kusanifu mtu mwingine na wa kuchimba mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, niseme mimi naunga mkono kwa asilimia mia Hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri. Kubwa, tumtafutie fedha ili aweze kutekeleza miradi iliyoko kwenye bajeti ya 2015/2016. Kabla sijaunga mkono niseme tu, wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha lazima aniambie namna alivyojipanga kutatua tatizo la maji katika Mji wangu wa Makambako na hususan Makambako na Njombe. Maji yako Luhuji pale, hebu tuone namna ambavyo mipango yako ya kutatua tatizo uniambie na hatimaye nitaunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Genzabuke ajiandae na Mheshimiwa Omari Nundu. Wote waliotajwa wapo, msiniletee vibarua vyenu sasa.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana. Nianze kwa jambo moja kubwa, kwanza, kumshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Namshukuru kwa sababu gani?

Namshukuru kwa sababu aliweka ahadi ya kuwezesha Muheza kupata maji kutoka katika chanzo cha Mto Zigi. Ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais ameirudia mara mbili na mwisho ameirudia mwaka 2014 mwezi Aprili na leo katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, japokuwa alipopata nafasi ya kuzungumza hakufikia ukurasa huo kwa kuisoma na kusoma Mradi wa Muheza, lakini upo katika ukurasa wa 97 na 98. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana yeye mwenyewe Profesa Maghembe, Waziri wa Maji, kwa jitihada kubwa ambazo amekuwa akizifanya kwa muda mrefu, kuhakikisha Mradi wa Maji Muheza unatafutiwa wahisani na unajengwa. Pamoja na jitihada ambazo amefanya, najua alikuwa anaelemewa kwa sababu nchi nzima kuna matatizo ya maji. Siyo rahisi kuweza kutekeleza kila kitu kwa asilimia 100, lakini nina imani kwa jitihada anazofanya, sehemu kubwa ya Tanzania Miradi itakamilishwa.

Naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Makala, amekuja Muheza, amejitahidi sana kuhakikisha anawafahamisha na kuwaelimisha watu wa Muheza wawe wavumilivu na wasubiri utekelezaji wa Mradi huu. Nakushukuru kwa kazi kubwa ambayo umeifanya.

Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Fedha, Mtarajiwa, Mwigulu Mchemba, amekuja Muheza na akatuambia kwamba, iwapo mhisani hatapatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Maji Muheza, yeye kama Waziri wa Fedha, katika bajeti hii atasimamia kuhakikisha fedha zinapatikana na kutengwa ili Mradi huo utekelezwe.

Mheshimiwa Spika, leo nachukua nafasi hii ya mwisho kumshukuru mhisani mwenyewe. Huyu ni mhisani kutoka nchi za nje anaitwa Eurofinsa kutoka nchi ya Hispania. Amekuja Muheza, ameangalia na amefanya utafiti yeye mwenyewe, ameridhika. Amekuja amefanya majadiliano na Wizara ya Fedha na Wizara ya Maji, majadiliano yamekwenda vizuri. Nina uhakika amefanya *commitment* ya kuweza kutoa fedha ili Mradi huo utekelezwe.

Jambo moja ambalo linatufurahisha Muheza ni kwamba, laiti kama jambo hilo lisingefanyika, Mradi usingeweza kutekelezwa. Jambo gani? Tathmini ya uharibifu wa mazingira, limefanyika na wamehakikisha Mradi ukijengwa hautaleta madhara yoyote katika mazingira wala hautaathiri upatikanaji wa maji katika Jiji la Tanga, ambao wanategemea kabisa maji yao yote kutoka katika chanzo hicho cha Mto Zigi kutoka katika Wilaya ya Muheza, Tarafa ya Amani.

Naomba niwaambie Watu wa Muheza kwamba, Mradi huu utakapotekelezwa kikamilifu, zile Kata zote katika Mji wa Muheza, zitapata maji kwa uhakika. Mipango ya uboreshaji wa miundombinu ya zamani inaanza mara moja na tuna uhakika vilevile jambo lingine kubwa ni kwamba, kwa sababu Mradi huu ni mkubwa, utaweza kurejesha pia mpango uliokuwepo zamani wa kupeleka maji katika Kata zifuatazo: Kata ya Kilulu ambapo lipo tenki kubwa la miaka na miaka ambalo sasa limekaa kwa muda mrefu bila kupata maji, tutahakikisha linapata maji katika programu hii. Tenki lililopo Mkuzi ambalo pia ni la miaka mingi,

nina uhakika litapata maji. Vilevile katika maeneo ya Kata ya Lusanga, Kibaoni na Kibada wote tutahakikisha watapata maji.

Naomba nichukue nafasi hii kumfahamisha Mheshimiwa Waziri kwamba, fedha alizotoa ili kukarabati kisima cha maji kilichoko katika eneo la Genge Polisi, kisima hicho kimekamilika. Kwa mara ya kwanza katika historia sisi hatukutumia umeme wa *TANESCO,* tumeweka *Solar* na leo maji yanatoka vizuri. Ninapozungumza hapa, upo mpango wa kuboresha eneo hilo na ambao umekwishaanza kwa fedha nyingine ambazo Mheshimiwa Waziri umetusaidia. Upo mpango wa kupeleka maji katika Hospitali yetu Teule Muheza.

Naomba pia nichukue nafasi hii kuwahakikishia Wananchi wa Muheza kuwa, Muheza ni moja kati ya Wilaya za mwanzo kabisa, tumenunua mashine mpya ya kisasa yenye uwezo wa kuchimba visima mpaka mita 150. Kazi imeanza, mimi binafsi nimechukua mashine hiyo na nimeipeleka katika Hospitali yetu moja ya Ubwari, tumechimba kisima na tumepata maji. Nimeichukua tena mashine hiyo nimeipeleka katika Hospitali Teule, tumechimba tumepata maji.

Nataka niwahakikishie Watu wa Hospitali Teule na wagonjwa, katika kipindi hiki ninachozungumza sasa, ile Miradi yote miwili ya kutoka Genge na Mradi wa kisima kilichoko pale pamoja na Ubwari, hospitali hizo zote mbili zitapata maji hata kabla Mradi huu mkubwa wa Maji haujaanza kutekelezwa.

Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi hiyo nzuri ambayo ameifanya, namwombea mwenyezi Mungu amsaidie, Wizara hii ipate fedha za kutosha ili Miradi mingi ya Kitaifa ya matatizo ya maji nchini iweze kukamilishwa.

Ninamshukuru pia Mheshimiwa Rais, alikuja tukafungua Mradi mmoja mkubwa wa Maji. Mradi huu ndiyo ulikuwa wa kupeleka maji Muheza mjini wa kutoka Ubembe – Kwemhosi. Kutokana na ahadi ya Rais, basi tukakubaliana tusubiri ahadi ya Rais ya maji kutoka Zigi na maji kutoka Ubembe tumeyapeleka Muheza Vijijini.

Mheshimiwa Spika, vijiji vingi vimepata maji kutoka barabara hii ya kutoka Ubembe kuelekea Bombani kushoto na kulia kote vijiji vinapata maji ya bomba. Kutoka ubembe kuja Muheza Mjini kote katika maeneo ya Misongeni, Kwasemgaya mpaka Mikwamba, pande zote mbili wanapata maji katika Mradi huo wa Ubembe – Kwemhosi. Hili tunalishukuru sana na ninasema Wilaya ya Muheza ni miongoni mwa Wilaya ambazo zimefanya vizuri katika Mpango wa Maji wa Benki ya Dunia, ukiondoa vijiji vichache ambavyo kwa bahati mbaya visima vilichimbwa lakini maji hayakupatikana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wananchi wa Muheza wawe watulivu, waache kusikiliza maneno ya hao wanaopiga propaganda. Baada ya kusikia mafanikio haya ya maji kupatikana, sasa wanakwenda wanawaambia Watu wa Muheza tutaleta sisi maji, tumejenga sisi Sekondari sijui ya wapi, Kerenge, tumejenga *Muheza High School;* siyo kweli. Katika Mkoa wa Tanga, Muheza ndiyo tunaongoza kwa kuwa na *High School.* Leo ninapozungumza tuna *Muheza High School* na tuna *High School* ya pili ambayo ipo katika Tarafa ya Amani. Naomba kuwaambia Watu wa Muheza wawe watulivu, mimi nipo kama watanihitaji. Nikisema nitoe nafasi nitatoa nafasi, lakini ninahitaji mtu wa uhakika mwenye ukweli atakayeweza kusimamia kazi hizi nilizozifanya, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha hati za mashamba zimefutwa. Kabla sijaondoka wanaanza kuleta watu kuanza kuwagawia mashamba, je, nikiwa sipo? Ndiyo watagawana mashamba yale yote na Miradi ya Maji haitakamilika, Miradi ya Barabara kwenda Amani pia haitakamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii tena kusema ninaunga mkono kwa dhati Hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nina imani kabisa wengine watachukua jukumu hilo. Majukumu ya kuwaadhibu watendaji yako mikononi mwetu katika Halmashauri zetu. Siwezi kuamini kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Maji atakuja kumhukumu Mhandisi wa Maji wa Muheza kwa mambo aliyoyakosea. Chombo chetu kiko pale, ni Baraza la Madiwani na sisi ni Wajumbe. Tuchukue hatua, mtu ambaye hatumuwezi ndani ya Baraza la Madiwani ni Mkurugenzi Mtendaji tu na taratibu zinasema hata yeye ataadhibiwa kwa kutumia Waziri katika Sekta au katika TAMISEMI. Waziri ndiyo anamuweza yule, lakini hawa Watendaji wengine wote wako chini ya Baraza la Madiwani na sisi ni Wajumbe, tuna haki ya kuwaadhibu na kutoa hata mapendekezo ya kuwafukuza kazi kama wanakosea.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapo kwa leo, nawashukuru sana kwa kunisikiliza na Watu wa Muheza msikate tamaa. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana kwa uzoefu wako, tunaendelea.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Aah, hakuna cha taarifa hapa, wewe ulipata nafasi sasa tuwape na wengine. Mheshimiwa Josephine Genzabuke. Tuwape na wengine nafasi sasa.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kupongeza Waziri wa Maji, Profesa Maghembe na Naibu wake, Mheshimiwa Makalla, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Watendaji wote wa Wizara ya Maji, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza na vilevile nawapa pole; ni watendaji wazuri, leo tunawasulubu hapa kwa sababu ya ukosefu wa pesa. Ninaamini kama wangekuwa na pesa za kutosha yasingeweza kuwakuta haya ambayo yanawakuta leo hii.

Namheshimu sana Profesa, Profesa ni jina kubwa sana, lakini ukishaingia kwenye siasa lazima ukubaliane na unayoyasikia. Pole sana lakini kaza buti.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imejaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji; mito mikubwa, mito midogomidogo, maziwa pamoja na bahari. Pamoja na vyanzo vyote hivyo, bado tuna tatizo kubwa la maji. Maji yameendelea kuwa kilio kikubwa, Wananchi wameendelea kuteseka kutokana na ukosefu wa maji. Kwa hiyo, naomba kuishauri Serikali ijipange kwa kutumia vyanzo tulivyonavyo hatimaye baadaye tumalize kabisa tatizo la maji katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni Sera ya Chama cha Mapinduzi kupeleka maji vijijini na mijini. Hii ni Sera yetu ya Chama cha Mapinduzi, tuliainisha kwenye Ilani ya Uchaguzi. Nina imani kabisa kwamba, tukijipanga vizuri tutatekeleza Ilani yetu kwenye baadhi ya maeneo na yale ambayo yatakuwa hayajatekelezeka, basi *Inshallah* Mwenyezi Mungu atatujalia, maeneo ambayo maji yatakuwa hayajaenda, tukijipanga vizuri tutayapeleka.

Mheshimiwa Spika, wanawake wanadhalilika sana kutokana na ukosefu wa maji. Ni kweli watu wengine wanaathirika, lakini wanawake ndiyo waathirika wakubwa sana kwa sababu kazi yoyote wanayofanya inaendana na maji, wakitaka kupika lazima wawe na maji, wakitaka kuosha vyombo lazima wawe na maji, yaani maji yanafanya kazi mbalimbali, ni sawa

na mtu unapokuwa umeishiwa na maji mwilini mwili unadhoofika unapata shida, lakini unapopata maji unapata nguvu mpya.

Mheshimiwa Spika, tujaribu kuangalia ni jinsi gani tunapata maji ili wanawake waondokane na kero hii, wajipange kufanya shughuli zao za kuwaletea maendeleo, kwa sababu muda mwingi sana wanautumia kwenda kutafuta maji, wanatembea umbali mrefu sana kutafuta maji. Wanaporudi kutafuta maji wanakuwa wamechoka na wakati mwingine usiku unakuwa umeingia, wanashindwa kupanga mipango yao ya kufanya shughuli za uzalishaji, matokeo yake wanabaki kuwa maskini. Vifo vingi vimetokea kutokana na ukosefu wa maji na magonjwa mengi yanasabishwa na ukosefu wa maji.

Mheshimiwa Spika, kuna shule za msingi na sekondari ambazo wanafunzi wanapata shida sana na hasa watoto wa kike. Watoto wa kike wanapata shida sana wakati mwingine kutokana na maumbile yao. Mtoto anashindwa kwenda shule kwa muda wa siku saba, kwa sababu hakuna maji anashindwa kuhudhuria masomo shuleni kutokana na maumbile yake kubadilika. Kwa hiyo, akishindwa siku saba kwenda shule, hebu zidisha mara mwaka mzima, lazima anaathirika kwa kiasi fulani kutokana kutokwenda shule kwa ajili ya ukosefu wa maji shuleni. Ninaishauri Serikali ijipange vizuri ili kutatua tatizo la maji, kusudi watoto wa shule na akina mama wanufaike kupitia upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Kasulu ipo Miradi iliyoanzishwa, lakini tangu imeanzishwa haijawahi kukamilika. Ipo Miradi katika Kijiji cha Nyumbigwa, Kasangezi, Nyarugusu na Lungwe Mpya.

Mheshimiwa Spika, Miradi hiyo imeanzishwa lakini kwa bahati mbaya kutokana na ukosefu wa fedha haijakamilika. Namwomba Mheshimiwa Waziri, aone ni jinsi gani anaweza akatusaidia ili tukamilishe Miradi hiyo ambayo imeshaanza lakini bado haijakamilika kutokana na ukosefu wa fedha. Watutafutie fedha watupelekee Kasulu ili kukamilisha Miradi ya MAJI Nyumbigwa, Kasangezi, Nyarugusu na Lungwe Mpya. Naamini watatusaidia.

Juzi nilipouliza swali Mheshimiwa Waziri alisema zilipelekwa shilingi milioni 300 Kasulu. Pamoja na shilingi milioni 300 kupelekwa, lakini kwa bahati mbaya hazikufanya kazi, asikate tamaa atuongezee pesa nyingine tutajipanga sawasawa kuhakikisha pesa hizo zikipelekwa zinafanya kazi ambayo imelengwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali ichimbe visima na mabwawa. Tumeshuhudia wakati mvua zinanyesha maji mengi yanatiririka na yanapotea, lakini tukichimba visima na mabwawa tutahifadhi maji na hayatapotea na hatimaye yatatumika katika shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo cha umwagiliaji.

Kaka yangu Rage anakushukuru kwa ajili ya kupeleka maji Tabora, ameniambia nikushukuru kabla sijakaa, kwa sababu ni jirani yangu na mimi ninapopita kwenda Kigoma huwa napitia Tabora. Tunashukuru kwa maji katika Mji wa Tabora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba Wizara ipeleke pesa Kasulu ili kukamilisha Miradi ambayo haijakamilika ili kuwaondolea kero Wananchi wa Wilaya ya Kasulu na katika vijiji nilivyovitaja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii ili pesa zipatikane tumalize kero ya maji na ili Wanawake wa Wilaya ya Kasulu na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla waifurahie Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Omar Nundu na Mheshimiwa Rachel Mashishanga ajiandae.

MHE. OMAR R. NUNDU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nichangie katika hoja ambayo inajadiliwa.

Awali ya yote, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima, kwa jitihada kubwa ambazo wanazifanya katika kuhakikisha si tu maji yanapatikana kwa sasa, lakini pia kwa kuangalia mbele. Wametupa hapa tafiti mbalimbali zinazotuonyesha tukoje katika hali ya maji. Hivi sasa tuna kilomita za ujazo 125 katika nchi, sasa hizi zinatufaa kwa kiasi gani au tutahitaji nyingi kwa kiasi gani.

Siyo hilo tu, wamekwenda mbali zaidi na kusema sasa hivi kila mtu anapata mita za ujazo 1,952, lakini miaka 20 kutoka sasa mita za ujazo ambazo zitakuwepo ni 883 tu. Kwa hiyo, kuna tatizo kubwa tunaliona huko mbele ya safari tunapokwenda. Ametueleza mipango kadha wa kadha ambayo wanaishughulikia sasa kuonyesha kuwa tukifika huko hatutapata matatizo. Naomba watilie bidii sana suala hilo.

Ukiangalia bajeti kama bajeti, shilingi bilioni 315 kwa maendeleo ya maji hazitoshi na hilo nitaliongelea baadaye kidogo kama muda utaniruhusu. Pamoja na hivyo ninakuja mahali ambapo pananigusa ingawa naangalia suala la maji kwa nchi nzima, Tanga. Tanga katikati ya mji tatizo la maji lilimalizika zamani sana, naishukuru Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya, iliyobaki ilikuwa ni vijijini na tangu mwaka 2010 ninavyomsumbua Mheshimiwa Waziri na amejitahidi kiasi sasa hivi vijiji vingi Miradi ya Maji imeshaanza.

Naibu Waziri alikuja Tanga tukashangiliwa sana watu walivyoona mambo yao yanavyokwenda, lakini tangu ameondoka ule Mradi umekuwa kidogo unasuasua, mpaka sasa Wakandarasi wanadai takribani shilingi milioni 500 ambazo hawajalipwa ili wakamilishe kazi, nilitegemea fedha hizo wangezipata kazi ile iishe.

Siyo vivyo tu, Mradi mzima ulitakiwa umalizike mwaka 2014, bado zimepatikana shilingi bilioni 1.8 tu, zinahitajika shilingi bilioni 2.6. Watu wanaoona kazi zinaendelea na wamepata matumaini makubwa sana ya kuwa sasa maji yanakuja mpaka wengine wanaamua kuchimba mitaro wao wenyewe, wanasubiri kwa hamu kuona kazi hizi zinamalizika.

Kuna mitaa na sasa hivi ni mitaa wala si vijiji tena, kwa sababu Mji wa Tanga wote sasa hivi ni Jiji la Tanga; Tongoni, Mwarongo, Kirare, Mapojoni, Mgwisha, Masiwanishamba, Machui, Ndawoya, Chunguliani, Mpirani, Kibafuta, Naruku na Mleeni, wote hao wameona jitihada zinafanyika na wana matumaini makubwa sana kuwa Miradi hiyo itakamilika. Wanaona mitambo imechimbwa, matenki yanajengwa, vioski vimejengwa, sasa ninachotaka ni kuona maji yanatoka. Wakazi wa Tanga na hasa wa kwenye vilivyokuwa vijiji, wanataka kujua Miradi hii itakamilika lini.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya katika *BRN* Tanga haipo, nimeangalia Wilaya karibu zote zimo lakini Wilaya ya Tanga haipo katika *BRN*. Bajeti inayoombwa hivi sasa ni shilingi milioni 359 tu, fedha hizi ni kidogo sana. Nilisema kule kuna shilingi bilioni 2.6 kwa kazi ambayo inaendelea. Sasa hivi tunapatiwa shilingi milioni 359, utaona wazi kuwa hizi fedha hazitoshi na mbaya zaidi 77% ya fedha hizo tunategemea wahisani. Nafikiri tutoke kwenye mambo ya wahisani, hili suala la maji Bungeni tusilipigie kelele tu, ni suala nyeti na zito na linatakiwa tufanye maamuzi ya dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, nina-*suggest* katika bajeti ya mwaka huu, bajeti ya shilingi bilioni mia nne na kitu mliyowekewa kwa Wizara nzima ni ndogo sana. Tuambiwe Bungeni iwekwe shilingi trilioni moja kwa ajili ya maendeleo ya maji tu. Maji yapewe kipaumbele cha kwanza na kesho tutaongelea umeme, shilingi trilioni moja iwekwe kumaliza matatizo yote ya maji katika vijiji. Tusitegemee watu kutoka nje waje watuwekee maji, watu wa nje waje watusaidie mambo mengine tu. Tuweke Mfuko wa Maji, wawekwe watu imara ambao hawapo pale kukiangusha Chama cha Mapinduzi, waufanye kazi kuhakikisha maji yanapatikana; maana wengine wakipelekewa pesa wanaona ndiyo njia eti ya kukiangusha Chama cha Mapinduzi wapate maneno ya kuja kusema hapa! *(Makofi)*

Ndugu yangu Mheshimiwa Mntangi ameongelea Muheza, sisi ndiyo tunategemea Zigi. Zigi kwa Tanga peke yake, lakini hivi sasa kwa hivyo vijiji tunavyoviongelea na Muheza, maji yale yataonekana machache sana. Tumechimba visima sehemu za Chongoleani. Visima kwa Tanga havifai kuna maji chumvi, lazima tutumie maji ya mto, lakini maji yanamalizika. Kuna teknolojia ya *desalination,* tangu ilipoanza mwaka 1972 mpaka sasa imekuwa ni rahisi sana. Wizara ianze kuangalia huko, tunafanyaje kutumia maji ya bahari pia, tutafute *desalination* ambayo ni rahisi ili Mradi huo utekelezwe maji yapatikane kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hii hoja lakini naomba Bunge tusimamie mwaka huu. Mwaka huu hakutakuwa na maneno mbele ya safari, tutakuwa sote tupo tunatafuta kura, kwa hiyo, hakuna kumsumbua Waziri. Itengwe shilingi trilioni moja, iwekwe na isimamiwe ili kuhakikisha maji yanapatikana sehemu zote Tanzania; hicho kiwe kipaumbele chetu cha kwanza. Shilingi trilioni moja katika zile sijui trilioni 23, *almost 5%* iwekwe kwa ajili ya maji tu, hili ndiyo wazo ambalo nataka Wizara mlichukue. Iwekwe na ipatikane.

Wizara ya Fedha ipo hapa inanisikia, fedha hiyo iwekwe ipatikane, tukate longolongo la maji. Watu wasiwe tena na la kusema kuhusu maji, halafu tuangalie mambo ya umeme. Kama tuna bajeti ya kwetu sisi wenyewe imalizie kazi kwenye Wizara tu, lakini hili ndiyo liwe jukumu ambalo tunalichukua kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa twende kwa Mheshimiwa Rachel Mashishanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Ole Medeye!

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja iliyopo mezani, hoja ya maji.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai. Ukitaka kujua maji ni uhai, tujaribu sisi Wabunge tukae siku saba hatujaoga ndiyo tutakapotambua maji ni uhai, tutatafutana humu ndani!

SPIKA: Tuanze lini sasa? *(Kicheko)*

MHE. RACHEL M. ROBERT: Tuanze leo! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba nijikite moja kwa moja kwenye mchango wangu ingawa nitaenda kwenye maeneo machache sana. Naomba nizungumzie suala la kuongeza bei ya maji hasa kwa Mamlaka ya Maji ya *SHUWASA* pamoja na *KASHUWASA*.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2013/2014 *SHUWASA* iliidhinishiwa ongezeko la bei kwa watumiaji wake pamoja na *KASHUWASA* na mwaka 2015/2016 tayari imeshaomba tena ongezeko la bei kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, mimi najiuliza; *KASHUWASA* sasa hivi anauza maji shilingi 605 *unit* anamuuzia *SHUWASA* kwa bei ya shilingi 750 mpaka shilingi 900 inategemea na *unit*. *SHUWASA* sasa hivi ameomba kuongezewa bei kutoka shilingi 700 mpaka shilingi 1,280. Nashindwa kuelewa kwa sababu najua *SHUWASA* inatoa huduma, siyo mamlaka ya biashara ni mamlaka ya kutoa huduma kwa Wananchi.

Sasa nauliza ni kwa nini inataka kufanya biashara kwa maana inataka kupata faida zaidi hata ya *KASHUWASA* kwa sababu *KASHUWASA* ndiyo anayetoa maji Ziwa Victoria na kuyasambaza kwa *SHUWASA*?

Mheshimiwa Spika, nashangaa kwa nini anataka atengeneze faida kubwa na mwisho wa siku Mwananchi wa mwisho ndiye anayeumia na hizi bei. Kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie upya suala hili.

Kama kuna uwezekano wa Serikali kuichukua *KASHUWASA* kama Serikali, iongezewe ruzuku na Serikali kwa sababu ni Mradi wa Serikali na ni Mradi mkubwa sana, basi Serikali ichukue kila kitu kama ni vipuri au mafuta na mishahara, Serikali ichukue ili ibaki *KASHUWASA* kusambaza tu maji na matokeo yake isambazie kwenye mamlaka na mwisho wa siku mtumiaji wa mwisho apate nafuu. Hii ni kwa sababu *SHUWASA* yenyewe mtandao wake bado mdogo sana ndiyo maana mzigo unakuwa mkubwa sana kwa watumiaji wachache ambao wanatumia.

Hata hivyo, naiomba *SHUWASA* iongeze mtandao kwa sababu ukiangalia ndani ya Manispaa ya Shinyanga, zipo Kata 17 lakini hizo Kata ni maeneo machache sana ambayo yamepata maji. Sasa wakiongeza mtandao nafikiri huu mzigo kwa watumiaji wa sasa utapungua na hili suala la kuongeza bei kila mwaka; kila mwaka wa fedha wao wanaongeza bei, sidhani kama ni sahihi.

Naomba kama kweli huu Mradi umekuja kuwakomboa watu wa Ziwa Victoria kwa maana ya Mkoa wa Shinyanga na maeneo mengine ya jirani, basi Serikali ibebe gharama zake. Haiwezekani mamlaka mbili zikafanye kazi katika sehemu moja, yaani *KASHUWASA* anataka fedha na *SHUWASA* anataka fedha, Kahama naye anataka fedha, mimi sidhani kama ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka naomba niende kwenye Mradi wa Vijiji Kumi. Mheshimiwa Azza amezungumza na mimi nataka nizungumzie kwenye Manispaa. Vipo Vijiji kwa mfano Ndembezi, kwenye kitabu amesema ni vituo 30, lakini hakuna hata kituo kimoja kwenye hiki Kijiji, kwa maana kwamba walikuja hawa Mabwana wakawaita Viongozi wa Kijiji wakakaa nao wakawaambia tutakuja baadaye, lakini jamaa wamesepa na hawajarudi mpaka sasa, lakini Kitabu cha Waziri kinasema kuna vituo 30! Mbali na hilo, kuna Kijiji kinaitwa Mwagala, nako walienda kufanya hivyohivyo, hawajaonekana mpaka leo lakini tunaandikiwa kwenye vitabu ni vijiji 30.

Mwamagunguli wameandika 42 lakini vipo kumi tu ndiyo vinavyofanya kazi. Bugimbagwe wameandika 24, lakini vipo vinne tu ndiyo vinavyofanya kazi. Mwamashele wameandika 30, lakini vipo vinane tu na hapa sasa ndiyo kuna shida, hivi vinane vyenyewe wameshimba sehemu ambayo maji ni machungu sana, Wananchi hawawezi kuyatumia na wanaambiwa wachangie shilingi 5,000; yaani kila kaya itoe shilingi 5,000 sijajua ni ya nini!

Tunaenda kwenye Kijiji kimoja kiko Kata ya Kolandoto kinaitwa Galamu, kule kila kaya wameambiwa walipe shilingi 30,000. Maana ya kutoa fedha hiyo eti waone uchungu na ule Mradi. Hivi kweli tuna nia ya kuwasaidia hawa Watanzania? Kwa nini tumewapelekea sasa hayo maji?

Mheshimiwa Spika, kaya moja kutoa shilingi 30,000 ni nyingi sana. Wananchi wetu tunawajua jinsi walivyo maskini. Sidhani kama mnawatendea haki hawa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni huu Mradi wa Maji wa kupeleka maji Kolandoto, Kishapu, Mwadui na Maganzo. Tunaishukuru Serikali lakini wanachokifanya sasa hivi siyo kizuri. Kutoka Ihapa kwenda kupita Mwamalili tayari mashamba yaliishavurugwa, Wananchi wamevurugiwa mashamba yao. Bomba limepita bila Serikali ya Kijiji kukaa na Wananchi, matokeo yake mazao yameharibiwa na hakuna fidia waliyolipwa na bomba linaendelea kupita.

Mheshimiwa Spika, Bunge lililopita Waziri alizungumza kuhusu Hospitali. Ninakumbuka siku hiyo nilimuuliza Mheshimiwa Waziri swali la nyongeza akanijibu Hospitali ya Kolandoto kufikia mwezi Agosti itakuwa imepata maji, lakini mpaka sasa hivi hakuna dalili zozote za mabomba kwenda wala nini. Sasa ninataka niseme kwamba, mkituacha mnatupa *credits* wenzenu, mnatupa cha kuzungumza. Msipopeleka maji mpaka mwezi Agosti, ninajua mwezi Septemba tunaingia kwenye kampeni, mimi nitalizungumza tu wala sitaogopa. Nitasema mmedanganya, ile hospitali ni kubwa sana na watu ni wengi kwenye ule mji tunaomba maji yaende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumzie kuhusu vijiji ambavyo viko ndani ya kilomita 12 hasa kwa Jimbo la Msalala; wamepitia na hili bomba, kuna baadhi ya vijiji vimepata maji na vingine havijapata. Ninaomba sasa Serikali wakati inatoa majibu, iniambie ni lini sasa hivi vijiji ambavyo vimebaki vitapata haya kwa sababu wamekuwa wakiyaona tu yanapita palepale.

Mheshimiwa spika, suala lingine ni Wilaya ya Ushetu. Hii wilaya ni mpya, lakini sijaona mkakati wowote wa Wizara au Serikali kupeleka maji kwenye hii Wilaya. Wananchi wanahangaika na kupata shida sana. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iangalie itawasaidiaje hawa Wananchi ili waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ziwa Victoria ni mkubwa sana na gharama zake za uendeshaji ni kubwa mno. Sasa ninaomba Serikali ijikite ihakikishe inasambaza maji katika Wilaya zote na Kata zote ambazo ziko Mkoa wa Shinyanga halafu ndiyo itoke kwenda sehemu nyingine, kwa sababu maji yameishia Manispaa tu, Wilaya zingine zote bado maji hayajafika. Ninaomba Serikali iliangalie hilo kwa umakini sana kuhakikisha huu Mradi unapanuka na matokeo yake utasaidia kupunguza gharama za uendeshaji wa hili Shirika la *KASHUWASA*.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba niseme kwamba, kabla Mheshimiwa Waziri hajasimama, ajipange vizuri kabisa kunijibu hizi hoja kwamba, kwa nini SHUWASA wanapandisha maji kila siku? Sielewi kama ni kuwakomoa Watu wa Shinyanga au vipi, lakini ninaomba aje na majibu ni kwa nini hizi bei zimekuwa zikipanda kila mara?

Mheshimiwa Spika, lingine, hawa Wanakijiji wa Mwamalili watalipwa lini fidia ya mazao yao ambayo yameharibiwa wakati bomba la maji linapita kwenda Kishapu? Hospitali ya Kolandoto, Mheshimiwa Waziri aje azungumze ni lini haya maji yataenda kwenye hiyo hospitali, kwa sababu ni kubwa na inategemewa sana.

Mheshimiwa Spika, mimi ya kwangu yalikuwa hayo tu kwa leo, kwa sababu mengi amezungumza mwenzangu Mheshimiwa Azza, ninaomba niishie hapo. *(Makofi)*

SPIKA: Haya ahsante. Sasa ninaomba nimwite Mheshimiwa Dkt. Goodluck Ole Medeye, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Laizer, Mheshimiwa Anastazia Wambura na Mheshimiwa Kafulila.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ninaomba nianze kwa kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwako wewe Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote na familia ya marehemu Eugine Mwaiposa, kwa msiba mkubwa huu ambao umetokea juzi.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ninawapa pole sana Wananchi wa Jimbo langu la Arumeru Magharibi, kwa kero kubwa ya maji ambayo inawapata, kiasi kwamba, pamoja na kuwa ni Wilaya ya siku sana nyingi hapa nchini, tokea Uhuru bado wanaendelea kutembea umbali mrefu sana wakitafuta maji.

Mwaka 2005 Mheshimiwa Rais aliahidi kero hiyo ingeondoka. Mwaka 2010 alipofika eneo la Ngaramtoni ambako ndiko alipofanyia mkutano wake, Wanawake walikuja wakiwa na ndoo kichwani zisizokuwa na maji na kumwonesha ya kwamba, wana kiu ya maji na ndipo alipotoa agizo uandaliwe mpango ambao ungetekelezwa na Serikali yake ili anapoondoka madarakani mwaka huu, aondoke kero hiyo ikiwa imeisha. Kwa bahati na kwa masikitiko makubwa, kero hiyo ipo kama ilivyokuwa mwaka 2010. Nimejitahidi kufuatilia sana, nimetumia nguvu kubwa ndani kutembea kwenye Ofisi za Waheshimiwa Mawaziri na Watendaji, lakini hadi leo kwa bahati mbaya hatujafanikiwa kuiondoa kero hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, ninaomba nitamke tu kwamba, nitasikitika, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri, nitambua juhudi zake anazofanya na pia ninampongeza Naibu Waziri kwa juhudi wanazofanya, lakini kwa bahati mbaya inaelekea Serikali haijakaa pamoja na kwa msingi huo jitihada zao hazijaweza kuzaa matunda yaliyotarajiwa. Kwa sababu hiyo ninatamka wazi kwamba, kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha au Waziri Mkuu, hatafika hapa na kutoa kauli kwamba, fedha za Sekta ya Maji za kutekeleza Miradi ya Maendeleo zitatoka wiki ijayo, sitaunga mkono bajeti hii, bajeti ya Wizara ya Fedha na Bajeti ya Serikali. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote tuungane bila kujali itikadi katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba, kuna Miradi iliyoanza mwaka 2007 ya Vijiji Kumi, ilipofika mwaka juzi ikabadilishwa jina ikaitwa *BRN*. Pamoja na kubadilishwa jina hakuna matokeo yoyote chanya yaliyoonekana hadi sasa hivi. Ningependa tu nimjulishe Mheshimiwa Waziri kwamba, nimeona orodha katika kitabu hiki cha hotuba yake kuwa kuna vijiji viwili ambavyo Miradi yao imekamilika. Ninaomba nimjulishe kwamba, kuna Mradi mmoja ambao haujakamilika, ule wa Kijiji cha Ulwegeruno, ni vizuri afuatilie ili atusaidie uweze kukamilika. Sasa hivi kilichofanyika ni kwamba, maji ya Kijiji cha Ilikirebi ndiyo yanagawanywa katika vijiji hivyo viwili. Tunaomba Mheshimiwa Waziri atupe fedha ili ule Mradi mwingine uweze kukamilika mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, tunayo Miradi mingine ya Vijiji; tuna Mradi wa Ngaramtoni. Huu ndiyo mji mdogo na ndiyo Makao Makuu ya Wilaya yetu, lakini hauna maji. Mradi wa Likamba, Mradi wa Lowavilukun, Mradi wa Nduruma, MIradi yote ile haijakamilika, imesimama kabisa. Ule wa Nduruma kidogo unaendelea kutokana na msaada wa Mheshimiwa Naibu Waziri alipotutembelea alitusaidia kupata fedha kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wenyewe unakimbia sana, ninaomba nifanye hivi; kwanza, nimeangalia Kitabu cha Maendeleo, kina fedha nyingi zimewekwa humo ndani. Ningeomba fedha zilizotengwa kwenye kifungu 1003, kasma 3436 - *Monitoring and Coordination*

of WSDP ziondolewe pale zipelekwe kwenye Miradi. *Monitoring and Coordination* Idara ya Mipango inafanya nini kwa shililingi bilioni 11? Hizo fedha ziondolewe pale.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Waziri aliomba shilingi milioni 100 za kuanzisha Mfuko wa Maji. Huo Mfuko uko wapi? Humu kwenye hotuba yake haujatajwa na wala hatujui kama umeanza ama haujaanza. Tungetaka kujua. Tulishauri kwamba, Mfuko huo uanzishe tozo maalum itakayochangiwa na watumiaji wakubwa wa maji na wale wa kati ili kuchangia Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, kuna fedha zinatumika hapa visivyo. Hii ni kwamba, pale Dar es Salaam kuna taasisi mbili; *DAWASA* na *DAWASCO*. *DAWASA* inafanya nini? *DAWASA* ivunjwe na majukumu yake yahamishiwe *DAWASCO;* kwa sababu tunatumia fedha nyingi bure kufanya kazi ambazo zingeweza kufanywa na taasisi moja. Kwa hiyo, mimi ninashauri *DAWASA* ivunjwe.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu ya Arumeru, kwa maana ya Arumeru Mashariki na Magharibi, hakuna Mradi wowote mahususi kama ambavyo wilaya nyingine zina Miradi mahususi ambayo imetajwa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Ningeomba Waziri atuambie ule Mradi wa Maji kutoka Mount Meru ulikuwa unaenda Longido ambao ungetoa maji kwa Kata za Oldonyo Sambu, Olkokala na Oldonyogwasi umeishia wapi? Tunaomba Mradi ule uwekwe kwenye mpango wa mwaka huu unaokuja na utekelezwe ili Wananchi wa eneo hilo wapate maji.

Mheshimiwa Spika, ombi lingine, tuliwahi kumwomba Mheshimiwa Waziri, tukamwandikia na tulimpelekea gharama, atusaidie kuchimba malambo kwenye Kata za Oldonyo Sambu, Mwandeti, Musa, Kisongo na Bwawani ili walau kupunguza kero tuliyonayo hivi sasa. Mifugo ikipata maji walau itakuwa imetupunguzia kero ambayo sasa hivi tunapata, kwa sababu hakuna maji na malisho na hivyo mifugo inakufa wakati wa kiangazi. Wafugaji wana raha kwa miezi mitatu tu kwa mwaka, baada ya masika kumalizika wanaanza kusumbuka kutafuta maji. Ningeomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie katika hili.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maeneo ambayo nilitaka nichangie, lakini pia ninashukuru kwamba, wamepanga Mradi Maalum kwa ajili ya Jiji la Arusha. Mradi huo kwa kuwa maji yanatoka Wilaya ya Arumeru, ihakikishwe yanatumika kwa wilaya zote mbili; wilaya ya Arumeru na Wilaya ya Arusha. Msije mkawatia Wananchi wa Arumeru hasira wakaanza kuhujumu Miradi ya Maji, kwa sababu asilimia 90 ya maji yanayotumika katika Jiji la Arusha yanatoka katika Wilaya ya Arumeru. Ningeomba sana maji hayo tugawane kwa sababu hayo ndiyo madini tuliyonayo sisi, hatuna madini mengine zaidi ya maji.

Mheshimiwa Spika, ili nisigongewe kengele, ninaomba nimalizie kwa kusema ninasikitika nitaunga bajeti hii nitaunga mkono baada ya kuambiwa kwamba, fedha zitatolewa na Serikali na kwa msingi huo miradi ambayo imekwama katika wilaya yangu iweze kutekelezwa Wananchi wapate maji. Ninawapa pole Wananchi wa Arumeru, ninawashukuru sana kwa uvumilivu wao, ninaomba tuendelee kushikamana, nipo bado na nitaendelea kuwepo na kwa ridhaa yenu, nitaendelea kuwawakilisha katika Bunge hili mkipenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Prof. Msolla kwanza, atafuatia Mheshimiwa Michale Laizer!

MHE. PROF. PETER M. MSOLLA: Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii nichangie hoja iliyo mbele yetu. Kwanza, ninaomba nieleze kwamba, mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoshughulikia Kilimo, Mifugo na Maji.

Niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote, kwa kufanya kazi nzuri sana licha ya kupewa fedha kidogo sana.

Tumesikia kutoka asubuhi kwamba, kwa upande wa fedha za maendeleo, Wizara hii kufikia mwezi Machi, ilikuwa imepata asilimia 26 tu ya fedha zote za maendeleo. Ukiangalia kutoka kwa Wadau wetu wa Maendeleo nao walikuwa wametoa asilimia 27 tu ya fedha zote ambazo zilikuwa zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, nimeshangazwa na watu kujadili jambo hili na kuwalenga Waziri na Naibu Waziri kwamba hawafai. Mimi ninasema katika hali ya namna hii, hata yeyote aliyeko kule Upinzani angepewa shughuli hii na kupewa *resources* ndogo kama hizi na yeye angekuwa katika hali kama hii.

Mheshimiwa Spika, nikumbushe tu kwamba, katika Mwaka wa fedha 2013/14, Bunge lilikataa hapa kupitisha bajeti ya maji, tukiomba jumla ya shilingi bilioni 184 za nyongeza. Fedha zile hazikutolewa na zile ambazo zilikuwa zimepitishwa nazo hazikutolewa zote. Mwaka jana katika mwaka huu wa fedha 2014/15, Bunge tena lilikataa kupitisha bajeti ya Wizara hii likiomba nyongeza ya shilingi bilioni 80, fedha zile hazikutolewa mpaka leo. Ile ambayo ilikuwa imepitishwa ndiyo hiyo asilimia 26 tu ambayo imepatikana. Kwa hiyo, siyo Waziri wala Naibu Waziri, tatizo liko kwenye Hazina.

Ndugu zangu kutokana na tatizo hilo Miradi mingi imesimama, Wakandarasi wengi wamesimama. Ukija katika Mpango wa Vijiji Kumi, Mradi ambao ulianza mwaka 2007, vijiji vingi bado havijapata maji. Nikitoa mfano katika Wilaya yangu ya Kilolo ni kwamba, Miradi iliyokamilika ni mitatu tu katika Vijiji Kumi. Iko Kivitono, Kipaduka na Ikuka. Vijiji vingine kama vile Mwatasi, Ng'uruwe, Lulanzi, Ihimbo, Ipalamwe, vyote hivyo viko katikati na mambo mengi hayajatekelezwa. Ninafikiri suluhisho ni Serikali kujipanga, tusiwategemee sana Wahisani. Tutenge fedha za kutosha za ndani kama alivyozungumza Mheshimiwa Dkt. Omari Nundu, ili kusudi tatizo la maji liweze kumalizika na hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Hazina nimeambiwa wao wanatoa fedha zaidi kwenye sekta za uzalishaji. Katika sekta zile za uzalishaji, Wizara ya Maji haimo na ndiyo maana wanakuwa na kigugumizi hata kutoa fedha. Mimi ninasema Wizara ya Maji ni sekta ya uzalishaji, inazalisha kwenye Kilimo kwa shughuli ya umwagiliaji. Inazalisha kwenye viwanda hata ukitengeneza sementi ni uzalishaji. Ukienda kwenye viwanda mbalimbali ni uzalishaji. Kwa hiyo, ili kuweza kupata maendeleo na kupata maji safi na salama, ninashauri Hazina nayo ione umuhimu wa Wizara hii, lakini zaidi tutenge fedha za kutosha ili Wizara hii iweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengine ambayo vilevile nayo yametakiwa kutekelezwa kwa umakini. Pamoja na ufinyu wa bajeti, ninapenda kuishukuru Wizara kwa kuelewa umuhimu wa maji katika Mji Mdogo wa Ilula, Wilayani Kilolo. Tarehe 29 Novemba 2013, nilimwomba Waziri aje ajionee mwenyewe na baada kuona aliona umuhimu wa kuutekeleza Mradi wa Ilula ili maji mengi yaweze kupatikana. Ninashukuru kwamba, mchakato huo unaendelea na sasa angalau kuna ahueni, watu wanapata maji ingawa ni kwa mgao.

Mheshimiwa Spika, ninataka kueleza kwamba, tarehe 2 Juni 2015, humu humu Bungeni, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Iringa, Mheshimiwa Ritta Kabati alisema, Ilula toka Mradi ulivyozinduliwa na aliyekuwa Makamu wa Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein, watu hawajawahi kupata maji katika sehemu ya Ilala.

Ninataka kulieleza Bunge na Mheshimiwa Mbunge huyo kwamba, anayosema ayafanyie utafiti kwanza kabla ya kutamka mbele ya hadhara, kwa sababu kule maji yanatoka na watu wanajua wanapata maji yale kwa zamu. Kwa hiyo, kutamka jambo Bungeni ni vizuri ukalifanyia kazi kabla ya kulitamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni tatizo la utoaji maji taka katika Jiji la Dar es Salaam. Katika Jiji la Dar es Salaam ambalo linakua kwa haraka na karibu litaungana na Bagamoyo, Kibaha na linakwenda Mkuranga, idadi ya watu kwa Jiji hili sasa hivi inafikia milioni 5, lakini watu wanaopata huduma ya kutoa maji taka ni asilimia kumi tu.

Mheshimiwa Spika, nimeshukuru Waziri amelieleza hili katika hotuba yake, lakini inafaa iwekwe mipango mikakati mizuri ili kadiri Jiji linavyopanuka, Wananchi wa Dar es Salaam waweze kupata huduma hii ambayo ni muhimu sana kwa mazingira yao safi.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimekuwa nikijiuliza; tunakaa hapa karibu miezi miwili kujadili Bajeti ya Serikali, lakini hatimaye kinachopatikana ni kiduchu! Bajeti ya Serikali inaanzia kwenye Halmashauri na Wizara na wanapewa *ceiling* kwamba, hapa ndiyo mwisho wenu. *Ceiling* hii inatolewa na Serikali. Tunakuja tunakaa hapa tunajadili, tunabishana na hata kile kidogo tunachokubaliana hakipatikani! Hivi kuna sababu ya kutumia fedha nyingi hivyo kukaa hapa kwa miezi miwili kumbe Serikali inajua ni nini ambacho ingeweza kutoa? *(Makofi)*

Mwaka jana tulikuwa na bajeti ya trilioni 19, mwaka huu trilioni 22. Kuna maajabu gani ambayo fedha hiyo inaweza kupatikana? Kwa nini tusingeambiwa *ceiling* ambazo ni muhimu ili kila Wizara ijipange hapa ije itueleze tu na sisi tufanye *rubber stamp* tuendelee na shughuli kuliko kuwa kuwapa watu matumaini huko vijijini wanasikia kumbe hatimaye Miradi hii haitekelezwi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kusema hayo yote, nitamke kwamba, ninaunga mkono hoja hii, kwa sababu nilichambua na Kamati yangu. Sasa pamoja na na haya yote ambayo ninasema, tunataka kuboresha hiyo bajeti, siyo kwamba tunaipinga.

Ninaunga mkono na ninashukuru kwa kupewa nafasi hii ya kuchangia. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Michael Laizer, atafuatiwa na Mheshimiwa Anastazia Wambura!

MHE. MICHAEL L. LAIZER: Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Wizara hii ya Maji. Niseme tu kwamba, Jimbo la Longido ni miongoni mwa Majimbo ambayo ni makame sana katika nchi yetu. Longido inastahili ingekuwa na maji kwa ajili ya kuokoa Wananchi na Mifugo yao. Niseme tu kwamba, maji ni muhimu kuliko chochote; maji ni uhai, maji ni chakula, maji ni afya, maji ni usafi.

Mheshimiwa Spika, Longido ina Miradi ya *World Bank* Vijiji Kumi. Tumeanza mwaka 2007 kama alivyosema Profesa Msolla na mpaka leo hatuna Mradi hata mmoja katika vijiji kumi ambao umekamilika.

Ninashukuru kuona katika bajeti kwamba, Mradi wa Maji kutoka Kilimanjaro kuja Mji wa Longido umetengewa shilingi bilioni mbili. Ninaomba hizi fedha zitoke haraka kwa sababu katika Mji wa Longido ambao unapanuka sana, kuna tatizo la maji kubwa sana pamoja na vijiji vinavyozunguka Longido, Olbomba, Ranchi, Oldebesi pamoja na Kijiji cha Engikareti, vyote vinategemea maji kutoka Mradi huo kutoka Mlima Kilimanajaro.

Mheshimiwa Spika, katika Miradi ya Vijiji Kumi wakandarasi ndiyo wanachelewesha Mradi huu. Pamoja na fedha kuchelewa, lakini zile fedha chache walizopewa wametengeneza Miradi ambayo iko chini ya kiwango na hakuna usimamizi. Tuna Halmashauri na hao watu wetu wa Halmashauri ndiyo wanasimamia Miradi hii, ninadhani tuna mfumo ambao hawa wataalamu wanatuchezea katika Miradi hii, kwa sababu Wizara ya Maji wanatoa pesa lakini hawawezi kusimamia Wataalamu walioko huko kawa sabbu wako chini ya Halmashauri. Halmashauri nao wako TAMISEMI, TAMISEMI limekuwa kubwa imekusanyiwa kila Wizara mpaka wameshindwa hata kujua wafanye nini; maji ni huko huko, afya ni huko huko, elimu ni huko huko, limekuwa lidudu likubwa ambalo wamejisahau hawawezi hata kufanya kazi. Huo ni mfumo mbaya sana ambao ninaona pesa zinazama huko. *(Makofi)*

Jambo lingine, ningependa kumpongeza Naibu Waziri wa Maji; tungekuwa na Mawaziri kama yeye tungepiga hatua. Waziri huyu alikwenda mpaka Mlima Gilai, ametembea kilomita 14 kupanda Mlima, akaenda mpaka kwenye chanzo cha maji ambacho ni kijiji kimoja kati ya Vijiji vya *World Bank* kuangalia Mradi huo, lakini ninasikitika mpaka leo fedha hazijaenda kwenye Mradi huo ambao alienda kuukagua. Mheshimiwa Naibu Waziri siyo kosa lako ni ufinyu wa bajeti. Kama alivyosema Profesa Msolla, tunataka leo tuulize bilioni 80 tulizowapa Wizara hii katika bajeti iliyopita kwa nini hazikutoka? Ninaomba hilo baadaye Serikali itujibu.

Jambo lingine ni suala la mabwawa, sikuona katika bajeti bwawa ambalo limepangiwa Wilaya ya Longido na mnajua ni Wilaya kame, Wilaya ya Wafugaji, bila kuwa na mabwawa mifugo haiwezi kuishi katika maeneo yale. Sikuona hata bwawa moja ambalo mmetupangia na ndiyo maana juzi nilisema katika Wizara ya Mifugo, tunaambiwa katika Wizara ya Mifugo kwamba mabwawa yako chini ya Wizara ya Maji, lakini kwenye Wizara ya Maji sikuona mabwawa tuliyopangiwa huko Longido. Napenda tupate majibu hayo mabwawa yako wapi ambayo tunayategemea katika Wilaya yetu ya Longido mifugo inategemea mabwawa ya maji?

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, Naibu Waziri Dkt. Mahanga, alipokuja Longido aliahidi mabwawa matatu; bwawa katika Kijiji cha Olpomba, Matale na Lang'ata Davashi; hizo hazikutoka mpaka leo. Mheshimiwa Waziri kwa kuwa Naibu Waziri alileta taarifa hiyo na fedha chache sana zimetoka katika mabwawa yale, ninaomba mkamilishe utoaji wa hizo fedha ili mifugo iweze kupata maji tusihamehame tena kwenda katika maeneo mengine na tukihamia maeneo mengine mnaanza kusema sisi ni wahamiaji haramu. Ninaomba katika bajeti hii tutengewe na sisi bwawa katika Wilaya ya Longido.

Nipende kusema kwamba, Ukaguzi katika Miradi ya *World Bank* haufanyiki, ingekuwa inafanyika na bahati mbaya sana katika mahesabu ya ukaguzi wa CAG, huwezi kuona Miradi hii ya *World Bank*. Tunaomba Miradi ya *World Bank* ifanyiwe ukaguzi nchi nzima, kwa sababu hapo ndipo mtaona wizi ulipo. Miradi ya *World Bank* ni wizi mtupu, tunaomba ukaguzi ufanyike nchi nzima, kila Mbunge akisimama hapa anakosoa Miradi hiyo, hakuna kilichofanyika mpaka sasa bado Wananchi hawajapata maji, fedha zimeliwa Miradi iko chini ya kiwango. Ninaomba sana Serikali ifanye ukaguzi kwa hizi fedha za *World Bank* katika vijiji vyote, kwa sababu hakuna fedha zinazoibiwa kama hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Anastazia Wambura, atafuatiwa na Mheshimiwa David Kafulila!

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia jioni hii ya leo. Kwanza, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Wizara kwa Hotuba nzuri na kwa kazi nzuri ambayo inajionyesha wazi. Ukiangalia bajeti ya Wizara hii ambayo ni zaidi ya shilingi bilioni 400, utaona kuwa zaidi ya asilimia 93 ni fedha za maendeleo; kwa hiyo, ni hatua nzuri sana.

Kati ya fedha hizo, asilimia 74 kama tulivyoambiwa ni fedha za ndani, inatia moyo na ninaomba Wizara iendelee na moyo huu na kazi hii nzuri, wakati mwingine tena itenge fedha nyingi za maendeleo ya maji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja hii kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Mtwara ipo baadhi ya Miradi ambayo imekamilika, labda niitaje michache; kuna Lwelu, Naumbu, Maramba, Matogolo, Likolombwe, Mbwinji na mingine. Wananchi wa maeneo haya wanashukuru sana kwa jitihada za Serikali kuwaletea maji katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ipo Miradi mingine pia ambayo ingeweza kukamilika kwa mujibu wa Wataalamu wa Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Mtwara, wanasema ingekamilika kufikia Juni, lakini kuna tatizo la uhaba wa Fedha. Labda nianzie tu Mtwara Vijijini, wao walikuwa wanahitaji shilingi bilioni mbili ili waweze kukamilisha Miradi hiyo. Cha ajabu walichopatiwa kimaandishi ni shilingi milioni 198 tu, lakini hata hivyo ambazo zimeingia kwenye akaunti ni shilingi milioni 98. Kwa hiyo, wanaulizia hiyo shilingi milioni 100 iko wapi. Kimsingi, walichokuwa wanahitaji ni hizo bilioni mbili zikamilike ili kusudi angalau kufikia Juni wangekuwa wamefikia angalau asilimia 74 ya upatikanaji wa maji vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuna Mradi mmoja wa Chihonga ambao umekamilika kabisa. Mradi ule ni wa shilingi bilioni moja, mkandarasi bado anadai shilingi milioni 700 na alicholipwa mpaka tarehe 22 Aprili ni shilingi milioni 300. Kwa hiyo, Wananchi wale hawapati maji, wanaishi katika mazingira magumu sana na wanaomba sana Serikali ilipe hizo fedha ili waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji kwa ujumla katika Mkoa wa Mtwara ni asilimia 40 Vijijini. Kati ya asilimia hizo 40 utaona asilimia 27 hadi 29 ni Newala. Kwa hiyo, Wilaya ya Newala inaongoza kwa uhaba wa maji katika Mkoa wa Mtwara. Hata hivyo, ukisoma vizuri Hotuba utaona kuna zaidi ya shilingi bilioni 60, ambazo zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa Mradi wa Makonde.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali ya CCM, kwa kutenga fedha hizi hasa kwa kuzingatia yale maeneo ambayo yana matatizo makubwa. Kimsingi, kutenga fedha ni kitu tofauti na kuzitoa ni jambo lingine. Kwa hiyo, ninachoomba fedha hizi zitolewe ili Mradi huu wa Makonde ukarabatiwe. Huu Mradi unahitaji ukarabati kwa sababu ni wa zamani, ni wa tangu mwaka 1953, watu wameongezeka sana na ninaomba fedha hii itolewe haraka sana ili kuwanusuru Wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kuna Mradi pia katika Tarafa ya Chilangala, kuna pampu moja ya Mtongwele imeharibika, Wananchi hawana maji pale wanahangaika. Tatizo ni hilo la pampu, ninaiomba Serikali inunue pampu haraka sana, kwa sababu hawa wana wajibu wa kutunza Chanzo cha Maji cha Mbwinji, ambacho maji yake yanaenda Masasi na Nachingwea. Tuwatie moyo na wao kwa kuwapatia maji ili waweze kutunza Chanzo cha Maji cha Mradi wa Mbwinji.

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Kitangali ina matatizo makubwa ya maji lakini ina chanzo cha maji cha Mitema; maji yanakwenda Mtwara Vijijini na yanakwenda Tandahimba. Maji yao hayawatoshi kwa sababu watu wameongezeka na hata ukienda katika kituo chao cha afya utakuta kuna tatizo kubwa la maji. Ninaomba Serikali iwatazame hawa kwa jicho la huruma. *(Makofi)*

Sitakuwa na mengi, nimalizie tu kwa kusema, nirejee Maandiko Matakatifu kwamba, Mwenyezi Mungu alipoumba ulimwengu alianza kwanza kuumba maji na akaifunika Dunia kwa asilimia 75 ya maji. Baada ya kuumba maji na viumbe vingine vyote akasema tumuumbe mtu kwa sura na mfano wetu.

Sasa ni ombi kwa Waheshimiwa Wabunge, niwaunge mkono Mheshimiwa Profesa Msolla na Mheshimiwa Omari Nundu, ambao walisema tuipe kipaumbele Sekta ya Maji. Waheshimiwa Wabunge, tukubali kuumbika kwa sura na mfano wa Mwenyezi Mungu, wakati mwingine tunapopanga mipango yetu tuweke kipaumbele katika Sekta ya Maji. Sidhani kama tutakubaliana sote kwa pamoja kwamba, Sekta hi iwe ya kipaumbele halafu Serikali ikakataa, sidhani kama itakuwa na ubavu huu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Waheshimiwa Wabunge, tuungane wakati mwingine Sekta ya Maji iwekewe kipaumbele. Ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kafulila, atafuatiwa na Mheshimiwa Kidawa Saleh! Mbona una haraka; haya endelea!

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nina haraka kwa sababu muda ni mfupi na tatizo ni kubwa na kimsingi inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Spika, siwezi kusema kuwa ni tatizo la Waziri peke yake katika jambo hili la maji, hili ni tatizo la Serikali nzima. Ukiangalia bajeti zote, utekelezaji ni asilimia 15, 25 mpaka 30. Kwa maneno mengine, ilitakiwa pengine tufanye kikao kimoja tu cha Bunge halafu tuiache hii Serikali ifanye kazi miaka mitatu mpaka mitano, ikimaliza bajeti ambayo tumepitisha ndiyo tukutane tena hapa kujadili bajeti upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ambao tunaufanya wa kila mwaka kujadili bajeti ambazo utekelezaji ni asilimia 20, kimsingi ni wizi, hatuwatendei haki Watanzania, kwa sababu uwezo wa Serikali kusimamia bajeti ambayo Bunge hili linapitisha, bajeti ya mwaka mmoja uwezo wa Serikali ni miaka mitano kukamilisha.

Tatizo la maji halina itikadi na wala siyo mjadala. Utafiti uliofanywa na *SYNOVATE* mwaka 2008, Taasisi ambayo ni ya tano Duniani kwa ukusanyaji wa maoni, umeonyesha kwamba, tatizo la maji ndiyo tatizo namba moja kwa Watanzania. Watanzania wanaona tatizo la maji kuwa ni kubwa kuliko hata rushwa, ni kwa sababu ya mateso ambayo wanayapata. Nchi hii haina sababu yoyote ya kukosa maji. Tanzania ni nchi ya 11 kwa mito mingi Duniani, Mheshimiwa Profesa unafahamu.

Tanzania ina vyanzo vya maji; Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Tanganyika peke yake lina asilimia 17 ya maji ya kunywa Duniani. Hiyo ni ripoti ya hali ya maji ya 2011. Sasa hivi inawezekanaje maji bado libaki kuwa tatizo katika mazingira kama haya? Hivi CCM ilitaka Mwenyezi Mungu aipe nchi yenye vyanzo vya maji kiasi gani kusudi iweze kuwapa Watanzania maji? *(Makofi)*

Havieleziki, labda kabla sijafika mbali niwasaidie majibu inagawa ninajua mnaondoka mwaka huu. Moja ya njia ya kuondoa tatizo la maji ni kuanzisha Mfuko Maalumu kwa ajili ya maji kama ilivyokuwa kwenye umeme *(REA)* na kwenye barabara. Maji ni tatizo kubwa kuliko barabara, maji ni tatizo kubwa kuliko umeme. *(Kicheko)*

Serikali ya UKAWA mwezi wa kumi ni moja ya maoni yangu, tuanzishe Mfuko Maalumu kwa ajili ya maji, ili kusudi pesa yake hiyo isiguswe. Kwa kufanya hivyo tunaweza kutatua tatizo la maji. Leo Jimboni kwangu, Mheshimiwa Waziri nimesoma hapa taarifa yake, anasema kuna vituo 68 kwenye Mradi wa Lukoma. Mheshimiwa Waziri hivi vitu ni utapeli hakuna kitu; Mradi wa Lukoma haujaanza haupo! *(Makofi)*

Leo Mradi wa Lukoma, Ilagala, Nguluka, Uvinza, Kandaga, ni zaidi ya mwaka mmoja wakandarasi wameshindwa kuendelea kwa sababu hakuna pesa! Zinatoka wapi pesa; hii Serikali kila siku inalia pesa, pesa?

Mheshimiwa Spika, ninaomba na wewe pia uchangie jambo hili, tatizo la Serikali hii ni wizi, Serikali hii inapiga mno! Hii nchi uchumi unavuja, fedha ya nchi inavuja, kuna watu wanatajirika mabilioni ya shilingi kwa kutumia *loophole* za Serikali hii dhaifu. Kuna wizi mkubwa, chukua mfano tu juzi tulizungumza hapa masuala ya *Escrow,* bahati mbaya ukanikatisha. Hoja ambayo tuliipitisha hapa Bungeni kwamba zisiendelee kulipwa 2.6 milioni dola ambazo ni zaidi ya bilioni tano kila mwezi, mpaka leo *TANESCO* wanalipa. Mimi hapa Mradi wa Maji Lukoma peke yake wanahitaji milioni 400 tu, milioni 399 waweze kukamilisha Mradi wa Maji wanasema pesa hakuana. Halafu kuna mtu mmoja, Singasinga mmoja, ambaye ameiweka Serikali mfukoni, anapokea bilioni tano bila kujali kama kazalisha umeme au hajazalisha. *(Makofi)*

Tukisema Serikali ya CCM iko mfukoni mnakataa nini? Bilioni tano, haiwezekani na hili ninalizungumza hapa kesho kwenye Nishati na Madini nitarudia, kwenye Wizara ya Fedha nitarudia, kwa sababu haiwezekani Serikali yetu iwekwe mfukoni na genge dogo la watu kwa faida yao. *(Makofi)*

Tunalia hapa Miradi ya Maendeleo nchi nzima. Pale Kigoma Mjini, sisi Watu wa Kigoma tuko mita mia moja kama urefu wa uwanja wa mpira kutoka Ziwa Tanganyika, ambalo ni chanzo chenye asilimia 17 ya maji yote ya kunywa Duniani eti na sisi tunalia maji! Hivi Kigoma wakiikataa CCM mtasema ni wabishi? Siyo kuna hoja ziko wazi, mnashindwa ku-*deliver* na mnashindwa ku-*deliver* kwa sababu Serikali ipo mifukoni mwa mafisadi.

Leo ndiyo maana mnaona pamoja na nchi kuwa na matatizo makubwa kabisa inaangamia hakuna maji, hakuna kitu, watu wanatangaza nia kila siku, mna wagombea mpaka sasa hivi sijui hamsini. Wana ujasiri utakafikiri watashinda. Wana ujasiri kwa sababu wahahisi hawa Watanzania pengine ni watu wa kawaida tu watakuwa wanawaachia tu muendelee. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haitowezekana! Hatutakabali nchi hii muigeuze kuwa gulio la kuchukua utawala kwa fedha na baadaye mtuendeshe kwa bajeti za asilimia ishirini kwenye maji mwaka mzima. Wahisani kwenye maji wameleta asilimia 27 peke yake, wanaleta asilimia 27 kwa sababu hii Serikali haiaminiki tena. Mheshimiwa Maghembe unalalamika tu kwamba Serikali haina pesa; tufanyaje sasa? Sisi tutaku-*attack* wewe, la sivyo jiuzulu! Hakuna kazi ngumu kama kufanya kazi chini ya Jakaya Kikwete, nawaambieni ukweli; ni Serikali ambayo inaendeshwa kwa *mission town,* hakuna utaratibu, pesa pale Hazina zinatoka kwa vimemo tu! Hakuna nchi ya namna hiyo, tunahitaji kuweka nidhamu katika uendeshaji wa Serikali. *(Makofi)*

Hazina inapaswa kusimamiwa kwa nidhamu. Mawaziri wote wanalia hapa, wakisimama kujitetea watasema kwa kuficha tu, lakini ukikutana nao kwenye korido wanalia. Hazina pale fedha zinatoka kwa vimemo, hakuna utaratibu. Serikali ni Taasisi, mnahitaji kuiendesha Serikali kwa ufanisi, tofauti na hivi mtabaki na Serikali za Kiswahili, ambazo hakuna Mipango inayotekelezeka mwaka hadi mwaka, halafu mnasema ni iena iena tunashinda uchaguzi; haiwezekani mwaka huu ni lazima mtoke. *You are too tired to continue my dear,* hamuwezi mmechoka mno kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza na haya wala siyo masuala ya itikadi, Serikali ya UKAWA ikiingia madarakani, Wana-CCM watapata maji, Yanga watapata maji, Simba watapata maji, nchi itakuwa sehemu nzuri ya kuishi. Hamna sababu yoyote ya kufanya mambo haya yazidi kukwama.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie tena, Uvinza, Lukoma, Kigoma Mjini pale, nilikuwa naongea na Meya tangu asubuhi; mkandarasi mwaka mzima anasuasua anasema hakuna pesa! Mwezi wa tano Kamati ya TAMISEMI waliwaambia Mradi utakuwa umekamilika, mpaka leo wanazungumza mwezi Novemba Kigoma Mjini. Kigoma Mjini pale ndiyo Jiji letu sisi Watu wa Kigoma. Sasa hata hapo hakuna maji? Haiwezekani!

Mheshimiwa Waziri, wewe ni rafiki yangu na wala sina ugomvi na wewe, lakini katika hili sina namna yoyote ile ni lazima utoe majibu ni lini Miradi ya Uvinza, Nguluka, Kandaga, Ilagala, Lukoma na Kigoma Mjini itafika mwisho?

Kama utaendelea kusema Serikali haikupi pesa, Mheshimiwa Waziri wewe ni Profesa, rudi Chuo Kikuu ukafundishe tu, hamna sababu ya kufanya kazi za namna hii za Kiswahili hizi. Wewe ni mtaalamu, ni msomi una-*deserve* kufundisha Chuo Kikuu, wanakufanyia mabajeti ya ujanja ujanja haya, watupie makaratasi yao nenda Chuo Kikuu ukafundishe. Mimi ningekuwa wewe nisingehangaika, hakuna sababu! Mnamchosha mzee huyu, mzee huyu anachoka kwa sababu hii Serikali inaendeshwa kiswahili, ni ujanja ujanja tu haiwezekani! *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nahitaji Waziri atakapokuja kufanya majumuisho, tupate hatima ya maji kwenye Miradi hiyo. Mwaka mzima Miradi imesimama Serikali inasema haina pesa, haiwezekani. Mheshimiwa Spika, nilikuomba mwongozo siku moja ukasema utatoa baadaye kadiri muda utakavyofaa, lakini mpaka leo hujautoa! Isaidie nchi hii; hii Serikali ina wezi mno, kama hatujadili hapa na kufanya maazimio hatuwezi kufika!

Mheshimiwa Spika, naomba ukumbuke nipate ujumbe wako hapa hapa kwamba, tunahitaji Taarifa ya Mafisadi wa *Escrow* iletwe Bungeni hapa tujadili. Watu wanasema imeshapita hii, tulikubaliana kabla ya mwisho wa uhai wa Bunge hili mtaleta taarifa tujadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nahoji mwongozo mbona unapiga chenga kwa masilahi ya nani? Haiwezekani! Tukikamata wezi mmoja mmoja tutaanza kujenga tabia ya watu hawa kupunguza wizi. Mimi naumia sana na wewe mama yangu inawezekana unaguswa, watu wanapata bilioni tano za wizi, bilioni tano kila mwezi, azalishe umeme asizalishe! Mahakama ya Kimataifa imekataa, Bunge limekataa …

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Sasa *definition* ya baadaye bado haipo. Baadaye nitatoa nafasi yangu, ninayo baadaye.

Mheshimiwa Kidawa Saleh ndiyo msemaji wetu wa mwisho kwa upande wa Wabunge.

MHE. KIDAWA HAMID SALEH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo Mezani. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia. La pili, nawapongeza na kuwashukuru akina mama wote wa Mkoa wa Kaskazini, kwa kuniwezesha kuwepo hapa Bungeni na kufanya kazi ambazo wamenituma kuzifanya na ushirikiano mzuri walionipa katika kipindi chote hiki cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kusema Serikali ya Chama cha Mapinduzi ipo na itaendelea kuwepo. Watanzania watakichagua Chama cha Mapinduzi kutokana na imani waliyonayo kwa Chama hicho. Serikali inafanya kazi nzuri, kila mwenye macho anaona. Huangalii tu sekta moja, lakini unaangalia sekta zote, angalia miundombinu ya kiuchumi, kijamii na huduma mbalimbali zinazotoa Serikali kwa kweli zinaridhisha. Ukifanya utafiti utaona ya jana siyo ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maji ni kipaumbele namba moja cha Watanzania na hasa Wanawake. Wanawake wa vijijini bado wanapata tabu ya maji katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, juhudi za Serikali zijikite zaidi kupeleka maji vijijini na kumalizia Miradi ambayo wameianza. Asilimia 55 tu ya Watanzania waishio vijijini ndiyo wanapata maji. Je, ile asilimia 45 wataishije na tunasema maji ni uhai na afya?

Asilimia 80 ya mwili wa binadamu tunaambiwa ni maji. Kwa hiyo, inaanzia hapo uhai wenyewe. Serikali ijitahidi kupeleka Miradi ambayo inatekelezeka na Wananchi wa Vijijini na Mijini wapate maji.

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kusema tatizo kubwa hapa siyo Wizara kutotekeleza Miradi yake, tatizo kubwa ni rasilimali fedha. Bajeti inayopangwa haiendi ya kutosha kutokana na ufinyu wa rasilimali fedha. Asilimia 26 tu ndiyo imekwenda kwa fedha za ndani na asilimia 27 ya fedha za wafadhili, wastani ni asilimia 26.5. Kwa kweli hapa hata kuwe na dhamira njema ya kiasi gani, siyo rahisi kutekeleza Mipango ya Maendeleo iliyopangwa. Hili linatupa *warning* kwamba, Serikali ijipange vyema katika kutekeleza Miradi ya Maji kwa fedha zake za ndani. Kwa sababu tumesema maji ni uhai! Huwezi kuchukua uhai wa Wananchi wako ukamkabidhi mtu mwingine ausimamie, kwa maana kuwa tuepukane kabisa na kutegemea wafadhili. Wafadhili wameshaonyesha kwamba wameshachoka kusaidia.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nashukuru kwenye bajeti ya mwaka huu kwamba ni asilimia 26 ndiyo ambayo tunategemea wafadhili, asilimia kubwa tunategemea fedha za ndani. Serikali ijipange vizuri, hiki kinachoombwa na Wizara wapatiwe, kama hawakupatiwa itakuwa stori ndiyo ileile hakuna kinachotekelezeka, inatekelezeka kwa asilimia ndogo tu na shida kwa Wananchi inaendelea kuwepo vilevile.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebarikiwa kuwa na vianzio vingi tu vya maji asilia; mito mikubwa, Maziwa makubwa, maji ya ardhini, lakini vyanzo hivi kama havikutunzwa na Watanzania wote, kila Mtanzania akawa msimamizi mzuri wa vyanzo vya maji, litakuja suala la upungufu wa maji. Kwa hiyo, elimu iendelee kutolewa kwa Watanzania wote kwenye Vijiji na Vitongoji, waendelee kulinda vyanzo vya maji, vinginevyo tutakosa maji na hata hiyo asilimia ndogo itakuwa haipatikani na itayeyuka kabisa.

Mheshimiwa Spika, uvunaji wa maji ya mvua ni kitu muhimu sana. Kuna nchi ambazo hazina kabisa vyanzo vya maji asilia, mojawapo ni Singapore, lakini asilimia kubwa ya maji ya mvua wanayavuna, wanaya-*treat* halafu yanatumika kuwa maji safi na salama na kuyatumia

kwa watu wao. Vilevile wanatumia hata maji taka, wana-*reclaim* halafu wana *re-use* yale maji. Wanasema wanatumia *grey water*, lakini si *grey water* kwa sababu wana-*reclaim,* wana *treat* wanatumia. Sisi hatujafikia huko kwa sababu vyanzo vingi vya maji tunavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkopo kwa huduma za maji Zanzibar. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa alipotoa hotuba yake hapa alisema kuna mkopo wa karibu milioni 92.18 ambao unakopwa kutoka Serikali ya India, unaosimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zanzibar imeleta maombi yake Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwa sababu mkopo ni jambo la Muungano. Hili ni jambo jema, tunasisitiza Serikali ya Jamhuri ya Muungano isimamie mkopo huo upatikane, kwa sababu na kule Zanzibar kuna matatizo ya maji vilevile. Kuna Vijiji mbalimbali bado maji hayajafika.

Kwa kusimamiwa mkopo huu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ukipatikana na kule Zanzibar tatizo la maji litapungua. Kuna Vijiji mbalimbali; kuna Fujoni, Mahonda, Kinduni na vijiji mbalimbali vingine ambavyo maji yanapatikana kwa shida, yanapatikana kwa mgao na wakati mwingine hayafiki kabisa katika Vijiji mbalimbali. Kwa hiyo, hili ni jambo jema, tunaomba sana Serikali ilisimamie huu mkopo upatikane na Wazanzibari kule tufaidike na maji safi na salama.

La mwisho, ni upotevu wa maji. Kwenye hotuba hapa imeainishwa kabisa kuna asilimia kubwa ya maji yanapotea kutokana na uchakavu wa miundombinu na mambo mengine ya wizi. Kwa mfano, Jiji linaloongoza kwa upotevu wa maji ni Dar-es-Salaam asilimia 57 na Miji mingine ya Mikoa asilimia 23. *Best practice* inaonyesha upotevu wa maji uwe ni asilimia 20 tu au chini ya hapo. Sasa hiki ni kitu gani? Hivi Serikali kweli tumeshindwa kusimamia jambo hili kiasi cha asilimia kubwa ya maji yanapotea kiasi hiki?

Watu wanalia maji lakini vilevile maji yanapotea kutokana na uchakavu wa mabomba yanapasuka siku zote maji yanamwagika! Hivi kweli Serikali imeshindwa kufuatilia? Kwa sababu mabomba yakipasuka yale maji yanayopatikana yanakuwa kidogo lakini hayapo salama, yanakuwa *contaminated* njiani, watu wakinywa yale maji wanaweza wakaathirika. Inabidi watu waelimishwe kuchemsha maji kutokana na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, lingine katika hili wanawake ndiyo wanateseka sana. Wanaamka alfajiri sana, wanaenda kuhangaika. Kutokana na haya ndoa nyingine zinavunjika, kwa sababu ameenda kubeba maji anachelewa kurudi, akifika nyumbani anaambiwa mbona umechelewa ulikuwa umeenda wapi? Ni tabu kubwa sana. Tusisitize Wizara ipewe bajeti ya kutosha ili lile lengo lake la kufikia maji asilimia 74 vijijini liweze kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ninasema Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kuwepo, kwa sababu inafanya mambo makubwa na mazuri. Changamoto zipo, tuzipiganie kuziondoa, lakini Serikali ya Chama cha Mapinduzi *is here to stay*.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Kuna Kamati yetu ya Bajeti na aliyemaliza kuzungumza ni Makamu Mwenyekiti. Safari hii kutokana na matatizo ya muda, kuna kitu kinaitwa mashauriano kabla ya *sector ministries* kupita hakikufanyika. Sasa nayo hiyo ni upungufu kwa upande huo. Kwa sababu hiyo, namwomba Waziri wa Fedha aseme kabla sijawaita watoa hoja waanze kusema.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kupata nafasi hii kwa mara ya kwanza toka Bunge hili limeanza. Hata huko nilikokuwa tulikuwa na kazi ngumu sana ya

kufuatilia utekelezaji huu wa bajeti yetu ambayo tunaikamilisha, lakini vilevile matayarisho mazuri ya bajeti yetu inayokuja mwaka 2015/16.

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mawili, matatu, ambayo nataka nichangie. Kwanza, nadhani nichukue fursa hii kumtaarifu tu Mheshimiwa Mbunge Kafulila, labda Sheria za Fedha huzifahamu, hakuna fedha inayotoka Hazina kwa *memo*. Nataka ulielewe hilo! Hakuna fedha inayotoka hazina kwa ki-*memo*, kama ingekuwa hivyo basi wewe ungezipata kirahisi zaidi. Kwa hiyo, naomba hilo ulifahamu, tusitafute *audience*, huu ni wakati muhimu sana kwa Watanzania kuweza kutetea masilahi ya maendeleo ya nchi hii. Siyo kusema tu sentensi au maneno ambayo hayana ukweli wowote. *(Makofi)*

Imetolewa kwa *memo?*

SPIKA: Mheshimiwa usiwasilikilize hawa, hee!

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, nadhani haijui *memo* ilivyokaa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna shilingi bilioni 80 ambazo zimeongelewa sana hapa tulizoziahidi katika Mwaka wa Fedha 2013/14 na kwamba, hili lilikuwa kama ni deni pale Serikalini. Tunaomba kutoa taarifa kwamba, sasa hivi Wizara ya Fedha tunaendelea kulipa madeni mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge wengi walizungumza kuhusiana na madeni ya Wakandarasi na Watumishi, kwa hiyo, hizi bilioni 80 tumeanza kuzilipa na mwaka huu wa fedha 2014/15, *allocation* ambayo tunayo kwa ajili kulipia *arrears* ambazo tumezihakiki mpaka Juni 2014, kwa mwaka huu wa fedha peke yake tutalipa *two hundred billion*. Mwaka ujao wa fedha *quarter* ya kwanza tunalipa *six hundred and fifty six billion*.

Mheshimiwa Spika, hii ni kwa sababu ya *space* ya bajeti ambayo tunayo. Tulifanya uhakiki wa madai yote ambayo Wizara mbalimbali zinadai, ambayo *suppliers* wanadai na maombi ama zile taarifa ambazo zilifika kwetu, zilikuwa ni kiasi ya shilingi trilioni 1.2, lakini madeni ambayo yalikubaliwa na yalikuwa na vielelezo na vigezo vyote sahihi vya kulipwa, yalikuwa shilingi bilioni 856.

Kwa hiyo, kwa mwaka wa fedha baina ya leo hadi mwisho wa mwezi, tutalipa takribani milioni 200 na kwa sasa *process* zinaendelea za kulipa *allocation* ambayo tumeipata kwa wiki iliyopita bilioni 57. Kwa hiyo, tunataka zote tuzilipe na hizi zitakuwemo shilingi bilioni 80 ambazo kama tulivyotoa ahadi kwamba nazo tutazilipa.

Vilevile ziada ya hapo kuna *ex-chequers* za bilioni 30 ambazo zipo kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali nazo zinafanyiwa utaratibu wa kuweza kulipa, hizi zote ni za Wizara ya Maji. Kubwa zaidi na la msingi, tayari tumeshakamilisha *negotiations* na matayarisho ya kusaini mkataba na Exim Bank ya India yenye thamani ya dola milioni 268.35 yamekamilika na tunatarajia mwezi huu kusaini mkataba huo ambapo fedha hizi zitatoka.

Si hivyo tu, kuna fedha ambazo tayari tumeshapeleka *request* yetu Exim Bank ya China zinazotimia dola bilioni 200 na wao tayari walikuwa wanasubiri hiyo *request* tumeshapeleka na taratibu zikikamilika, tutasaini mkataba kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Miradi mikubwa ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna angalizo, Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti alitoa kuhusiana na fedha za Mradi wa *Sanitation* kule Zanzibar. Exim Bank ya India baada ya kukamilisha uchaguzi na kulikuwa na Waziri Mkuu mpya ndiyo ameingia, kidogo walikuwa wana *constrain* hii ya ukopeshaji.

Sasa muda huo wao walituuliza nini ni priority yetu na sisi tukawaambia *priority* yetu ilikuwa ni maji. Kwa hiyo, hizi dola milioni 268 ni pamoja na *priority* yetu ya *Sanitation Project* ya Zanzibar, nayo tunakamilisha taratibu ili mkataba upate kusainiwa nazo zitoke. Kwa hiyo, *priority* yetu *both* Tanzania Mainland na Zanzibar ilikuwa ni maji na wenzetu wamekubali na taratibu zinakamilika kwa ajili ya kusaini na hivyo Miradi hii kuendelea kutekelezwa. *Otherwise,* fedha hizo nyingine kama nilivyosema, tunaendelea na taratibu za kuzitoa na zitatoka.

Mheshimiwa Spika, *priority* yetu ni maji na tutasimamia kuhakikisha hizi fedha zinatoka na Miradi ya Maji inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru. *(Makofi)*

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, haya aliyoyaeleza Waziri, naiomba Kamati ya Bajeti ika-*firm up* kwamba haya waliyosema yapo katika vitabu inavyostahili. Kwa hiyo, Kamati ya Bajeti mtafanyia maelezo haya kazi, kwa sababu sasa ni suala la bajeti siyo suala tu kuchangia. Kwa hiyo, haya maneno ya Waziri atarudia mtajua yana-*fit* wapi katika vitabu vyetu.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, dakika 20.

Jamani Wizara hii kawaida huwa tunachangia siku mbili, sasa kujibana katika siku moja wengi mngependa kuogelea humu kama mnatoka ama hamtoki lakini mngependa, sasa haiwezekani. Kwa hiyo, hata katika Kamati ya Matumizi ni watu saba tu kutokana na vyama. Kwa hiyo, mjue hivyo ndivyo ilivyo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninashukuru na mimi kupata nafasi hii kuweza kuchangia Hotuba ya Wizara ya Maji. Kwanza na mimi niungane na wenzangu kutoa pole kwa msiba uliotokea kwa mwenzetu Eugen Mwaiposa na Mheshimiwa Capt. Komba; nawapa pole sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie muda huu pia kuwashukuru Wananchi wa Jimbo la Mvomero na wengine wawakilishi wao wapo hapa, kwa imani kubwa ambayo wameionyesha kwangu. Nami ninawaahidi tu kwamba, katika watu wanatajwa kutangaza nia ya Urais mimi sipo, kwa sababu ni kazi maalum kwa Jimbo la Mvomero.

Kwa hiyo, ninaamini kabisa yapo mambo makubwa ambayo Wananchi wa Mvomero wanayategemea kwangu na mimi nisingependa kuwakwaza. Muda huo kwangu bado haujafika, sifa ninazo, muda utakapofika nitatangaza nia, lakini kwa sasa nitafanya kazi na Wananchi wa Jimbo la Mvomero. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Kamati yetu ikiongozwa na Profesa Msolla, kwa taarifa nzuri. Wameeleza mambo mbalimbali ambayo kwetu sisi itatusaidia, hatuwezi kujibu hoja moja moja lakini niseme tu kwa ufupi kwamba, tumefanya nao kazi vizuri na ushauri wao ndiyo uliotufikisha hapa na wenyewe wamesimama wameeleza kwa uhalisia namna ambavyo kwa kadiri tulivyoweza, sisi kama Wizara ya Maji tumejitahidi sana.

Mheshimiwa Spika, tumepokea Hotuba ya Kambi ya Upinzani, kwa yale mazuri tutayachukua na kuyafanyia kazi na yale mengine ni utekelezaji tu wa majukumu ya msingi. Wao kama Wapinzani ni lazima wafike kuikosoa Serikali, lakini yale ya msingi mazuri tutaendelea kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumeongelewa mambo mengi. Nianze na hotuba yetu na viambatanisho ambavyo tumeviweka katika hotuba ile. Tuliona ni namna bora ya kuwa wawazi zaidi, kwamba, tupate na utekelezaji wa Vijiji Kumi tulivyovifanya, tupate takwimu za kutosha. Mimi nataka kusema kwamba, hiyo yote ilikuwa kwa nia nzuri kabisa. Niseme tu kwamba, takwimu hizi zinaandaliwa na binadamu na sisi ni binadamu na wale wanaoweza kunielewa '*garbage in, garbage out*'. Kwa hiyo, kama tumepata takwimu baadhi zinaweza kuwa zina hitilafu, basi mtupe muda sisi tutazirekebisha zaidi, lakini hatukukusudia hivyo. Tulikuwa na nia nzuri, lakini takwimu hizi zinakusanywa na binadamu na mwingine unaweza kumwambia tuhesabie vituo vya maji, akakutajia katika kioski kuna mabomba sita akahesabu ndiyo vituo vya maji. Kwa hiyo, ukachanganya kati ya kioski na bomba la maji kwamba, katika kioski kunaweza kuwa na mabomba manane yanatoa maji na yeye akahesabu hivyo.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema kwamba, tutaleta Bungeni takwimu sahihi ili kuweza kuweka mambo vizuri na takwimu hizo ziwe na matumizi mazuri zaidi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, hatukukusudia kuchakachua. Hata katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi tuliahidi tukipewa ridhaa tutatekeleza na tutahakikisha tunapeleka maji kwa asilimia 65. Tumefika kwa kusema ule ukweli, kwa sababu matarajio na uhalisia tungeweza kufoji lakini hatuna nia hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia wapo wenzetu wa *World Bank* wamekuja wamesema hata hiyo asilimia 55 mliyoisema, inaonekana ninyi mmechukua zile fedha tu za Serikali, mngeunganisha na taasisi binafsi na *NGOs* ambazo zimeweza kusaidia maji mngeenda juu zaidi, lakini sisi hatukutaka kuchakachukua. Vilevile hata sensa ilipofanyika 2012, ilionesha asilimia ya watu wanaopata maji ingekuwa labda 57, lakini sisi kwa kutumia *BRN* tumekuwa wakweli zaidi kwamba ni asilimia 55.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa yale ambayo yana upungufu, basi yasifute zile jitihada kubwa ambazo zimefanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kutekeleza Miradi mikubwa ya Maji katika maeneo mbalimbali. Kwa hiyo, nilitaka kuweka sawa hilo.

Mheshimiwa Spika, pili, ilikuwa kuhusu suala la maji katika Jiji la Dar es Salaam. Limeongelewa na Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam, limeongelewa na Mheshimiwa Susan Lyimo, limeongelewa na rafiki yangu Matiko. Wote kwa pamoja mmeeleza matatizo yaliyopo katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, mahitaji halisi ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ni lita milioni mia saba hamsini kwa siku, lakini uzalishaji ni lita milioni mia nne hamsini. Uzalishaji uliopo ni lita milioni mia tatu kwa siku. Kwa hiyo, kuna upungufu na hii inapelekea maji yanakuwa hayafiki maeneo mengine. Maeneo ambayo yana miinuko hayafiki na maeneo mengine ambayo yana miundombinu kabisa na hasa mabomba ya Mchina maji hayafiki.

Nataka niseme tu kwamba, nia ya Serikali ni kuhakikisha Jiji la Dar es Salaam linapata maji ya kutosha na ndiyo maana kuna Miradi hii mikubwa ya Ruvu Chini, Ruvu Juu, Kimbiji na Mpera inatekelezwa. Hii yote ikikamilika, itapelekea upatikanaji wa maji kwa Jiji la Dar es Salaam kuwa lita milioni mia saba hamsini, kwa hiyo, mahitaji yote tutakuwa tumeweza kuyatekeleza na maeneo yote ambayo hayapati maji yataanza kupata maji, lakini pia na maeneo yale ya miinuko yataendelea kupata maji.

Mheshimiwa Spika, hatuishii hapo, tunaelewa kwamba, Dar es Salaam miundombinu imechoka, imechakaa, kuna uvujaji mkubwa wa maji. Kwa hiyo, sasa Serikali tunajipanga na tunatafuta wakandarasi, fedha zimeshapatikana ili tuweze kubadili miundombinu ya maji hiyo iliyochakaa na mingine mipya tuijenge mpaka maeneo ya Makongo na Changanyikeni, watu waweze kupata maji kwa uhakika zaidi.

Kwa hiyo, ninawaomba sana tuwe na subira na tuendelee kushirikiana kuona jambo hili linatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuharibika kwa miundombinu ya maji, lakini lipo pia tatizo la wizi wa maji na hili tumelifanya. Nimeona wakati fulani tumefanya bila kujali itikadi zetu, Wabunge wote tumeshirikiana kwa pamoja kukamata wezi wa maji na tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Sasa hivi tumeona ili angalau kuboresha na kukabiliana na wizi huo, hata Menejimenti sasa imebadilishwa, tumepata Mkurugenzi mpya na ameanza kazi. Kwa muda mfupi tu hata mwezi haujaisha, maeneo ambayo yalikuwa hayapati maji sasa watu wanaanza kupata maji.

Ninawaomba sana tuwe na subira wakati Serikali ikichukua hatua mbalimbali, lakini mtupe ushirikiano Serikali kufichua wezi wa maji ili maji yanayopotea yasiwe mengi kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, limeongelewa suala la *DAWASA* na *DAWASCO*. Mimi nataka niseme tu kwamba, kama ambavyo imeelezwa, kazi za *DAWASA* wao wanajenga miundombinu. Serikali ikitaka kujenga Miradi mikubwa ya Maji hii ya Ruvu Juu, Ruvu Chini, Kimbiji, Mpera, fedha zinapitia *DAWASA* wanajenga miundombinu ya maji. Hawa *DAWASCO* wao wanaendelea kufanya matengenezo madogo madogo na kuuza maji. Tunatazama ushauri mlioutoa hata sisi tumeanza kuufanyia ili kutoa majukumu mapya kwa *DAWASA* na *DAWASCO*.

Tumetuma wataalamu wetu wameenda Durban na Ujerumani wamejifunza. Ipo miji ambayo ina mamlaka mbili na wanafanya kazi vizuri. Kwa hiyo, tunataka kuona *DAWASCO* tunawapa majukumu yao, lakini *DAWASA* nao pia wazalishe maji wayapeleke kwenye matenki wawauzie *DAWASCO* ili *DAWASCO* wawajibike moja kwa moja kuyauza maji hayo kwa Wananchi. Kwa hiyo, sisi kama Serikali, hili nalo tumeliona tutaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la maji taka tunaelewa kwamba, maji yakishakuwa mengi Dar es Salaam, maana yake lazima kuwe na miundombinu ya maji taka. Kwa hiyo, hili pia tupo katika hatua za kukubaliana na wenzetu wa China kuona tunajenga miundombinu ya maji taka ili kuzuia kusije kutokea milipuko ya magonjwa pale ambapo patakuwa hakuna miundombinu ya maji taka.

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kwenye hoja mbalimbali za Wabunge nikianza na Mheshimiwa Herbert Mntangi. Ninakushuku sana Mheshimiwa Mntangi, kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa ushirikiano kwa muda mrefu kwa Waziri wangu, mimi mwenyewe na Naibu Waziri wa Fedha, umetutaja. Tumefika hapo kwa nia moja tu na wewe unajua ya kuwasaidia Wananchi wa Muheza. Umekuwa ukishauri na sisi tumefuata ushauri wako na hatimaye tumepata wafadhili.

Mimi ninaamini kabisa kwamba, Eurofinsa hawa Wahispania, wakitoa fedha tutayatoa maji Mto Zigi na tatizo la maji pale litakuwa limeisha.

Tumefanya ziara pale, zipo jitihada ambazo kama Serikali inayowajali Wananchi, tumezifanya pale angalau kupunguza tatizo la maji. Mwisho wa yote tukiyatoa maji Mto Zigi, tatizo la maji pale litakuwa limekwisha. Ninakushukuru sana na uzuri ni kwamba, Wananchi pia walikuja mpaka hapa tumewaeleza, lakini na kule tulikokuwa tuliwaeleza kwamba, tatizo siyo la Mheshimiwa Mntangi, lakini Mheshimiwa Mntangi amekuwa msaada mkubwa sana wa kuishauri Serikali kuona tatizo la maji kwa Mji wa Muheza tunalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, mama yangu Zabein Mhita, bahati mbaya sana nikupe pole, lakini yeye yupo kwenye eda asingeweza kusimama hapa na kuchangia, lakini mchango wake tunauthamini. Nikutoe wasiwasi tu kwamba, kuna Mradi mkubwa wa Ntomoko; Kijiji kile cha Ntomoko tumetoa maji kwenye kitongoji tu. Maji ambayo sasa yanapelekwa mpaka katika Wilaya ya Chemba bado hayatoshi. Serikali kwa kutambua umuhimu wa hawa wanaotunza chanzo, tunafanya mpango kwa wakati huu hata tuchimbe kisima kirefu ili Wananchi hawa waweze kupata maji.

Kuhusu andiko la kuboresha maji katika Mji wa Kondoa, pamoja na jitihada za Serikali tulizozifanya, bado tunaendelea kushughulikia. Kulikuwa na Mradi wa bilioni 1.6 tumetoa fedha kidogo, tutaendelea kutenga fedha kuona tatizo la maji katika Mji wa Kondoa nalo tunaendelea kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa Mheshimiwa Esther Matiko aliongelea Mradi wa Gibaso. Mradi huu kuna wakati ulijengwa, lakini kisima cha maji kile maji sasa hayatoshi. Kwa hiyo, ninaahidi kwamba tumeshapanga tutachimba visima vingine viwili katika Mradi huu, maji ya pale hayatoshi ili kuona Mradi huu unakuwa na manufaa na unawanufaisha Wananchi wa Gibaso.

Mheshimiwa *Jah People* aliongelea suala la Makambako na Njombe. Niseme kwamba, maeneo yote aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge wa Makambako pale nimefika, nimefika mpaka Njombe. Serikali inafanya utaratibu wa kuweza kupata wafadhili kwa ajili ya Mradi mkubwa pale Makambako.

Kwa vijiji ambavyo bado Miradi haijatekelezwa, hili niliseme tu kwa nchi nzima kwamba, kama alivyosema Waziri wa Fedha, sisi tukiwezeshwa tu Wizara ya Maji, hatujawahi kuwaza wala kufanya na hatutafanya, kuhujumu au kuwa wazembe katika kutekeleza Miradi ya Maji. Tutaendelea kutekeleza kadiri fedha zitakavyokuja, sisi kwa upande wetu hatuna tatizo.

Ninawaahidi tu na Mheshimiwa Mbunge wa Makambako nikuahidi vijiji hivyo ambavyo nimefika na nimeviona, tukipata fedha tutavitekeleza.

Mheshimiwa Spika, pia nimeenda pale Njombe Mjini kuna kazi kubwa imefanyika na sasa fedha zimekwama. Nimpongeze sana Mkurugenzi wa pale Bwana Majani, anafanya kazi nzuri sana, lakini hawana gari, tulishakubaliana na Waziri gari lolote lililopo pale Wizarani ambalo lipo katika Mradi hawa watu wanafanya kazi kubwa wapatiwe gari sasa. Fedha zitakapopatikana Miradi hii ya Lugenge na Kisilo itakamilika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abdul Marombwa ameelezea kuhusu suala lake la Mradi mkubwa wa Maji pale Kibiti. Nimeenda naye pale, Mradi ule ni mkubwa, Kamati ile ya Maji bado haiwezi kumudu usimamizi wa uendeshaji Mradi mkubwa kama ule. Tuliwashauri paundwe Bodi ambayo itakuwa mamlaka na Wajumbe wateuliwe ili waweze kumudu kuendesha Mradi huu ni mkubwa sana. Kwa hiyo, hili ninaamini lipo katika *process* na likitekelezwa basi itakuwa limetusaidia sana. Tukaenda pale Mradi ambao ameupigia kelele Mradi wa Jaribu Mpakani, huu nao tutautekeleza bila tatizo.

Mheshimiwa Azza Hilaly ameelezea Mradi wa Tinde. Kweli kwa miaka yote Tinde pamekuwa na tatizo kubwa na upo Mradi ambao ulikuwa utekelezwe wa Kagongwa – Isaka – Tinde. Fedha zilitengwa lakini hazijatoka, kwa hiyo, sisi kama tungepata fedha hizo tungetekeleza tu. Kwa kuthamini na kuwajali Watu wa Tinde wakiwa na shida ya maji, nilifika pale na tumechimba visima kama unavyosema na tukatanguliza milioni mia moja, lakini hata

sasa kwa taarifa tu ni kwamba, tayari tumeshakamilisha fedha zote na Mradi huo mwingine tumeshatekeleza zile fedha ambazo zilikuwa zimebaki, kwa hiyo, Tinde mambo yatakuwa safi na yataenda vizuri. Ule Mradi mwingine wa Kagongwa – Isaka – Tinde, tumeshawatumia *KASHUWASA*, wamefanya upembuzi na usanifu ukikamilika na bajeti imeshatengwa tutatekeleza Mradi huo.

SPIKA: Tumekuongezea dakika tano zaidi.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ole Medeye kuhusu Mradi anaousema mkubwa wa Arusha ni kweli na sisi Sera yetu ni kwamba, tunapoyachukua maji huko Arumeru ni haki ya hawa watu kupata maji. Kwa hiyo, nikuhakikishie tu kwamba, Mradi huu utakaohudumia Jiji la Arusha ilimradi maji yanatoka Arumeru, basi sisi tutahakikisha Wananchi wa Arumeru wananufaika na Mradi huu.

Mheshimiwa Laizer ameongelea kuhusu Mradi mkubwa wa Maji ambao ulikuwa ni ahadi ya Rais na mimi wakati ninaenda Longido Mheshimiwa Rais alinielekeza akasema hakikisheni mwaka huu mnatenga fedha ni ahadi yangu.

Mimi nimekwenda mpaka Siha, nimeoneshwa ambako maji yatachukuliwa, lakini pia niliwaomba Serikali ya Mkoa kupitia *RAS*, wakae kati ya Serikali ya Wilaya ya Siha na Longido ili wote kwa pamoja wakubaliane maji yaweze kuchukuliwa kutoka Mto Simba na mwaka huu tumetenga shilingi bilioni mbili za kuanzia kutekeleza Mradi huo. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi kwamba tutatekeleza.

Mheshimiwa Bwanausi ameongelea kuhusu Mradi wake wa Chiwambo. Nataka niseme tu kwamba, Mradi huu sasa tutautekeleza na upo katika bajeti yetu wa bilioni 1.8 kwa vijiji 27. Nimefika pia katika Mradi wa Mbwinji, nimekwenda Nachingwea, kwa hiyo, vipo vijiji ambavyo viko kandokando ya bomba lile navyo tutavitekeleza. Nilikwenda Nachingwea na Wilaya ya Ruangwa pale kwa Mheshimiwa Majaliwa, kulikuwa na watu wanadai fidia na tumewalipa. Kwa hiyo, vile vijiji ambavyo vinastahili kupata maji pembezoni mwa bomba hilo, tutahakikisha wanapata maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mheshimiwa Keissy, kwanza, nimpongeze kwa jitihada ambazo ameendelea kuzifanya, ameshirikiana sana na ofisi yetu, Mheshimiwa Waziri na mimi mwenyewe, tumekuwa tukishauriana, ametueleza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kupeleka pesa hata kama si kwa kiwango kile cha ahadi, lakini zile ambazo zimepelekwa ametueleza kwamba, kuna ubadhirifu. Sisi kupitia Katibu Mkuu, alishaagiza ufuatiliwe Mradi huo kuona kuna ubadhirifu kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, wakati Katibu Mkuu ameshaagiza kufuatilia jambo hili, Mheshimiwa Keissy aliandika barua kwa Waziri Mkuchika na mimi aliniletea kopi kwa ajili ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, mimi ninamwomba sana kaka yangu kwamba, sisi tunaendelea kufuatilia kwa upande wetu na ikibidi kufika maeneo husika, lakini hili la TAKUKURU tayari limeanza kushughulikiwa, awe na uvumilivu tu kwamba majibu yatapatikana na ukweli unaweza ukajulikana.

Mheshimiwa Nkamia alielezea kuhusu Bwawa la Farkwa, tayari tathmini ya kimazingira imeshakamilika na usanifu wa kina unakamilika. Wakati wowote likishakamilika, tutatangaza

kumpata mkandarasi kwa ajili ya Bwawa la Farkwa ambalo litakuwa manufaa kwa Wananchi wa Wilaya yake na vilevile hapa Dodoma Mjini.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja ya Mheshimiwa Shabiby ya pale Gairo, nami nakubaliana naye kwamba, pale Gairo kuna tatizo kubwa la maji. Kulikuwa na mradi mkubwa wa maji, lakini maji ya pale yana chumvi nyingi na unahitajika mtambo. Mheshimiwa Rais na hata yeye mwenyewe tumefika pale na alielekeza kwamba hata ikinunuliwa hiyo mashine, wananchi watashindwa kumudu gharama za mradi huu. Kwa hiyo, kwa sasa tulifanya jitihada za haraka na niliendanaye na Mheshimiwa Waziri alienda na aliekeza, kumechimbwa visima na sasa tunafanya jitihada za wananchi wapate maji angalau kwa dharura.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alielekeza mbele yangu na Katibu Mkuu kwamba huu mradi wa Chagongwe yatolewe maji kule milimani. Nasi kama Wizara tulianza kutekeleza, tulishawatuma Wataalamu wetu, wanaendelea kukamilisha kazi hiyo, wafanye usanifu. Ile ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Nimeona hapa ameniambia siungi mkono hoja! Naomba tu atukubalie na kwamba kazi hiyo ikikamilika sisi tutatekeleza mradi huo bila tatizo lolote. Nami natambua kwamba anawapigania wananchi wake na kwamba, pale pana tatizo la maji. Atupe muda, tutaweza kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, zipo hoja nyingine hapa za Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla wake kwamba kwa nini miradi ya Vijiji 10 imeendelea kuchelewa?

Mheshimiwa Spika, japo zipo changamoto mbalimbali, fedha ni moja ya changamoto hiyo, lakini pia, ikumbukwe tu miradi hii ilianza muda mrefu, lakini baada ya kuanza ni kwamba, kulikuwa na masharti mengi makubwa makubwa ya kuweza kutekeleza miradi hii; masharti hayo yaliondoka mwaka 2007. Kwa hiyo, zamani ilikuwa Mkandarasi mwenyewe anaajiriwa na Wizara ya Maji. Kwa hiyo, kwa sasa wanaoajiri Wakandarasi ni Halmashauri yenyewe. Kazi yetu ni kuzipeleka fedha hizi kule na tukipita ni kukagua hii miradi ya maji.

Mheshimiwa Spika, pia katika utafiti wa maji kuna maeneo maji yalikosekana, kuna maeneo maji yalipatikana. Kwa hiyo, sababu zote hizi tatu kwa pamoja, zinasababisha miradi hii kwa kiasi fulani kuchelewa.

Mheshimiwa Spika, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, sisi ni sehemu ya Baraza la Madiwani, tuko katika Kamati mbalimbali. Tuendelee kwa pamoja, tusitegemee Wizara ya Maji na TAMISEMI. Tushirikiane kwa pamoja kudhibiti na kuona miradi hii inatekelezwa. Sisi Wabunge ni Wajumbe wa *Finance Committee* na Kamati mbalimbali; tushirikiane kwa pamoja kule katika Halmashauri zetu. Kwa sababu, leo Mkandarasi haajiriwi na Mheshimiwa Maghembe au Katibu Mkuu wake, anaajiriwa na Halmashauri husika kule chini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukiwa tuko pale kwa pamoja, tufanye kazi kwa pamoja, tutaweza kuzuia ubadhirifu, tutapata Wakandarasi wazuri, tutahoji matumizi mazuri ya fedha. Kwa hiyo, naomba sana niseme suala hili ni letu sote kwa pamoja, tufanye kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, suala la maji linatuleta pamoja. Maji haya yote yanatuleta bila kujali itikadi. Sijawahi kuona kwamba nimeenda kuzindua mradi, maji yakatoka bendera ya kijani au bendera ya *CHADEMA* au bendera ya *CUF*. Ni maji kwa matumizi ya binadamu wote.

Kwa hiyo, yote haya tuwe kwa pamoja kuona kwamba maji hayatupeleki katika suala la itikadi. Pale ambapo tunafika mahali unakuta wananchi wameshakabidhiwa mradi, wanataka kuupanua, wanatakiwa kutengeneza tu mfereji au mtaro. Lakini unakuta kuna watu wanaweza

wakaingiza siasa wakasema hakuna kuchimba mtaro, lakini wanaopata matatizo ya maji ni wale wale wananchi wa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mdogo wangu Mheshimiwa Ester Bulaya ameongelea suala la miradi ile ambayo ameitaja ya vijiji hivyo. Nilitoa tamko hapa kwamba, wananchi wasikubali kupokea miradi ya maji ambayo ina kasoro. Kwa sababu, hawa Wakandarasi wanapofika maeneo hayo, wananchi wanapewa taarifa kwamba hapa patakuwa na *DP* kadhaa, kutakuwa na kitu fulani na kutakuwa na sehemu ya kunyweshea ng'ombe. Kwa hiyo, mradi utakuwa umekamilika kama ambavyo imeelezwa katika mkataba huo. Kwa hiyo, wananchi wapokee mradi ambao umekamilika na wasikubali kupokea miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nimefika hata Mheshimiwa Waziri, tumeendelea kusisitiza; wakipokea mradi ambao una matatizo, Kamati ile bado inakuwa ni ndogo sana, unakuta baada ya muda fulani wanashindwa kuuhudumia ule mradi. Kwa hiyo, wapokee mradi uliokamilika ili Kamati ile au Jumuiya ya Watumia maji itakapopewa majukumu ya kuendesha mradi huo, basi ukiwa umekamilika uweze kuwa endelevu, waweze kumudu matengenezo madogo madogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Ester Bulaya suala lako ni sahihi kabisa. Kauli na msimamo wa Serikali ni wananchi kutoendelea kupokea miradi ambayo haikamilika.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa vijiji 40 wa maji ya Ziwa Viktoria. Mheshimiwa Kitwanga, pale kwenye Kijiji cha Nyang'amango ambacho umekitaja, ni miongoni mwa vijiji ambavyo vitaweza kunufaika na mradi huu wa Vijiji 40. Kwa hiyo, wananchi wawe na subira, tutaendelea kuutekeleza mradi huu na hasa mkitupitishia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Kwa kweli, katika suala kama hili mmeonyesha *concern* yenu ya pamoja; nasi Wizara ya Maji tunachosubiri ni kupatiwa fedha tuweze kufanya kazi. Narudia tena; hatukuwahi kuwaza, hatutafanya na hatujawahi kufanya, kuwa wazembe katika utekelezaji wa miradi ya maji. Pale ambapo fedha zimepatikana kwa kiasi hicho cha asilimia 28 tumejitahidi sana kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja, dakika 50!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kutupatia nafasi hii ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kama ambavyo mjadala ulivyoendelea leo, uliona jinsi gani Wabunge walivyokuwa wamechangia hoja hii kwa hisia kali. Hisia hizi kali za Waheshimiwa Wabunge, zinatokana na tatizo kubwa sana la maji ambalo liko hapa nchini kwetu. Waheshimiwa Wabunge 31 walitoa hoja zao kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge 23 walitoa hoja zao kwa kusema hapa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru sana kwanza wengine kwa kusema kwa ukali kabisa mpaka mate yatoke; na wengine kusema na kusahau kabisa ile staha ya humu ndani kwenye Bunge. Basi siyo kwamba wanafanya mzaha ni kwa sababu ya tatizo la maji lilivyo kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingi zilizotolewa ni nzuri; na kama ulivyoona hatuwezi kupata nafasi ya kuzijibu zote. Tutajaribu sana tupitie zote kwa weledi iwezekanavyo, lakini pale ambapo zitakuwa zimebaki, basi tutaziletea majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, napenda kuishukuru sana Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa Taarifa nzuri ambayo wameitoa. Kwanza napenda kutoa taarifa kwamba Kamati hii imetembelea miradi yetu katika Mikoa karibu yote hapa nchini na kutoa taarifa ambayo ni nzuri sana. Kwa sababu hiyo, taarifa yao ni halisi ambayo ina weledi wa kuangalia jinsi hali ilivyo huko vijijini na maeneo mbalimbali huku mjini. Kwa hiyo, tumezingatia sana mawazo ambayo yametolewa na Kamati na tunaendelea kuishukuru Kamati hii na tunaahidi kuendelea kufanya kazi nayo na kuyatekeleza mawazo waliyoyatoa kwa kadiri ambavyo tunaweza kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, fedha zimekuwa ndiyo moja ya tatizo kubwa sana katika utekelezaji wa miradi yetu ya maendeleo. Kama unakumbuka, katika mwaka 2013/2014 pamoja na nyongeza ya fedha za Shilingi bilioni 184, ni asilimia 53 peke yake ya fedha hizo ambazo zilipokelewa na Wizara kwa ajili ya kutekeleza miradi. Aidha, katika mwaka huu unaokwisha sasa wa 2014/2015 fedha za maendeleo za ndani zimetoka kwa asilimia 26, fedha za Wafadhili zimetoka kwa asilimia 27 na fedha za *OC* kwa ajili ya kusimamia miradi hii zimetoka kwa asilimia 23. Kwa hali hiyo, inakuwa vigumu sana kufikia malengo yote ambayo mmejipangia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tuliandaa kwa ajili ya utekelezaji miradi 1,814 na miradi hiyo imeanza hatua mbalimbali za kujengwa. Iko ile ambayo imesanifiwa na usanifu umekamilika, inangoja Mkandarasi kuanza kazi; lakini iko miradi ambayo imetekelezwa na imefikia asilimia 70 za utekelezaji; na iko miradi 262 katika Wilaya zote hapa nchini ambayo utekelezaji wake uko kati ya asilimia 71 na 95. Aidha, iko miradi 975 ambayo imetekelezwa na kukamilika.

Mheshimiwa Spika, nimepata changamoto sana hapa watu walipokuwa wanasema; mtu anasimama anasema takwimu hizi ni za ubabaishaji! Hatuna takwimu hata moja ya ubabaishaji katika kitabu chetu cha Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuna tafsiri tofauti za kituo cha maji, *kiosk* cha maji na vituo vya kuchotea maji. Katika Ripoti hii vituo vya kuchotea maji, inawezekana katika *kiosk* kimoja, kuwa kuanzia sita, nane mpaka 10 kutegemeana na mabomba ya kuchotea maji yako mangapi. Vile vituo ambavyo vimeelezwa, ni *point* za kuchotea maji, siyo vioski vya maji. Kwa hiyo, unapohesabu *kiosk* kimoja unahesabu na vituo vilivyotajwa, ni idadi ya vile vituo ambavyo watu wanaokuja kuchota maji wanaweza kufungua maji wakayapata au kuyakosa. Kwa hiyo, dada yangu Mheshimiwa Hillal, hiyo ndiyo tafsiri yetu na kwa sababu, hiyo usingeweza kuhesabu vituo 68.

Mheshimiwa Spika, katika mradi alioutaja Mheshimiwa Kafulila, mradi ule umekamilika kwa asilimia 74. Kwa maana hiyo, mradi ule haufanyi kazi kwa sababu haujakamilika; na kwa sababu hiyo anaweza kushangaa kwa nini vimeandikwa vituo? Lakini katika ujenzi wa mradi na vituo ni sehemu au ni *component* ya mradi. Kwa hiyo, ujenzi ule kama umefika asilimia 74 unaweza kuwa umelaza bomba lile kubwa, umelaza mabomba yale ya usambazaji wa maji na kuanza kujenga vituo ambapo mradi ukikamilika maji yatachotewa, lakini ukawa haujawekewa pampu za maji na matanki labda hayajakamilika, na kadhalika. Lakini kwamba, zile namba zimeandikwa kwa mradi uliokamilika kwa asilimia 74, ni sehemu ya ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kwanza nishukuru majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nielezee kidogo *rationale* ya kuweka *DAWASA* na *DAWASCO* katika Jiji la Dar es Salaam. Jiji la Dar es Salaam lina watu wengi sana; hivi sasa tunakaribia kuwa watu milioni tano katika Jiji la Dar es Salaam na mahitaji ya maji na miondombinu ya maji ni makubwa sana. Hivi sasa *DAWASA* inasimamia ujenzi wa Mradi wa Ruvu Chini ambao karibu unakamilika. Mtambo wa maji umekamilika na bomba la maji limebakiza Kilometa 1.5 likamilike.

Mheshimiwa Spika, lakini mradi wa Ruvu Juu bado unaendelea ujenzi. Mtambo umekamilika kwa asilimia 70, lakini ulazaji wa bomba bado haujafikia asilimia 50 kwa hiyo, usimamizi unaotakiwa ni mkubwa na kazi ya kuhakikisha kwamba miradi hiyo inatekelezwa ni mkubwa sana.

Pamoja na hayo, tunachimba visima vya uzalishaji wa maji katika eneo la Kimbiji na Mpera na tunachimba visima 20 vya uzalishaji. Kati ya visima hivyo, ni kisima cha tano sasa ndiyo kinachimbwa. Tunachimba visima vingine vinane vya utafiti pale na kati ya hivyo, visima saba tayari vimechimbwa na kazi ya kusimamia na kuchukua takwimu ya mradi huo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, juu ya hapo, Mji wa Dar es Salaam unahitaji kujengea upya mtandao wa kusambaza maji katika jiji hilo ili kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo sasa hayapati maji, yanapata maji. Pia, Jiji la Dar es Salaam linatakiwa kupanua mtandao wa majitaka na kujenga mitambo ya kutibu majitaka ili kuhakikisha kwamba utoaji wa majitaka katika Jiji la Dar es Salaam unakuwa salama.

Aidha, Mji wa Dar es Salaam hata mvua kidogo ikinyesha tu, mji unakuwa katika *confusion, traffic* haiendi, maji yanalundikana kila mahali! Kwa sababu hiyo, maji ya mafuriko yanafurika pia kwa majitaka. Kwa hiyo, tumeandaa mradi sasa ambao unatekelezwa na *DAWASA* wa kuhakikisha kwamba uondoaji wa majitaka, usambazaji wa maji kwa maeneo ambayo hayajapata maji mpaka sasa na uondoaji wa maji ya mafuriko inafanywa kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali ya Korea ya Kusini imetupatia Dola za Kimarekani milioni 89 kwa ajili ya kutekeleza mradi. Benki ya Dunia imechangia katika mradi huo Dola 220. Aidha, Serikali ya Korea kupitia Benki ya Dunia, pia tunazungumza nayo ili tuweze kupata Dola za Kimarekani nyingine milioni 100 kwa ajili ya kukamilisha mradi huu wote wa utatu ambao unaondoa na kutibu majitaka, unasambaza majisafi kwa maeneo yote ya Dar es Salaam na unaondoa maji ya mafuriko na maji ya mvua kutoka katika mitaro ya Dar es Salaam ili kuhakikisha kwamba mji wetu unakuwa msafi na watu hawapati magonjwa ya kuambukiza ambayo hayana maana.

Mheshimiwa Spika, tumeteua Uongozi mpya katika Jiji la Dar es Salaam kwa ajili ya Shirika la *DAWASCO*. Uongozi huu katika muda mfupi ambao tumeuteua umeonesha kuwa mahiri sana na kuhakikisha kwamba maji yanapatikana katika maeneo mengi yale ambayo maji yalikuwa hayaendi.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, tushirikiane na uongozi huu ambao unafanya kazi nzuri sana ili kuhakikisha kwamba ishara hii nzuri ya maji kupatikana katika maeneo yote ya Kimara, Buguruni na katika maeneo mengi ambayo maji yalikuwa hayaendi, ndiyo wakati mwingine yanakwenda kwa zamu au kwa mgawo, lakini angalau yanafika zaidi ya pale ambapo yalikuwa hayafiki kabisa. Basi, tushirikiane na Uongozi huu, tuwatie moyo na tuwaoneshe maeneo ambayo maji yanavuja na kuharibika, ili waweze kushughulika na matatizo hayo na tuwaachie *DAWASA* na kazi ya kuhangaika na ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu vizuri suala lililoulizwa na Mheshimiwa Azza Hillal. Napenda tu kuongeza kwamba zile fedha Shilingi milioni 200 ambazo Mheshimiwa Azza amezitaja, tayari zimeshapelekwa na kupokelewa katika Halmashauri ya kwake na kwa sababu hiyo hatuna haja ya kuahidi tena hapa kwamba fedha hizo zitapelekwa lini. Fedha hizo tayari

zimepelekwa na zimefika na ninatumaini watu wake watakuwa na furaha kubwa kwamba mambo yanakwenda.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mwaka 2014 tulikuwa tumetenga Shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuhudumia matatizo ya maji katika Miji hii ya Kagongwa, Isaka na Tinde. Lakini kwa bahati mbaya na kwa kutopatikana fedha, kazi ile haikufanywa kama ambavyo tulitegemea. Katika mwaka huu wa fedha, tulianza usanifu wa kina kwa mradi ambao unatoa maji katika Kijiji cha Solwa, Nzega, Igunga, Tabora, Sikonge na Urambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kufanya usanifu wa kazi hiyo, pia ilihusu kupeleka maji katika Miji ya Kagongwa, Isaka na Tinde.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameeleza hapa kinaganaga; asubuhi nilisema, makubaliano ya fedha yasainiwe mwezi huu na hili ndilo ambalo Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema na tumejipanga kwamba mradi huu unavyosainiwa, basi tunatangaza na kumpata Mkandarasi ili kazi ya ujenzi ianze katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme tu kwamba lengo letu ni kuanza ujenzi wa mradi huu kabla ya mwezi Novemba mwaka huu wa 2015. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia tu Mheshimiwa Azza kwamba jambo hili tunalifikiria kwa undani na tatizo la maji la pale tunalijua na tunalihangaikia mpaka likamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa utekelezaji wa miradi hii ya maji ya vijiji ilikuwa inasimamiwa moja kwa moja na Wizara. Ilikuwa ni lazima Benki ya Dunia itoe *no objection* kwa kumpata Mkandarasi wa kusimamia miradi na ilikuwa lazima Wizara itoe *no objection* kwa kumteua Mkandarasi. Tukaona kwamba inakwenda pole pole sana na kwa sababu Halmashauri ni mamlaka kamili, tukachukua miradi hii tukaikasimu kwenye Halmashauri ili Halmashauri ziweze kusimamia kujenga na kukamilisha miradi hii. Kitu ambacho tulihakikisha tunafanya vizuri ni kuhakikisha kwamba Sekretarieti za Mkoa zinafuatilia na kusimamia na sisi tunafuata nyuma kwa kuwapa utalaam, kuwajengea uwezo, kuwapelekea fedha kila tunapopata ili Halmashauri ziweze kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kitu cha kisikitisha sana kwamba Mheshimiwa Mbunge anapelekewa fedha katika Halmashauri yake, halafu fedha zinaibiwa na wafanyakazi wake alio na mamlaka nao. Halafu anakuja hapa Bungeni analalamika anasema wameiba, wamefanya nini; umefanya nini wewe? Wewe mwenyewe umefanya nini kuzuia wizi? Hao wezi mmewachukulia hatua gani? Kwa sababu ninyi ni mamlaka kamili na mna uwezo wa kuwakamata na kuwafunga. Kwa sababu gani hamkufanya? Kwa sababu gani inakuwa hapa ndiyo mahali pazuri pa kuja kupiga parapanda hiyo? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sana sisi kama Madiwani, kama sehemu ya mamlaka kamili ya Wilaya, tushirikiane na Wilaya zetu katika kuhakikisha kwamba wadokozi na wezi na watu wote mafisadi na kila mtu katika Halmashauri zetu tunawashughulikia.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mheshimiwa Keissy alituletea tatizo hili. Sisi Wizara ya Maji tumetuma timu ya *Auditors* kule, wanafanya kazi hiyo. Pia tulimwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais anayeshughulikia utawala bora alipekele suala hili katika shirika letu la TAKUKURU. Tukishaipa kazi TAKUKURU tunaipa nafasi ifanye kazi hiyo. Lakini ingekuwa vizuri kwa Mheshimiwa Mbunge kulifuatilia jambo hili nyuma akashirikiana na TAKUKURU kwa kuwapa taarifa alizonazo ili basi TAKUKURU wapate mahali pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, kama mfanyakazi wa Halmashauri anakodi gari kwa Shilingi milioni 12 na Halmashauri hiyo hiyo mwingine anakodi kwa Shilingi milioni tatu; tungefurahi ungetuambia mmechukua hatua kadhaa kadhaa kwa ajili ya kufanya mambo ambayo siyo mazuri.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, huyo mfanyakazi hata Mkurugenzi… *(Kicheko)*

SPIKA: Mheshimiwa Keissy!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mbele ya Kikao cha Halmashauri… *(Kicheko)*

SPIKA: Ayayayayayah! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Keissy, hili Bunge siyo kikao cha peke yake. Tunaongea kwa utaratibu! Mheshimiwa Waziri, endelea. *(Kicheko/Makofi)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, aliongelea vizuri suala la mradi wa masoko ambao uko katika Wilaya ya Rungwe na suala hili amelileta kwetu mara nyingi. Kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge analihangaikia jambo hili, jambo hili tumelihangaikia kwa muda mrefu sana. Kiongozi wa kwanza kwenda Rungwe kushughulika na jambo hili alikuwa Naibu Waziri, wakati huo Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge na alipokuwa kule walimsimamisha Mkandarasi ili uchunguzi ufanywe kwamba tatizo ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, tulifanya uamuzi kwamba Mkandarasi huyu afukuzwe ili tuteue mwingine. Lakini Baraza la Madiwani likakutana na nusu wa Madiwani wakawa wanaunga mkono hatua tuliyochukua na nyingine ikasema kwamba Mkandarasi huyo aendelee kubaki. Uamuzi huo ulipofanywa, mkandarasi naye akasema kama anabaki, hataki asimamiwe na mhandisi huyo ambaye anamsimamia ambacho ni kinyume kabisa na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mkadarasi huyo tumemsimamisha kazi na Mhandisi Mshauri huyo tumemsimamisha kazi. Tumepeleka fedha, Shilingi milioni 400 ili utaratibu wa kumtafuta Mkandarasi mwingine ufanywe na baada ya hapo, Mkandarasi huyo aanze kazi. Katika bajeti ya mwaka 2015/2016 Shilingi bilioni 1.8 zimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi huo unajengwa na kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, liko suala ambalo linakuja kila siku kutoka Mkoa wa Mara na hili swali ni la ujenzi wa mradi wa Bunda. Nataka kuweka jambo moja vizuri na jambo hilo ni kwamba Mkandarasi anayejenga mradi wa Bunda siyo mzuri sana. Hiyo ni kweli! Lakini kwa muda mrefu mradi pia haukuwa umepelekewa fedha kwa ajili ya kuuhudumia na kwa sababu hiyo ujenzi ulikwenda polepole sana.

Mwaka juzi, 2013 na mwaka jana, 2014 tumepeleka fedha zaidi ya Shilingi bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa mradi huu na ujenzi huu umeendelea na sasa umebaki kidogo sana. Tulitegemea kwamba ujenzi ungekamilika katika kipindi cha miezi mitatu tangu mradi ulipowekewa jiwe la msingi, lakini kwa bahati mbaya tulipoondoka baada ya kuweka jiwe la msingi, ziwa lilichafuka, mvua ilikuwa nyingi mno. Kwa hiyo, kazi ya kujenga *intake* na kupeleka bomba mita 180 ndani ya ziwa ilikuwa shida na kwa sababu hiyo kazi ilisimama ili mvua ipite na ukame uanze tena. Kwa sababu ukame umeanza, kazi ya ujenzi imeanza na ninategemea kwamba hivi punde kazi hiyo itakamilika.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumenunua mabomba kwa sababu tuliona kwamba Mkandarasi yule tukimpa fedha za kununulia mabomba anaweza asinunue mambomba hayo na kuendelea kutuchelewesha katika mradi huo. Kwa hiyo, tuliondoa fedha za mradi ambazo zilikuwa bado hazijatumika tukanunua mabomba yote ambayo yanahitajika. Kwa hiyo, kazi ya Mkandarasi sasa ni kuyaunganisha hayo mabomba na kufunga ili maji yatoke katika Mji wa Bunda. Aidha, kazi ya kusambaza maji mjini, mkandarasi mpya naye ameanza kazi na tunategemea atamaliza kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, nimemsikia Mheshimiwa Esther, lakini alipoongea juu ya mradi wa Mgeta na Mradi wa Ngangaranga. Nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Esther kwamba nitatuma timu ya wataalam pale waende wakakague ule mradi ulivyo kabla mwananchi yeyote hajaupokea mradi huo.

Mheshimiwa Spika, kama Naibu Waziri alivyosema katika kujibu swali siku za karibuni, tusingependa wananchi wowote nchini Tanzania wapokee mradi ambao hawana uhakika nao. Kwa hiyo, wananchi msipokee huo mradi mpaka watalaam wa Wizara waje waukague na waungalie wahakikishe kwamba uko vizuri.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwa miradi ya Kahama, katika eneo la Tenki, lakini pia na maeneo mengine ya Mji wa Kahama ambayo usambazaji wa maji haujakamilika; mwaka 2014 tulitenga Shilingi milioni 500 kwa ajili ya kufanya kazi hiyo, bahati mbaya fedha hizo hazikutoka. Lakini kama mlivyosikia, kama fedha hizo zitatoka, basi fedha hizo zitapelekwa ili kazi hiyo ikamilike. Hivyo hivyo itafanywa katika Tenki la *Old* Shinyanga ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaolinda tenki wanapatiwa maji ili wasibaki kulinda tenki peke yake.

Mheshimiwa Spika, mradi wa kupelekea maji Kishapu kupitia Kolandoto, Maganzo, Mwadui na kadhalika, mradi huo umeanza kutekelezwa. Nami napenda kuwapongeza sana watu wa KASHWASA kwa kazi nzuri ambayo wanafanya. Wamesanifu mradi huo, wamenunua mabomba haraka sana, sasa hivi wanalaza mabomba na kazi inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kuwaeleza kwamba ule Mji wa Kishapu na maeneo yote ambapo zile Wilaya ambapo bomba hilo linapitia ili kufika kwenye mji huo, yana shida kubwa sana ya maji. Lengo letu ni kuhakikisha kwamba katika kipindi kifupi iwezekanavyo, lakini kutegemeana na upatikanaji wa fedha, mradi ule tutaujenga na utakamilika.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niseme kwamba maji yatapelekwa Kolandoto, Maganzo na Mwadui. Kwa hiyo, mamlaka yanayohusika na kuweka maji Hospitali, yajiandae tu kwa sababu mradi utafika Kolandoto hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, nilimsikiliza Mheshimiwa Dvid Silinde nikasikia maneno yake nikasema basi labda *temperature* imepanda kule Momba, kwa hiyo, tumsamehe tu bure, lakini mradi wa maji wa Tunduma umeshasanifiwa na tumepata msaada kutoka Ubelgiji, wenyewe utajengwa hivi punde. Kwa hiyo, asikate tama. Miji mingine ile aliyonayo, yote iko kwenye bajeti yetu hii tunayoendelea nayo, kama fedha zikitoka, basi tutaishughulikia.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tufike mahali hata hizi Kanuni zetu tuanze kuzibadilisha maana inaelekea mtu anaweza kupiga yowe ya kila aina ndani ya Bunge lako Tufuku.

Mheshimiwa Spika, nimemsikia kwa makini sana Mheshimiwa Mgimwa akielezea juu ya tatizo la maji katika Jimbo lake, tatizo la maji ya kunywa katika Vijiji vya Magunga lakini pia tatizo la maji ya mifugo. Kama ambavyo tulizungumza na Mheshimiwa Mgimwa alipokuja

kufuatilia jambo hili ofisini kwangu, Wizara yangu punde ikipata fedha tutautekeleza huu mradi ili kuondoa hili tatizo ambalo limekuwa ni kubwa sana katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imepokea kwa furaha pongezi ambazo tumepewa na Mheshimiwa Mbunge wa Kwimba. Ni kweli kwamba mradi wa Ngudu tuliutekeleza kwa haraka, lakini haraka iliyotumika katika kutekeleza mradi ulitegemea upatikanaji wa fedha. Nataka niseme hivi, tumetekeleza mradi wa Ngudu lakini pia tulitekeleza Mradi wa Karatu na Miradi mingine ambayo tumeitekeleza katika maeneo mbalimbali na sehemu ya miradi 975 ambayo tumeitekeleza na tumeitekeleza kwa hela hizi ndogo ambazo tumepewa.

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu kwa kazi ambayo tumefanya na tunaendelea kuifanya kila siku mgetupa moyo. Msingekuwa mnatulaani hivi kama watu ambao hawafanyi kazi. Mnajua kati ya Shilingi bilioni 488 tumepata Shilingi bilioni 129 lakini tumefanya kazi hiyo tuliyofanya.

Mheshimiwa Spika, halafu kuna watu wengine wanapenda sana kutumia hili neno; "miaka 50" ndiyo tumefikia asilimia 55 ya maji. Yaani utadhani kwamba watoto hawa wanajua mahali pengine pa miaka 50 walipofikia mahali pazuri! Inaniruhusu sana nisikilize na…

SPIKA: Naomba msiwajibu watu wowote wanaoropoka huko mbele mbele! *(Kicheko)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, wengi wa watu hawa wanasema "miaka 50" wamekwenda duniani kwakuwa wewe uliwapeleka kwenye *study tour*. Kwa hiyo, dunia hawaijui! Ndiyo maana wanasema, "miaka 50." Hakuna mtu ambaye haelewi hapa kwamba Bara la Afrika ni Bara ambalo lina umaskini mkubwa.

WABUNGE FULANI: Aaaah!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunaweza kuwa na rasilimali kubwa tu…

SPIKA: Usiwasilikize hao watu!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, lakini tuwe na uwezo wa …*(Minong'ono)*

SPIKA: Ngoja kwanza Mheshimiwa Waziri. Unajua mkianza kuropoka hivi, anachukuliwa mmoja mmoja kuondoka nje sasa hivi. Maana yake nitamtaja mtu fulani atoke na atatoka. Tusikilize kwa sababu ninyi mlisema kwa nguvu zenu zote, naye aseme, ndiyo ustaarabu wenyewe. Muache aseme!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ni vizuri…

SPIKA: Mheshimiwa Waziri! Mheshimiwa Waziri, mimi nikizungumza wewe husemi. *(Kicheko)*

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Kwa hiyo, mwacheni Waziri aseme kwa sababu na ninyi mlisema. Atafanya mbwembwe *style* kama ya kwenu vilevile. Mna *style* za mbwembwe kweli kweli! Haya, tafadhali endelea. Mwacheni ajibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, wananchi wa Tanzania sio watu tu ambao unaweza kuwasemesha na maneno ya kuwahadaa kwamba sisi tutachukua nchi, mnachukua nchi mnaiweza! *(Makofi/Kicheko/Kelele)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shabiby alileta mchango wake wa maandishi, ambao alielezea vizuri tatizo la maji katika Wilaya yake na hasa katika mji wa Gairo. Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu eneo hilo vizuri lakini ningependa kuongeza kwamba, eneo la mto ambao uko katika milima ya Ukaguru ambayo wataalamu walikwenda kuikagua, ni kweli ni chanzo kizuri cha maji, watalaamu wanaendelea kukipima chanzo hicho; na baada ya kukamilika kwa upimaji na usanifu wa mradi huo, basi utekelezaji wa mradi utaendelea.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Abdallah, aliongelea juu ya Mji wa Lindi. Ni kweli kwamba Mji wa Lindi una umeme ambao hautabiriki vizuri, lakini *TANESCO* walipokea maombi yetu ya kuufanya umeme wa Lindi utulie na taarifa niliyoletwa ni kwamba kumekuwa na maendeleo makubwa sana katika utulivu wa umeme katika mji wa Lindi na hivyo kupunguza athari kubwa za ukatikaji wa umeme.

Aidha, ni kweli kwamba maji katika Mji wa Kibiti yana rangi na hivyo watalaamu wetu wa ubora wa maji wamekwenda kuchukua sampuli za maji katika eneo lile ili kuangalia kwamba hakuna madini mazito ambayo yako kwenye maji ambayo yanaweza kudhuru afya za binadamu.

Mheshimiwa Spika, nililetewa pia mchango wa Mheshimiwa Margaret Sitta, aliyekuwa anataka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia maji ya uhakika watu wa Urambo. Taarifa hii nimeitoa kwamba hivi sasa usanifu wa kupeleka maji Urambo kutoka Tabora unafanywa na punde utakapokamilika utaunganishwa na mradi wa Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Mradi wa Jibondo uliotajwa katika hotuba ya Msemaji wa Upinzani kwamba umejengwa sifuri; mradi huu siyo sifuri. Mradi huu tayari mabomba yamenunuliwa kwa ajili ya kuvusha maji kutoka kisiwa kikubwa na kuyapeleka katika kisiwa kidogo na fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, tayari zimepelekwa kwenye Wilaya ya Mafia na hivyo mradi utaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja ambayo ilitolewa kuhusu idadi ya visima ambapo vilipochimbwa wakati wa utekelezaji wa mradi wa vijiji 10, vilitoa maji. Vijiji vyote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tumevihakiki na kuvitoa kwenye kijitabu kidogo ambacho kiligawanywa kwa Waheshimiwa Wabunge wote katika Mkutano wa Kumi na Nane. Katika taarifa ile, jumla ya visima vilivyokuwa vimechimbwa katika programu hiyo, ilikuwa visima 1486. Visima ambavyo vilikosa maji ni visima 496, na visima ambavyo vilipata maji ni 990.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, asilimia 67 ya visima hivyo vilikuwa na maji. Nilikuwa naangalia hapa visima vilivyochimbwa katika Mkoa wa Mwanza, vilikuwa visima 51, visima 10 vilikosa maji na visima 41 vilipata maji. Kwa hiyo, siyo kweli kabisa kwamba visima vyote vya Mwanza vilikuwa havina maji.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja pia kwamba maeneo mengi ya Mjini Mwanza hayapati maji. Taarifa zetu za *performance* ya *MUWASA (Mwanza Water Authority)* inaonyesha kwamba asilimia 96 ya Jiji la Mwanza linapata maji safi na salama. Maeneo ambayo hayapati maji ni maeneo yale machache ambapo mji umepanuka, lakini pia na maeneo yale ya juu ya milima.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unaokuja wa Benki ya Uwekezaji ya Ulaya, ikishirikiana na Serikali ya Tanzania na Shirika la Ufaransa la Misaada Duniani, Euro milioni 104.5 itafanya kazi hiyo. Kazi ya usanifu wa mradi itakamilika mwezi Septemba, mwaka huu (2015) na ninategemea kwamba baada ya hapo Mkandarasi atatueuliwa na kazi ya ujenzi itaanza Mwanza, Misungwi, Magu na Lamadi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru tena kwa nafasi uliyonipa na nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge muunge mkono hoja yetu hi ili sasa tupate fedha twende tukaendelee na utakelezaji wa miradi ambayo bado haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA CHAKULA, KILIMO NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Ahsante, hoja hiyo imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, kesho kipindi cha saa 8.30 baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge, kuna hili shirika letu la *CCBRT*, watakuwa na Kampeni ya Uhamasishaji wa Vita Dhidi ya Ugonjwa wa Fistula kwa Mkoa wa Dodoma. Kampeni hiyo kama nilivyosema, itafanyika katika Viwanja vya Uwanja wa Mashujaa kuanzia saa 8.30. Nafikiri ni pale *Nyerere square*. Kauli mbiu ya Kampeni hiyo ni kwamba "Usione Aibu, Jitokeze, Fistula Inatibika." *(Makofi)*

Fistula nadhani, kama hamjui basi ni magonjwa yanayompata mwanamke wakati wa kujifungua, hasa wanawake ambao ni wadogo. Wakipata ujauzito, matatizo ya kujifungua na hasa wakijifungulia nyumbani huko, wapi, wanaweza wakapata matatizo hayo na ikawa wakati wote ama choo ndogo au kubwa inatoka wakati wote. Matokeo yake ni kwamba, wengi wananyanyapaliwa wanaachwa na watoto wao, basi wanaachwa tu ovyo ovyo. Lakini huu ugonjwa unatibika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kama Wawakilishi wa wananchi, afya yao pia mjali. Kwa hiyo, nawaombeni mhudhurie kile kikao, hiyo Semina itakuwepo pale nje, itakuwa ni Kampeni kubwa. Inasema "Usione Aibu, Jitokeze, Fistula Inatibika." Kwa hiyo, ni saa 8.30, mkipata hapa mnaweza kwenda pale. *(Makofi)*

Tangazo la pili ni kwamba, wale ambao wameteuliwa kushiriki msiba kesho kuzika, ndege itaondoka saa 2.30. Kwa hiyo, watu wawepo pale *airport* 2.00 na tutakwenda kuzika, baada ya kuzika ndege inarudi kutoa *airport* 10.00. Kwa hiyo, wale watakaokwenda, wanarudi kesho hiyo hiyo. Nataka kuamini kwamba wanaokwenda wanajifahamu.

MBUNGE FULANI: Taja majina!

SPIKA: Nitaje majina hamkusikia jana?

MBUNGE FULANI: Wengine hawakuwepo.

SPIKA: Haya basi, ngoja niwaambieni. Kuna Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Mheshimiwa John Mnyika, nadhani yuko huko huko; Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah-, Mheshimiwa Juma Sururu Juma-, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura-, Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir na Mheshimiwa Naomi Amy Mwakyoma Kaihula-,

Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed-, Mheshimiwa Tauhida Cassian Nyimbo-, Mheshimiwa Susan Jerome Lyimo, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Eng. Athumani Mfutakamba, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari-, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga na kutoka Ofisini yuko Ndugu Mathew Kilapilo.

Sasa kama katika hawa niliowataja hawataweza kwenda kwa sababu moja ama nyingine, basi watoe taarifa mapema jioni hii kwa Ndugu Mathew Kilapilo, kusudi aweze kwenda mtu mwingine. Katibu!

KAMATI YA MATUMIZI

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, hii Wizara kwa kawaida huwa inajadiliwa siku mbili, lakini kwa sababu ya hali halisi, imebidi tubanane katika siku moja. Kwa hiyo, ndivyo itakavyokuwa. Katibu!

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 49 - Wizara ya Maji

Kif. 1001 – *Administration & HR Mgt* … … Sh. 4,212,705,000/=

MWENYEKITI: Nimeandika kanuni! Kwa mujibu wa Kanuni Chama Tawala kitakuwa na watu wane; CHADEMA wawili; vyama vingine vyote mmoja mmoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rage!

MHE. ISMAIL A. RAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, sikusudii kushika Shilingi hata kidogo! Ninachomwomba tu Mheshimiwa Waziri, Mamlaka za Maji katika nchi nzima zinafanya kazi nzuri sana, lakini jambo linalosikitisha ni kwamba mpaka sasa hivi wanadai zaidi ya Shilingi bilioni 17. Ukitoa mfano kwa mamlaka ya maji ya TUWASA Tabora, wao peke yao wanadai zaidi ya Shilingi bilioni 1.5. Je, Mheshimiwa Waziri, ili hizi mamlaka ziweze kufanya kazi zake vizuri kusaidia watu kupata maji kadri tunavyoweza, kama tulivyoweka katika ilani ya Chama cha Mapinduzi, una mpango gani wa kuhakikisha wanapata fedha zao? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Hii ni pamoja na Wizara ya Fedha itasaidia. Mheshimiwa Waziri wa Fedha! Wewe Waziri wa Maji pumzika kidogo.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kama nilivyosema awali, kulikuwa kuna *constrain* ya *areas*, lakini nasimama hapa natoa *commitment* kwamba hizi fedha zote zitalipwa mwaka huu. Kabla ya kumaliza mwaka huu wa fedha, tutalipa Dola bilioni 200 na kuanzia mwaka ujao wa fedha tutalipa Shilingi bilioni 856, ikiwemo pamoja na yale madeni ambayo mamlaka inadai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, nataka tu kutoa taarifa kwamba, kuanzia mwaka ujao wa fedha madeni haya yatakuwa yanalipwa moja kwa moja kutoka Hazina. Maana fedha zikiwa zinaingia katika ule mkondo wa taasisi wa Wizara, zinakuwa haziendi kama vile zilivyopangwa. Kwa hiyo, tutakuwa tunazikata pale na tutakuwa tunalipa ikiwemo na madeni ya umeme. *(Makofi)*

MWENYEKTI: Nimesema Kamati ya Bajeti iyasikilize haya maneno anayosema Waziri wa Fedha na mkayafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ahmed Ali Salum!

MHE. AHMED ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Namshukuru tu Mheshimiwa Waziri kwa kazi anayoifanya Jimboni kwangu; na nilipenda tu kujua, katika ile miradi ya *World Bank* ambayo Wizara yenyewe walituruhusu kuendelea kuweka mikataba katika vile vijiji 10 vya *World Bank* na tukafanya hivyo na tukawapa Wakandarasi na wameendelea na kazi, lakini imefika mahali wamesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa miradi hii yote inasimamiwa na Wizara ni pamoja na vile vijiji vitano ambavyo vinasimamiwa na KASHWASA, ambako sasa hivi Mheshimiwa Maghembe, uliahidi utatuletea fedha. Sasa miradi hiyo imesimama.

Mheshimwia Mwenyekiti, naomba sasa kujua kwamba kwa kuwa tayari hii miradi ya *World Bank* 10 na Wakandarasi wameshafanya na wamesimama kwa sababu ya fedha, ni lini sasa fedha hizi utatupatia ili tuendelee na mradi huo pamoja na vilevijiji vitano ambavyo KASHWASA wenyewe wanasimamia na imeshakuwa *designed* tayari kila kitu na Mkandarasi tayari? Mheshimiwa Waziri wa Maji tunaomba hizo fedha na kwa kuwa Waziri wa Fedha yuko hapa, watuahidi ni lini sasa zije hizi tuendelee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwa kweli suala hili la Tinde, Mheshimiwa Makalla alikuja pale kwenye ziara ile, tukapewa maji; tukanywa maji machafu yale, lakini Mheshimiwa Makalla kwa ujasiri akasema mimi siogopi hii kwa sababu nina uwezo wa kutatua hili tatizo. Akanywa yale maji machafu, nami nikanywa. Lakini leo amejibu majibu mazuri sana, fedha ziko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Tinde pale namshukuru sana kwamba tatizo limeisha.

Napenda kuwaambia Kijiji cha Shishilulu kwamba tatizo lile la maji kutoka pale, wasipate matatizo wala wasiwe na taharuki ya aina yoyote; tumeshaongea na Wizara, tumeshaongea na Mkurugenzi wa KASHWASA ni kwamba watapaka kioski kimoja Shishilulu, waache matatizo, mambo yataenda vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa, nilikuwa najaribu kuelewa…

MHE. AHMED ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba majibu kwa Wizara. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Majibu gani ya kuomba fedha tu! Habari ya maji sasa ni mchanganyiko. Kuna *issue* moja ya kwanza ya maji, ile ya pili aah, siyo yenyewe.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza hapa namna ambavyo kwa uwezo ule ambao tumejaliwa tumeweza kutekeleza mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Halmashauri zote zimeendelea kusaini mikataba na Wakandarasi wengi wameacha kufanya kazi. Mimi nasema tu ni faraja kwamba Waziri wa Fedha yuko hapa na ameahidi, sisi kama Wizara ya Maji, tuko tayari tutakapopatiwa fedha hizo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutazisambaza haraka sana katika Halmashauri zote ili tusiendekee kudaiwa na Wakandarasi na Wakandarasi hao waweze kurudi katika *sites* na kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la KASHWASA, ni vilevile tu kwamba mara fedha itakapopatikana, hivyo vijiji vitano vitatekelezwa.

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwangu ni fupi tu. Nilikuwa naomba ufafanuzi. Katika Jimbo langu la Vunjo kuna vijiji vitano vinavyotakiwa vipate maji. Kilema Kaskazini kuna Makame Juu na Makame Chini na kwenye makisio nimeona *1.2 billion*. Imo Makuyuni; kuna Makuyuni (Kilimo) na Lotima pamoja na Mawanjeni, *4.4 billion*. Lakini nimejaribu kuangalia fedha hizi kwenye vitabu sizioni. Nimeona kama Shilingi milioni 400. Naomba ufafanuzi kuhusu hivyo vijiji vitano, hasa Mheshimiwa Makalla, ulimtuma Mheshimiwa Waziri akaja Himo; waambie watu wa Vunjo pale Himo uliona nini na njiapanda? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Hiyo wala siyo sera, lakini ah, jibu tu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kweli nilifanya ziara na nilifika Himo pale na moja ya tatizo ni kwamba kuna kituo cha maji kilikuwa kimefungwa kwa sababu tu ya uzembe; mtu kala hela halafu wakafunga. Niliagiza na kikafunguliwa ili wananchi wale watendewe haki, ashughulikiwe yule kwa kesi ya wizi wa fedha lakini wananchi wa pale waendelee kupata maji. Kwa hiyo, tatizo hilo nililimaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo Mheshimiwa anavisema tutaendelea kutekeleza miradi hiyo, nalitambua hilo na ametuandikia, lakini pia amekuwa akija Ofisini mara kwa mara. Kwa hiyo, hivyo alivyovitaja wa Kilema Juu na vingine vyote tutatekeleza kadiri tutakavyopata pesa, lakini nia yetu ni kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata maji.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mkiwa! Kwani imekuwaje? Mchungaji… *(Kicheko)*

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nina suala moja nataka kuongelea, tunaposema kwamba maji ni uhai na maji ni afya pia; lakini nataka kutoa mfano mdogo tu wa Mikoa ambayo iko kando kando mwa Ziwa Victoria, hasa nikiangalia Mkoa wa Mwanza katika Wilaya ya Nyamagana na Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitaji ufafanuzi kwa sababu haya majibu yaliyojibiwa hapa leo na mwaka wa 2014 katika Wizara hii ya Maji nilijibiwa majibu haya haya, lakini kuna baadhi ya maeneo mengi sana hayapati maji. Hatukatai maji kwenda Shinyanga, kwenda mpaka Tabora lakini Mwanza mnatuachaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mradi mkubwa ambao uko Sangabuye tulikwenda kuutembelea na tuliambiwa mwezi wa pili mwaka 2014 kufikia mwezi wa Saba mradi ule ungekuwa umekwisha. Hapa kwenye bajeti tuliambiwa kwamba mradi ule utakwisha lakini mpaka leo mabomba hayajatandazwa kwa kiasi kikubwa na bado watu wanatumia maji ya ziwani na mpaka watu wamefikia kuchukuliwa na viboko na mamba kwa ajili ya kwenda kutafuta maji na wakati wako watu kando kando ya maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amejibu kwamba Mkurugenzi wa MWAWASA amemwambia kwamba watu wanapata maji kwa asilimia kubwa, ninafikiri ni watu wa mjini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni lini sasa haya mabomba ambayo mwaka 2014 mlituambia yatatandazwa, kwa sababu hayajatandazwa; yatatandazwa lini katika hizi Kata nne ambazo zinatakiwa kutumia mabomba yale ili ziweze kupata maji salama na ya uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Naomba mjibu! Wizara hii hakuna sera, ni huko huko kwao kila mtu!

WAZIRI WA MAJI: Eee, kila mtu anakwenda nyumbani, maana ndiko kura zilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Mkiwa ni kweli kwamba kwanza kwa ajili ya mradi ule mkubwa, majibu ya mwaka jana (2014) na mwaka huu (2015) yamefanana kwa sababu utekelezaji wa mradi kwa maana ya ujenzi haujaanza. Mwaka jana ndiyo tulifikia makubaliano ya utoaji wa fedha. Hatua ya pili ilikuwa ni usanifu wa mradi huu na kazi hiyo inaendelea sasa.

Katika eneo lile ulilolitaja la Sangabuye mradi ule ambao unatekelezwa pale tukishapata fedha tutawapelekea fedha za kukamilisha huo mradi. Siwezi kusema lini, kwa sababu sijui lini tutapata fedha hizo. Lakini ningependa tu nikusihi kwamba uone juhudi ambazo zinafanyika na kwamba mara tu baada ya kupata fedha tutaukamilisha mradi huo na watu wa Sangabuye watapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maeneo ya vilimani ambayo hayana maji sasa na maeneo ambayo yako nje kwenye viunga na mji unapoelekea na yenyewe yatakuwa sehemu ambayo itapatiwa maji na mradi mpya. Mategemeo yetu hasa ni kwamba mradi huo utaanza mapema mwaka 2016 ukianza.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

MWENYEKITI: Kwa sababu Mheshimiwa Msigwa, ali...

Ahaa, Mheshimiwa, vipi? Hujajibiwa!

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Labda naona kama vile Mheshimiwa Waziri anachonijibu ni kitu kingine. Huu mradi mngeupa kipaumbele ukaisha kwa sababu una miaka zaidi ya minne na hauishi. Huu kama siyo mwaka wa tano ni wa sita.

MWENYEKITI: Unaitwaje?

MHE. MKIWA A. KIMWANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sangabuye, wamejenga tenki kubwa ambalo linapaswa litumike kuliko kuujenga mradi huu kwa miaka kama kumi halafu unakuwa hauna faida kwa wananchi. Pesa ya Serikali imelala pale, haifanyi kazi yoyote! Hamwoni haja ya kuupa kipaumbele basi muumalize ili tuusubiri huo mnaosema wa vilimani?

MWENYEKITI: Haya, mwelewane hapo!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndicho nilichosema, kwamba mara tukipata fedha tu tutaukamilisha mradi huo. Tumeahidiwa hapa kwamba fedha zitatolewa. Kwa hiyo, punde zikitolewa, tutaushughulikia mradi wa Sangabuye

MWENYEKITI: *Okay!* Mheshimiwa Msigwa alikuwa amesimama *wrongly*, sasa nikuhalalishe, Mheshimiwa Mchungaji.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mimi nianze kwa kidogo kumshukuru Waziri kwa ajili ya Jimbo la Iringa Mjini kwa kuwa tunapata maji asilimia 95 hivi. Hii ni kuwakumbusha wakazi wa Manispaa ya Iringa kwamba tairi linalopiga kelele ndilo huwa linawekewa *grease*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi ni kwamba mwaka wa jana tulitengewa bajeti ya Shilingi bilioni 510, lakini Waheshimiwa Wabunge tunasahau karibu Bunge zima lilipigia kelele sana kwamba pesa hii haitoshi kutokana na matatizo ya maji; nami ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo. Baada ya kupiga kelele, Serikali iliahidi hapa kwamba itaongeza Shilingi bilioni 184, Waziri Mkuu alisimama hapa kui-*rescue* bajeti hii, *and this is not personal Professor.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali hii ililidanganya Bunge na Watanzania kwa ujumla? Kwa sababu hata katika bajeti ile ya 510 imekuja asilimia 28. Waheshimiwa Wabunge tunasimama hapa tunasifu kwamba tunaipongeza Serikali kwa kazi nzuri mnayofanya. Profesa ni kweli kuna kazi nzuri tunayoifanya hapa? Unawezaje kufanya kazi nzuri kwa asilimia 28 yaShilingi bilioni 510 ambayo haikuja, bado una nyongeza ya Waziri Mkuu Shiligi bilioni 180 haikuja! Tunapongezana nini hapa? Wengi wetu hapa tunakotoka hakuna maji! Mimi ninakotoka kuna maji.

Mheshimiwa Profesa Msolla naye amesema hapa anakotoka ni Mwenyekiti, hakuna maji. Mheshimiwa Mwakyusa unakotoka hakuna maji, ndio wakongwe kwenye hii Kamati ya Kilimo…

MWENYEKITI: Aaah, ingia kwenye hoja, habari ya majina ya watu achana nayo!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupata majibu ya kuridhisha, kwa sababu hapa Mheshimiwa Tundu Lissu aliwahi kusema *another silly season,* tunakuja tunakaa hapa na suti zetu tunajadili mambo lakini mambo haya ni viini macho! Hakuna hela! Tulimlaumu sana aliposema *another silly season!* Tunamaliza miaka mitano ya ahadi mliyoitoa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisipopata majibu mazuri, natoa Shilingi kwa sababu ni lazima Serikali ituambie. Alisimama Waziri Mkuu hapa mkatuahidi hazikutoka; zimekuja asilimia 28, halafu tunapiga makofi hapa, tunapongezana. Maji yako wapi? Tunapongezana hapa, watu wanakufa na ndilo tatizo kubwa katika nchi yetu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa Shilingi kama sitapata majibu ya kuridhisha.

MWENYEKITI: Hata suti leo hukuvaa kwa sababu hiyo? *(Kicheko)*

Waziri wa Fedha amesema, labda hamkuwepo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba urudie! Mheshimiwa Keissy, naomba twende kwa utaratibu. Hajatoa Shilingi, anasema anataka maelezo. Mheshimiwa Waziri wa Fedha!

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimefurahi hata Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ume-*admit* kwamba angalau asilimia 93 ya maji inapatikana *at least* huko unakokwenda. Kwa hiyo, *efforts* zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyokuwa nimesema kwamba kuna fedha nyingi ambazo ziko kwenye *process* na tunatarajia kuzipata.

Kwa mfano, kuna fedha ambazo zitaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambazo ni mkopo wa kibiashara *(external loans concession borrowing)* ambapo tunatarajia kupata kutoka *China Development Bank* Dola milioni 200 na vile vile fedha nyingine ambazo tunatarajia kupata kutoka *Rand Merchant Bank* ya *South Africa* Dola milioni 500. Hizo zote kwa pamoja zitafanya Dola milioni 800 ambazo ndani yake kuna fedha hizo ambazo tumeahidi zitaongezwa; na zenyewe zitaongezwa.

Kwa hiyo, *process* ipo Mheshimiwa na ahadi yetu tutaitekeleza kama vile ambavyo tulivyokuwa tumeitoa.

MWENYEKITI: Ili kukamilisha hili, nimeagiza Kamati ya Bajeti iione hii hizo hela zimekaa wapi. Maana vinginevyo, mnataka kufanyaje? Mimi nimeagiza Kamati yangu ya Bajeti. Haya aliyosema Mheshimiwa Waziri, tunataka kuambiwa na Kamati ya Bajeti yamekaa vipi? Maana yake hivi hivi, tutakuwa tunazungumza tu hapa. Mheshimiwa Msigwa!

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuelewa unachokisema, lakini hizi ni ahadi za mwaka wa 2014. Hiyo anayoleta ni mwaka mwingine. Tunazungumza mwaka uliopita kulikuwa na *commitment* ya Serikali. Haya mambo ya kusema kuna ahadi ambazo wamepewa sijui wapi, *this is the coming year*! Mimi nazungumza mwaka 2014 Waziri Mkuu aliji-*commit* hapa kuongeza. Zile zilizokuwa kwenye bajeti zilikuja asilimia 28. Huu ndiyo uhai wa nchi!

Kwa hiyo, hizi kamba anazotumbia Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni Bajeti inayokuja ya mwaka mwingine. Mapatano yenu na wananchi yanakwisha sasa Oktoba, mnatuambiaje mwaka mwingine? *How far are you sure* ninyi mtakuwepo kwenye *next Government*? Mbona mnataka kutuzunguka! *How far are you sure* kwamba mtakuwepo? Tunazungumza bajeti tunayomaliza. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge waniunge mkono, kwa sababu majibu haya hayaridhishi; tulijadili suala hili. Kwa sababu ilikuwa ni bajeti ya mwaka uliopita! Hii inayokuja ni ya mwakani, mnayosema mtakopa, mnaweza msipate. Hatuna *commitment* hapa, wananchi wanakufa huko tunakotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wananchi bila kujali itikadi za Vyama. Mimi kwangu maji yanatoka, sijui kwenu akina Mheshimiwa Keissy, akina *Jah People* sijui kwenu hakuna maji! Naomba mniunge mkono tuijadili Serikali ilieleze hapa.

MWENYEKITI: Acheni siasa hapa! Mheshimiwa Waziri rudia! Sisi tuliokuwepo hapa, nilimwandikia, eleza habari ya Shilingi milioni 80, eleza habari ya mfuko tulioahidi mwaka 2014, nimemwelekeza Waziri wa Fedha ndiyo maana akaitwa akaja hapa aeleze. Sasa tunataka ueleze tena Mheshimiwa Waziri. Hebu eleza tena, wengine hawakuwepo wakati unajibu.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza hizi fedha ambazo nasema, ni fedha za mwaka huu wa fedha 2014/2015 na siyo fedha za mwakani. Hizi ni fedha ambazo zimekuwa *located* katika mwaka huu wa fedha ambao tunamaliza. Lakini nimetoa *commitment* kwamba zile fedha, Shilingi bilioni 80 tutaendelea kuzilipa kwa sababu tayari tumeshaanza kuzilipa, tayari kuna *list* ya Makandarasi hapa pamoja na madeni mengine ambayo tunaendelea kulipa. Kwa kipindi hiki cha wiki mbili tayari tumelipa Shilingi biloni 57 *across* madeni ambayo yanadaiwa Serikalini na mengine tutaendelea kuyalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna *exchequers* za Shilingi bilioni 30 ambazo zote zinakwenda Wizara ya Maji. Tunazifanyia *process* na zenyewe vile vile zitoke. Pia kuna fedha za miradi mingine mikubwa ambapo mingine tutasaini mwezi huu. Kwa hiyo, fedha zile ambazo ni za 2014/2015 zipo. Vile vile kuna miradi mikubwa ambayo itakwenda ku-*rescue* hali hii ya maji ambayo tutasaini karibuni na itaanza kutekelezwa.

MWENYEKITI: Ndiyo maana nikasema, kwa sababu mara ya mwisho tuliwaachia peke yao, ikawa vile haikuwa. Ndiyo maana sasa nikasema Kamati yetu ya bajeti na Sheria ya Bajeti imesainiwa. Wakafuatilie maneno yote! Mheshimiwa Waziri kaniandikia na nimempa Makamu pale wakafuatilie watakuja ku-*report* wakati wanatoa taarifa humu ndani. Vinginevyo mtabishana tu mpaka kesho, haiwezekani!

Tunayo Kamati ya Bajeti, ni wakati sasa Kamati ya Bajeti ifanye kazi yake. Kamati ya Bajeti inawajibika Bungeni, haiwajibiki kwa Waziri wa Fedha wala kwa mtu mwingine yeyote. Bahati mbaya kipindi kile tulikuwa tunafanya kwa hisani tu, lakini sasa ni hivyo tunavyosema; Kamati ya Bajeti inakwenda kusikiliza haya aliyoyasema Waziri.

Mheshimiwa Moses Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naamini kwa ufahamu wangu kwamba siyo Sera ya Serikali kufanya *transaction* ya fedha kutoka kwenye Wizara moja kwenda kwenye Halmashauri mbalimbali nchini; na kwamba pale sasa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinapokuwa zimeshindwa kusimamia matumizi mazuri ya rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, mathalan miradi ya maji, halafu sasa Serikali Kuu ije ijitoe, kwamba wale wameshindwa na kwamba tumeishia mahali hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza hivi kwa sababu kuna *argument* moja ambayo nimesikia Waziri wa Maji akizungumza, anasema kwamba Madiwani na Waheshimiwa Wabunge wanaonekana kwamba kule ni wasimamizi wa fedha ambazo zinakuwa zimetolea na Serikali. Sasa tunao ushahidi kwamba baadhi ya Halmashauri zimeshindwa ku-*perform*, zimekuwa zina Madiwani hawa wanaoshiriki kufanya biashara na *Council,* matokeo yake miradi mbalimbali imekwama. Kwa mfano, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Serikali kwa nia njema ilipeleka fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji kwa Mji wa Kasulu. Zaidi ya Shilingi milioni 300 zimepotea, zimetafunwa, pesa hizi hazijulikani ziko wapi. Taarifa ya *Internal Auditor* wa Halmashauri imetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wiki jana baada ya Kamati yako ya TAMISEMI ambayo inashughulika na *Local Government,* ilifanya ziara mwezi Januari mwaka huu (2015) wakabaini Halmashauri ya Kasulu haifanyi vizuri na Halmashauri nyingine. Kamati ikaagiza Kasulu ifanyiwe *special audit*. Wamenza mchakato! Imeshabainika kuna upotevu wa Shilingi bilioni 5.9. Miongoni mwa pesa hizo ni Shilingi milioni 300 za maji Kasulu Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata *position* ya Serikali na kama sikuridhika nakusudia kutoa Shilingi. Ni kwa nini Serikali wakati mwingine kunapotokea mambo mazito huko Wizarani, mnasema na ninyi Waheshimwia Wabunge ni Madiwani, mnashindwa kushughulika nao sijui Wakuu wa Idara isipokuwa Mkurugenzi? Kwa nini Seriklai inaji-*contradict* kwenye kutoa majibu ambayo inakuwa ni utata mtupu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule wameharibu ndiyo maana ukiangalia kwenye vifungu vyenu kwa mfano kwenye kasma hii mmetenga pesa za *travel in-country*, lengo ni kwamba Waziri uweze kusafiri kwenda kukagua miradi ya maendeleo inaendeleaje. Sasa unapojivua jukumu hilo, hizi pesa mnatenga kwa shughuli gani? Lengo siyo kwamba ili mkikuta Madiwani wameshindwa na Wakuu wa Idara wameshindwa muweze kuwawajibisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata *position* ya Serikali; maeneo kama haya ya Kasulu ambayo mmetoa pesa halafu hazikutumika na hazieleweki ziko wapi, inaonekana ni ufisadi; Serikali inachukua hatua gani? Wananchi wanakosa maji kwa sababu ya uzembe wa watu wachache, likiwemo na suala la Mheshimiwa Ally Keissy ambalo ametueleza mahali hapa. Naomba kupata *position* ya Serikali kuhusiana na mambo haya.

MWENYEKITI: Maelezo!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala ni la uelewa tu, kwa sababu kila ngazi ya Serikali ni mamlaka kamili. Haina maana kwamba ziko Serikali tatu au nne ndani ya

nchi, hapana. Serikali ni moja! Sasa kama Wahasibu wamekagua na wameona kwamba kuna ubadhilifu wa fedha zote hizo, watu hao ambao wamehusika, ni lazima sheria ichukue mkondo wake. Hakuna msalie Mtume hapo! Hilo la kwanza.

La pili, ni kama hili ambalo lililetwa na Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Keissy!

WAZIRI WA MAJI: Ni Mbunge wa Nkasi, au siyo! Ndivyo nilivyosema.

MWENYEKITI: Anasema, Mheshimiwa Keissy, Mbunge wa Nkasi!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kimetushangaza ni kwamba imechukua muda mrefu kwa Halmashauri yenyewe kutochukua hatua yoyote. Lakini sasa hapa tulipofika, TAKUKURU wameanza kazi na *auditors* wameshakwenda kule, watakagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeyote ambaye amefanya ubadhirifu na kama ambavyo alisema, siyo kitu cha uongo alichosema.

Maana yake anachosema Mheshimiwa Keissy na anarudia mara nyingi nami naomba nirudie jambo hili, ni kwamba mfanyakazi mmoja ana nyumba zaidi ya tano za kupangisha na amezijenga zote kwa mpigo kwa mara moja. Ni lazima kuna jambo ambalo siyo la kawaida. Kwa sababu sasa Wahasibu wamekwenda, TAKUKURU itakwenda kufanya kazi hiyo, ni vizuri tusaidiane nao ili tujue ni kitu gani kimetokea. Kama kuna watu ambao wamefanya ubadhirifu, wameiba, wamefanya ufisadi sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kujitoa hapa, isipokuwa ninachosema, katika ngazi ile tusijitoe haraka. Tuchukue hatua, maana tuna mamlaka. Sheria inatupa mamlaka katika ngazi ile na katika *Central Government* pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri amesema hakuna kujitoa. Sasa nina swali moja ambalo ningependa Serikali inijibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwamba baada ya chombo kama Kamati ya Bunge kufanya ziara kwenye maeneo mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Kasulu; na fedha hizi ni za mwaka 2011/2013 kiasi cha Shilingi milioni 300 ambazo zilitolewa na Serikali kwa nia njema ili kuboresha miundombinu ya maji kwenye Mji wa Kasulu, kwa sababu leo hii upatikanaji wa maji ni kama asilimia 40 kwenye Mji wa Kasulu; pesa hizi hazijulikani zipo wapi! Ni taarifa ya *Internal Auditor*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata kauli ya Serikali chini ya Wizara ya Maji, mwananchi wa Kasulu ambao wameendelea kukosa maji na hata maji wanayopata sasa hivi ni maji machafu kutoka kwenye bomba: Je, Serikali inawasaidiaje wananchi hawa ambao wanataabika kwa sababu ya uzembe na ufisadi wa watu wachache? Wanakosa maji kwenye maeneo tofauti na pengine hata watu ambao wanaweza kuwa wamehusika, majuzi wamehamishwa kupelekwa kwenye Halmashauri nyingine ambapo imani yangu naona kwamba watakwenda kule tena wataharibu halafu hakutakuwa na tija.

Naomba kujua kwamba hizi Shilingi milioni 300 za maji kwa ajili ya Mji wa Kasulu Mjini, pale pale Kasulu Mjini, zitapatikana lini na watu wote waliohusika watachukuliwa hatua zipi? Sitaki kutoa Shilingi naomba tu anipe majibu.

MWENYEKITI: Wala isingewezekana kutoa Shilingi, ni gumu sana hilo.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hapa kuna suala la msingi kwamba hatuwezi kuwaadhibu wananchi wa Kasulu kwa sababu ya watu walioiba fedha na pili; hatuwezi kuwasamehe watu walioiba fedha kwa sababu ni kwenye Halmashauri. Lakini ninachoweza kusema ni kwamba Serikali itahakikisha kwamba mradi ambao ulikuwa unatekelezwa, utatekelezwa kama ulivyokuwa umepangwa lakini wadokozi na wezi tutahangaika nao mpaka sheria ifike mwisho wa mkondo wake.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mfutakamba!

MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye ukurasa wa 86 na 87 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ametaja vijiji mbalimbali vya Uyui kwenye bomba la maji kutoka Ziwa Victoria.

Sasa napenda angalau Mheshimiwa Waziri avitaje vile vijiji vya Uyui kwa sababu sehemu yangu kuna vijiji nimeandika kwenye mchango wangu wa maandishi. Sasa wana Igalula wangependa kujua kama nao watafaidi maji ya lile bomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Aah! Mbona walitaja wakati wanajibu! Wewe hukuwepo? Waziri hebu sema tena. Siyo la kisera kabisa!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza hatua mbalimbali ambazo mradi huu wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Igunga, Nzega na Tabora kupitia Uyui. Kwa hiyo, nataka niseme vijiji bado hatujaweza kuvibainisha vizuri. Usanifu wa kina utakapokuwa umekamilika, tutatoa orodha ya vijiji vyote ambavyo vitakuwa vinahusika katika mradi huo. Lakini Uyui kuna vijiji ambavyo vitapata maji. Kwa hiyo, awe na subira tu, usanifu utakapokuwa umekamilika, tutatoa orodha ya vijiji hivyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lediana!

MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Hoja ya kwangu ilikuwa hiyo hiyo ya Sera ya Maji lakini kwa bahati nzuri Waziri wa Fedha ameshajibu kwamba karibu madeni yote watayalipa. Nami naomba niwapongeze kwa hatua hiyo. Mamlaka ya Maji Safi Iringa inadai Shilingi milioni 430. Kwa hiyo, kwa vile nimekuwa nafuatilia kila siku, naomba hiyo nayo izingatiwe na Wakandarasi wa Iringa Vijijini, Mradi wa Lumuli bado wanadai fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sitarajii kutoa fedha na maelezo aliyoyatoa, nina hakika atazingatia kwamba Iringa Vijijini tunadai na Manispaa. Ndiyo, tunapata maji, lakini madeni ni makubwa kiasi kwamba tunaweza kushindwa kulipa umeme na maji yakashindwa kupatikana. Hilo ndilo lilikuwa tatizo lakini naona limejibiwa nami nitaendelea kufuatilia.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Tumebakiza wiki tatu ili kumaliza mwaka huu wa fedha na leo tunapitisha bajeti ya maji. Lakini bajeti hii ya maji pamoja na mambo mengine ina chagamoto ambazo siyo mpya, ni changamoto ambazo zilikuwepo mwaka 2012/2013; 2013/2014 na 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeainishwa hapa kwamba ni pesa. Sasa umetoa maelekezo kwa Mheshimiwa Waziri lakini akili ya kawaida inatuambia kwa kuwa Serikali ni moja na kwa kuwa Waziri wa Fedha alikuwa anajua kwamba leo tunakuja kujadili bajeti ya maji, alitakiwa ajue kwamba atakuja kutoa majibu gani hapa ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba fedha za ndani za maendeleo ni asilimia 26, zinazotakiwa kwenda vijijini ni asilimia 28, wafadhili ni asilimia 27; unaielekeza Kamati ya Bajeti ikakutane. Tunajuaje Kamati ya Bajeti ikikutana huko, kutakuwa hakuna uhusiano na maamuzi ambayo tungeyafanya leo wakati tunapitisha hii bajeti? *(Makofi)*

Kwa hiyo, nataka nipate majibu kutoka Serikalini kwa sababu najua unasimama hapa kama Waziri wa Fedha lakini Serikali inafanya kazi *collectively*. Hizo fedha unazotuhadithia unatarajia kuzipata, zitapunguza kwa kiwango gani fedha ambazo zilikuwa zimetengwa kwa matumizi ya maendeleo kwa miradi ya maji ya vijijini na kwa mijini? Ni kwa kiwango gani itakuwa imeathiri, kwa mantiki ya kwamba imepunguza fedha za *donors?* Kwa sababu tunaambiwa katika zote walizoziahidi zimekuja asilimia 27, fedha zetu za ndani ambazo katika zote tulizoziahidi imekuja asilimia 26. Itapanda mpaka asilimia 70 itaishi 50 itafika 80 au itafika 100? Ili tujiridhishe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu maneno haya unajua, mwaka 2014 walizungumza haya haya; mwaka 2013 walizungumza haya haya; tumebakiza wiki tatu kumaliza mwaka huu wa fedha. Tuambieni, ikifika tarehe 30 Juni, 2015 Wizara ya Maji itakuwa imepata kiasi gani ili Kamati ikienda kutekeleza wajibu wake, wakati tumeshapitisha, tunajua mlifanya *commitment* hapa kama Serikali. Lakini biashara tunasema funika kombe, tunalifunika, tunamwachia huyu jamaa, anaondoka. Mkienda kule uchochoroni, zinakuja *sound* zile zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wangu wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam umeathirika kwa sababu ulitakiwa umalizike mwezi Machi, 2013 lakini leo mwaka 2015 tunaambiwa kwamba Mkoa wa Dar es Salaam unamalizika mwezi wa Sita…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: *Hallow*! Kengele imegonga!

MHE. HALIMA J. MDEE: Kwa hiyo, watoe majibu *in terms of percentage* siyo kutupa *story* tu hapa. *(Kicheko)*

MWENYEKITI: Haya, Waziri wa Fedha! Hayo ni maswali ambayo yanasaidia Kamati ya Bajeti kwenda ku-*cross check*.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji kwa kumalizia mwaka huu wa fedha tuliahidi kuipatia Shilingi bilioni 110 kwa ajili ya kumalizia miradi yao. Nimetoa *commitment* kwamba hizo fedha zitapatikana. Tutazitoa kwa sababu ni fedha ambazo *source* yake ni fedha za ndani. Kwa hiyo, hizo zitatoka.

Vilevile nimesema kuna *exchequers* za Shilingi bilioni 30 zenyewe, tutazi-*cash*. Tupo kwenye *process* mpaka leo mchana tulikuwa tunazungumza na Mhasibu Mkuu wa Serikali, tupo kwenye *process* ya kuzitoa hizo fedha kwa ajili ya kupata *cash*. Kwa hiyo, hilo litawezekana. Sasa itabakia upande wa utekelezaji na ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wamejipanga vizuri, *once* wakipata tu hizo fedha wataweza kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na fedha za *donors*; tukizungumzia *donors* siyo kwamba tu wao wanatoa fedha bila kuangalia *performance*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, tujue kwamba *donor* anatoa fedha kutokana na *performance* ya mradi wowote. Hatoi fedha tu.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nadhani na hilo tuliangalie *in terms of performance* ya miradi yenyewe *how much* inadaiwa, yaani *in terms of reporting, in terms of implementation power, in terms of procurement plan* ili *donors* na wao waweze ku-*facilitate* kutoa hizo fedha. Lakini kwa fedha za ndani Shilingi bilioni 110 nimetoa miadi na *commitment* kwamba hizo fedha tutazitoa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1002 - *Finance and Accounts* … … …Sh. 1,563,199,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … … … Sh. 4,197,029,000/=
Kif. 1004 - *Government Comm. Unit*… … …Sh. 403,683,000/=
Kif. 1005 - *Legal Service Unit*... … … … … …Sh. 491,560,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1006 - *Procurement Mgt Unit* … … … … Sh. 918,019,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo!

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Kifungu kidogo 221100 - *travel out of the country*, kimetengewa Sh. 1,000,000/= na hizi ni gharama kwa ajili ya safari za nje. Naomba kujua Sh. 1,000,000/= inaweza ikamsafirisha nani nje ya nchi?

MWENYEKITI: Mmekiona? Ni *sub-vote* 1006, kuna Sh. 1,000,000/= tu!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ni Sh. 1,000,000/= lakini fedha hizi zimewekwa hapo kama kushikia hicho kifungu tu kwa sababu hakuna *foreign travel* inayoweza kufanywa kwa Sh. 1,000,000/=.

MWENYEKITI: Maana yake nini?

WAZIRI WA MAJI: Tumefanya hivyo kwa sababu ya ufinyu wa bajeti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, hayo ni maswali mawili tofati. Ufinyu na kushikiwa fedha, hayo ni majibu mawili tofauti. Sasa jibu hasa ni lipi? Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo Sh. 1,000,000/= ni kutokana tu na ufinyu wa bajeti.

MWENYEKITI: Sasa hii ni *traveling,* kwa hiyo, hakuna kusafiri? Hiyo ni *Procurement Management Unit,* sasa ni kwamba hakuna kusafiri au ni nini?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ina maana kwamba katika mwaka huu wa fedha hawatatumia bajeti yao kwa ajili ya kusafiri kwa sababu fedha zilizotengwa ni kidogo sana.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1007 - *Mgt Information Sys*… … … … … Sh. 492,285,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1008 - *Internal Audit Unit* … … … … … Sh. 676,243,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najielekeza pale kwenye kasma ya 221400 – *Hospitality, Supplies and Services,* ukiangalia *trend* ya pesa imekuwa ikiongezeka kila mwaka, sasa hizi pesa naomba kupata ufafanuzi ni sababu gani zinazowafanya Wizara kwenye *section* au *unit* ya *Internal Audit* kuongeza pesa kwa kiasi kikubwa namna hiyo kwenye mambo haya kwa sababu nimengalia kwenye maeneo mengine nyuma kuna mahali ambapo wamejitahidi kupunguza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za msingi ni zipi? Napenda tupate kauli ya Serikali, hizi pesa huko kwenye miradi ya maendeleo tumeona kwamba mmelalamika kuna pesa kidogo na nyingine hampati. Naomba Mheshimiwa Waziri atueleze, ni sababu gani zilizopelekea pesa itoke Sh. 5,000,000/= mpaka kufikia Sh. 14,000,000/=? Ni ni pesa za utafunaji hizi!

MWENYEKITI: Maneno mengine! Hebu mtoe maelezo!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la fedha hii ni kutokana na kuongezeka kwa vikao vya kujadili *report* za ukaguzi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika *program* ya maji inayoendelea. Kwa hiyo, ni vikao ambavyo vitakuwa vinafuatilia ukaguzi wa miradi ya maji.

MWENYEKITI: Pamoja na ile ya Kasulu! *(Kicheko)*

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 - *Water Resources* … … … … … Sh. 7,409,978,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sabreena!

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nipo kwenye kifungu kidogo cha 220300 kwenye *Fuel, Oil and Lubricant.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka 2014 ilitengwa Sh.15,200,000/= lakini mwaka huu kuna Sh. 116,000,000/=. Ongezeko hilo ni kubwa sana. Napenda tupate ufafanuzi kwa nini imeongezeka kwa kiasi hicho. Ahsante!

MWENYEKITI: Mmekiona?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko hili linatokana na kupanda kwa gharama ya vipuri kwa maana ya kubadilika kwa bei, kwa hiyo, ndiyo maana imeongezeka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia nahoji kifungu hicho hicho ingawa majibu ya Mheshimiwa Waziri hayaridhishi kabisa. Haiwezi ikapanda kwa asilimia 765 tofauti ya mwaka 2014 na mwaka huu (2015).

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2002 - *Central Zone* … … … … … … …Sh. 412,012,000/=
Kif. 2003 - *Water Laboratory* … … … … … Sh. 2,916,057,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 - *Urban Water Supply and Sanitation*... ... ... Sh. 4,100,466,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Susan Lyimo!

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha 220200 - *Utilities Supplies and Services.* Kwenye randama inaonyesha kwamba fedha hizi ni kwa ajili ya kulipia umeme kwa mamlaka za maji za Daraja C na B pamoja na mamlaka za maji za miradi ya Kitaifa kwa ajili ya kuendesha mitambo ya kusukuma maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimamia kifungu hiki kwa sababu ukiangalia mwaka 2014 zilikuwa Shilingi bilioni tatu na mwaka huu Shilingi bilioni moja, wakati Mijini hasa Dar es Salaam kumekuwa na tatizo kubwa sana la pampu hizi na umeme kukatika kwa maana ya kwamba hawalipi fedha za umeme.

Sasa kama mwaka huu tumekuwa na tatizo kubwa hivyo na zilikuwa ni Shilingi bilioni tatu, mwaka huu zinakuwa Shilingi bilioni moja, tutaendelea kuwa na matatizo makubwa sana ya maji kwenye Miji na Majiji. Naomba kujua ni kwa nini fedha hizi zimepungua kwa kiasi kikubwa namna hii zaidi ya Shilingi bilioni mbili?

MWENYEKITI: Na kwamba mnatanyaje kazi? Ndiyo kikubwa hicho! Mheshimiwa Waziri, mmekiona kifungu anachokisema Mheshimiwa Susan?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekiona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miji hii ambayo inalipiwa umeme kwa sababu haijiwezi yenyewe ikalipia mishahara, umeme na madawa; *status* ya miji hii inabadilika mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, Mji wa Singida ulikuwa kwenye *category* hii mwaka 2014, lakini kwa sababu mradi wa maji wa Singida umekamilika na upatikanaji wa maji umeongezeka mpaka asilimia 86, Mji huo umetoka sasa *category B* umeingia *Category A* ambao unajitegemea wenyewe.

Kwa hiyo, ipo miji ya namna hii ambayo inategemea kuondoka huko ukiongeza na Musoma na kama tukimaliza kwa wakati mradi wa Kigoma pamoja na Lindi, miji hiyo itaondoka na kwa sababu hiyo deni tunategemea lipunguwe.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 - *Rural Water Supply* … … … … ...Sh. 2,249,583,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mangungu!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nataka nipate ufafanuzi kutoka kwenye Wizara kwamba, ukiangalia kwenye kifungu hiki, jumla ya fedha ambazo zimetengwa ni shilingi bilioni 2.4, Mjini kwenye *Urban Water Supply* imetengwa shilingi bilioni 4.1. Hivi Wizara…

MWENYEKITI: Ngoja kwanza tuwe pamoja, mimi sijakuelewa. Unazungumzia wapi?

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho cha 4001.

MWENYEKITI: Enhe, kifungu kidogo kipi!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Nimeichukua jumla yote!

MWENYEKITI: Aah, haiko hiyo kazi ya kujumlisha kwa jumla. Mheshimiwa Ole-Medeye!

MHE. GOODLUCK J. OLE – MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye kasma ya 220200 - *utilities Supplies and Services*.

MWENYEKITI: *Sub-vote 4001, item 220200.*

MHE. GOODLUCK J. OLE – MEDEYE: Eeh, kasima 220200.
MWENYEKITI: Ni *item!*

MHE. GOODLUCK J. OLE – MEDEYE: Ndiyo! Sasa swali langu ni kwamba…

MWENYEKITI: Inahusu nini? Inahusu *Utilities Supplies,* siyo!

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Ndiyo!

MWENYEKITI: *Okay!*

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Katika kasima hii zimetoka Shilingi milioni 170. *Of course* zimeshuka kutoka Shilingi milioni 511 mwaka juzi kwa maana ya mwaka ule uliopita, kuja Shilingi milioni 162 mwaka uliopita na sasa hivi Shilingi milioni 170.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye umesema *item* gani?

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Nimesema kasma 220200.

MWENYEKITI: Eeh, sasa inasema *Utilities Supplies and Services!*

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Ndiyo!

MWENYEKITI: Hiyo hesabu mbona haifanani?

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Naam!

MWENYEKITI: Hesabu siyo yenyewe. Hesabu mwaka mmoja ni *zero;* mwaka huu ni nine…

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Kifungu 4001 - *Rural Water Supply,* kasma 220200

MWENYEKITI: Ndiyo.
MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Jamani, mimi nazungumza kilichoko kwangu!

MWENYEKITI: Eeh, zungumza. Lakini naona kama unasema *figure* ambayo siyo.

MBUNGE FULANI: *Figure* siyo.

MWENYEKITI: *Figure* siyo. Kwanza mwaka …

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Aah, *sorry*! Samahani imewekwa sifuri.

MWENYEKITI: Mwisho ni sifuri hivyo hivyo.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Ni sifuri.

MWENYEKITI: *Okay!*

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza juu ya kasma hii kwa sababu kama tunavyojua ni kwamba mojawapo ya kazi za kasma hii nadhani ni kusaidia mamlaka za maji ambazo ziko vijijini ambazo hazina uwezo wa kujilipia gharama za umeme na nyinginezo.

Sasa kwangu mimi tuna Mamlaka ya Maji ya Arusha Vijijini na ambayo mara ya mwisho nilipokutana na Meneja mwezi uliopita alinijulisha moja ya changamoto alizonazo ni gharama za umeme kwenye visima wanavyosukuma maji. Sasa naomba tu Mheshimiwa Waziri anieleze kwamba kwa mamlaka kama hizo wanasaidiaje gharama za umeme?

MWENYEKITI: Kifungu chenyewe hakina hela! Wewe huwezi kutafuta kifungu kinacholingana na haya.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikaulizia kwa sababu kama hakuna fedha na sisi tunahitaji kusaidiwa, watatusaidiaje?

MWENYEKITI: Uliza ni kwanini hapa hakuna fedha? Tafadhali, tunaomba utujibu hapo!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki hapa kinaonekana hakina fedha lakini malipo hayo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 yatafanyika kupitia Idara ya Utawala.

MWENYEKITI: Kifungu hicho kinaafikiwa?

MBUNGE FULANI: Ndiyooo!

WABUNGE FULANI: Badooo!

MWENYEKITI: Aah, ndiyo nilikuwa na wengi kweli, samahani. Yupo Mheshimiwa Machali kwanza, halafu Mheshimiwa Suzan.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma 221400 - *Hospitality Supplies and Services* tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kama nilivyouliza kwenye kifungu kile kilichotangulia; mwaka 2014 ilikuwa *zero* na mwaka 2013 ilikuwa *zero* na mwaka wa fedha 2015/2016 inaonekana kwamba Wizara inaomba Shilingi milioni 18. Naomba ufafanuzi, kama ilikuwa *zero* kule, hawakuona sababu ya kutenga fedha mwaka 2013 na mwaka 2014, inawezekana labda walitenga kwenye utawala. Kwanini mwaka unaofuata pengine mmetenga fedha nyingi namna hiyo kutoka kwenye sifuri? Naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Tulijifunza kuwa *precise*. Sasa jibu Mheshimiwa Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2014/2015 kifungu hiki hakikupewa fedha kutokana na ufinyu wa bajeti. Kwa hiyo, safari hii tumeweka fedha hizo.

MWENYEKITI: Ni kwa ajili ya kazi gani?

NAIBU WAZIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinagharamia vyakula na maji katika vikao vya kazi pamoja na kumlipa mfanyakazi bora wa Idara.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suzan!

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Niko kwenye kifungu kidogo cha 221000 - *Travel - in - Country*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika randama inaonesha wazi kwamba fedha hizi zinatumika katika kugharamia safari za kikazi ndani ya nchi kwa ajili ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama katika kifungu hiki kwa sababu ni wazi kwamba bado vijijini ndiko kwenye miradi mingi na ndiko kwenye watu wengi na vilevile bado kuna tatizo kubwa la maji. Lakini ukiangalia *trend* ya hiki kifungu ukilinganisha na kile cha *urban* utaona kwamba kwa *rural* hizi fedha zimekuwa zikipungua kila mwaka wakati kifungu hicho hicho kwa mjini kimekuwa kikipanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali, ni kwanini fedha zinaendelea kushuka wakati ilitakiwa huku vijiji ndiyo fedha ziwe nyingi kwa sababu ndiko kwenye watu wengi na vilevile ndiyo

sehemu ambayo bado kwa kweli wananchi wengi hawapati maji safi na salama? Kwa hiyo, naomba ufafanuzi, ni kwanini mijini wamepewa fedha nyingi katika kifungu hiki na vijijini wamepewa fedha kidogo sana? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Suzan Lyimo. Tumeweka fedha hizo na zinaendelea kushuka tu. Ni kwa sababu ya *trend* nzima ya kupokea fedha za *OC*. Fedha hizi ni kwa ajili ya kufuatilia miradi, lakini pia zimetengwa katika miradi ya maendeleo kwa maana ya kufuatilia huko pia.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba nitumie mamlaka niliyonayo kuongeza dakika 30 baada ya saa ya kuahirisha Bunge. Endelea!

Kif. 4002 - *Water Sector Program Coordination Unit* … … … … ... ... Sh. 396,758,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nazungumzia kasma 210300 - *Personal Allowances.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi wa tofauti ya kazi zinazofanywa na kitengo hiki na zile zinazofanywa na Idara ya Mipango. Kwa sababu utakapoenda kwenye miradi ya maendeleo, utakuta kwamba fedha kwa ajili ya *coordination* ya *WSDP* zipo Idara ya Mipango. Sasa ningetaka nijue tofauti ya kazi zao ni nini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika makubaliano ya uendeshaji wa programu hii ya maendeleo ya Sekta ya Maji, kuna mjadala wa karibu kati ya Serikali na wale wafadhili ambao wanachangia fedha kwenye kikapu *(basket fund)* ya programu hii. Hayo makubaliano ni pamoja na kuwa na kitengo maalum kinachosimamia mfuko huo, lakini pia kinachoratibu miradi ambayo itatakiwa kuje mbele ili kuhakikisha kwamba hatumalizi fedha za mwaka huu bila kujua kwamba mwaka kesho tunakwenda wapi na mwaka kesho kutwa tunakwenda wapi. Hicho pia ndicho kitengo ambacho tunapata msaada wa kitaalam kutokana na Wafadhili ambao tunashirikiana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kina kazi mahsusi kabisa tofauti na Idara ya Mipango ile ya Wizara.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 5001 - Water Dev. & Mgt Institution.. ... Sh. 334,071,000/=

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 6001 - *Drilling and Dam Construction Agency*… … … … ... ... Sh. 869,429,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mangungu!

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nilitaka kufahamu tu kwamba katika kifungu hiki fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya mishahara tu. Kitengo hiki kwa sisi tunaotoka vijijini ndicho kinachotusaidia kuchimba visima na kuweka mambo yetu vizuri katika suala la maji. Je, watafanyaje kazi na hawakutengewa fedha?

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Waziri hebu jibu.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana. Hii ni moja ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Serikali imeinunulia vifaa kwa ajili ya kuchimba visima na pia inafanya kazi ya ujenzi wa mabwawa. Katika kazi hizi huwa inachukua tenda na kwenda kufanya hasa ile miradi ya Serikali kule Wilayani na maeneo mengine. Katika miradi hii wanatakiwa waitekeleze kwa kulipwa. Kwa hiyo, kitu ambacho Serikali inahakikisha ni kuwapa vifaa, kuwalipa mishahara na gharama nyingine zote, ni lazima wajiendeshe wenyewe na katika faida yao ni lazima walipe kodi.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 49 – Wizara ya Maji

Kif. 1001 - *Administration and HR Mgt*… Sh.12, 410,290,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Suzan Lyimo!

MHE. SUZAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho 3308, hizi fedha ni kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Wizara pamoja na Ghala za Bohari Kuu, kule Boko. Ukiangalia jumla ya hizi fedha, sasa hivi zitakwenda Shilingi bilioni 26. Naomba kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, jengo hili la ofisi liko katika *status* gani? Kwa sababu kama ni pale Chuo cha Maji ambapo napita kila mara, ndiyo kwanza wanaanza. Sasa nilikuwa naomba kujua, hizi fedha ambazo zimeshatumika miaka yote hiyo zimefanya kazi gani?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, maelezo!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba jengo hili limekuwa linaendelezwa, nadhani huu sasa ni mwaka wa pili. Lakini unaelewa kwamba jengo linapoanza kujengwa fedha hazilipwi zote kwa mara moja. Zinalipwa kutokana na kazi iliyokamilika. Kwa hiyo, fedha hizo ambazo zitapokelewa zitaendeleza ujenzi pale ulipofikia.

MWENYEKITI: Ni *foreign*.

WAZIRI WA MAJI: *Foreign?*

MWENYEKITI: Eeh, ni *GTZ*.

WAZIRI WA MAJI: *Yes,* kwa sababu wanashiriki pia Washirika wa Maendeleo wa *basket funding*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa pale tulipo tumepewa *notice* ya kuhama kwa sababu eneo lile litakuwa sehemu ya kujenga *fly over* pale kwenye makutano makubwa ya Ubungo. Kwa hiyo, ujenzi umeanza na ninategemea utaenda kwa haraka ili kazi hiyo ikamilike na Wizara ihamie kule.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 1003 - *Policy and Planning* … … … Sh.15,227,256,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye.

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa kwenye Kitabu cha Matumizi ya Kawaida nilizungumzia juu ya uhusiano wa *unit* ile ya *coordination of WSDP*…

MWENYEKITI: Ukienda kwenye *item* unatupa raha zaidi kuliko *unit*.

MHE. GOODLUCK J. OLE – MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa, ni kasima 3436. Wakati nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli hii iliyoainishwa hapa ni nyingi sana; Shilingi bilioni 11 kwa ajili ya kazi ya *monitoring and coordination*. Uka-*coordinate* nini kama miradi ya kutekelezwa haipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hujapeleka fedha kwenye miradi, unatenga fedha zitakazokaa ofisini kwa ajili ya watu wa mipango kutumia, kufanya nini? Nilipendekeza kwamba fedha hizi zihamishwe ziende kwenye miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atueleze kazi zitakazofanyika katika kifungu hiki ni zipi na ni kiasi ambacho yuko tayari kutoa ili ziende kwenye *rural water* ambako ndiko kwenye mahitaji makubwa sana.

MWENYEKITI: Tunaomba maelezo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Wizara yetu inatekeleza miradi ya *BRN*, lakini pia miradi hii maeneo mengi; ipo miradi mikubwa ya Kitaifa, Kimikoa na miji. Kwa hiyo, maana yake kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, huo ndiyo uratibu hasa wa miradi kwa maana ya sisi mnapotutaka tufuatilie na tusijitoe katika hizo lawama, tushirikiane kwa pamoja maana Wizara ya Maji imetenga fedha hizo kwa maana ya kufuatilia na kuratibu miradi hiyo kote; iwe ya vijiji 10, *BRN*, miradi mikubwa ya Kitaifa na miradi ya kimkakati yote, ndiyo maana yake hasa.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 2001 - *Water Resource* … … … … Sh. 34,794,782,400/=
Kif. 2003 - *Water Laboratory*... … … … …Sh. 7,537,834,000/=

(Vifungu viilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 3001 - *Urban Water Supply and Sanitation... ... … … … … …*Sh. 167,540,236,000/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mashishanga!

MHE. RACHEL M. ROBERT: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilikuwa nataka kuzungumzia *sub-vote 3001 item 3403 Lake Victoria* kwa maana ya KASHWASA. Naona mwaka huu fedha imepungua zaidi ya Shilingi bilioni mbili. Naka kujua ni kwanini kwa sababu kutokana na mchango, wangu nimezungumzia kwamba tunahitaji mradi huu upanuke ili watumiaji wawe wengi na gharama zipungue kwa mtumiaji wa mwisho. Nilikuwa naomba ufafanuzi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli fedha hizi zimepungua na hasa miradi hiyo ya Kagongwa, Isaka, Tinde na maeneo mengine ambayo aliyoyataja. Yote hii inatokana tu na ufinyu wa bajeti.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima Mdee!

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kidogo cha 3437 ambacho kinahusiana na upanuzi ama usambazaji wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam ambao unahusu Ruvu Chini na Ruvu Juu; nataka tu nipate ufafanuzi wa Serikali. Mradi wa Ruvu Chini ulitakiwa umalizike mwaka 2013. Leo kwenye Hotuba yake Mheshimiwa Waziri ametuambia utamalizika mwezi Juni ambayo ndiyo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nijue hizi fedha zilizotengwa hapa, zina uhusiano na Ruvu Chini kwa mantiki ya kwamba tutarajie mradi usimalizike mwezi huu, tutarajie miezi kadhaa ijayo kwa sababu kumbe ulikuwa haujakamilika kama inavyotakiwa? Kwa hiyo, nataka nijue tu kwamba, hizi fedha zina uhusiano gani na kukamilishwa kwa Mradi wa Ruvu Chini ambao una-*cover* Jimbo zima la Kawe!

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Mwezi wa Sita leo kama ambavyo wamesema ndiyo biashara kule tumemaliza ama vipi? Ni hayo tu.

MWENYEKITI: Mnamaliza ile nyingine halafu hii inabakia. Mnamaliza Ubunge, Mheshimiwa Waziri!. *(Kicheko)*

WAZIRI WA MAJI: Anaogopa huyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Halima Mdee kwa swali lake zuri.

Kitu ambacho kimetuchelewesha katika bomba lile kukamilisha ni *Court injunction* ambazo tumepewa 14 na hivi sasa ni mbili tu zimekalika ambazo tumepata. Hilo ndilo tatizo kubwa, sasa fedha hizi ambazo zimetengwa hapa zinahusu pia mradi wa kusambaza maji kuanzia Tegeta na maeneo yote mpaka kufika Bagamoyo.

Kwa hiyo, fedha hizi zinahitajika na mradi huu utaanza wakati wowote ili kuhakikisha kwamba maji yanasambazwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lolesia!

MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti,sante sdana kwa kunipa nafasi. Niko kwenye *sub-vote 3001,* kifungu cha 3309 - *Reginal Headquoter Water Project*. Nilitaka tu kujua…

MWENYEKITI: Ngoja tuwe pamoja. Ni kifungu gani?

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: 3309 - *Regional Headquoter Water Project*.

MWENYEKITI: *Okay!*

MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kupata ufafanuzi kutokana na kwamba kuna hii Mikoa mipya ambayo inahitaji fedha nyingi sana kwa ajili uanzishwaji wa miradi ya maji katika Mikoa hii mipya ukiwemo Mkoa wa Geita, ningependa kupata ufafanuzi: Je, hizi fedha pia zina-*include* Mikoa mipya?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sahihi kabisa kwamba fedha hizi zinahusika na Mikoa mipya ikiwemo, Geita, Simiyu na Mikoa mingine.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila Mabadiliko yoyote)

Kif. 4001 - *Rural Water Supply* … … … ... Sh.189,747,505,600/=

MWENYEKITI: Mheshimiwa Matiko! Aah, Mheshimiwa Ester Bulaya kwanza! *(Kicheko)*

Naomba msimame wale ambao nilikuwa nimewaita!

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nami nilikuwa ninaulizia sub *vote 3280* nilitaka kujua Mheshimiwa Waziri kwamba, katika fedha hizi zilizopo kwasababu sijaona mradi wa Bunda hapa ukiwa umetajwa, nilitaka kujua, katika fedha hizi zilizopo…

MWENYEKITI: Hebu, mimi sikufuatilia. Kaeni wapendwa. Unazungumzia item ngapi? Ngapi?

MHE. ESTER A. BULAYA: 3280.

MWENYEKITI: Ngapi?

MHE. ESTER A. BULAYA: Kasma 3280.

MWENYEKITI: Endelea!

MHE. ESTER A. BULAYA: Nilikuwa nataka kujua kwamba kwenye hizi fedha zilizopo, ni miongoni ambapo mtaenda kukamilisha ule mradi wa Bunda? Maana pia kwenye maelezo yako nimekusikiliza vizuri, hakukuwa na Ziwa kuchafuka wala hakuwa na mvua kama ya Dar es Salaam ya kufanya mradi huu usiendelee. Maana mimi nilikuwepo wiki mbili katika mashindano ya *Ester Cup*.

Kwa hiyo, nataka kujua kwenye hizi fedha mradi wa Bunda unahusika hapa au tayari Mkandarasi mmeshampa pesa?

MWENYEKITI: *Ester Cup* pamoja na Esther Matiko au Vipi? Mheshimiwa Naibu Waziri! *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ni kwa ajili ya utekelezaji wa vijiji vyote kumi na vile vya matokeo ya haraka sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, zinaenda katika Halmashauri mbalimbali kutekeleza hivyo vijiji kumi na vile vya matokeo ya haraka. Kwa hiyo, mradi wa Bunda nao uko katika bajeti nyingine.

MHE. ESTER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, niko kwenye hiyo *subvote 4001 - Rural Water Supply* lakini kifungu kidogo cha 3216 ambayo ni *expansions and rehabilitations of rural water supply*. Hapa inaonyesha wametenga Sh. 16,445,000,000/= fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kuuliza na hii pia ni kufuatia ule mradi wa Kijiji cha Gibaso ambao ulitumia zaidi ya Shilingi milioni 350 na kwenye kitabu wameainisha, una vituo 18 na Waziri amejibu kwamba unaendelea kutoa maji, lakini kiuhalisia kuanzia mwaka 2012 haujatoa maji hata tone.

Sasa hapa wameonyesha kwenye randama kwamba ni kupanua na kukarabati miradi ya maji vijijini. Vile vile kwenye swali langu la msingi nilitaka kujua kwa mwaka 2014 waliomba hizo fedha za ndani Sh. 16,445,000,000/= lakini hadi wanawasilisha randama hii, walikuwa wamepokea Shilingi bilioni 1. 7 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua ni kwa nini sasa tusiwe na bajeti ambayo ina uhalisia, unajua kabisa mwisho wa siku hamwezi kupokea hizi Shilingi bilioni 16, lakini mnaendelea, sijui mnafanya *copy and paste,* mnaendelea kuweka Shilingi bilioni 16. Ni kwa nini msingeweka angalau Shilingi bilioni tano na mkabajeti miradi ambayo mtaitembelea kwa mwaka huu? Siyo kuweka hela nyingi wakati mnajua mwaka unaisha mna Shilingi bilioni mbili au Shilingi bilioni 1.7. Ndiyo swali la msingi.

MWENYEKITI: Sasa hilo swali; haya, hebu jibu!

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mheshimiwa Esther unauliza swali gumu namna hiyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesema hapa ya kwamba fedha zote zile ambazo tunadaiwa zitatoka. Kwasababu hiyo, hizo fedha ambazo tutapewa zikishakuwa *factored* kwenye bajeti ya *current year,* hiyo ambayo imeonyeshwa hapo itabadilika. Kwa hiyo, tunategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikusemea *specifically* huo mradi wa Gibaso, lakini fedha hizi tukizipata na hawa wataalamu ambao watakwenda kukagua ile miradi ya Bunda, hao hao watakwenda pia na Gibaso waangalie na waone ni jinsi gani tunaweza kuukwamua huo mradi ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Machali!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Njielekeza pale kwenye Kasma 3341 *Same, Mwanga and Korogwe Water Project*. Hapa nina maswali kama mawili ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri.

Moja, nilikuwa naomba Serikali itusaidie, katika *project* hii mwaka 2014 zilitengwa takriban Shilingi bilioni *30 plus. Project* hii imepata pesa kiasi gani hadi sasa hivi tunapokutana?

Pili, ukifanya *analyisis* ya *allocation* ya fedha kwa ajili ya miradi mingine, unakuja kuona inawezekana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa ndio mwenye dhamana au anatenga fedha nyingi kwa ajili ya kwenda kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili Mheshimiwa Waziri anapaswa ku-*declare interest* kwasababu ukiangalia kwenye vifungu vingine, unakuta kwamba miradi imetengewa fedha kidogo. Unaweza kuangalia pale, kwa mfano, hata ile *Rural Water*…

MWENYEKITI: Usitupige *lecture* hapa, tunamalizia. Huu ni mradi *in a forex.*

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia.

MWENYEKITI: Eeeh!

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kile kifungu cha 3216 amesema kwamba kwa nchi nzima zimetengwa pesa hizo...

MWENYEKITI: Wewe unaongelea cha thelathini na...

MHE. MOSES J. MACHALI: Aaah, natoa mfano tu kuonyesha kwamba….

MWENYEKITI: Hapana tumepita hapo. Unaingia 3341 ndiyo swali lako.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, najenga hoja, ni kifungu 3341 kwamba ukiangalia kule sehemu nyingine wametenga fedha kidogo kwa nchi nzima lakini unakuta *project* moja hii; sasa sijui ni kwa sababu pengine Mheshimiwa Waziri *project* iko kwake, wanatenga fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba watueleze, katika fedha ya mwaka tariban Shilingi bilioni 30 *plus;* kwanza walipata kiasi gani? Pili, kwa mwaka huu wa fedha ni kwa nini wanaendelea kutenga fedha nyingi kwenye *project?* Au ni kwasababu pengine Mheshimiwa Waziri *project* iko kwake? Tunaomba aweze kutupa *statement* ni kwa nini wanafanya hivi, halafu maeneo mengine yanatengewa fedha kidogo.

NAIBU WAZIRI: Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni mradi wa Kitaifa ambao unajumuisha Same na Mwanga na mpaka utaenda Korogwe. Mradi huu umekuwepo kabla Mheshimiwa Maghembe hajawa Waziri. Kwa hiyo, hapa siyo kwamba inatengwa kwasababu yeye ni Waziri lakini *so far* mpaka sasa Mkandarasi amelipwa Shilingi bilioni tano. Shilingi bilioni tatu ni fedha za ndani na nyingine Shilingi bilioni mbili ni fedha za nje. Kwa hiyo, kama ulivyosema, mradi huu unagharamiwa pia na nchi wahisani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sabreena!

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nami niko kwenye *item 6276 - Management Support to Local Government Authorities.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyo mkakati wa Serikali kwamba ni lazima sasa zile sekta ambazo ni muhimu kama Sekta ya Maji tutegemee fedha za ndani kuliko fedha za nje, lakini hapa ukiangalia kwa mwaka huu wa fedha imetengwa Shilingi bilioni 3.2 na fedha za nje

zikiwa ni Shilingi bilioni 10.6. Sasa kama kweli tuna lengo la kujitegemea, ni kwa nini kila siku tunakuwa tunategemea kiwango kikubwa cha fedha kutoka nje badala ya fedha za ndani? Nilitaka ufafanuzi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa, umeona anachoulizia?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujasema kwamba tunaacha kupokea fedha za misaada kutoka nje, lakini tumesema tutajenga uwezo hatua kwa hatua ili bajeti yetu ijitegemee kabisa. Kama ambavyo umeona sasa, tunajitegemea hapa kwa asilimia 74 hivi kwa fedha za maendeleo na asilimia 26 ndiyo fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndivyo tumeanza safari. Katika bajeti nzima ya Serikali ukichukua sasa *average,* Mheshimwia Waziri wa Fedha atatueleza baadae, tumeendelea kupunguza utegemezi wa nje katika miradi yetu ya maendeleo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ole-Medeye!

MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nazungumza juu ya Kasma 3223 ambayo ni *Borehole Driling and Dams Constructions*. Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba tumekutana mara nyingi kwa *request* yake au ya kwangu kuzungumzia changamoto zinazowakabili wananchi wa Arumeru Magharibi kuhusu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasilisha maombi kadhaa kwake, mojawapo ikiwa ni ujenzi wa wa Malambo maeneo ambayo visima haviwezekani kuchimbwa, lakini kwa muda mrefu tunategemea kwamba baadaye tunaweza kupata maji ya mtiririko yaje huko lakini kwa muda tuanze kutumia maji ya mvua ambayo tutayashika kwa kutumia malambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atoe kauli yake, kama kwa fedha hizi zilizotengwa Shilingi bilioni 42 kama sehemu yake nayo itanufaisha maeneo haya ambayo tuliwahi kumwomba atusaidie.

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Naibu Waziri!

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilizotengwa, Shilingi bilioni 42 ni kwa ajili ya mabwawa 12 ambayo yametajwa Mti Mmoja, Lodekese, Salamakati, Nyambori, Wegero, Kawa, Mihama, Kisanga, Morogoro, Bulenya, Kwa Maligwa, Nkoma na Masuguru.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

SPIKA: Mheshimiwa Haroub na wenzako, hatuongeagi wakati Siwa inawekwa.

T A A R I F A

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati na kujadili Bajeti ya Wizara ya Maji Fungu namba 49 kifungu kwa kifungu bila ya mabadiliko yoyote. Naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali na kuyapitisha matumizi ya Wizara ya Maji kama ambavyo yamejadiliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kufikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 –
Wizara ya Maji yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Kwa hiyo, Bajeti ya Wizara ya Maji imepitishwa lakini kama nilivyoagiza, Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Kamati ya Bajeti, wafuatilie kwasababu mwaka juzi tuliamua kabisa kwamba Wizara ya Maji ipate *priority* inayostahili. Ikafika mahali sijui imekuwa nini, ndiyo maana sasa baada ya kuwa na Sheria yetu ya Bajeti kupita, tunapenda sasa tufanye kazi na suala la maji tusilifanyie utani kwasababu ni suala muhimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuwapongeze wataalamu pamoja na Waziri mwenyewe kwa kazi hiyo na naomba tufanye kazi kwa uaminifu kwasababu ni kazi ya uhai, ni kazi inayoweza kulinda uhai wa nchi yote. Nawashukuru sana kwa yote. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu!

HOJA YA KUTENGUA BUNGE

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE): Mheshimiwa Spika, naomba nilete maelezo ya hoja ya kutengua Kanuni za Bunge mbele ya Bunge lako Tukufu.

KWA KUWA chini ya masharti ya Kanuni ya 28 (15) Bunge hukutana siku zote za juma isipokuwa siku ya Jumamosi, Jumapili na siku za mapumziko na kwa kuwa ratiba ya vikao vya Bunge iliahirishwa kwa siku mbili za Jumanne na Jumatano kutokana na msiba wa Mbunge mwenzetu wa Jimbo la Ukonga Mheshimiwa Eugine Elishininga Mwaiposa uliotokea siku ya Jumanne tarehe 2 Juni, 2015 nyumbani kwake hapa Dodoma;

NA KWA KUWA katika kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika tarehe 3 Mei, 2015 kuzingatia upya ratiba ya Mkutano wa Ishirini wa Bunge, Wajumbe wote waliohudhuria waliazimia kuliomba Bunge likubali siku ya Jumapili tarehe 7 juni, 2015 itumie kwa ajili ya shughuli za Mkutano wa Bunge. Hivyo basi, ili kuliwezesha Bunge kukamilisha mijadala ya Hotuba za bajeti za Wizara zilizosalia na wakati huo huo kuliwezesha Bunge kuendelea na shughuli nyingine kama zilivyopangwa kwenye ratiba ya Mkutano huu;

Bunge linaadhimia kwamba Kanuni ya 28 (15) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Bunge halitakutana siku za Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuu, itenguliwe na badala yake Bunge likutane siku ya Jumapili tarehe 7 Juni, 2015, kwa ajili ya kuendelea na mjadala wa hotuba ya bajeti ya Wizara iliyopangwa kuanzia saa 5.00 asubuhi hadi saa 9.00 alasiri, isipokuwa kwamba siku hiyo hakutakuwa na kipindi cha maswali.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kufikiwa)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Kilichotokea baada ya tatizo la msiba tulilokuwa nalo tarehe 8, 9 na 10 ilikuwa kazi ya Bajeti *Commitee* ikae na Wizara kuangalia mafungu. Maana kina Mamlaka pia ya kuhamisha, ndiyo maana pale mnaweza

kupata hata *adendum* katika baadhi ya vifungu. Hata kama mmepitisha hapa, kuna uwezekanio wa kupitia *addendum*.

Sasa kutokana na ule msiba, hata siku ile ya mashauriano ya ndani kabisa nayo yamepungua kwasababu tunatakiwa kumaliza Wizara, ilitakiwa tumalize leo zote, halafu tuanze kazi ya kufanya mashauriano. Lakini haikuwezekana, Mwenyezi Mungu ndivyo alivyopanga. Hatuna *alternative* isipokuwa Wizara ya Fedha ifanyike siku ya Jumapili, Wizara ya Ardhi siku ya Jumatatu; *Budget Committee* ifanye kazi *less than two days* kitu ambacho siyo vizuri.

Kwa hiyo, kwa misingi hii naahirisha kikao hiki mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 2.18 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumamosi,
Tarehe 6 Juni, 2015 saa Tatu Asubuhi)